Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 15 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:**

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma na Hesabu Zilizokaguliwa kwa Miaka ya 2007/2009 na 2008/2009.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. DIANA M. CHILOLO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati na Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. JOHN J. MNYIKA-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Nishati na Madini Kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 238

**Ripoti ya Uchunguzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi ya Ubungo**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza**:-**

Tarehe 15 Machi, 2009 Serikali kupitia Waziri Mkuu iliagiza ufanywe uchunguzi maalum kuhusu makusanyo ya kituo cha Mabasi cha Ubungo ili kuboresha mapato ya Jiji la Dar es Salaam. Tarehe 28 Julai, 2009, Serikali ilikabidhi ripoti ya uchunguzi huo kwa *CAG* ambayo pamoja na mambo mengine ilieleza kasoro za ukusanyaji na tuhuma za ubadhirifu wa mapato ya kituo.

(a) Je, ni lini Serikali itaweka wazi taarifa hiyo?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani juu ya kasoro zilizobainishwa kuhusu mikataba ya kampuni ya *Smart Holdings*, *Rick Hill Hotel*, *Abood Bus Services*, *Clear Channel*, *Globe Accounting Services na Scandinavian Express Services*, ambayo imesababisha hasara na upotevu wa mapato?

(c) Je, Serikali iko tayari kufuatilia na kuchukua hatua za haraka juu ya malalamiko yanayotolewa na ukusanyaji wa mapato unaofanywa sasa ili kunufaisha umma kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NAQ SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, lenye (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali *(CAG)* alifanya uchunguzi maalum katika kituo Kikuu cha Mabasi cha Ubungo na kubaini kasoro mbalimbali. Aidha, hoja zilizojitokeza katika taarifa ya Uchunguzi ya *CAG* katika kituo hicho zimejitokeza pia katika taarifa ya mwaka ya ukaguzi ya *CAG* ya mwaka 2009/2010 ambayo iliwasilishwa hapa Bungeni na hoja hizo zimeaza kufanyiwa kazi na Halmashauri ya Jiji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa kasoro zilizojitokeza katika Kituo hicho, Serikali inapitia upya mikataba ya makampuni na kuhuisha viwango vinavyotakiwa kukusanywa kulingana na sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inayosimamia ushuru huo.

Marekebisho ya viwango hivyo yatasaidia kuongeza mapato yanayokusanywa katika kituo hicho na kuondoa kasoro zilizokuwepo za ukusanyaji wa mapato.

Ukusanyaji wa ushuru katika kituo hicho kwa sasa unafanywa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia kwa Wakala aitwae *KONSAD INVESTMENT LIMITED* ambaye anakusanya ushuru huo kwa wastani wa shilingi milioni 4 hadi milioni 5.7 kwa mwezi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingaia malalamiko yaliyopo, Serikali tayari imebadilisha Menejimenti ya kituo na itaendelea kuboresha miundombinu yake. Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imetenga kiasi cha shilingi milioni 85 kwa ajili ya kufanya matengenezo katika eneo a maegesho ya magari. Mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kukijenga upya kituo cha Mabasi kama ilivyoainishwa katika mpango wa biashara wa mwaka 2007.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majibu yaliyotolewa, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu Naibu Waziri ameeleza kwamba mkandarasi *KONSAD Investment* anakusanya milioni Nne hadi milioni Tano kwa mwezi, lakini kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni kwamba toka Mkandarasi aingie mkataba mwezi Oktoba mwaka 2010, kwa mujibu wa Mkataba alipaswa kukusanya shilingi milioni 5.6 lakini alifanya hivyo kwa siku mbili tu (mara mbili tu) baada ya hapo toka wakati huo Oktoba 2010 mpaka leo amekuwa hatekelezi mkataba na ameandika barua Ofisi ya Waziri Mkuu na inaelekea anakingiwa kifua kuutekeleza huu mkataba.

(a) Ningependa kupata kauli kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na ninajua inafahamu hili jambo kwa undani, Je, iko tayari sasa kuiruhusu Jiji la Dar es Salaam liweze kuvunja huu mkataba ambao haunufaishi wananchi wa Dar Es Salaam?

(b) Suala la udhaifu wa kimikataba wa kituo cha mabasi ya Ubungo ambayo yanahusisha vile vile sehemu ya eneo litakalohusiana na mradi wa mabasi yaendayo kasi ambayo linahusiana na Kampuni ya *UDA* yamefikia kiwango cha juu sana, ninaelewa kwamba ofisi ya Waziri Mkuu iliandika barua ya kusitisha taratibu za uuzwaji wa hisa za kampuni ya *UDA* ambazo zimeuzwa na upotevu wa mali nyingi; ninaomba kauli ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusiana na ufisadi uliopo kwenye kampuni ya *UDA* unaoendelea hivi sasa, na iko tayari kutoa maelekezo kwa Jiji la Dar es Salaam kuweza kusitisha taratibu zinazoendelea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NAQ SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme hapa kwamba, Waziri Mkuu alikwenda akamwelekeza CAG aende katika kituo hiki cha mabasi, akamtaka afanye uchunguzi pale. Walipokwenda pale kwa mara ya kwanza walikuwa wanakusanya milioni 1.5 kwa siku.

*CAG* alipofanya marekebisho yale wakafanya na mahesabu na wakamaliza wakaweka na Menejimenti nyingine pale, ikapanda mpaka milioni 5.7 ninazozizungumza, siyo kwa mwezi ni kwa siku, na kama alivyosema Mbunge kwamba kampuni ilikusanya kwa siku ya kwanza na siku ya pili na baadaye kukawa na matatizo hawakukusanya kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mnyika analifahamu jambo hilo kuliko sisi sote hapa, tunachojua ni kwamba kuna kampuni nyingine mpya ambayo imekwenda pale inafanya kazi na hivi tunavyozungumza hapa wanao huu mgogoro anaozungumza na wameanza kupelekana mpaka mahakamani, kuna mambo ambayo wakati anakwenda ku-operate ameona kwamba yanakwenda kinyume na jinsi walivyokuwa wamekubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza hapa sasa hivi, tumemwita Mkurugenzi Mtendaji Kingopi hapa Dodoma tukamuuliza hili analolizungumza hapa, wameniambia kwamba hili wameliona na wanalifanyia kazi.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mnyika ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri hii tunayoizungumza yaani *(DCC)* avute subira katika jambo hili. Hili jambo jingine jipya sasa linaanza kwa sababu huyu ni mpya ambaye tumesema kwa taratibu hizi mpya akaye pale, kama ikiwezekana tukubaliane leo tukitoka hapa nimwuite Kingobi na wenzake tukae na tuseme ni nini kilichotokea kwamba kiasi hiki sasa hakiendelei kukusanywa kama ilivyokuwa siku ya kwanza na siku ya pili kama anavyosema Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *DART* analolizungumza hapa, huu ni mpango mwingine unaokuja, *DART* tunasimamia sisi Ofisi ya Waziri Mkuu na ujenzi ule utafanywa chini ya Wizara ya Ujenzi, na hili suala la UDA analolizungumza hapa kwa pamoja mimi ningemuomba tukutane kwa sababu linahitaji details zaidi ili tuliangalie pamoja na lile ambalo tumelizungumzia.

Na. 239

**Upatikanaji wa Maji Kata ya Mkundi, Mkululu, na Chiungutwa**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Kwa sababu Serikali imedhamiria kuondoa tatizo la maji nchini.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza miundombinu ya kusambaza maji kutoka chanzo cha uhakika cha maji ya Mkululu ili kusaidia kuondoa tatizo la maji kwenye vijiji vilivyopo kwenye Kata za Mkundi, Mkululu na Chiungutwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NAQ SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali laMheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mbunge kuwa dhamira ya Serikali ni kuwapatia wananchi wake huduma za maji. Chanzo cha maji cha Mkululu kilichoko

umbali wa kilometa 3 kutoka Kata za Mkundi na Mkululu ni chanzo cha uhakika ambacho kingeweza kusaidia katika kuondoa tatizo la maji katika Kata hiyo.

Ili kutatua kero za maji zilizopo Serikali katika mwaka 2009/2010 iliidhiinisha shilingi milioni 134.79. Fedha hizi zilitolewa mwezi Juni, 2010 na kutumika katika mwaka 2010/2011 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kupitia mpango wa Maji na usafi wa mazingira Vijijini.(RWSSP). Kazi zilizofanyika ni uchimbaji wa visima 12 katika vijiji vya Mpitimbi, Shaurimoyo, Nanganga, Mkaliwata, Sindano, Mraushi, Lilala, Mtakuja, Mihina na Nambawala ambavyo vilipewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango wa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 Serikali imeidhinisha shilingi bilioni 1.3 kupitia mpango wa maji na usafi wa Mazingira kwa ajili ya miundombinu ya maji kwenye mradi wa vijiji kumi unaoendela kutekelezwa katika Halmashauri na shilingi milioni 300 zimetengwa kwa ajili ya kujenga uwezo. Katika utekelezaji wa miradi hii mitandao ya mabomba itatandazwa kijijini karibu na makazi ya wananchi ili kupunguza adha ya kutembea umbali mrefu kufuata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kutumia chanzo cha maji Mkululu utaingizwa katika bajeti ya mwaka 2012/2013 baada ya kukamilisha kwa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji kumi vya *RWSSP* unaoendelea. Aidha, suala la vijiji vipi viingizwe katika utekelezaji wa *RWSSP* huamuliwa na wananchi wenyewe na kupitishwa na Halmashauri husika kupitia Baraza la Madiwani.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na majibu amzuri ya Naibu Waziri naomba nijibiwe maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Ningependa kupata maelezo ni lini visima kumi na mbili alivyovianisha katika majibu yake Naibu Waziri, vitapatiwa *pump* na kusambaza maji kwa sababu sasa wananchi wamekuwa wakiendelea kupata shida ya maji wakati visima vile vimeshachimbwa.

(b) Je, Serikali ipo tayari kupeleka watalaam kutoka Wizara ya Maji ili waweze kwenda kufanya tathmini ya mradi wa maji ya Mkululu ambao utanufaisha Kata ya Mkululu, Kata ya Mkundi na Kata ya Chiungutwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimhakikishie kwamba baada ya kwamba visima 12 vimeshachimbwa awamu itakayofuata ni kujenga miundombinu. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba kazi hiyo itafanyika na Halmashauri pamoja na mtalaam mshauri wanasimamia kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupeleka watalaam, naomba nimhakikishie tu kwamba namwomba tu Mheshimiwa Bwanausi akubali na kupitisha Bajeti ya Wizara ya Maji ili tuweze kupeleka watalaam wakaangalie na kuweza kushauri kitu gani kifanyike.

Na. 240

**Tatizo la Msongamano wa Magari Jijini Mwanza**

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA** aliuliza:-

Wakati Serikali iko mbioni kutatua tatizo la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam tatizo hilo hilo limeanza kujitokeza katika Jiji la Mwanza.

Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kudhibiti tatizo hilo kwenye Jiji la Mwanza kabla ya hali haijawa mbaya zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua tahadhari mbalimbali katika kudhibiti tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Mwanza. Zifuatazo ni baadhi ya hatua zinazotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na mamlaka nyingine ili kupata ufumbuzi tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Mwanza.

(i) Halmashauri ya Jiji la Mwanza kupitia mradi wa kuendeleza Miji Tanzania *(TSCP)* kwa uhisani wa Benki ya Dunia ina mpango wa kujenga barabara za mzunguko (*Ring Roads*) zenye njia mbili kila upande wa Pasiansi – Buzuruga na *Tunza-Loop* kwa kiwango cha lami ili kuwafanya watu wanaokwenda kiwanja cha ndege wakitokea maeneo ya Igoma, Nyakato, buzuruga kutolazimika kupita Mjini na kwenda moja kwa moja Kiwanja cha Ndege cha Jiji la Mwanza.

Mradi huu utatekelezwa kwa kujenga jumla ya kilometa 18.3 za barabara za katikati ya Jiji kwa gharama ya shilingi bilioni 24.8. *(Makofi)*

(ii) Halmashauri ya Jiji la Mwanza katika mwaka wa fedha 2011/2012 inatarajia kutumia kiasi cha shilingi bilioni 1.28 fedha kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya miundombinu ya barabara, madaraja na vivuko mbalimbali ili barabara hizo ziweze kupitika wakati wote. Aidha, zimejengwa barabara za pembezoni ili kupunguza msongamano katikati ya Jiji, mfano barabara iliyojengwa kwa tabaka la mawe kutoka Bugando kupitia Igogo mpaka barabara ya lami iendayo Shinyanga.

(iii) Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na wadau ilihamisha stendi kuu ya mabasi katikati ya Jiji na kuipeleka nje ya Mji ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji. Stendi ya Mjini kwenda Nyegezi kwa magari yaendayo Shinyanga, Dodoma na Dar e Salaam na Buzuruga kwa magari yaendayo Musoma na Silari; na

(iv) Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ina mpango wa kujenga soko la Kisasa (*Shopping Moll*) katika eneo la Ghana nje ya Jiji.

Mradi huu unatarajia kutumia shilingi milioni 30 na utekelezaji wake utaanza katika mwaka wa fedha 2011/2012. Lengo la mpango huu ni kupunguza idadi ya watu wanaoingia katikati ya Jiji kufuata mahitaji mbalimbali zikiwemo shughuuli za biashara. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Halmashauri kuwa na mpango wa kujenga barabara kujenga barabara ya mzunguko kutoka Pasiansi hadi Buzuruga kwa njia mbili kila upande, nina uhakika kabisa kwamba kuna baadhi ya nyumba za watu zilizo nzuri na zilizojengwa zikiwa imara zitaguswa.

(a) Je, Serikali mmejiandaa kwa malipo sahihi ya kuwafidia wananchi hawa?

(b) Wakati wa ujenzi wa barabara inayotoka Mjini kuelekea *airport* kuna baadhi ya nyumba ziliguswa hapo hapo Pansiansi unapopaongea Mheshimiwa Naibu Waziri, zikiwemo nyumba zilizojengwa zaidi ya miaka 70 iliyopita.

Mpaka leo kuna baadhi ya Wazee hawajalipwa hata shilingi ya kubomolewa nyumba zao. Naitaka Serikali iwaeleze watu hawa ambao hawajalipwa ni lini watalipwa fidia ya nyumba zao? (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa ya mipango mahususi inayofanywa na Jiji la Mwanza katika kupunguza msongamano wa magari  na hasa kwa kuanza kujenga barabara ya kutoka Pasiansi hadi Buzuruga mradi utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Pia katika mpango mwingine tuna mpango wa kutengeneza barabara nyingine ya kutoka Usagara hadi Kisesa kilometa 17 itakayorahisisha magari yanayotoka Kenya na magari makubwa yanayokwenda nchi jirani yasiwe yanapita Jiji la Mwanza.

Kuhusu wale waliobomolewa kutoka Mjini kwenda *Airport* hakuna hata mmoja atakayelipwa fidia kwa sababu walivunja sheria cap. Namba 167 ya mwaka 1967 iliyoanza kutumika tangu mwaka 1932 ikafanyiwa *amendment* mwaka 1954 ikafanyiwa tena *amendment* mwaka 1967 na ikafanyiwa *amendment* kupitia sheria namba 13 ya mwaka 2007. Kwa hiyo, watu wote ni lazima wazingatie sheria kwa sababu ni msumeno na sheria tumeipitisha sisi wenyewe. (*Makofi*)

Kwa barabara inayotoka Pasiansi kwenda Buzuruga wale wakaokuwa nje ya *road reserve* watalipwa fidia kwa mujibu wa sheria nilizozitaja. (*Makofi*)

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri mimi nina swali moja tu.

Kwa kuwa huko nyuma Serikali ilitaifisha majengo mengi ambayo yalikuwa yanapakana na barabara nchi nzima ikiwemo Mwanza na Dar es Salaam. Kwa haya majengo ambayo yako kandokando na barabara yalikuwa ni mali ya Serikali kwa kuwa yalitaifishwa. Kwa kuwa sasa msongamano umekuwa mkubwa wa magari katika miji yote mikubwa ikiwemo Mwanza, Dar es Salaam na Arusha.

Je, Serikali haioni ni vizuri sasa kubomoa majengo yote yaliyoko kando kando ya barabara na kuwapa *compensation* ili ku-*widen* barabara zote kubwa tupate kama *line* tano tano ili tuweze kumaliza tatizo zima la msongamano wa magari katika Miji mikubwa ya Dar es Salaam na Mwanza, hamwoni ni wakati muafaka kama fedha hazipo basi tukope ili tuweze kufanya hivyo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nimrod Mkono, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba katika miji yetu mingi ikiwemo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha hata Dodoma kwa sasa hivi suala la msongamano wa magari limeanza kujitokeza.

Suala la kutatua msongomano wa magari katika miji yetu haliwezi likatatuliwa tu kwa kupanua barabara. Ni masuala mengi ambayo yanatakiwa kuzingatiwa ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria za watu kuwazuia kufanya biashara barabarani, watu kuacha kujenga vituo vya mafuta barabarani, watu kuzingatia sheria zote ambazo zinatakiwa ambazo zinaweza zikasaidia kupunguza msongamano.

Ninakubaliana pia katika swali lake kwamba kuna umuhimu sasa wa kuanza kuangalia ni kwa namna gani tunaweza tukapanua barabara zetu. Lakini katika sheria ambayo nimeitaja *Road Act* namba 13 ya mwaka 2007 ambayo imepitishwa na Bunge hili na kufanyiwa *regulations* zake za mwaka 2009 na barabara hii kwa mfano ukichukua Dar es Salaam, upana wa barabara ya Dar es Salaam kuanzia Ubungo hadi Kibaha upana wake ni futi 400 kila upande. Kwa hiyo, unaweza ukajenga hata barabara kumi kila upande na bado barabara ikapitika.

Kwa hiyo, kinachotakiwa na mimi ningependa nitoe wito kwa Watanzania wote na Halmashauri za Wilaya na kila mmoja anayewajibika kuhakikisha kwamba tunazingatia sheria ambazo zimepitishwa na Bunge hili ili kuhakikisha kwamba suala la msongamano linaanza kupungua na ikiwezekana kumalizika kabisa ikiwa ni pamoja na kutengeneza *ring road* ambazo zimekuwa zikitengenezwa katika miji yetu.

Na. 141

**Athari za Mgao wa Umeme katika Huduma za Afya Nchini**

**MHE. SYLIVESTER MASSELE MABUMBA** aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni Taifa letu limegubikwa na tatizo sugu la mgao wa umeme ambalo limeathiri huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi:-

Je, ni wananchi wangapi wamepoteza maisha yao katika Hospitali za Serikali tangu mwaka 2009 – 2011 kutokana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Masselle Mabumba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa zilizopokelewa kutoka kwa Waganga Wakuu wa Mikoa kwa kipindi hiki ambacho kumekuwepo na mgao wa umeme hakuna kifo cha mgonjwa kilichohusishwa moja kwa moja na mgao wa umeme.

Hospitali nyingi zimechukua hatua za tahadhari za kuhakikisha kwamba umeme mbadala umekuwepo wakati wote kwa kutumia jenereta, umeme wa *solar* na aina nyingine za vyanzo salama vya mwanga katika hospitali zao kama karabai.

**MHE. SYLIVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la umeme bado ni tatizo sugu na kwamba hatujapata mkakati madhubuti wa kuliondoa katika siku za karibuni.

Je, Serikali inawahakikishia Watanzania katika hospitali zote ambazo huduma zake zinategemea umeme hasa *x- ray, Ultra Sound* na nyinginezo kwamba hazitakuwa *disturbed* kutoka na mgao wa umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna tatizo la umeme ndio sababu tumeanza kusaidiana na Halmashauri kununua majenereta katika Hospitali zetu ambayo yanakuwa ni *standby*. Jukumu kubwa la hizo genereta kwanza ni kuwasha umeme katika *theatre* zetu kusudi tusishindwe kufanya *operation* za *emergency*.

La pili katika *dispensary* zetu nyingi sana tumeanza kuwashawishi Halmashauri waweke umeme mbadala wa *solar* ili tuweze kutumia kwa ajili ya *fridge* za *vaccination* pamoja na kutumika katika maabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba tatizo kubwa la maradhi yanayosumbua Watanzania ambayo tusipoweza kujitambua mapema mtu atakufa ni

malaria. Siku hizi tumechukua hatua moja tumepata sasa vipimo vya malaria ambavyo vinaitwa *malaria rapid diagnostic test* ambayo haitumii umeme hata kama huna mwanga unatumia tochi yake unatengeneza unapata majibu ambayo ni sahihi kwa asilimia 87. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, mambo ya umeme leo ndio mahali pake.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, magereza ya Ngudu – Kwimba yalijengwa mwaka 1962 na mkoloni ilijengwa bila vyoo, wala maji. Wafungwa katika magereza hii wanatumia mitondoo, maana yake ndoo za chuma.

Wanapokwenda kumwaga mitondoo hii hawaisafishi na wala wenyewe hawasafishi mikono yao.

Je, Mheshimiwa Waziri ni lini atatembelea magereza ya Ngudu Mjini ikiwezekana alale pale siku moja ili ashuhudie tatizo kubwa la kiafya ambalo linaendelea katika magereza hii? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, swali la msingi lilihusu mgao wa umeme.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kwamba tatizo ambalo analizungumzia ni tatizo ambalo tumekuwa tunalishughulikia na nimekuwa nalitaja hapa na nadhani Mheshimiwa Mbunge, aelewe kwamba kubwa ambalo linatutatiza ni rasilimali fedha. Kwa kweli tumefanya jitihada kubwa kwa sababu tuna magereza mengi, tunazungumza tatizo la nchi nzima.

Nimwambie kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, atakapotoa hotuba yake siku chache kuanzia leo ni katika mambo ambayo ataeleza na nina uhakika Mheshimiwa Mbunge atapata afuani katika majibu ambayo atayatoa ambayo yatakuwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Naweza nikakujibu tu kwamba hili ni suala tunalifahamu na tunajua kwamba watu walioko magerezani ni Watanzania wana haki kama wewe na mimi na mwingine yeyote yule ukiondoa kwamba wana hatia ya mambo ambayo yamewapeleka magerezani lakini ni jambo ambalo tunalizingatia na haki za binadamu zinazingatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ule wito wa kwenda kulala ndani ya Gereza la Ngudu. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 242

**Ugonjwa wa Saratani Nchini**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Ugonjwa wa Saratani unazidi kuongezeka kila siku hapa nchini:-

(a) Je, ni nini kwa sababu za kuongezeka ugonjwa huo?

(b) Kwa sababu iko hospitali moja tu, *Ocean Road* inayoshughulikia ugonjwa huu. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka huduma za uchunguzi wa saratani kwenye kanda ili kuokoa maisha ya wananchi yanayopotea kwa kushindwa kuhudhuria matibabu *Ocean Road?*

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Magdalena nimhakikishie Mheshimiwa Leticia, kwamba mimi nitatembelea Mwanza halafu nitakuja kwenye hilo Gereza halafu nitawafundisha namna ya kufundishana kunawa mikono ili tupunguze maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zinazochangia ongezeko la ugonjwa wa saratani nchini ni kama ifuatavyo:-

(i) Mabadiliko ya tabia ya watu kula vyakula visivyo asilia na ongezeko la matumizi ya vyakula vya kusindikwa ambavyo kemikali zake huweza kusababisha saratani.

(ii) Kuwepo kwa magonjwa ambayo huambatana na saratani hususan UKIMWI ambapo saratani aina ya *Kaposis Sarcoma*, hujitokeza sana sambamba na saratani ya kizazi kwa wakina mama walioambukizwa magonjwa ya zinaa ya aina ya *Papilloma Virus.*

(iii) Ongezeko kwa matumizi ya bidhaa za tumbaku ambazo husababisha saratani ya midomo na mapafu.

(iv) Kuelimika na kuhamasika kwa wananchi kujitokeza katika vituo vya tiba ili kupima afya zao. Wengi wanaopima ugonjwa huo wanafika katika vituo vya huduma kwa uchunguzi na tiba, hali ambayo inaongeza takwimu zetu. Pia uwezo wa watalaam kutambua ugonjwa na kuweza kushughulikia mapema.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa tiba ya saratani inasogezwa kwa wananchi wote Serikali imeanzisha idara ya kutibu magonjwa ya saratani katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando, kwa Kanda ya Ziwa. Taratibu zinafanyika

kuanzisha huduma hii katika Hospitali za Rufaa za *KCMC* na Mbeya. Lengo ni kutoa huduma hii ya saratani katika Hospitali zote za Rufaa za Mikoa, Kanda na Taifa.

Vile vile, Serikali inashirikiana na Mashirika mbalimbali kama MEWATA, *Tanzania 50 plus Campaign* na mengine ambayo yanajishughulisha na kampeni za tiba ya saratani nchini. Naomba nitoe shukrani kwa mashirika haya yote mawili.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanawake wengi ambao wanapata tatizo la kansa ya kizazi wanafika hospitalini wakiwa wamechelewa sana kwa sababu wengi wanakaa vijijini. Kwa hiyo, wanafika hospitalini wakati wako kwenye *stage* ya mwisho kwamba haitibiki tena, kwa hiyo wengi wanaishia kupoteza maisha.

(a) Ningependa kujua Serikali ina mpango gani mahususi wa kuhakikisha elimu inatolewa vijijini ili wananchi akina mama waweze kugundua dalili za matatizo haya mapema?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zilizofanyika na vyama vya saratani huko *South Africa* na Marekani zimegundua kwamba tunakoelekea kila mwanaume mmoja kati ya wanaume 6 wataathirika na kansa ya pezi dume *(Prostate Cancer)* hapa *Tanzania Protest Cancer* imekuwa ni tatizo kubwa kwa akina baba na hata watoto mpaka miaka mitano, sita wanakumbwa na tatizo hili.

Je, Serikali haioni sasa ni muda maalum wa kuweka mipango mahususi wa kushughulika na tatizo hili kwa namna ya peke kama inavyofanya kwa wagonjwa wa *TB*, malaria na UKIMWI ikienda sambamba na utoaji wa elimu ili kuondoa tatizo hili? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba akina mama wengi wenye matatizo ya *cancer* ya shingo ya kizazi wanafika hospitalini wakiwa wamechelewa. Nafikiri hiyo imekuwa ndio changamoto katika kutoa tiba ya maradhi haya**.** Naomba niseme kwamba sasa hivi Serikali kupitia kitengo chake cha afya ya jamii inajaribu sana kutoa elimu kuhusu *cancer* ya shingo ya kizazi.

Kubwa zaidi imegundulika kwamba kansa ya shingo ya kizazi ina mahusiano makubwa na *human papilloma virus* ambayo ndio inachochea hii kansa kuongezeka ndio sababu sasa tunatoa elimu katika *clinic* zetu za uzazi wa mpango kuhusu usafi wa akina mama na matumizi ya kondomu kwa sababu ni ugonjwa unaoambukizwa kwa njia ya kujamiani ili tuweze kupunguza matatizo hayo na ndio sababu tunaendesha hili zoezi la jando kwa wanaume kwa sababu bila jando wanakuwa ndio *career* wa ile *virus. (Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kusema ni kwamba MEWATA wanajitahidi kutoa elimu na sisi tunapotoa mafunzo kwa wahudumu wetu wa afya wanaokwenda vijijini tutasisitiza watoe hiyo elimu kwa sababu tutaanza ule mpango sasa wa kuanzia *screening* ya kansa ya *Cervix*.

Kuhusu kansa ya *prostate* ni kweli matatizo ya kansa ya *prostate* yanaonekana kwamba yameongezeka. Lakini siyo kwamba yameongezeka ni kwa sababu sasa watu wengi wanagiangalia zaidi afya zao na tuna vipimo sahihi vya kuweza kupima.

Ninachoweza kusema naomba wanaume wajitokeze kwa wingi daktari yeyote ambaye amemaliza *MD* anaweza akakupima kwa kutumia kidole chake tu akajua kwamba kweli kuna hatari ya kuwa na kansa ya *prostate* na akakupeleka pale ambako tutafanya vipimo vya uhakika zaidi ili uweze kupata matibabu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Usukumani, Unyamwezini jando huku. Sasa watu mmesimama. (*Kicheko*)

**MHE. AL-SHYMAR J. KWAGYR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. kwa kuwa ugonjwa wa saratani umekuwa ukiwapata sana watu wazima, lakini kwa miaka ya hivi karibuni ugonjwa huu umekuwa ukiwapata watoto wadogo na mimi ni shuhuda kwa sababu nimejiwekea tabia ya kwenda *ocean road* kuwatembelea wagonjwa, nimekuta watoto wadogo wengi sana wana saratani. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia ni nini tatizo linalosababisha saratani kwa watoto wadogo. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USATAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba nimjibu Mheshimiwa Al- Shymar Kwegyr, Mbunge wa Viti Maalum, kutokea Tanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ukienda *ocean road* sasa hivi utawakuta watoto wengi ambao wana *cancer,* naomba niseme hivi, *cancer* ambayo watoto wengi wanayo kule *ocean road* inaitwa *bacis limfoma* ambayo ni *cancer* ambayo inavimbisha shavu la mtoto, kwa hiyo, zamani walikuwa wanafikiria kwamba ni tambazi au majipu. Kwa hiyo, siku hizi kwa sababu tiba ipo wagonjwa yanapelekwa ocean road kwa ajili ya matibabu kwa sababu wanagundulika mapema na naomba niseme kwamba ile *cancer* inatibika.

Kwa hiyo, naomba nitoe wito kwa wazazi wa watoto kwamba mtoto akivimba shavu kwa sababu yeyote ile mpeleke kwa mganga wa meno aone kwamba sio tatizo la meno kusudi mtoto aweze kupelekwa *ocean road* aweze kupata matibabu na pale wapo wengi kwa sababu ndiyo *center* pekee inayotoa matibabu ya *bacis limfoma* mpaka tutakapofungua center nyingine kwenye hospitali zetu kubwa za rufaa KCMC, Bungando na Mbeya.

Na. 243

**Mahitaji ya Umeme Jimbo la Mikumi**

**MHE. ABDULSALAAM S. AMEIR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kupeleka umeme katika Kata za Zombo,Ulaya,Kisanga na Kijiji cha Mhenda?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mhehsimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulsalaam Suleiman Ameir, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mikumi kuna vijiji vinapata umeme wa gridi kutokea kituo cha kilosa na vijiji vingine vinapata umeme wa gridi pia kutoka kituo cha Kidatu. Kata ya Zombo Ulaya na kijiji cha Mhenda bado havijapatiwa umeme, *TANESCO* inafanya tathmini kujua gharama za utekelezaji wa mradi wa kufikisha umeme katika maeneo hayo.

Tathmini hiyo inajumuisha pamoja na mambo mengine kuandaa mchoro, kufanya makadirio na kutengeneza ratiba ya utekelezaji wa kazi. Tathmini hiyo imeanza tangu mwaka 2010 na inatarajiwa kukamilika mwaka huu wa 2011 ili kuwasilishwa *REA* kwa hizi Kata na Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na tathimini iliyofanmyika katika Kata ya Kisanga, mradi wa kupeleka umeme Kata ya Kisanga, shule ya sekondari Msolwa, kijiji cha Uleling'ombe, Kisanga pamoja na *TAZAMA Pipeline*, unakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 3.3. fedha hizi zitatumika katika ujenzi wa kilomita 83 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33, kilomita 22.5 za njia za msongo wa kilovoti 0.4 na ufungaji wa transformer kama 6 hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina nia ya kusambaza umeme katika maeneo yote ya nchi yetu ili kuchangia katika kuleta maendeleo ya wananchi. Kufanikiwa kwa lengo hili la kusambaza huduma ya umeme kutategemea kukamilika kwa juhudi za kuongeza uwezo wa uzalishaji kwenye gridi na kwenye vyanzo na mitambo nje ya gridi. Serikali inaelekeza jitihada za makusudi katika upatikanaji wa umeme wa dharura katika kipindi cha muda mfupi na mikakati mingine ya muda mrefu ili kufanikisha azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Mikumi wavute subira wakati Serikali inatafuta fedha pamoja na kukamilisha jitihada nyingine zitakazowezesha kupatikana kwa umeme katika maeneo haya kama alivyoyataja. *(Makofi)*

**MHE. ABDULSALAAM S. AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye matumaini. Kuna taasisi moja ya kidini ina mpango wa kujenga au kutumia maporomoko ya Mto Yuvi kwa ajili ya kutoa umeme kwenye Kata ya Kisanga.

Je, Serikali iko tayari kushirikiana na taasisi hiyo ya kidini ili waweze kupata msaada wa Serikali waweze kutoa umeme kwa ajili ya Kata ya Kisanga na Kata iliyoko jirani na Kata ya Kisanga?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulsalaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kushirikiana na waendelezaji na hiyo taasisi ya kidini kwa sababu hiyo inaendana na malengo ya kuanzishwa kwa *REA*.

Kwa hiyo, ninaomba tuwasiliane na hao watu wa taasisi ya kidini waje Wizarani tuwaelekeze *REA* ili kwa pamoja wafanye tathmini wajue kama kwenye hayo maporomoko panaweza pakapatikana umeme wa kutosha kwa bei nafuu yenye ufanisi kwa hizi Kata zote ambazo zimekusudiwa.

**MHE. MWIGULU L. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tatizo la umeme kwa sasa ni janga la Taifa. Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu ameongelea usambazaji lakini tatizo lililopo ni kwamba hakuna umeme, huwezi ukasambaza bila kuwepo na umeme kwanza.

Ukosefu wa Umeme ni janga la Kitaifa kwa sababu sasa hivi wanaofanya kazi saluni, wanaofanya kazi ya kuchomelea vyuma, wanaofanya kazi ya kwenye mashine za kusaga na kuchomea na kadhalika, wanalala na njaa kwa sababu kazi hazifanyiki. Maji hayapatikani, viwanda havifanyi kazi, ajira zinakosekana. Kwa hiyo, litakalofuatia ni wizi utaongezeka sana sana. Uchumi unashuka kwa sababu uzalishaji unashuka kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Je, kwa kuwa hili suala ni la kikanuni?

Je, Serikali sasa itakuwa tayari kurekebisha kanuni zake ambazo labda zinazuia kupatikana vifaa vya dharula ili lichukulie hili suala kwamba ni la udharura na kuweza kuagiza vifaa vya haraka viweze kunusuru Taifa kwenye suala hili kama ambavyo ingechukulia udharura wa kubadilisha kanuni kama nchi hii imevamiwa ili kuweza kuondoa kabisa tatizo la umeme na wananchi waweze kufanya kazi na kuweza kujipatia chakula na Maendeleo yao kwa ujumla?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwigulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Mwigulu amesema tufanye utaratibu wa kununua mitambo ya dharura, maana yake ni kwamba ni lazima twende sasa kwenye masoko ya mitambo hiyo ambayo inapatikana kwa muda wa mwezi mmoja, miwili, mitatu, lakini maana yake ni kwamba itabidi tununue mitambo iliyotumika. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ni utaratibu wa kawaida kwa nchi zingine kununua mitambo kama manuari, mengine na kadhalika, majenereta, treni, engine za treni na kadhalika, sasa wenzetu huko wanabadilisha mitambo hii kulingana na kubadilika kwa teknolojia sio lazima saa nyingine mitambo hii inakuwa na uhai wa mika kumi, kumi na tano lakini teknolojia imebadilika wanaiondoa.

Kwa hiyo, kwetu ni suala la maamuzi, ni lazima tukubaliane ni suala la maamuzi, suala hili linahusu kufanya mabadiliko katika utaratibu wa manunuzi ambayo ziko kwenye kanuni na taratibu za Waziri wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nimelipokea na kwa maana hiyo nimesikia na ninaamini wahusika wote tunaweza kulifanyia tathmini ya faida na hasara zake halafu na sisi pia tulifikishe Idara zingine za Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu amelisikia ili tulifanyie maamuzi.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niungane na Wabunge waliozungumzia suala hili, lakini na kwa ujumla ndiyo *feelings* za tulio wengi juu ya tatizo kubwa hili la umeme na hasa katika kipindi hiki ambacho tungependa kutafuta ufumbuzi wa haraka sana.

Kama alivyosema Naibu Waziri nadhani jambo hili liletwe sisi wote, ni kweli kabisa kwa nia njema kanuni zile zilikuwa zinakataza ununuzi wa mitambo, mashine mbalimbali isipokuwa kama ni mtambo mpya tu, lakini katika mazingira tuliyonayo, ukizungumza mtambo mpya kwa maana ya *generator* mpya inaweza ikatuchukua si chini ya miaka miwili, mitatu sasa tuko katika hali ngumu hili jambo ni kubwa, linahitaji udharura wa pekee.

Kwa niaba ya Serikali nzima nimesema wacha nilichukue jambo hili, tutalifanyia kazi haraka iwezekanavyo, tutashirikisha Kamati za Bunge zinazohusika zote na tutahakikisha vile vile kwamba katika hatua yeyote itakayochukuliwa basi mashine hizo au mitambo hiyo iwe ni mitambo ambayo imekuwa *certified* kwamba ni mitambo mizuri. Tuhakikishe vile vile kwamba isiwe ni mitambo ambayo imetumika miaka mingi kupita kiasi, ili mradi tupate kitu ambacho katika miezi mitatu hii tuliyonayo kingeweza kuongeza kasi na wingi wa upatikanaji wa umeme wakati hatua za muda mrefu zinachukuliwa. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Na. 244

**Utoaji wa Leseni Maalum kwa Wageni**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Tanzania ina rasilimali nyingi hasa Madini na rasilimali watu wenye taaluma ya juu ya Jiolojia Elimu ya Madini amabo wanasajiriwa katika Migodi mbalimbali ndani na nje ya nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamisha utoaji a leseni maalum *Special Mining Licence* (SML) kwa wageni katika maeneo mapya ya madini hususan madini ya dhahabu na badala yake Serikali ifikirie kumiliki Migodi yake kwa kuajiri Wataalam wa kigeni katika maeneo ambayo Watazania hawana uzoefu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufungua mgodi mkubwa wa uchimbaji madini hapa nchini ni lazima kufanya utafutaji madini wa kina ili kugundua mashapo ya madini yanayoweza kuchimbwa kwa faida. Kazi hii haina uhakika kwa kupata mashapo hayo na unahitaji uwekezaji mkubwa wa fedha katika kufanya shughuli za utafutaji madini.

Vile vile pamoja na gharama kubwa, utafutaji huo huweza kuchukua muda mrefu wengine wanafanya utafutaji huo kwa takriban miaka hata kumi(10) kabla ya kugundua kiasi cha mashapo yanayoweza kuchimbwa kwa faida. Kwa mujibu wa sheria ya madini 2010 utafutaji mkubwa wa madini hufanywa na mtu binafsi au kampuni yeyote. Kampuni hiyo inaweza kuwa ya Kitanzania au ya kigeni yenye kumiliki leseni kubwa ya utafutaji madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na sera ya madini ya mwaka 2009 na sheria ya madini ya mwaka 2010 Serikali inaweza kushiriki kimkakati katika miradi ya utafutaji na uchimbaji madini nchini hususan miradi mikubwa. Ushiriki huo ni kwa kupata hisa katika miradi husika kupitia chombo cha Serikali kama vile *STAMICO* au *NDC* kama wasimamizi wakuu wa shughuli za madini katika miradi hii mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina mpango wa kusimamisha utoaji wa leseni maalum (*Special Mining Licence*) kwa wageni kwa maeneo mapya badala yake itaweka mipango thabiti ya kushiriki Kimataifa katika miradi mipya.

Vile vile Serikali itaendelea kuimarisha Shirika la *STAMICO* ili liweze kuwa chombo muhimu cha Serikali na kwa wananchi wote kwa niaba ya Watanzania kushiriki katika miradi mbalimbali ya utafutaji na uchimbaji madini siku zijazo kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Swali la kwanza ni kwamba kwa kuwa Watanzania wamekuwa na malalamiko mengi ya kwamba madini yanachukuliwa na wageni.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba shirika la *STAMICO* linakuwa na nafasi kubwa ya kumiliki migodi mikubwa nchini?

(ii) Kwa kuwa Watanzania wengi wanashiriki katika uchimbaji wa madini mdogo mdogo. Je, Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba sasa Watanzania hawa wanapatiwa nyenzo za kisasa zaidi ili waweze kuboresha ushiriki wao katika Pato la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Masele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ambayo tulitokana nayo kwenye sheria ya madini ya mwaka 2010, tuliweka mkakati maalum na wa makusudi kabisa kusema kwamba sasa hivi kwanza kupitia *element* ile ya *free carried interest*, lakini ya pili ni kuiwezesha *STAMICO* kama itakavyokuwa kwa *TPDC* katika masuala ya mafuta na gesi iwe muhimili wa Taifa katika maeneo yale.

Sasa jambo moja tunalofanya ni kwamba kwa mfano kwenye utoaji wa leseni sasa hivi, tunalenga kwamba utoaji wa leseni kwenye maeneo ambayo ni nyeti yazingatie leseni hizo kupitia *STAMICO* ili *STAMICO* sasa wao wataingia ubia na mwendelezaji, hiyo inawapa nafasi ya kuwa na nafasi fulani katika utekelezaji wa mradi huo wa asilimia 20, 30 kwa manufaa yetu sisi wote na pia watakuwa wanaanza tangu mwanzo wa shughuli yenyewe. *(Makofi)*

Hili la uchimbaji mdogo naomba niseme tu kwamba kwa muda sasa tumekuwa tunazungumzia suala la kuwa na mfuko wa wachimbaji wadogo, mwaka jana zilitengwa bilioni 1.2 ni chache, lakini ni mfuko ambao unaanzia hapa sasa hivi lakini baadaye tutatafuta wachangiaji wengine ambao wataweza kuchangia kwenye mfuko huo. Mwaka huu kwenye Bajeti hii zimetengwa pesa kama za kiasi hicho, lakini kimsingi ni kwamba tunatarajia kwamba uchimbaji mdogo kwanza tutawatengea maeneo lakini pili tutauboresha zaidi huu mfuko wa wachimbaji wadogo, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa vile leo tutashughulika na Bajeti ya Nishati na Madini, naomba wale ambao mna nia hiyo hiyo basi tushughulike wakati huo.

Na. 245

**Ujenzi wa Daraja la Mto Malagalasi**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga daraja linalounganisha Ilagalana Sunuka katika Mto Malagarasi?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Malagalasi unapita sehemu kuu nne katika barabra zinazohudumiwa na Wizara yangu katika Mkoa wa Kigoma. Sehemu hizo ni barabara kati ya Kasulu, Kibondo, Kidawe, Tabora na Simbo Ilagala na Kalya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya msingi kwa ajili ya ujenzi wa daraja la kudumu kuunganisha vijiji vya Ilagala na Sunuka katika barabara ya Simbo - Ilagala - Kalya yameanza.

Wakala wa barabara Mkoa wa Kigoma umeingia mkataba na Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni za daraja hilo katika barabara ya Simo-Ilagala-Kalya. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa usanifu na hivyo kujulikana kwa makisio ya gharama za ujenzi, Serikali itaanza kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuanza ujenzi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha kivuko cha Ilagala ili kiweze kutoa huduma bora kabla ya kukamilika kwa ujenzi wa daraja. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J.GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kivuko kinachofanya kazi katika Mto Malagalasi, kinachounganisha vijiji vya Kata ya Ilagala, Helembe, Kalago na Sunuka hufanya kazi mchana na kuishia saa nne usiku na baada ya masaa hayo, mawasiliano ya vijiji hivyo hukatika nakupelekea wananchi wa maeneo hayo wakiwemo wanawake na watoto kukosa huduma ya usafiri kuwapeleka kupata matibabu pale wanapokuwa wameugua gafla na matatizo mengi huwa ni ya akina mama wajawazito kuweza kupata huduma ya upasuaji na wakati mwingine watoto wadogo kuongezewa damu.

Je, Serikali inasema nini kuhusu kujenga daraja hilo haraka iwezekanavyo ili kunusuru maisha ya wanawake na watoto wanaoishi katika maeneo hayo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Ngenzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa juhudi zake kubwa anazozifanya katika kufuatilia masuala ya barabara pamoja na vivuko katika Mkoa wa Kigoma. Pia ninapenda kumthibitishia

Mheshimiwa Mbunge kwamba, Kivuko cha Ilagara ambacho kiliwekwa pale mwaka 2004, tutaendelea kukikarabati ili kuhakikisha kwamba, kinafanya kazi katika kipindi chote. Mbali na hivyo, Serikali imekuwa na juhudi nyingine kubwa za kufungua ile barabara ambayo ni karibu kilometa 140 kutoka pale Ilagara kuelekea Mpanda. Mpaka hivi sasa zaidi ya jumla ya shilingi milioni 854 zimetumika katika kuifungua hiyo barabara.

Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, madaraja yote yaliyoko katika Mkoa wa Kigoma pamoja na barabara zinapitika. Kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba, kwa hivi sasa tunafanya *feasibility study* na *detailed design* ili tujue gharama halisi za kujenga daraja hilo ambalo linaweza likatumika katika Mto Ilagara. Tukishamaliza kazi hiyo, maandalizi mengine ya kujenga daraja hilo ili kuondoa usumbufu kwa Wananchi itaendelea kutekelezwa kikamilifu. *(Makofi)*

Na. 246

**Kufungwa kwa Kiwanda cha *Tanganyika Packers***

**MHE. NAMELOCK E. M. SOKOINE** aliluliza:-

Kiwanda cha *Tanganyika Packers* kilifanya kazi nzuri ya kuchinja ng'ombe na kusindika nyama na kuuza nje ya nchi na kuipatia Serikali mapato:-

Je, kwa nini Kiwanda hicho kilifungwa wakati malighafi ilikuwepo na bado ipo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Namelock Edward Moringe Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *Tanganyika Packers* ambacho kilianza kujengwa mwaka 1948 na uzalishaji kuanza mwaka 1952, kilisimamisha uzalishaji mwezi Septemba, 1993 kutokana na mitambo ya kiwanda hicho kuwa chakavu sana na kusababisha ubora wa nyama iliyokuwa inasindikwa kutokidhi Viwango vya Kimataifa (*International Sanitary Certification*) hasa kwa Soko la Ulaya, ambalo lilikuwa linanunua nyama iliyokuwa inasindikwa kiwandani hapo. Aidha, kutokana na Kiwanda hicho kuwa na madeni sugu, mali zake zilikabidhiwa rasmi kwa mfilisi mwezi Oktoba mwaka 1993 ili zifilisiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la ufilisi lilifanyika na tarehe 19 Aprili, mwaka 2002 mali za Kiwanda hicho zilizoko Kawe, Jijini Dar es Salaam, ziliuzwa kwa Kampuni ya *Al Ghurair Investement L.L.C.* ya Falme za Kiarabu *UAE* ili wazitumie kwa ajili ya kujenga vitega uchumi vya kitalii kwa eneo la ufukweni; pamoja na kujenga maduka makubwa (*Shopping Malls*) katika eneo lililokuwa la kiwanda; na kujenga majengo ya biashara na makazi katika eneo lililokuwa na kambi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana, ubinafsishaji wa kiwanda hiki uliofanyika kupitia ufilisi wa mali, haukulenga kuendeleza kiwanda cha nyama katika eneo hilo kutokana na ukweli kuwa, eneo limezungukwa na makazi ya watu na hivyo kutokufaa kwa kiwanda cha nyama. Kiwanda cha nyama kinahitaji eneo kubwa ambalo liko mbali na makazi ili kuwa na nafasi ya kujenga eneo la kuhifadhia mifugo kulingana na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na viwanda vya nyama ili kuongeza thamani ya nyama nchini, tayari kuna viwanda vinne vya nyama vinavyofanya kazi hivi sasa. Viwanda hivyo ni Kiwanda cha SAAFI cha Sumbawanga, Kiwanda cha *Kongwa Beef* na Kiwanda cha *NICO*, vyote vya Dodoma na *Tan Meat* cha Dar es Salaam. Aidha, kuna juhudi pia za kuanzisha viwanda vipya vya nyama huko Arusha chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)*, Ruvu na Kagera chini ya Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)*.

**MHE. NAMELOCK E. M. SOKOINE:** Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(i) Kwa kuwa Kiwanda kiliuzwa; ni nini hatima ya wafanyakazi wanaokaa hapo na hawajalipwa?

(ii) Kwa kuwa kiwanda hakina ufanisi; je, Serikali haioni kuna haja ya kuanzisha kiwanda mfano Mkoani Arusha ambako tunahitaji viwanda kama hivyo ili kuanzisha ajira kwa vijanana akina mama wa Mkoa wa Arusha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimpongeze sana Mheshimiwa Sokoine, kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba, Wafugaji wa Tanzania wanapata huduma bora, wanapata bei bora na wanapata masoko bora kwa kuongeza viwanda vya nyama nchini. Ninaomba nijibu swali lake kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali inafahamu kwamba, wafanyakazi wote waliofanya katika viwanda vyetu mbalimbali nchini, kikiwepo Kiwanda hiki cha *Tanganyika Packers*, wanastahili haki zote chini ya Sheria za Ajira na pale ambako haki hizo hazijapatikana, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba, haki hizo zinapatikana kwa kuwafuatilia wale ambao walikuwa ni waajiri wao.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwanza, kiwanda hiki kilikuwa kinafanya vizuri sana. Kilikuwa kinazalisha nyama nyingi, kilikuwa na soko la Ulaya na niseme katika mwaka 1952, ambako kiwanda hiki kilianza kazi hadi mwaka 1993 ambapo kiwanda hiki kiliacha kufanya kazi, ilipita miaka 41 ya faida. Kuna watu ambao hawakuitendea hii nchi uaminifu kwa sababu katika hali ya kawaida na tunasisitiza viwanda vyote vinavyofunguliwa na Serikali aidha ni Serikali yenyewe au na ubia na mashirika mengine; ni sharti wanaohusika wahakikishe kwamba, wanaendelea kuwekeza katika vile viwanda na siyo kukiacha mpaka kife halafu uingie katika madeni. Ninatoa

wito kwa wote ambao wanahusika na mali za umma kuwa makini kwa sababu tabia kama hii hatutaweza kuiruhusu itokee tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, tunaazimia kuanzisha kiwanda kingine cha nyama katika Mkoa wa Arusha chini ya utaratibu unaofanywa na Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* na sambamba na taratibu zingine za uanzishaji wa viwanda vipya vya nyama. Cha muhimu katika viwanda vya nyama kwanza ni lazima eneo liwe kubwa. Pili, lazima liwe mbali na makazi ya watu kwa sababu lazima uwe na eneo ambalo unatunzia mifugo kabla ya *processes* hazijafanyika. Usafi, uwekezaji na vifaa vya kisasa ili viweze kufikia viwango vya kimataifa vya kuweza kuuza nyama katika masoko ya nje na masoko yetu ya ndani.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Mwekezaji huyu *Al Ghurair* alipewa kiwanda mwaka 2002 licha ya kwamba, alikuwa hajalipa fedha zote. Pili, kikubwa alichokifanya ni kung'oa mashine pamoja na kuuza viwanda akishirikiana na mdau mwenzake Adam Jee. Sasa kuna taarifa licha ya upungufu huo wote kwamba, Serikali ipo katika majadiliano na mwekezaji huyu ambaye amekiuka matakwa ya mikataba ili waangalie watamlipa vipi walichukue lile eneo. Sasa nilitaka kupata kauli kutoka Serikalini; ni kweli wapo katika majadiliano na kuna tija gani ya kujadiliana na mtu ambaye badala ya kufanya kile ambacho alitakiwa akifanye hajafanya na fedha hajalipa na Serikali inashindwa kuchukua hatua; sasa nilitaka Serikali initaarifu hali ya *Tanganyika Packers* kwa mtazamo wenu ikoje ukizingatia kwamba mwekezaji hajakidhi vigezo vyovyote; hajatekeleza mkataba kama anavyotakiwa na licha ya kwamba hakulipa fedha zote? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niseme kwamba, *Tanganyika Packers* pamoja na kufilisiwa na kuuziwa kampuni hii ya *Al Ghurair Investement* ya *UAE,* bado ilikuwa na mali zingine, kwanza, sehemu ya *holding ground* pale Kibamba, ambapo Serikali imekabidhi Chuo Kikuu cha Muhimbili ili kiweze kutumia hilo eneo katika kujiendeleza.

Pili, kulikuwa na kiwanda kingine Shinyanga ambacho kilishauzwa kwa Kampuni ya *Triple S,* lakini mpaka sasa hivi kiwanda hicho hakifanyi kazi na tunategemea kukirudisha Serikalini. Tatu, kuna eneo la kuhifadhia ng'ombe katika eneo la Kitara pale Singida, ambalo liko chini ya *Consolidated Holding* na mwisho ni Kiwanda cha *Mbeya Packers,* ambacho mpaka sasa hivi pia hakijauzwa. Heka 180 katika eneo la Kawe nazo bado hazijauzwa. Hili lilikuwa ni eneo la makazi ambalo lipo pale Kawe. Utaratibu wowote ambao utatumika kubinafsisha hili eneo la hekari 180 na nilitaka nimhakikishie Mheshimiwa Halima Mdee, hautafanyika bila kushirikiana na Shirika letu la Nyumba la Taifa.

Nimalizie kwa kukubaliana naye kwamba, katika makubaliano ya uwekezaji kati ya Serikali na *Al Ghurair Investement LLC* ya Falme ya Kiarabu, kulikuwa na mambo mengi ya kufanya ya wazi. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, kwanza, kulikuwa na kujenga vitega uchumi katika eneo la ufukweni ambavyo siyo vyote vimefanyika. Pili, kulikuwa kuna kujenga maduka makubwa makubwa *(Higher Shopping Malls)* katika eneo lililokuwa la Kiwanda na wote tunafahamu kwamba, hilo eneo lililokuwa la

kiwanda bado liko vilevile. Tatu, kulikuwa na kujenga majengo ya makazi katika maeneo mbalimbali ambayo bado hayajafanyika. Serikali itafanya utaratibu kama tulivyoeleza wa kuhakikisha kwamba, tunapitia upya ubinafsishaji wa hiki kiwanda na kuhakikisha kwamba, maslahi ya nchi kwa vyovyote vile yanalindwa.

Na. 247

**Upatikanaji wa Vitambulisho vya Uraia**

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID** aliuliza:-

Utaratibu mzuri wa Kiongozi anayeongoza Wananchi ni lazima kuwatambua Wananchi anaowaongoza kwa njia ya kuwapatia vitambulisho vya uraia ukitofautisha na ukaazi:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha zoezi la kutoa vitambulisho vya uraia?

(b) Je, mfumo huo wa vitambulisho utatumika vipi katika ngazi za chini za Viongozi wa Kata na Wilaya?

(c) Je, mpango mzima utagharimu kiasi gani cha fedha hadi kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali inafanya maandalizi ya kutoa Vitambulisho vya Taifa. Kama mnavyojua, Serikali ilitiliana saini Mkataba wa Kutekeleza Mradi wa Vitambulisho na Kampuni ya *IRIS* kutoka Malaysia. Tayari Wizara yangu imeshaomba fedha za malipo ya awali ya Tsh. Bilioni 47 kwa ajili ya Kampuni ya *IRIS* ili aanze kuagiza vifaa muhimu vya Mradi. Iwapo Wizara yangu itazipata fedha hizi haraka, tunatarajia kutoa Vitambulisho vya Taifa mwisho wa mwaka 2011 kwa awamu ya kwanza. Katika awamu hii, mamlaka ya vitambulisho itatoa vitambulisho kwa Wafanyakazi wa Serikali, Wanafunzi wa Sekondari, Vyuo na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa Vitambulisho vya Taifa utatumika kuwasaidia Viongozi wa Kata na Wilaya katika mambo yafuatayo: Kusaidia kumtambua mhusika anapohitaji kupatiwa huduma katika taasisi mbalimbali za kijamii mfano benki, taasisi za mikopo na huduma za afya; kudhibiti vitendo vya uhalifu; na kuwatambua Wananchi wenye uraia halali wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi huu utagharimu kiasi cha fedha za Kitanzania zipatazo shilingi bilioni 355 kwa kipindi cha miaka mitano. Fedha hizi

zitajumuisha malipo ya mkandarasi, mshauri wa mradi na ujenzi wa ofisi katika Wilaya zote Tanzania Bara.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Ninashukuru Mheshimiwa Naibu Spika.

(i) Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kiukweli ni kwamba, vitambulisho ni moja katika njia ambazo zinategemewa kuongeza mapato kutoka kwa wale ambao wanatakiwa wawe walipa kodi, lakini kwa namna fulani hawajulikani. Sasa ni kwa kiasi gani Mradi huu wa Vitambulisho umeunganishwa na mfumo wa *TRA?*

(ii) Ni kwa kiasi gani ambacho Serikali inategemea kuwatambua wasiokuwa walipa kodi kwa kipindi cha sasa ambao wanategemewa kesho wawe walipa kodi baada ya kuwa na vitambulisho?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, amegusa pale pale ambapo vitambulisho vinalenga. Maana yake upo ushahidi wa kutosha kwamba, watu wengi katika Taifa letu hawalipi kodi. Mfumo mzima wa kuwatambua jinsi ya kuwapata waweze kulipa kodi waweze kuchanga katika mapato na uchumi wa nchi yetu imekuwa tatizo.

Kwa hiyo, hii siyo kwamba, maana yake ni mfumo mzima na itakwenda katika *TRA*, itakwenda katika huduma za Mabenki, kuna wale wanaochukua mikopo wanaingia mitini hawalipi. Kuna watu ambao wamefanya vitendo vya uhalifu, wanarudia tena kufanya vitendo vya uhalifu, wanakuwa hawatambulikani, kwa sababu kunakuwa hakuna *Data Base.* Kwa hiyo, shabaha kubwa na lengo kubwa ni katika maeneo mbalimbali ikiwemo hili suala la ukwepaji wa kulipa kodi na tayari *NIDA*, chombo kinachohusika na utaratibu mzima wa Vitambulisho hivi vya Taifa, imekuwa na mazungumzo na vyombo mbalimbali na taasisi mbalimbali ili kuweza kutengeneza mfumo wa kuwatambua Watanzania na wale ambao siyo Watanzania kwa sababu hivi ni Vitambulisho vya Utaifa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Ninashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Vitambulisho ni nyenzo muhimu katika kuwatambua Watanzania; je, Serikali ina utaratibu gani kuhakikisha kwamba Watanzania hawa na vitambulisho hivi vinakuwa na *details* zote zinazotakiwa kwa mfano *physical address?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakika vitambulisho hivi, *system* ambayo tumeichukua ni *system* ya *smart card* na utakuta nchi za jirani ambao kwa mfano kama Kenya, walikuwa na ile *BACO,* ambayo *by nature* kile kitambulisho huwezi ukaweka *additional information;* lakini huu utaratibu wa *system* ya vitambulisho tulivyochukua *BACO* yna *flexibility* ndani yake kiasi kwamba inaweza kuchukua *all the relevant information* ambazo tutakuwa nazo. Muhimu katika Kitambulisho hiki cha Utaifa ni kujua huyu mwenye kitambulisho ni nani.

Pili, huyu mwenye kitambulisho anafanya katika Tanzania. Tatu, huyu mwenye kitambulisho anapatikana wapi, anakaa wapi. Kwa hiyo, inalenga katika mambo hayo yote na ninadhani *concerns* za Mheshimiwa Mbunge zitakuwa *addressed* kwa utaratibu wa *smart card.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kipindi cha maswali umetuishia kabisa. Ninawashukuru sana kwa kushiriki kwa uchangamfu. Wageni tulio nao hapa Bungeni ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Waziri William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, ambao ni pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu David Jairo, karibu sana. Tuna Mkurugenzi wa Mipango na Sera, Bwana Swai; Ndugu Kafumu, Kamishna wa Madini; Kaimu Kamishna wa Nishati, Ndugu Seofil Bwakea; Mkurugenzi wa Utawala, Ndugu Theresia Mhanga; na Mhasibu Mkuu, Ndugu Rose Vaniha. *(Makofi)*

Vilevile, wapo Jeneral Robert Mboma, Mwenyekiti wa Bodi *TPDC*; karibu sana Jenerali. Ndugu Yona Kilagane, Mkurugenzi Mkuu *TPDC;* Balozi Ame Mpungwe, Mwenyekiti *REA;* Dkt. Mwakahesya; na Mkurugenzi Mkuu *REA* na vijiji vya Kongwa kule usisahau. *(Kicheko)*

Ninaomba kumtambulisha Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO*, Mbunge aliyestaafu, Mheshimiwa Bwana Semindu Pawa. Mheshimiwa Semindu Pawa karibu sana. Kwa Wabunge wa siku nyingi, wanafahamu umahiri wako katika kuzungumza ndani ya Bunge. Nikuhakikishie, rekodi yako bado haijavunjwa; ilikuwa Semindu Pawa akisimama viti karibu vinapasuka humu ndani. *(Makofi)*

Yupo Mkurugenzi Mkuu *TANESCO*, William Mhando; Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO*, Ndugu Ramadhani Hatibu; Ndugu Grey Mwakalukwa, Mkurugenzi Mkuu *STAMICO;* Ndugu Haruna Masebu, Mkurugenzi Mkuu *EWURA;* Profesa Idrissa Kikula; Mwenyekiti wa Bodi *GST;* Profesa Kikula sijamwona, ambaye pia ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma; na Profesa Abdulkarim Mruma, Mtendaji Mkuu *GST*, ahsante.

Pia yupo Dokta Yamungu Kayandabila; Mwenyekiti *TMAA*, ahsante. Injinia Paul Masanja, Mtendaji Mkuu *TMAA;* na Ndugu Stephano Ndabasi, Mkuu wa Chuo Cha Madini Dodoma. Watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini mliopo, ambao sijawataja, ninaomba msimame. Ninaona wapo huku; karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Nina wageni wangu; Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge Mstaafu kutoka Jimbo la Masasi; karibu sana Mheshimiwa Mrope. Alikuwa ni Mbunge wetu wa Jimbo la Masasi katika Bunge lililopita tu la tisa, hapa ndani. Bahati mbaya katika uchaguzi huu hakuweza kurudi, kuna Mbunge wa Viti Maalum sasa ni Mbunge wa Jimbo, amechukua nafasi. Kwa hiyo, Wabunge wa Majimbo, msiwaangalie kwa wepesi Wabunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Mrope karibu sana. Vilevile amefuatana na Ndugu Arbogasti Owiso na wanaoshughulika na masuala ya uwekezaji katika maeneo ya gesi. *(Makofi)*

Wanafunzi 15 kutoka Shule ya Sekondari Kigwe, Wilaya ya Bahi, Dodoma; Wanafunzi wa Kigwe karibuni sana. Kwa Waheshimiwa Wabunge wasiofahamu

Kigogo, Kiswahili ndiyo Kigwe lakini Kigogo ni Chigwe; kwa hiyo, karibuni toka Chigwe; Wagogo hawana Ki, wana Chi. *(Makofi)*

Wanafunzi 50 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi ya Mbezi Dar es Salaam. Karibuni sana Wanafunzi na Walimu kutoka kule Mbezi, Dar es Salaam. Wanafunzi, hili ndiyo Bunge lenu, tunawategemea mkikua na ninyi mtakuwa sehemu ya Bunge hili; karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wainjilisti 20 kutoka Kanisa la Wa-Adventisti Wasabato kutoka Dodoma, ninadhani. Wainjilisti kutoka Kanisa la Wasabato, karibuni sana. Tunaomba mwendelee kuliombea Bunge letu, tusitembelewe na Maruhani, tuendelee kuwa na amani. Ahsanteni sana na karibuni Wainjilisti. *(Makofi)*

Ninaomba kuwatambua wanafunzi saba kutoka Jimbo la Iramba Magharibi, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Lameck Mwigulu, Mchemba. Ahsanteni sana, karibuni sana Bungeni. Mbunge wenu, Ndugu Mwigulu, anafanya kazi nzuri hapa Bungeni, tupelekeeni salamu huko. *(Makofi)*

Ninalo tangazo la Mheshimiwa Amos Makala kwa Wabunge wote kwamba, kesho Uwanja wa Jamhuri, saa 9.00 alasiri, kutakuwa na Mechi ya Kirafiki kati ya Timu Mahiri ya Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndugu zetu wa *PSPF,* saa 9.00 jioni. Wabunge wote tunaombwa kwenda kuishangilia Timu yetu ya Bunge, ambayo ni machachari kweli kweli na Wakazi wa Dodoma vilevile wanakaribishwa kuona mechi hii.

Tangazo la Semina; Ofisi ya Bunge, inaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba, keshokutwa, Jumapili, tarehe 17 Julai, 2011 saa 4.30 asubuhi. kutakuwa na Semina itakayotolewa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na itahusu uzoefu wa utoaji elimu huria na *ESAFA.* Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hii bila kukosa; nyote mnakaribishwa.

Baada ya matangazo hayo, sasa ninaomba Katibu tuendelee na hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012
### Wizara ya Nishati na Madini

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, kama mtakavyoona *Order Paper* yetu ya leo ni Wizara ya Nishati na Madini. Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, maombi ambayo tumepata mpaka sasa ni mengi, karibu tunafunga daftari;

lakini ili msiniandikie sana hapa Mezani, kwa kiasi kikubwa inavyoelekea watakaochangia ni wale ambao ama hawajachangia kabisa au waliochangia mara moja tu. Waliochangia baada ya hapo, itakuwa nadra sana kupata nafasi.

Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ngeleja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia mimi pamoja na Bunge lako Tukufu, uhai ambao unatuwezesha kuendelea kufanya shughuli ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzingatia Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2010/11 na kukubali kupitisha Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kwa mara nyingine kuliongoza Taifa letu katika muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa heshima na taadhima, ninamshukuru kwa kuniteua tena kuongoza Wizara ya Nishati na Madini katika awamu hii ya pili ya uongozi wake. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dokta Mohamed Gharib Bilal, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuteuliwa kwa mara nyingine tena kushika wadhifa wa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Spika, lakini pia kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Naibu Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge na Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge, kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wenyeviti wa Bunge hili Tukufu. Vilevile, ninaipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Januari Yusufu Makamba, Mbunge na Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge, kwa kuteuliwa kwao kuiongoza Kamati hiyo. Aidha, ninawapongeza Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa umakini waliouonesha wakati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa 2010/11 na Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote, kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo. Vilevile, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, kwa kuchaguliwa na Wananchi na kuteuliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. Ninawaahidi ushirikiano wa hali ya juu, mimi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wangu katika kutekeleza majukumu yetu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote waliowasilisha na kupitishwa bajeti zao. Aidha, ninawatakia kila la heri Waheshimiwa Mawaziri watakaowasilisha bajeti zao baada ya hii ya kwetu ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninawasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2010/11 na Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara kwa Mwaka 2011/12, ikiwa ni baada ya Serikali kutayarisha, kuzindua na kutangaza na Bunge lako Tukufu kuridhia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), kwa utekelezaji mwezi Juni, 2011. Ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kubaini umuhimu wa Taifa letu kurejea utaratibu mzuri wa kuwa na mipango ya maendeleo ya miaka mitano mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali, Bunge lako Tukufu, Ofisi ya Rais (Tume ya Mipango), chini ya uongozi wa Katibu Mtendaji Dokta Phillip Mpango na Naibu Makatibu Watendaji wake pamoja na wadau wote walioshiriki kufanikisha maandalizi ya Mpango huo. Mpango huo umefungua ukurasa mpya kwa Taifa letu katika juhudi za kuharakisha kasi ya maendeleo ya nchi yetu kwa kulifanya suala la upatikanaji wa nishati ya umeme toshelevu na ya uhakika kwa mahitaji ya ndani na kuuza katika nchi jirani kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vya kwanza katika utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyobainishwa kwenye Mpango, malengo ya utekelezaji ni kuongeza uzalishaji wa umeme kufikia kiasi kisichopungua *MW* 2,780 na kuboresha njia za usafirishaji na usambazaji umeme. Kwa hakika Serikali yetu ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Bunge lako Tukufu chini ya uongozi wako Mheshimiwa Spika, Anne Makinda, pamoja na wewe Naibu Spika na Wenyeviti wote, tutakumbukwa na historia ya nchi yetu kwa kufanikisha Mpango huo kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Mpango huo utatuwezesha kufikia malengo yetu ya kuwafikishia umeme angalau asilimia 30 ya Watanzania ifikapo mwaka 2015 kutoka asilimia 14.5 kama ilivyo sasa na kupunguza upotevu wa umeme kwenye mifumo yetu ya usafirishaji na usambazaji kutoka asilimia 21 kama ilivyo sasa hadi kufikia asilimia 15 ifikapo mwaka 2015. Wizara yangu imejipanga ipasavyo kufanikisha malengo ya Mpango huo mahususi kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Sengerema kwa kuwa na imani na mimi na kwa kunichagua tena na kunipitisha bila kupingwa kwenye uchaguzi uliopita na kuwa Mbunge wao na kwa jinsi wanavyoendelea kuniunga mkono katika utumishi wangu wa umma kwa Watanzania. Ninawaahidi kuwatumikia kwa uadilifu. Ninaishukuru familia yangu, hususan, mke wangu Blandina na watoto wetu Brian, Brigette na Braid-Bill Junior na wazazi wangu, kwa kunitia nguvu na kunipa moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaomba nitoe taarifa; kwa utaratibu wa kawaida wa miaka iliyopita, siku kama ya leo, mke wangu Blandina Ngeleja, angeweza kuwepo kwenye *Gallery*, lakini kwa sababu tuna mtoto mchanga mwenye miezi mitatu na nusu, nimemwombea radhi kwamba, hatakuwepo leo kushuhudia. Ninaamini popote alipo mke wangu mpenzi, anaendelea kushuhudia taarifa hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2010/11, ulizingatia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (2000 – 2015); Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya MKUKUTA; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; Ahadi za Serikali Bungeni za Mwaka 2009/10; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti 2010/11 – 2013/14; kaulimbiu ya Kilimo Kwanza; Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali; na maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2010/11, maeneo yafuatayo yalipewa kipaumbele: Kuendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya na Miradi ya Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini; kujenga mitambo ya kufua umeme ya *MW* 100 Ubungo, Dar es Salaam na *MW 60* Nyakato, Mwanza; kuimarisha na kuboresha mifumo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kuendeleza na kuhamasisha utafutaji wa mafuta na gesi asili; kuimarisha na kupanua miundombinu ya gesi asili, kuendeleza taratibu za kuanzisha hifadhi ya Taifa ya mafuta na uagizaji wa mafuta kwa pamoja; kuhamasisha uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala; na matumizi bora ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yaliyopewa kipaumbele ni kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini; kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; kuimarisha ukaguzi wa shughuli za migodi katika maeneo ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira; kuimarisha Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA)* katika ufuatiliaji na ukaguzi wa shughuli za uchimbaji na mazingira; kuliwezesha Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* kutekeleza majukumu yake mapya; kuwezesha Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* na Chuo cha Madini kutekeleza majukumu yake; kuendeleza na kusimamia Mgodi wa Makaa ya Mawe ya Kiwira, kumarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2010/11, Wizara ilipata mafanikio mbalimbali. Mafanikio katika Sekta ya Nishati ni pamoja na kukamilika kwa upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Kishapu, Rorya na Longido; kuanza kufanya kazi kwa mitambo ya *MW* 7.5 ya kufua umeme kwa kutumia gesi asili iliyopo Somanga Fungu na jenereta zenye uwezo wa kufua *MW* 6.25 zinazotumia mafuta mazito zilizofungwa Mjini Kigoma; kukamilika kwa Mradi wa *Way Leave Village Electrification* katika eneo la Kilwa, Wilaya ya Rufiji, ikijumuisha Bungu, Somanga, Muhoro, Nyamwage, Nangurukuru, Kindwitwi, Kibiti, Utete, Tingi, maeneo ya Njia Nne na Hospitali ya Mchukwi; na kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa *kV*132 kutoka Ubungo hadi Makumbusho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni kufungwa kwa mita maalumu zijulikanazo kama *smart meters* kwa watumiaji wakubwa wa umeme, utaratibu uliosaidia kupunguza upotevu wa umeme kutoka asilimia 26 hadi asilimia 21 kwa sasa; kuongezeka kwa uwekezaji katika uzalishaji wa umeme kupitia mfumo maalumu wa kushirikisha wazalishaji wadogo kwa miradi isiyozidi *MW* kumi, ambapo hadi sasa mikataba mitano imesainiwa kati yao na *TANESCO*; na kuimarisha na kupanua miundombinu ya umeme kwa ajili ya Taasisi ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia iliyopo Tengeru, Arusha. Mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa Chuo cha Ufundi cha *TANESCO* kwa msaada wa Serikali ya Japani kilichopo Masaki, Dar es Salaam; na kudhibiti uchakachuaji wa mafuta kutoka asilimia 70 mwezi Mei, 2009 hadi asilimia 23 mwezi Mei, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine katika Sekta ya Nishati ni kupungua kwa siku za kuunganisha umeme kwa wateja walio ndani ya mita 30 kutoka siku 270 hadi ndani ya siku 109 kama ilivyobainishwa katika Ripoti ya Benki ya Dunia inayohusu *"Doing Business 2011"*; kuanzishwa kwa kituo cha miito ya simu *(call centre) TANESCO* kwa ajili ya kuboresha huduma ya umeme kwa wateja; kukamilika na kuanza kutumika kwa viwango *(standards)* vya vifaa vya umeme jua; kuzinduliwa kwa Programu ya Kitaifa ya Uendelezaji wa Biogesi katika ngazi ya kaya; kukamilika kwa Kanuni za Uagizaji wa Mafuta wa Pamoja *(Bulk Procurement)*; na *EWURA* kupitisha mradi wa upanuzi wa mitambo ya kusafisha gesi asili Kisiwani Songo Songo unaotekelezwa na Kampuni ya *Songas* kutoka futi za ujazo milioni 105 hadi 140.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni kugunduliwa kwa gesi asili kwenye kina kirefu *(deep-sea)* kwenye Kitalu Na. 4 (visima vya Pweza - 1 na Chewa - 1) na Kitalu Na. 1 (kisima cha Chaza - 1); kuongezeka kwa idadi ya viwanda na taasisi zinazotumia gesi asili kutoka 33 hadi 37. Viwanda na taasisi zilizoongezeka ni *Bautech II, MMI Steel II, Iron & Steel* na Gereza la Keko, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Madini, mafanikio ni pamoja na kuanza kutumika kwa Sheria Mpya ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake; kukamilika kwa Marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Baruti na vibali vya matumizi ya baruti kuanza kulipiwa, hivyo kuongeza wigo wa ukusanyaji wa maduhuli; Serikali kukusanya shilingi milioni 709 kutoka kwa wamiliki wa migodi mikubwa ya dhahabu, kutokana na kazi ya ulinganisho wa malipo ya mrabaha *(royalty reconciliation)* iliyofanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA)* mwaka 2009/10, kiasi ambacho kisingelipwa endapo ulinganisho huo usingefanyika; Serikali kupata shilingi bilioni 32.26 zilizolipwa kwa mara ya kwanza kama *Corporate Tax* kutoka Kampuni ya Madini ya *Resolute Tanzania Limited (RTL)*, kutokana na ukaguzi wa hesabu za kampuni hiyo uliofanywa na *TMAA* kwa kushirikiana na *TRA*; kupatikana kwa mbia mpya wa mgodi wa *Buckreef* ambapo Serikali kupitia *STAMICO* inamiliki hisa asilimia 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni Kitengo cha Uchambuzi wa Almasi *(TANSORT)* kufanya shughuli zake hapa nchini baada ya kuhamishwa kutoka London, Uingereza; kuwezesha utafutaji wa madini hadi kufikia hatua ya kuandaa Mradi wa

Machimbo ya Madini ya Urani Wilayani Namtumbo; kuwawezesha wachimbaji wadogo na wa kati kupitia Mfuko wa Wachimbaji Wadogo ambapo hadi kufikia Juni, 2011 jumla ya shilingi milioni 525 zilikuwa zimetolewa; kutolewa mafunzo kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya Handeni na Kilindi kuhusu usalama, afya na utunzaji wa mazingira; na kutolewa kwa matangazo kila wiki kwenye magazeti ya hapa nchini kuelezea viwango vya bei za madini. Hii imewasaidia wachimbaji wa ndani kuuza madini yao kwa bei inayolingana na thamani yake na pia imeongeza mapato ya Serikali; Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* kupata vituo vipya katika maeneo ya Mtwara na Geita vitakavyofungwa mitambo ya kupimia matetemeko ya ardhi na kufanya jumla ya vituo hivyo kufikia tisa nchini; na kukamilisha masharti ya kujiunga na Tasnia ya Uziduaji *(Extractive Industries Transparency Initiative – EITI)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara ilikusanya Shilingi 109,806,131,964, ambayo ni asilimia 107.2 ya lengo la Wizara la kukusanya Shilingi 102,442,231,000. Mafanikio haya pamoja na mambo mengine, yametokana na usimamizi thabiti wa utekelezaji wa Sheria Mpya ya Madini na kuimarishwa kwa Ofisi za Madini za Kanda kwa kuzipatia vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya mafanikio yaliyopatikana, changamoto mbalimbali zilijitokeza katika utekelezaji. Changamoto katika Sekta ya Nishati ni pamoja na bei za juu za mafuta katika soko la dunia; kufikia lengo la asilimia 30 ya Wananchi wanaopata umeme ifikapo mwaka 2015; upatikanaji wa malighafi zenye ubora na zinazopatikana hapa nchini kwa ajili ya Miradi ya Umeme; kupunguza upotevu wa umeme; kupanuka kwa wakati kwa miundombinu ya kusafisha na kusafirisha gesi asili ili kuwianisha upatikanaji na mahitaji ya gesi; kuwianisha upatikanaji wa nishati yenye uhakika ili kuendana na mahitaji ya watumiaji yanayoongezeka kwa kasi; na mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababisha upungufu wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa Sekta ya Madini, changamoto ni kukua haraka kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji madini ikilinganishwa na uwezo wa usimamizi; kampuni za madini kulipa viwango vipya vya mrabaha na kodi nyingine za uchimbaji kulingana na mikataba iliyopo kati ya wawekezaji na Serikali kwa kuzingatia Sheria Mpya ya Madini ya Mwaka 2010; kuimarisha Sekta ya Madini ili iweze kuvutia uwekezaji; upatikanaji wa masoko ya bidhaa za madini kwa wachimbaji wadogo; kutekeleza ipasavyo Mkakati wa Kuwasaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini ili kuongeza mchango wao katika Pato la Taifa; kuongeza kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya kisasa na ongezeko la uwekezaji katika uchimbaji mdogo; kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira, hususan, wakati wa mfumuko wa ugunduzi wa madini *(mineral rush);* kuhakikisha mazingira ya maeneo ya migodini yanatunzwa kwa usalama wa Wananchi; na kudhibiti biashara haramu ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia changamoto nyingine ni upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; uwepo wa watumishi wa kutosha wenye ujuzi unaohitajika kulingana na mahitaji; na kuporomoka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania

kunakosababisha kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa mafuta na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayopata fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maelezo ya utekelezaji, shughuli za umeme na gesi asili zilikua kwa asilimia 10.2 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2009. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya umeme nchini na ongezeko la matumizi ya gesi asili. Mchango wa sekta hizo katika Pato la Taifa kwa mwaka 2010 ulikuwa asilimia 2.1 (kwa bei za mwaka 2001), sawa na mchango wake kwa mwaka 2009 ambao nao ulikuwa ni asilimia 2.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme uliozalishwa kwenye Gridi ya Taifa uliongezeka hadi kufikia saa za gigawati *(GWh)* 5,189.32 mwaka 2010 ikilinganishwa na GWh 4,668.78 mwaka 2009. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme utokanao na gesi asili na mafuta mazito *(HFO).* Aidha, mahitaji ya juu *(Maximum Demand)* kwenye Gridi ya Taifa yalifikia MW 832.55 ilipofikia mwezi Novemba, 2010 ikilinganishwa na MW 755.41 Novemba, 2009, sawa na ongezeko la asilimia 10.21.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya umeme uliozalishwa nchini ulitokana na gesi asili na mafuta mazito. Hali hii ilitokana na upungufu mkubwa wa maji kwenye mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya kuzalisha umeme na hivyo kuleta upungufu wa umeme nchini. Ili kujihakikishia upatikanaji wa nishati ya umeme toshelevu na ya uhakika zaidi, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, iliendelea kujielekeza zaidi kuwekeza na kuendeleza vyanzo mbalimbali vya nishati ya umeme, hususan visivyotegemea maji. Lengo ikiwa ni kuiondoa nchi kutoka kwenye utegemezi wa umeme unaotokana na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za Serikali za kuachana na utegemezi wa umeme unaotokana na kiasi kikubwa na maji, zilianza kipindi cha kati ya mwaka 2005-2010, ambapo Serikali ilibuni Miradi minne iliyokusudiwa kuongeza kiasi cha MW 645 za umeme unaozalishwa kwenye Gridi ya Taifa. Miradi hiyo ilikuwa ni Kiwira (Mbeya), ambako unatokana na makaa ya mawe tulikuwa tunatarajia kuzalisha MW 200, na Mradi huo uliotarajiwa kukamilika mwaka 2009/2010; Mradi mwingine ulikuwa ni mradi wa Mnazi Bay Mtwara, ambao unategemea gesi ya asili tulikotarajiwa kuzalisha MW 300 na uliotarajiwa kukamilika mwaka 2010; mtambo wa kuzalisha umeme MW 100, kwa kutumia gesi ya asili ulionunuliwa na Serikali na kufungwa Ubungo, ulianza kazi mwaka 2008 ikiwa ni mmoja wa Miradi iliyobuniwa kipindi hicho. Mtambo wa kuzalisha umeme MW 45, kutokana na gesi asili ulionunuliwa na Serikali na kufungwa Tegeta – Dar es Salaam, ulianza kazi mwaka 2009, ikiwa ni sehemu ya Miradi minne iliyobuniwa mwaka 2005 hadi 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na dhamira hiyo njema ya Serikali, kati ya MW 645 zilizotarajiwa kuzalishwa kwa kipindi cha mwaka 2005-2010, ni MW 145 tu (Ubungo MW 100 na Tegeta MW 45) ndizo zilizopatikana baada ya Mradi wa Kiwira (MW 200) kukwama kukamilika ndani ya wakati kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo taratibu za ubinafsishaji wake. Aidha, Mradi wa Mnazi Bay Mtwara (MW 300)

ulichelewa kukamilika kama ilivyopangwa awali kutokana na mdororo wa kiuchumi ulioikumba dunia kwenye miaka ya 2007-2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na upungufu wa umeme nchini, Serikali ilichukua hatua mbalimbali ikiwemo kununua mafuta ya kuendeshea mitambo ya *IPTL.* Aidha, *TANESCO* iliingia mkataba wa mpito wa kuuziana umeme na Kampuni ya Symbion, ambayo inamiliki mitambo yenye uwezo wa kuzalisha MW 112.5 iliyopo Ubungo, Dar es Salaam. Kampuni hiyo tayari imeanza kuzalisha umeme na kuiuzia *TANESCO.* Vilevile, *TANESCO* ilisaini mkataba wa mwaka mmoja na Kampuni ya *Aggreko International* kwa ajili ya kufua MW 100 kuanzia mwezi Agosti, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Kufua Umeme Dar es Salaam MW 100 na Mwanza MW 60. Katika kuongeza na kuimarisha uwezo wa ufuaji umeme, *TANESCO* ilisaini mikataba na Kampuni za M/S *Jacobsen Electro AS* ya Norway kwa ajili ya ununuzi wa mtambo wa MW 100 wa kufua umeme kwa kutumia gesi asili utakaofungwa Ubungo, Dar es Salaam na *M/S SEMCO Maritime AS* na *Rolls Royce Marine AS* pia za Norway kwa ajili ya mtambo wa kufua umeme wa MW 60 kwa kutumia mafuta mazito utakaofungwa Nyakato, Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitambo ya kufua umeme MW 7.5 kwa kutumia gesi asili iliyopo Somanga Fungu ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, mwezi Agosti, 2010. Mitambo hiyo imeanza kufua umeme ambao umesambazwa katika Miji ya Somanga, Tingi, Nangurukuru, Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Bungu, Muhoro, Nyamwage, Kindwitwi, Kibiti, Utete, Tingi, maeneo ya Njia Nne na Hospitali ya Mchukwi kama nilivyoelezea hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi hii unaendelea ambapo Mradi wa MW 100 unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2011 na Mradi wa MW 60 unaofungwa Mwanza unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kufua Umeme Kinyerezi MW 240, ili kuendeleza Mradi huu, makubaliano yalifikiwa kati ya *TANESCO* na Kampuni ya *Sumitomo Corporation* ya Japani kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu, ambapo mkataba na mtaalamu/mhandisi mshauri ulisainiwa mwezi Septemba, 2010. Majadiliano kuhusu masuala ya kiufundi na kifedha kati ya Sumitomo na *TANESCO* yanaendelea. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kufua Umeme wa Mnazi Bay MW 300, majadiliano kati ya *TANESCO* na mjenzi wa Mradi huu yalikamilika na mkataba wa ujenzi ulisainiwa Oktoba, 2010 kati ya *TANESCO* kwa niaba ya Serikali na Kampuni ya *CMEC* ya China. Maandalizi ya umilikishwaji wa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kupozea umeme katika Mikoa ya Mtwara na Singida umefanyika na malipo ya utayarishaji wa mipango miji yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kufua Umeme wa Kiwira MW 200, kulingana na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme wa Mwaka 2009 -

2033, unatarajiwa kuanza kufua umeme wa MW 200 ifikapo mwaka 2013/14. Taratibu za kisheria za kuhamisha hisa za *Tan Power Resources Limited* katika Mgodi wa Kiwira kwenda Serikalini zipo katika hatua za mwisho. Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, imekubali kutoa mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya kuendeleza Mradi huo. Mawasiliano kati ya Serikali hizi mbili yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa kufua Umeme wa Ruhudji MW 358. Serikali ilikamilisha utaratibu wa kuajiri washauri katika maeneo ya fedha na ufundi wanaohitajika kuishauri Serikali kwenye majadiliano na maandalizi ya mikataba ya uendelezaji wa Mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadidu za rejea kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamii katika utekelezaji wa Mradi huu zimeridhiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC).* Tathmini inaendelea kufanyika ili kujua idadi ya vijiji vitakavyoathiriwa na ujenzi wa njia ya umeme, pamoja na kuangalia hali halisi ya mazingira. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Kufua Umeme ya Stiegler's Gorge MW 2,100; Mpanga MW 165; na Somanga Fungu MW 230. Serikali imeunda timu ya wataalamu itakayosimamia taratibu za kuendeleza Mradi wa Stiegler's Gorge. Aidha, wawekezaji kutoka China wameonesha nia ya kuendeleza Mradi huo kwa kutumia utaratibu wa Serikali kupata mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Kuhusu Mradi wa Mpanga wa MW 165, RUBADA kwa kushirikiana na mwekezaji kutoka China, wamesaini mkataba wa awali (MoU) na Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2015/2016. Aidha, mwekezaji binafsi *(IPP)*, amesaini Mkataba wa awali na Serikali kupitia *TANESCO* kutekeleza Mradi wa Somanga Fungu wa MW 230 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kufua Umeme wa Makaa ya Mawe Ngaka wa MW 400 na Mchuchuma wa MW 600. Kampuni ya Tancoal inakamilisha taratibu za kutekeleza mradi wa Ngaka wa MW 400, ambao Serikali kupitia *NDC* inamiliki asilimia 30. Aidha, *NDC* imefikia makubaliano ya kuingia ubia na Kampuni ya *Sichuan Hongda Corporation Ltd (SHC)* ya China ili kufua umeme wa MW 600 kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma. Katika ubia huo, Serikali kupitia Shirika la *NDC* itamiliki asilimia 20 ya hisa na mwekezaji atamiliki asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi iliyo chini ya Ufadhili wa *MCC*, utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia maji ya Mto Malagarasi ulisitishwa kutokana na sababu za kimazingira. Upembuzi yakinifu na tathmini ya awali ya mazingira vilivyofanywa upya, vimewezesha kubuniwa Mradi mbadala, yaani *Igamba stage III,* unaoweza kuzalisha hadi MW 41 za umeme. Uandaaji wa ramani ya eneo la Mradi mpya umekamilika na TANESCO imelipa fidia kwa njia za umeme zilizothaminiwa. Pia, *TANESCO* kupitia Halmashauri za Wilaya ya Kigoma na Kasulu imeendelea kuwalipa walioathiriwa na Mradi huu na ambao tathmini ya mali imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ulipaji fidia ya mali zitakazoathiriwa na Mradi wa Kuimarisha na Kupanua Usambazaji Umeme katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Dodoma, Morogoro, Iringa na Mbeya inaendelea. Kazi ya usafishaji na upimaji wa njia za umeme katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro na Mwanza inaendelea. Usanifu wa uwekaji wa mkongo wa umeme baharini *(submarine cable)* kutoka Dar es Salaam hadi Unguja ulikamilika. Mkandarasi wa usanifu na ujenzi wa njia ya juu ya ardhi (*Over Head Line - OHL)* ya umeme wa msongo wa kV 132 kutoka Ubungo hadi Ras Kilomoni kupitia Tegeta (Dar es Salaam) na Ras Fumba hadi Mtoni kwa upande wa Zanzibar amesaini mkataba wa kuanza kazi mwezi Aprili, 2011. Kazi ya ujenzi wa vituo vya kupoza umeme inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma yake ya kupeleka Umeme Makao Makuu ya Wilaya na Vijijini, Serikali imekamilisha upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Kishapu, Rorya na Longido na ufungaji wa jenereta katika Miji ya Kasulu na Kibondo. Upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Ngorongoro, Namtumbo na Nkasi uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyo kandokando ya bomba la gesi *(wayleave villages)* la Songo Songo Wilayani Rufiji ikijumuisha Bungu, Somanga, Muhoro, Nyamwage, Nangurukuru, Kindwitwi, Kibiti, Utete, Tingi, maeneo ya Njia Nne na Hospitali ya Mchukwi yamepatiwa umeme. Pia, Mradi ulihusisha ujenzi wa njia ya umeme wa Gridi ya Taifa katika vijiji vitano; viwili Wilayani Temeke (Chamazi na Mbande); na vitatu Wilayani Mkuranga (Mwanambaya, Dundani na Kimbangulile/Mipeko); na ujenzi wa mfumo wa umeme katika Kisiwa cha Songo Songo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia, imewezesha upelekaji wa umeme katika Vijiji vya Mbwewa, Galagaza na Miswe (Kibaha), Buganguzi na Buganda (Muleba), Nyamahana (Iringa Vijijini), Wareta, Dirma na Simbay (Hanang), Zuzu (Dodoma Vijijini), Seela, Ilikisongo, Mlangarini-Manyire, Sambasha, Ilikiding’a na Timbolo (Arumeru), Songwa na Kizumbi (Shinyanga Vijijini), Ifwagi (Mufindi), Bukangilija na Ng’hami (Maswa), Busiya na Kisiba (Rungwe), Kwale (Mkinga).

Miradi mingine ni pamoja na kupeleka umeme katika zahanati na Kituo cha Watoto Walemavu cha Amani (Mvomero), Zahanati ya Malindi (Lushoto), Shule ya Sekondari ya Dkt. Asha Rose Migiro (Mwanga) na Shule ya Msingi ya Mother Kevin (Same). Ruzuku kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo manne ya kibiashara ya Kilulu, Igaganulwa na Nkololo (Bariadi) na kwenye pampu ya maji Wilayani Sengerema ilitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini katika Mikoa 16 ya Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Rukwa na Tabora ulianza. Miradi hii iliyopata ruzuku ya shilingi bilioni 100.75 kutoka Mfuko wa Nishati Vijijini inahusisha ujenzi wa njia za umeme za msongo wa kV 33 pamoja na kV 11 zenye jumla ya takriban kilomita 1,600; ufungaji wa transfoma 350 za

ukubwa tofauti; na ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kV 0.4 zenye jumla ya kilomita 900 na uunganishwaji wa wateja wa awali 20,000. Mradi huu unatekelezwa na wakandarasi wa ndani na nje ya nchi kwa utaratibu wa *Turnkey* chini ya usimamizi wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Nishati Vijijini uliwezesha ujenzi wa mtambo wa majaribio wa kufua umeme kutokana na maporomoko madogo ya maji katika eneo la Matombo Mkoani Morogoro; ufungaji wa zaidi ya mitambo 130 ya kuzalisha umeme kutokana na nguvu za jua *(solar systems)* katika shule za sekondari, zahanati, vituo vya afya na vituo vidogo vya polisi katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Singida na Pwani; upembuzi yakinifu wa vyanzo 12 vya maporomoko madogo ya maji katika Wilaya za Muheza na Lushoto Mkoani Tanga; usambazaji wa taa 1,200 zinazotumia nguvu ya jua Mkoani Mara; na kutoa mafunzo ya kujenga matanuri sanifu ya kukaushia tumbaku kwa wakulima Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi wa *Lighting Rural Tanzania* unaohamasisha matumizi ya nishati yenye mwanga bora ili kupunguza au kuondokana na matumizi ya taa za chemli, vibatari na mishumaa vijijini ulianza. Mradi huo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni moja unatekelezwa na waendelezaji kumi walioshinda kwenye shindano la *Lighting Rural Tanzania 2010* katika Mikoa ya Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Iringa, Manyara, Kagera, Mara, Shinyanga na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Nishati Vijijini uliendelea kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Usambazaji Umeme wa Gridi Vijijini, inayotekelezwa na *TANESCO* na wakandarasi binafsi. Katika mwaka 2010/2011, uwekezaji kwenye uzalishaji wa umeme kupitia mfumo maalumu wa kushirikisha wazalishaji wadogo, kwa miradi isiyozidi MW kumi umeongezeka. Hadi sasa mikataba mitano imesainiwa kati ya *TANESC*O na wazalishaji wadogo wafuatao: *TANWAT (MW 2.7); TPC (MW 20); Sao Hill (MW 16); Ngombeni (MW 0.5)* na *Mwenga (MW 3.36).* Mwaka 2010, Kampuni za *TPC* na *TANWAT* zilianza kuuza umeme kwa *TANESCO* chini ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa kwa gharama za kuunganisha umeme ni pamoja na zifuatazo; Wateja kupata mikopo ya Benki ya Akiba Commercial ili kupunguza gharama kubwa ya kuunganisha kwa mara moja na haya ni makubaliano yaliyoingiwa kati ya Shirika la *TANESCO* pamoja na Benki hii, wateja kulipa kwa kiasi kidogo kidogo, yaani *installments*, kwa kipindi hadi kufikia miaka miwili ili kuwawezesha wateja wengi zaidi waweze kumudu gharama za kuunganishiwa umeme.

*REA* na *TANESCO* wanatathmini matumizi ya teknolojia ya bei nafuu, yaani *low cost design* katika kupunguza gharama za kuunganisha wateja na uwepo wa Miradi ya *SIDO* na *REA,* ambayo wateja wanalipia *VAT* peke yake, ambayo ni kodi ya ongezeko la thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilisaini mikataba na Washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Dunia *(WB),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* Shirika la Maendeleo la Japani *(JICA),* Taasisi ya Fedha ya Korea Kusini *(ECDF)* na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB),* kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Njia Kuu ya Usafirishaji Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Iringa kupitia Dodoma, Singida hadi Shinyanga yenye urefu wa kilomita 650. Mtaalamu Mshauri amekamilisha upembuzi yakinifu wa kuvipatia umeme vijiji vitakavyopitiwa na njia mpya ya umeme. Shirika la Maendeleo la Swideni *(SIDA)* na Shirika la Maendeleo la Norway *(NORAD),* yameonesha nia ya kufadhili Mradi huo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/14.

Taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro zinaendelea. Tathmini ya athari za mazingira na mali zitakazoathirika wakati wa utekelezaji wa Mradi na usanifu wa njia ya umeme vimekamilika katika Mkoa wa Kilimanjaro, ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa eneo la kujenga Kituo Makuyuni. Taratibu za zabuni za ununuzi wa *distribution component* zinaendelea. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Usafirishaji Umeme ya Msongo wa kV 220 kutoka Bulyanhulu kupitia Geita hadi Nyakanazi, umegawanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza, inahusisha ujenzi wa km 80 za njia ya msongo wa kV 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita, ambapo mkataba wa mkopo kwa ajili ya ujenzi wa mradi ulisainiwa mwezi Januari, 2011. Makubaliano ya mkopo yalifikiwa kati ya Serikali na *BADEA* na *OFID* ya Sudan katika utekelezaji wa Mradi kuanzia Bulyanhulu hadi Geita, ambapo *BADEA* na *OFID* watatoa mkopo wa US$ milioni 20 na Serikali itachangia US$ milioni tatu.

Awamu ya pili itahusisha ujenzi wa km 130 za njia ya msongo wa kV 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi kwa gharama ya US$ milioni 30. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014. Aidha, Serikali ya China imeonesha nia ya kufadhili Mradi wa Njia ya Umeme kV 220 *(North- west grid extension)* kutoka Nyakanazi-Kigoma-Rukwa hadi Mbeya. Rasimu ya mkataba wa mkopo imewasilishwa Serikalini kwa ajili ya mapitio na taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Makambako - Songea kV 132: Serikali ilisaini mkataba wa mkopo na Serikali ya Swideni mwezi Agosti, 2010 kwa ajili ya Ujenzi wa Njia ya Umeme ya kV 132 yenye urefu wa km 250 kutoka Makambako hadi Songea na vituo vya kupozea umeme Madaba na Songea. Sambamba na ujenzi wa njia hiyo, upanuzi wa njia za usambazaji umeme umbali wa km 900 utafanyika katika Miji/Wilaya za Songea, Namtumbo, Mbinga, Makambako, Njombe na Ludewa. Maandalizi ya umilikishwaji wa maeneo ya ujenzi wa vituo vya kupozea umeme vya Madaba na Songea pamoja na kulipa gharama za uthamini kwenye Halmashauri husika yanaendelea. Mshauri Mwelekezi (*Consultant*) wa kusimamia ujenzi wa mradi alipatikana mwezi Juni, 2011 na ataanza kazi mwezi Agosti, 2011. Mradi utakamilika

mwaka 2014/2015. Kazi atakazozifanya mwaka huu ni kutayarisha zabuni za kuwapata wakandarasi watakaojenga Mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuunganisha Gridi ya Taifa na za nchi jirani: Serikali iliendelea na juhudi za kuunganisha Gridi ya Taifa na Gridi za umeme za Zambia na Kenya. Serikali ilipata msaada wa fedha kutoka Serikali ya Norway za kufanya upembuzi yakinifu sehemu ya Mradi ambayo ni kuunganisha Gridi za Tanzania na Kenya kutokea Singida kwenda Arusha hadi Nairobi. Mshauri mwelekezi anaendelea na upembuzi yakinifu, ambao unatarajiwa kukamilika Februari, 2012. Aidha, kwa upande wa Zambia (Pensulo-Kasama), mtaalamu mshauri kwa ajili ya kufanya tathmini ya mazingira ameajiriwa na anaendelea na kazi hiyo. Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi zimepatikana na utaanza kutekelezwa baada ya tathmini ya mazingira kukamilika mwezi Septemba, 2012. Sehemu ya Mradi kutoka Kasama hadi Mbeya bado haijapata ufadhili kwa ajili ya kuiendeleza. Matarajio ni kuwa sehemu hii itaendelezwa baada ya ufadhili wa Mradi mzima wa Zambia-Tanzania-Kenya (ZTK) kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mshauri mwelekezi wa kutekeleza Mradi wa *Electricity V* alipatikana mwezi Aprili, 2011 na kusaini mkataba wa ushauri na usimamizi wa mradi. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Usambazaji wa Umeme, utawezesha usambazaji wa umeme katika Vijiji, Miji Midogo na Makao Makuu ya Wilaya katika Mikoa ya Arusha, Geita (Bukombe), Mwanza (Magu na Kwimba) na Shinyanga (Bariadi). Taratibu za malipo ya awali zinaendelea. Mradi huu unagharimiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Serikali ya Japani kupitia Shirika lake la Maendeleo *(JICA)*, ilifadhili Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Usambazaji Umeme katika maeneo ya Masaki, Mikocheni na Oysterbay. Kazi iliyokuwa imebaki ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme ilikamilika Septemba, 2010. Aidha, Serikali ya Japani imefadhili ujenzi wa Chuo cha *TANESCO*, kitakachotoa mafunzo ya usafirishaji na usambazaji umeme. Chuo hicho kipo eneo la Masaki, Dar es Salaam.

Kampuni ya Ophir kwa kushirikiana na Kampuni ya *British Gas (BG)*, ilichimba visima vitatu katika eneo la bahari la kina kirefu kwenye Kitalu Na. 4 (Pweza – 1 na Chewa – l) na Kitalu Na.1(Chaza – 1) na ilithibitishwa visima hivi vina gesi asili. Aidha, vielelezo vya kijiofizikia na kijiolojia viliendelea kukusanywa kwa ajili ya kuwasilisha Umoja wa Mataifa katika utetezi wa ombi la Tanzania la kuongezewa eneo la ukanda wa bahari unaozidi maili 200 (*extension of Tanzania's exclusive economic zone).* Katika kuhakikisha utekelezaji wa mipango ya usambazaji gesi asili katika Jiji la Dar es Salaam unatekelezwa, michoro ya bomba la kusafirisha gesi asili kutoka Ubungo hadi Mikocheni katika eneo la viwanda ilikamilika. Aidha, *TPDC* kwa kushirikiana na Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania*, iliendelea kutekeleza mradi hamasishi wa kuzalisha na kusambaza gesi asili iliyoshindiliwa *(Compressed Natural Gas).* Hadi kufikia Mei, 2011 magari 25 yaliyokuwa yanatumia petroli yalibadilishwa mifumo yake na kuanza kutumia gesi asili na viwanda na taasisi 37 zilikuwa zinatumia gesi asili ikilinganishwa na 33 katika kipindi cha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa gesi asili ili kukidhi mahitaji iliendelea kufanyiwa tathmini. Aidha, *TPDC* ilikamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha gesi asili kwa njia ya bomba kutoka Mnazi Bay (Mtwara) na Songo Songo (Kilwa) kwenda Dar es Salaam. Upembuzi yakinifu ulibainisha kuwa ujenzi wa bomba hilo una manufaa kiuchumi. Makubaliano ya awali ya ujenzi wa bomba la gesi asili yalisainiwa Juni, 2011 kati ya Serikali na Kampuni ya China *Petroleum Technology and Development Corporation.* Miradi ya Gesi Asili ya Songo Songo na Mnazi Bay, michoro na zabuni za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mtambo wa kusafisha gesi ya Songo Songo unaotekelezwa na Kampuni ya Songas imekamilika. Ujenzi wa mtambo huo na uongezaji wa uwezo wa usafirishaji wa gesi kwenye bomba hilo kwa njia ya *compression* unafuatia kuongezeka kwa mahitaji ya gesi asili katika uzalishaji wa umeme na matumizi ya viwandani. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Artumas iliyouza hisa zake kwa Kampuni ya Wentworth ya Kanada, iliendelea kuzalisha umeme kwa maeneo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara, ambapo mitambo iliyofungwa ina uwezo wa kufua umeme wa jumla ya MW 18 wakati mahitaji ya juu ya umeme kwa sasa ni MW 12. Hadi kufikia mwezi Mei, 2011, Serikali ilikuwa imetoa jumla ya Shilingi bilioni 18.7, ikiwa ni sehemu ya mfuko wa kufidia bei za umeme *(National Tariff Equalization Facility - NTEF)* kwa sehemu hiyo. Ujenzi wa njia ya umeme Mtwara, Lindi, Masasi, kazi za ujenzi wa Gridi Ndogo inayounganisha Miji ya Mtwara, Lindi na Masasi, kupitia Nyangao na Ndanda *(Northern feeder)* na ujenzi wa njia ya umeme ya kuunganisha Mtwara na Tandahimba, pamoja na Newala na Masasi *(Southern feeder)*, zilikamilika na tayari maeneo husika yanapata umeme unaozalishwa na gesi asili ya Mnazi Bay. Kazi ya ujenzi wa njia ya umeme inayounganisha Mtwara na Msimbati (kV 33) ilikamilika na taratibu zinafanyika kwa ajili ya kusambaza umeme kwa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kuendeleza matumizi ya umeme wa jua unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden kwa kushirikiana na Tanzania, uliendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Singida na Manyara, ambapo mafunzo juu ya matengenezo ya mifumo ya umeme wa jua pamoja na uboreshaji wa biashara ya kuagiza mifumo ya umeme wa jua iliyo bora na yenye viwango vinavyokubalika, yalitolewa kwa mafundi mchundo na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya mafundi mchundo 30 na wafanyabiashara wa mifumo ya umeme wa jua 30 walipata mafunzo. Vilevile, zaidi ya walimu 52 kutoka Vyuo vya *VETA* walipatiwa mafunzo kufuatia kuanzishwa kwa mtaala mpya wa mafunzo ya umeme wa jua katika Vyuo vya *VETA* nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuendeleza matumizi ya umeme wa jua, Serikali iliendelea kutekeleza mradi wa kuondoa vikwazo vya ukuzaji wa soko la umeme wa jua, katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP/GEF).* Mradi huu umewezesha kufungwa mifumo ya umeme wa jua ya maonesho *(pilot project)* katika Shule za

Sekondari 12 na Vituo vya Afya 77 kwa nia ya kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya kuingiza miradi ya umeme wa jua kwenye bajeti za maendeleo.

Jumla ya mafundi 200 na wafanyabiashara wa umeme wa jua 120 wamepata mafunzo ya ufundi na biashara na wanatoa huduma za umeme wa jua katika Mikoa iliyotajwa. Pia, zaidi ya walimu 17 wa Vyuo vya *VETA* katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa wamepatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakadiriwa kuwa Tanzania imepunguza uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na hewa ya ukaa *(carbon monoxide)* itokanayo na matumizi ya bidhaa za petroli kwa ajili ya kuzalisha umeme na kutoa mwanga kwa kiasi cha takriban tani 4,088 baada ya kutumia nishati jadidifu, hususan, umeme wa jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa Julai na Agosti, 2010 utafiti wa kijiokemia na kijiofizikia ulifanyika katika Ziwa Ngozi eneo la Songwe Mkoani Mbeya kwa ushirikiano kati ya Wizara, *GST, TANESCO* na Taasisi ya Utafiti ya Ujerumani *(BGR).* Lengo la utafiti huo ni kubainisha mahali pa kuchoronga visima kwa ajili ya utafiti zaidi wa jotoardhi kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Power Pool East Africa Limited* imekamilisha upembuzi yakinifu na tathmini ya kimazingira kwa ajili ya kuzalisha umeme kutokana na upepo Mkoani Singida. Kampuni hiyo imeingia ubia na Shirika la Maendeleo la Taifa *(National Development Corporation – NDC)* katika kutekeleza mradi huo. Kampuni nyingine ni *Wind East Africa Ltd* ambayo wabia wake ni *Six Telecom* kutoka Tanzania, *Ken-Tec* ya *Denmark* na *Aldwych* ya Uingereza ilifunga *wind mast* Singida ili kupata takwimu za upepo zinazohitajika.

Mwezi Juni, 2011 Benki ya Dunia iliridhia Mkakati wa uendelezaji wa Mradi huo kama hatua za mwanzo za kutoa mkopo. Kwa kuanzia, kampuni hizo mbili kila moja itajenga mitambo yenye uwezo wa kuzalisha MW 50 na kuunganisha kwenye gridi ya Taifa pale Singida ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013 na tunaomba ikiwa zaidi ya hapo tutafurahi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Sino Tan Renewable Energy Limited* ilifanya upembuzi yakinifu pamoja na tathmini ya mazingira kwa ajili ya mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo *MW 100* katika eneo la Makambako Mkoani Iringa. Kampuni iko katika hatua ya kukamilisha majadiliano ya kuuziana umeme na *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa mafunzo ya uelewa wa masuala ya biyofueli kwa wadau mbalimbali yamefanyika katika mikoa ya Arusha, Lindi, Manyara na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa biogesi ulipewa umuhimu kama chanzo muafaka cha nishati ya kupikia. Jitihada zilielekezwa zaidi katika kuendeleza matumizi ya nishati hiyo katika taasisi kama mashule, Kambi za jeshi na Magereza

ambazo kiasi kikubwa cha kuni hutumika kupikia. Uzinduzi rasmi wa programu ya kuhamasisha matumizi ya biogesi nchini ulifanyika mwezi Machi, 2011. Serikali kupitia *CAMARTEC* iliendelea na programu hiyo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutekeleza mipango mbalimbali ili kupunguza matumizi ya nishati na kutumia fursa zilizopo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa *(UNDP)* kupitia *UN Joint Programme on Environment* ilifanikisha ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau katika utambuzi wa vifaa vinavyotumia umeme kwa wingi ili kuwezesha kuandaa viwango. Takwimu za vifaa hivyo zilikusanywa kutoka majengo ya biashara na taasisi mbalimbali ili kupata mwelekeo wa ubora wa matumizi ya nishati wa vifaa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mpango huu, ziara ya mafunzo ilifanyika nchini Kanada kwa wataalamu wa Wizara wakiwamo wataalamu kutoka taasisi za *EWURA, REA, TBS,* na *TANESCO* ili kupata uzoefu wa kuandaa na kusimamia mikakati mbalimbali ya matumizi bora ya nishati na vifaa vya umeme. Maandalizi ya sheria, kanuni pamoja na viwango vya ubora wa nishati *(energy efficiency standards)* kwa vifaa vya umeme vitakavyotengenezwa na kuingizwa nchini yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa matumizi bora ya tungamotaka *(Programme for Biomass Energy Conservation – ProBEC)* ulitoa mafunzo kwa wadau mbalimbali katika tasnia ya utengenezaji majiko bora ya kupikia na mabani ya kukaushia tumbaku. Mpango huo wa miaka mitano uliofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani, ulikwisha muda wake mwezi Desemba, 2010. Ili kusimamia kikamilifu uendelezaji endelevu wa matumizi ya tungamotaka, shughuli za programu hiyo zilikabidhiwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Septemba, 2010 *EWURA* ilianza kuweka vinasaba *(fuel marking)* katika mafuta ya taa, dizeli na petroli. Utaratibu huu uliiwezesha *EWURA* kugundua kwa urahisi mafuta yaliyochanganywa *(adulterated)* au mafuta ya magendo ambayo hayakulipiwa ushuru. Kwa sasa *EWURA* inatumia maabara zinazohamishika *(mobile laboratories)* zenye teknolojia ya kisasa inayotumika kuchukua sampuli na kupima ubora na kutoa majibu papo kwa hapo. Jumla ya vituo 235 vilikaguliwa katika Mikoa 18, kati ya hivyo, vituo 54 sawa na asilimia 23 vilikutwa na makosa ya ama uchakachuaji au kuuza mafuta yasiyolipiwa ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya vinasaba ni pamoja na kuzuia uchanganyaji wa mafuta ya taa na dizeli (kuchakachua); kuzuia bidhaa za mafuta kwa ajili ya nchi jirani yasitumike nchini *(fuel dumping)* au kuingizwa kimagendo nchini; na kupata takwimu sahihi za mafuta ya petroli, dizeli na ya taa yanayotumika nchini.

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2010 hadi mwezi Aprili, 2011 Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ilitoza zaidi ya Shilingi milioni 300 ikiwa ni adhabu kwenye bidhaa za mafuta zilizobainika kutumika nchini pasipo kulipiwa kodi. Mbali na kiasi hiki, kutokana na ongezeko la ubora wa takwimu za matumizi halisi ya mafuta ya

petroli, dizeli na taa nchini, *TRA* ilikusanya kodi zaidi ya Shilingi bilioni tano kwa mwezi kwenye mafuta ya petroli na Shilingi bilioni tisa kwa mwezi kwenye mafuta ya dizeli. Takwimu zilionyesha kushuka kwa matumizi ya mafuta ya taa nchini kwa asilimia 37 kwa mwezi, ambapo matumizi ya mafuta ya petroli yaliongezeka kwa asilimia 27 kwa mwezi na mafuta ya dizeli kuongezeka kwa asilimia 26 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EWURA* kwa kushirikiana na Shirika la Viwango, Tanzania *(TBS)* iliweka viwango vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta, hususan, maghala ya kuhifadhi mafuta, Vituo vya Mafuta na magari ya kusafirisha mafuta. Mamlaka hufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kutoa miongozo kwa wamiliki ili waweze kuboresha miundombinu yenye kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Mamlaka pia inatoa vibali vya ujenzi na kufuatilia kama ujenzi unafanyika kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha utekelezaji wa Mfumo wa Uagizaji Mafuta wa Pamoja *(bulk procurement),* Serikali ilikamilisha kanuni za kusimamia mfumo huo. Kanuni hizo zilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali, tangazo Na. 164 la tarehe 03 Juni, 2011 na kuanza kutumika. Kwa sasa *EWURA* inakamilisha taratibu za uagizaji wa mafuta wa pamoja ambao utaanza mwezi Desemba, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za mafuta ziliendelea kupanda hapa nchini kutokana na kupanda kwa bei hizo katika soko la dunia, kupanda kwa bima za meli zinazosafirisha mafuta hayo kutoka sokoni na kuingiza nchini na kutokana na matukio mbalimbali ya uhalifu yanayofanywa na maharamia wa Kisomali katika Bahari ya Hindi. Kupanda kwa bei hizo pia kulichangiwa na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha ukuaji wa shughuli za madini na uchimbaji mawe mwaka 2010 kilikuwa asilimia 2.7 ikilinganishwa na asilimia 1.2 mwaka 2009 (kwa bei za mwaka 2001). Mchango wa shughuli za kiuchumi za madini katika Pato la Taifa kwa mwaka 2010 ulikuwa asilimia 2.4 ikilinganishwa na asilimia 2.5 mwaka 2009 (kwa bei za mwaka 2001).

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,103.4 mwaka 2009 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,508.7 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 36.7. Asilimia 93 ya mauzo ya madini yote nje ya nchi ilichangiwa na mauzo ya dhahabu, ambayo yalifikia dola za Marekani milioni 1,436.2 mwaka 2010, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,076.1 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 33.5. Ongezeko hilo kwa kiwango kikubwa lilichangiwa na kuongezeka kwa bei ya dhahabu kutoka wastani wa dola za Marekani 1,039.46 kwa wakia mwaka 2009 hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 1,224.53 kwa wakia mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 17.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 kwa lugha ya Kiswahili ilikamilika. Aidha, kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Madini ya Mwaka

2010 na kukamilika kwa Kanuni zake, Sheria hiyo ilianza kutumika rasmi Novemba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliainisha maeneo mapya ya uchimbaji mdogo katika maeneo ya Mpambao na Maruga (Iramba) na Mwau (Singida Vijijini). Taratibu za kisheria za kukamilisha utengaji na ugawaji wa maeneo hayo kwa wachimbaji wadogo zinaendelea. Aidha, Shilingi bilioni 1.2 zilitengwa kwa ajili ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011 jumla ya shilingi milioni 525 zilitolewa. Fedha hizi zilielekezwa katika kusaidia miradi ya uchimbaji, uchenjuaji, uongezaji thamani na utengenezaji wa zana na nyenzo za uchimbaji mdogo wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongozo ya kusaidia wachimbaji wadogo iliandaliwa katika nyanja za teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini, usalama na afya, utambuzi wa madini ya vito, utunzaji wa mazingira, matumizi sahihi na salama ya baruti katika machimbo yao na ujasiriamali katika masuala ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutoa leseni, vibali na vyeti vinavyosimamia shughuli za uingizaji nchini, usafirishaji, hifadhi na matumizi ya baruti. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mzinga, iliendesha mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya baruti *(Safe Handling, Storage and Use of Explosives)* kwa wachimbaji wadogo 36 wa madini. Pia, mafunzo ya usalama migodini na utunzaji wa mazingira yaliendeshwa kikanda katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji mdogo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za utumiaji baruti katika migodi mikubwa, ya kati na midogo zilikaguliwa kupitia Ofisi za Madini za Kanda na za Afisa Madini Mkazi na taarifa ziliandaliwa, kufanyiwa tathmini na kuhifadhiwa katika kanzidata. Taarifa hizo ziliwezesha kujua kwa usahihi kiasi cha baruti kilichoingia na kilichotengenezwa nchini na kiasi kilichotumika na maeneo husika. Takwimu hizi ni muhimu katika udhibiti wa matumizi ya baruti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la pili kwenye kanuni za baruti za mwaka 1964 linalohusu tozo, lilifanyiwa marekebisho ili kuimarisha na kuboresha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na leseni, vibali na vyeti mbalimbali vya baruti. Lengo la marekebisho hayo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa leseni, vibali na vyeti vyote vya baruti vinalipiwa, tofauti na awali ambapo ni baadhi tu vilikuwa vinalipiwa. Tozo mpya zilianza kutumika rasmi mwezi Septemba, 2010 na zimechangia kiwango cha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kwa takriban Shilingi milioni 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa migodi mikubwa na ya kati ulifanyika katika migodi ya Bulyanhulu, Geita, North Mara, Williamson Diamond, Golden Pride, Buzwagi, Tulawaka na TanzaniteOne ili kuhakikisha shughuli za uchimbaji zinaendeshwa kwa kuzingatia kanuni za usalama, afya na utunzaji wa mazingira. Aidha, migodi ya wachimbaji wadogo sehemu mbalimbali za nchi yetu pia ilikaguliwa ili kuhakikisha wachimbaji hao wanazingatia usalama, afya na mazingira katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliwataka wamiliki wa migodi mikubwa kuwasilisha maboresho ya taarifa za ufungaji migodi *(Mine Closure Plans)* ili ziweze kuhakikiwa na kupitishwa rasmi kwa mujibu wa kanuni za usalama, afya na utunzaji wa mazingira. Hatua hiyo inalenga kutekeleza Sheria Mpya ya Madini ya Mwaka 2010, inayowataka wawekezaji kuweka dhamana ya fedha za kukarabati mazingira *(rehabilitation bond),* na gharama halisi ya ukarabati huo hujulikana kupitia taarifa ya ufungaji mgodi husika.

Upitiaji wa rasimu ya mpango wa ufungaji mgodi wa Golden Pride ulikamilika na kuidhinishwa rasmi kwa mujibu wa sheria. Mgodi huo unatarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwaka 2012 ikiwa hakutagundulika mashapo ya ziada. Gharama za ukarabati wa mazingira hadi kufikia tamati ya ufungwaji ni dola za Kimareiani milioni 9.56.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni za sheria kwa ajili ya kusimamia shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, utunzaji, usafirishaji na biashara ya madini ya urani zilikamilika na kuanza kutumika. Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Nguvu za Atomiki Nchini na Tume ya Nguvu za Atomiki Duniani imeanza kujenga uwezo wa watumishi wake kwa kuwapeleka kwenye mafunzo ya muda mfupi kuhusu usimamizi wa shughuli za madini hayo na taaluma ya mionzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu wa mradi wa utafutaji wa Urani katika mto Mkuju ulikamilika na kubainisha kuwepo kwa tani milioni 65.5 za mashapo ya urani yanayoweza kuchimbwa kwa faida. Tathmini ya athari ya mazingira *(Environmental Impact Assessment – EIA)* inaendelea kabla ya kupatiwa leseni ya uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano ya uendeshaji wa mgodi wa Mwadui kati ya Serikali na kampuni ya *Petra Diamonds Limited* yalikamilika, ambapo masuala ya msingi katika mkataba wa ubia kwenye mgodi huo yalifikiwa. Masuala hayo ni utaratibu wa upatikanaji wa mtaji wa kufufua mgodi, utaratibu wa kutambua na kulipa deni la nyuma la *Williamson Diamonds Limited (WDL)*, utaratibu wa mgawo wa mapato kwa wanahisa kwa kuzingatia ulipaji wa deni, ukomo wa juu wa gharama za mauzo ya almasi na shughuli za *TANSORT* katika mazingira mapya ya soko la almasi za *WDL*. Taratibu zinaandaliwa ili Mkataba huo uweze kusainiwa. Kwa sasa mgodi huo unaendeshwa kwa mujibu wa mkataba wa ubia wa mwaka 1994.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kukamilisha mchanganuo wa namna ya kuboresha uendeshaji wa kituo cha uchongaji mawe na vito kilichopo Arusha *(Arusha Gemstone Carving Centre)* kupitia mradi wa usimamizi endelevu wa raslimali ya madini unaogharimiwa na Serikali ya Tanzania na mkopo wa Benki ya Dunia. Lengo ni kukiwezesha kituo hicho kutoa mafunzo mbalimbali ikiwemo ya uongezaji thamani madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia madini ya *tanzanite* kutangazwa kuwa madini ya vito maalumu *(special stones),* Serikali kupitia Tamko lake (GN) Na. 146 la

mwezi Aprili, 2010 iliamuru kusitishwa kwa usafirishaji nje wa *tanzanite* ghafi yenye uzito kuanzia gramu moja na zaidi, kwa lengo la kuhamasisha uongezaji thamani madini hayo. Utekelezaji wa amri hiyo umeleta changamoto kubwa ikiwemo kuongezeka kwa utoroshwaji wa madini hayo kwenda nchi jirani na pia wafanyabiashara wengi kuhifadhi madini yao kwa muda mrefu kutokana na kutokuwa na uwezo wa kuyasanifu. Changamoto hizi ziliikosesha Serikali mapato na hivyo, kuilazimu kuanzisha tena majadiliano na wadau ili kuona namna bora ya kutekeleza amri hiyo bila kuathiri soko na kuongeza udhibiti wa utoroshwaji wa madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, mojawapo ya hatua ambazo Serikali imechukua ni kuanzisha utaratibu wa kuwa na cheti maalumu *(Certificate of Origin)* kwa kila mfanyabiashara au mchimbaji atakayehitaji kusafirisha madini ya *tanzanite* nje ya nchi. Serikali inaendelea kuwasiliana na nchi ambazo ni wanunuzi wakubwa duniani wa madini hayo ili wasikubali madini haya yaingizwe kwenye nchi zao bila kuwa na cheti hicho kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuhamishiwa nchini kitengo cha *TANSORT* kilichokuwa London – Uingereza, kumewezesha kuongeza wigo wa shughuli za uchambuzi wa almasi zinazozalishwa hapa nchini badala ya almasi inayozalishwa na *WDL* pekee, hivyo, kuliwezesha Taifa kupata taarifa na mapato sahihi kutokana na madini ya almasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanza kutumika kwa Sheria Mpya ya Madini ya mwaka 2010, utoaji wa leseni za madini nchini umeboreshwa ambapo baadhi ya leseni hizo zilianza kutolewa na Maafisa Madini wa Kanda. Leseni hizo ni pamoja na za uchimbaji mdogo na biashara ya madini. Hatua hii itawezesha utoaji wa leseni za uchimbaji mdogo kuwa wa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, jumla ya maombi 5,921 yalipokelewa na kuingizwa kwenye mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni. Kati ya hayo, maombi 4,171 yalikuwa kwa ajili ya leseni za uchimbaji mdogo wa madini *(Primary Mining Licence - PML),* maombi 60 ya uchimbaji mkubwa na wa kati *(Mining Licenses – ML)* na maombi 1,690 kwa ajili ya utafutaji mkubwa wa madini *(Prospecting Licences - PLR na PL).* Jumla ya leseni 2,508 zilitolewa, ambapo kati ya hizo leseni 1,982 ni za uchimbaji mdogo, leseni 12 za uchimbaji wa madini wa kati na mkubwa na leseni 514 za utafutaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati Tekelezi ya *TEITI (Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative)* ilikamilisha ripoti ya kwanza ya ulinganisho wa malipo yaliyofanywa na kampuni za uchimbaji madini na gesi asili na mapato yaliyopokelewa Serikalini kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Ripoti hiyo ilitolewa kwa umma mwezi Februari, 2011. Tathmini ya utekelezaji wa vigezo vya uwazi *(EITI Validation),* ilikamilika na kuwasilishwa kwenye Bodi ya Kimataifa ya *EITI* iliyopo Oslo, Norway kwa ajili ya kutolewa uamuzi juu ya uanachama kamili wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya kwanza ya ulinganisho wa malipo yanayotolewa na uchimbaji wa madini na gesi asili kwa Serikali na mapato yaliyopokelewa Serikalini kwa hesabu za mwaka 2008/2009, ilionyesha kuwa kuna tofauti ya kiasi cha dola za Marekani milioni 36. Kamati Tekelezi ya *TEITI* ilianza uchunguzi wa tofauti hiyo kwa kumshirikisha Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kazi hiyo ya uchunguzi ilithibitisha malipo mengine yasiyoripotiwa na kuyatolea taarifa. Kwa sasa tofauti hiyo imebaki kuwa dola za kimarekani 531,841 tu na uchunguzi unaendelea ili kubaini tofauti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa mawasiliano wa *TEITI* unaoainisha namna taarifa za asasi hii zitakavyowafikia wadau na wananchi kwa ujumla ulikamilishwa na warsha za uelimishaji na uhamasishaji umma, kuhusu mpango wa utekelezaji wa *EITI* zilifanyika jijini Dar es Salaam, mwezi Desemba, 2010 na katika Wilaya za Tarime, Geita na Kahama, mwezi Januari, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango wa *EITI* hapa nchini ulikuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa sheria inayosimamia utekelezaji wa mpango wa *EITI*, ufahamu mdogo wa wananchi juu ya tasnia ya uziduaji, na namna ya kupanua wigo wa utekelezaji wa *EITI* kwa kuhusisha mikataba *(MDAs)* na tathmini ya matumizi ya mapato yatokanayo na tasnia ya uziduaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini nchini, Wizara iliendelea kuimarisha Ofisi za Kanda na Mikoa. Wizara ilikamilisha kwa asilimia 95 ujenzi wa jengo la Ofisi ya Madini Kanda ya Kati lililoko Mjini Singida. Tathmini na gharama za ujenzi wa Ofisi za Mtwara na Mpanda imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kupata takwimu sahihi za madini yanayozalishwa nchini na kuuzwa nje na migodi mikubwa kufuatia ukaguzi na udhibiti wa shughuli za madini unaofanywa na *TMAA*. *TMAA* kwa kushirikiana na *TRA* ilifanya ukaguzi wa hesabu za fedha za mwaka 2008 hadi 2009 na kodi za Kampuni ya Madini ya *Resolute Tanzania Limited (RTL)* na kuwezesha Serikali kukusanya shilingi bilioni 32.26 zilizolipwa kwa mara ya kwanza kama *corporate tax* na kampuni hiyo ya madini. Aidha, kazi ya ulinganisho wa malipo ya mrabaha *(royalty reconciliation)* iliyofanywa na *TMAA* mwaka 2010/2011, iliwezesha Serikali kukusanya shilingi milioni 728.8 kutoka kwa wamiliki wa migodi mikubwa nchini, kiasi ambacho kisingelipwa endapo ulinganisho huo usingefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakala ulifungua ofisi Mkoani Mwanza kwa lengo la kutoa huduma kwa karibu zaidi kwa wateja katika Kanda ya Ziwa, ambapo kuna migodi mingi mikubwa na midogo ya madini pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* ulikamilisha utayarishaji wa ramani za jiolojia na jiokemia katika *QDS* nne (4) za 136, 159, 176 na 161 kwenye maeneo ya Sikonge, Manyoni na Bahi, ramani 30 za jiolojia na jiokemia za ukanda wa kati wa nchi ziliwekwa kwenye mfumo wa dijitali, ramani maalumu tatu za

jiolojia na uwepo wa madini za Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Mbeya na maeneo ya Chunya zilichapishwa. Aidha, utafiti wa kina kuhusu upatikanaji wa nishati ya jotoardhi katika maeneo ya Ziwa Ngozi (Mbeya) na Kisaki (Morogoro) ulifanyika na taarifa kuandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala ulichapisha katalogi inayoonyesha matukio ya matetemeko ya ardhi nchini kwa kipindi cha kati ya mwaka 1900 hadi 2010, kijitabu cha madini yapatikanayo katika kila Wilaya za Tanzania Bara, *Gemstone Guide Book;* vijarida vinne vya kufundishia wachimbaji wadogo kuhusu jinsi ya kutambua, kuchambua na kuthaminisha madini na miamba, matumizi ya *borax* kwenye uchenjuaji wa dhahabu, usalama migodini kwa kuzingatia viashiria vya kijiolojia *(geological indicators)* na utambuzi wa maeneo yenye mbale *(ore);* na elimu ya afya na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha miundombinu na kujenga uwezo wa kitaalamu, wakala umekamilisha ujenzi wa jengo la kutunzia kumbukumbu za kijiosayansi *(national geo-museum)* na ghala la kuhifadhi sampuli za choronge za miamba Mkoani Dodoma. Aidha, maeneo kwa ajili ya kujenga vituo viwili (Mtwara na Geita) yamepatikana na kufanya idadi ya vituo vya kudumu vya kupima matetemeko ya ardhi nchini kuwa tisa. Vilevile, watumishi 18 walipelekwa kwenye mafunzo ya muda mrefu katika kuongeza uwezo wa kupima matetemeko ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Chuo cha Madini – Dodoma kilitoa mafunzo ya ngazi ya cheti na stashahada kwa jumla ya wanafunzi 196 katika fani za jiolojia na utafutaji madini, uhandisi migodi na uhandisi uchenjuaji madini. Mafunzo mengine yaliyotolewa ni kwa wachimbaji wadogo kuhusu ujasiriamali madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya chuo uliendelea ambapo ujenzi wa Zahanati, Karakana ya Uhandisi Migodi, Maabara ya Jiofizikia, Maabara ya Jiokemia na Maabara ya Petrolojia na Minerolojia ulikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo kiliendelea kuimarisha ushirikiano wa kitaaluma na vyuo, taasisi na migodi ya madini nchini. Chuo kilianzisha ushirikiano na Chuo cha Rockies cha Kanada kwa lengo la kushirikiana katika kuandaa wafanyakazi wanaokidhi mahitaji ya soko la ajira katika Sekta ya Madini. Aidha, makubaliano ya kimsingi ya ushirikiano yalisainiwa baina ya Chuo cha Madini na kampuni za utafutaji madini za *TANCAN* na *TANZAM* 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* liliendelea kuhuishwa ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake mapya. Miongoni mwa mambo yaliyofanyika ni pamoja na marekebisho ya Sheria ya Mwaka 1972 iliyounda Shirika pamoja na kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati wa Miaka Mitatu, muundo mpya wa Shirika na muundo wa utumishi. *Business Analysis* ya Shirika pia imeandaliwa ambayo itakuwa ni msingi wa kuandaa *Business Plan*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kumpata mbia mpya kwa mgodi wa dhahabu wa Buckreef ulikamilika mwezi Desemba, 2010 kwa njia ya ushindani ambapo Kampuni ya *Tanzania Royalty Exploration Corporation* kutoka Kanada ilipatikana. Katika ubia huo, Serikali kupitia *STAMICO* inamiliki asilimia 45 ya hisa katika mgodi huo. Kazi zote za kuendeleza utafiti na kufungua mgodi zitagharimiwa na mbia mwenza. Aidha, *STAMICO* imekabidhiwa eneo la mgodi wa Buhemba. Kwa sasa Shirika linaendelea na taratibu za kumpata mbia kama ilivyofanyika kwa mgodi wa *Buckreef*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza uwezo wa kitaaluma na kiutendaji, Wizara iliwapeleka mafunzoni watumishi 140 wa kada mbalimbali ili kuwajengea uwezo. Kati yao watumishi 113 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na 27 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufungaji wa mfumo wa kompyuta wa taarifa za kiutumishi na mishahara *(Human Capital Management Information System)* ulikamilika. Mfumo huu ni kwa ajili ya kurekebisha mishahara ya watumishi baada ya kupandishwa cheo na kuwatoa wale ambao utumishi wao ulikoma kwa sababu mbalimbali kama kustaafu, kuacha kazi na kufariki.

Kituo cha Madini cha *Southern and Eastern African Mineral Centre – SEAMIC*. Mwaka 2010/2011 nchi ya Sudani ilijiunga na Kituo cha Madini *(SEAMIC)* kilichoko Kunduchi Dar es Salaam na kufanya jumla ya nchi wanachama kufikia nane. Nchi nyingine ni Angola, Comoro, Ethiopia, Kenya, Msumbiji, Uganda na mwenyeji Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Kituo kimeendelea kutoa huduma za kitaalamu kwa nchi wanachama. Baadhi ya huduma zilizotolewa na Kituo ni mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa madini ya vito, utambuzi wa madini, huduma ya uchenjuaji wa madini, na utafiti wa matumizi mbalimbali ya madini ya viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi wanachama ikiwamo Tanzania, zililipa michango yake ipasavyo iliyokiwezesha kituo kutimiza majukumu yake na kutekeleza miradi mbalimbali katika nchi wanachama pamoja na kushirikiana na washirika wa maendeleo hasa Jumuia ya Nchi za Ulaya *(EU)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2011/2012, yamezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016), Malengo ya Maendeleo ya Milenia (2000 – 2015), Malengo ya Taifa ya MKUKUTA awamu ya pili, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010, Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati na Madini 2011/2012 – 2015/2016, Maagizo Na. 6 na Na.9 yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akifungua Bunge mwezi Novemba, 2010; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti 2011/2012 – 2015/2016, Kilimo Kwanza, ushauri uliotolewa mwezi Juni, 2010 na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuimarisha na kuboresha Sekta ya Nishati na kuongeza fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine ili kuwawezesha

wananchi kuendesha shughuli za maendeleo kwa ufanisi na kuongeza mchango wa sekta hizo katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma hiyo, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Sekta ya Nishati kwa mwaka 2011/2012 ni kuboresha na kuandaa sera za nishati, kuongeza uzalishaji wa umeme; kupanua na kuboresha njia za kusafirisha na kusambaza umeme, kuwezesha *REA* kutekeleza majukumu yake, utekelezaji wa miradi kupitia *TEDAP*, kuimarisha na kupanua miundombinu ya gesi asili, kuendeleza shughuli za gesi na mafuta na kuendeleza nishati jadidifu na mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa mitambo ya kufua umeme ya *MW 100* Ubungo, Dar es Salaam na *MW 60* Nyakato, Mwanza. Mradi wa *MW 100* unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2011 na wa *MW 60* mwezi Juni, 2012. Baada ya Serikali kuingia makubaliano ya awali ya uendelezaji wa mradi wa Kinyerezi wa *MW 240* mwezi Septemba, 2010 chini ya mwendelezaji - Kampuni ya Sumitomo, Serikali itaendelea kupitia mapendekezo ya kitaalamu na kibiashara kwa kushirikiana na *TANESCO*. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka 2011 na kukamilika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuendeleza mradi wa *Mnazi Bay MW 300* ambao unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa *KV 300 (HVDC)* yenye urefu wa kilometa 1,100 kutoka Mtwara hadi Singida ili kuunganisha Kituo cha Kufua Umeme kwenye gridi ya Taifa. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2014/2015. *TANESCO* itaendelea kufanya tathmini ya maeneo yatakayoathiriwa na ujenzi wa mradi pamoja na kufanya tathmini ya athari za mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwekezaji wa mradi wa kufua umeme wa Somanga Fungu MW 230 anaendelea na maandalizi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Ruhudji *MW 358.* Baada ya kukamilisha zoezi la kuajiri washauri watatu *(legal, financial and technical advisors)* watakaosaidia Serikali katika majadiliano ya mikataba na mwekezaji kupitia Kamati ya Taifa ya Majadiliano, Serikali itaendelea na majadiliano na mwekezaji ili kukamilisha mkataba wa awali wa uendelezaji wa mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mgodi na Mradi wa Kufua Umeme wa *MW 200* wa Kiwira utaanza baada ya *Consolidated Holding Corporation (CHC)* kukamilisha kazi ya ukaguzi maalumu ya kutathmini mali na madeni ya Mgodi. Baada ya zoezi hili kukamilika, Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* na *STAMICO* watakamilisha taratibu za kupata fedha za kujenga mradi kutoka taasisi za fedha za China. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwendelezaji wa mradi ataendelea kukamilisha upembuzi yakinifu wa Mradi wa kufua umeme wa Ngaka, mradi ambao unalenga

kuzalisha umeme wa *MW 400* ili kuwezesha uendelezaji wa mgodi wa makaa ya mawe na mradi wa kuzalisha umeme. Mradi huu unatarajiwa kukamilika 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kufua umeme wa Mchuchuma unaratibiwa na *NDC* kwa kushirikiana na mwekezaji *Sichuan Hongda Corporation Ltd* ya China. Mradi huu utatekelezwa katika awamu kuu mbili. Awamu ya kwanza zitazalishwa *MW 300* zitakazotumika kuyeyusha chuma cha Liganga na awamu ya pili zitazalishwa *MW 300* ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya Taifa. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/12, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda itaendelea na taratibu za kuendeleza mradi wa Murongo/Kikagati ambao unalenga kuwapatia umeme wananchi waishio katika mpaka wa Tanzania na Uganda. Katika kipindi hiki makubaliano ya awali *(MoU)* baina ya Uganda na Tanzania yatatiwa sahihi baada ya Serikali hizi mbili kuridhia yaliyomo kwenye *MoU* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea na taratibu za utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa *MW 63* kwa kutumia nguvu za maji wa Rusumo. Mtaalamu mshauri anayefanya upembuzi yakinifu wa mradi huo anatarajiwa kuwasilisha ripoti yake ya mwisho mwezi Oktoba, 2011. Aidha, taarifa ya utekelezaji wa mpango wa fidia *(resettlement Action Plan)* nayo pia inatarajiwa kuwa tayari ifikapo mwezi huo wa Oktoba, 2011. Chini ya usimamizi wa *NELSAP*, taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi zimeanza kufanyika.

Mhesimiwa Naibu Spika, chini ya usimamizi wa RUBADA, Serikali itaendelea kujadiliana na wawekezaji binafsi wanaoonyesha nia ya kuendeleza mradi wa Stiegler's Gorge wa *MW 2,100*. Aidha, majadiliano yataendelea kati ya Serikali na kampuni ya Sinohydro kutoka China kuhusu taratibu za utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Mpanga MW 165. Mradi wa Mpanga unatarajiwa kukamilika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Rumakali upo katika maeneo ya Makete, Kyela na Mbeya. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa *KV 220*. Mradi unatarajiwa kugharimu dola za kimarekani milioni 700. Mradi unatarajiwa kuendelezwa kupitia uwekezaji wa Sekta Binafsi *(IPP)* ambaye ni Kampuni ya *Zarubezhstroy OJSC* ya Russia. Mkataba wa makubaliano ya awali *(MoU)* kati ya Serikali na Kampuni ya *Zarubezhstroy OJSC* ulisainiwa Septemba, 2010 kwa nia ya uendelezaji wa mradi. Mwendelezaji huyo kwa sasa anaandaa makabrasha ya mapendekezo ya utekelezaji wa mradi kwa andiko la Kiufundi na Kifedha kwa ajili ya kuliwasilisha Serikalini. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika azma ya kupunguza makali ya mgawo wa umeme, *TANESCO* imeanza kutekeleza hatua zifuatazo: imeingia mkataba wa kukodisha mitambo ya Symbion yenye uwezo wa kufua *MW 112.5* ambayo ilianza kufua umeme mwezi Juni, 2011, imekamilisha taratibu za kukodi mitambo ya Aggreko ya kufua *MW*

*100* kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Agosti, 2011, inakamilisha taratibu za kununua mitambo ya *MW 70* itakayofungwa Majani Mapana, Tanga na inakamilisha taratibu za kununua mitambo ya kufua umeme ya *MW 150* itakayofungwa Ubungo, Dar es Salaam. Aidha, mitambo ya *IPTL* itarekebishwa ili iweze kutumia gesi asili na mafuta mazito mara baada ya migogoro iliyoko Mahakamani kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya za Nanyumbu (Mtwara), Bukombe (Geita), Namtumbo (Ruvuma), Nkasi (Rukwa) na Ngorongoro (Arusha). Aidha, upelekaji wa umeme katika Makao Makuu ya Wilaya mpya utaendelea kutekelezwa kupitia *REA* kwa kadiri fedha zitakavyoendelea kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufungaji wa jenereta tisa zenye uwezo wa kufua umeme wa *MW 1.25* kila moja kwa ajili ya Makao Makuu ya Wilaya za Sumbawanga, Nkasi, Ngorongoro na Namtumbo unaendelea kufanywa na mkandarasi ambaye ni kampuni ya *Zwart Techniek* ya Uholanzi, ambapo katika Wilaya ya Sumbawanga jenereta nne zenye uwezo wa *MW 5* zimefungwa. Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi (Namanyere) yatapata huduma ya umeme kutoka Mjini Sumbawanga baada ya kukamilika ujenzi wa njia ya usafirishaji na usambazaji umeme. Katika Wilaya ya Ngorongoro jenereta nne zenye uwezo wa *MW 5* zimefungwa. Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji kwenye miji hii inatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2011. Jenereta moja yenye uwezo wa kuzalisha *MW 0.4* ambayo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2011 itafungwa katika Makao Makuu ya Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Nishati Vijijini utaendelea kuratibu utekelezaji wa mradi kabambe wa kusambaza umeme katika Mikoa 16 ya Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Rukwa na Tabora. Mradi huu utakamilika mwanzoni mwa mwaka 2012. Aidha, Wakala utaendelea kuibua, kuhamasisha na kuwezesha uendelezaji wa vyanzo vya nishati jadidifu kwenye maeneo ya vijijini yaliyo mbali na Gridi ya Taifa pamoja na kuhamasisha waendelezaji wa miradi hiyo kupata fedha kutoka kwenye mpango wa kupunguza hewa ukaa *(Carbon Development Mechanism).* Aidha, Wakala utakamilisha mradi wa mfano wa kupunguza gharama za miundombinu ya kusambaza na kuunganisha umeme vijijini *(low cost design project)* unaotekelezwa katika Wilaya za Mbozi na Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuimarisha na kupanua njia za usambazaji wa umeme katika Mikoa sita hapa nchini. Ufuatiliaji wa mrejesho kutoka *MCA-T* kuhusu taarifa za uthamini wa mali za watu zitakazoathiriwa utafanyika kufuatia kukamilishwa kwa taarifa hiyo na kuwasilishwa kwa *MCA-T*. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa *submarine cable* kutoka Dar es Salaam hadi Unguja, Serikali itaendelea na uchambuzi wa zabuni za ujenzi wa vituo vya

kupozea umeme wa msongo wa *KV 132* kutoka Ubungo hadi Ras Kilomoni. Majadiliano yataanza baada ya kukamilika kwa kazi ya usanifu wa waya za baharini na tathmini za ufundi. Upembuzi yakinifu katika maporomoko ya Igamba *Stage III* kwenye Mto Malagarasi pamoja na tathmini ya athari za mazingira inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa *Sustainable Solar Market Package I (SSMP I)* Wilayani Sumbawanga Vijijini (Rukwa) kwa kufunga mifumo ya umeme wa jua kwenye maeneo ya huduma za kijamii yaliyobaki na kwa watu binafsi. Jumla ya mifumo 35 itafungwa kwenye huduma za kijamii na zaidi ya mifumo 8,000 kwa wateja binafsi ikijumuisha kaya na sehemu za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya mradi huo *(SSMP II)* inatarajiwa kuanza mwaka 2011/2012 na itahusisha Wilaya nane katika Mikoa mitano ya Kagera (Biharamulo na Chato), Kigoma (Kibondo na Kasulu), Geita (Bukombe), Tabora (Sikonge) na Ruvuma (Tunduru na Namtumbo). Huduma ya umeme wa jua kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima wa chai na kahawa huko Rungwe (Mbeya) na Mbinga (Ruvuma) zitaendelea kusimamiwa na Wizara kupitia mradi wa *Commercial Solar PV Cluster.*

Kupitia mradi huo wa majaribio, jumla ya mifumo 1,000 inatarajiwa kufungwa ifikapo mwezi Septemba, 2011. Matarajio ni kupeleka miradi kama hiyo maeneo mengine nchini yaliyo mbali na gridi ya Taifa kwa kutumia uzoefu, mafanikio na mafunzo yatakayopatikana katika mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kusaidia na kuhamasisha wawekezaji katika miradi midogo ya kuzalisha umeme utokanao na vyanzo vya nishati jadidifu na pia kupata mikopo ya muda mrefu kutoka benki za hapa nchini kupitia *credit line window* na ruzuku ya kuunganisha wateja kutoka Wakala wa Nishati Vijijini chini ya mradi wa *TEDAP*. Kupitia mpango huu zaidi ya wateja wapya 2,000 wanatarajiwa kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi na uboreshaji wa njia za kusafirisha umeme. Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa *KV 400* kutoka Iringa hadi Shinyanga kupitia Dodoma na Singida unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka 2012 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2014/2015. Aidha, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa *KV 132* kutoka Makambako hadi Songea utaanza baada ya kukamilisha upimaji wa njia ya umeme na ulipaji fidia na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014.

Vilevile, upanuzi wa gridi ya Kaskazini – Magharibi yenye msongo wa *KV 220* kutoka Mkoa wa Shinyanga (Bulyanhulu) hadi Mbeya kupitia Mkoa wa Kigoma na Rukwa utafanyika. Ukarabati wa vituo vya umeme na njia za usafirishaji wa umeme katika Mkoa wa Kilimanjaro utafanyika kwa msaada wa Serikali ya Japani na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014. Pia ukarabati wa Kituo cha Kufua Umeme

cha Hale utafanyika chini ya ufadhili wa *SIDA* na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014. Ukarabati huu utarejesha ufuaji wa umeme katika kiwango cha awali cha *MW 21*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kuwatafuta wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa ujenzi wa njia ya umeme ya *KV 220* ya Bulyanhulu – Geita – Nyakanazi itafanyika baada ya kumpata mshauri mwelekezi mwezi Septemba, 2011. Kazi ya kutayarisha zabuni za kandarasi za ujenzi itakamilika mwezi Juni, 2012. Ujenzi wa njia ya Bulyanhulu hadi Geita na vijiji katika njia hiyo utaanza mwezi Julai, 2012 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014. Maombi yamewasilishwa *BADEA* kwa ajili ya kugharimia ujenzi wa njia ya kutoka Geita hadi Nyakanazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa njia ya umeme ya *KV 400* ya Morogoro – Chalinze – Tanga – Moshi hadi Arusha, makubaliano ya awali *(MoU)* kati ya Serikali na kampuni ya *TBEA* ya China ya kuendeleza mradi yalisainiwa mwezi Agosti, 2009 na mkataba wa ujenzi ulisainiwa mwezi Aprili, 2011. Kazi ya tathmini ya mazingira inafanywa na *TANESCO* na majadiliano ya mkopo kwa ajili ya kutekeleza mradi yanaendelea. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu wa mradi mradi wa Tanzania - Zambia *Interconnector* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia *Nile Basin Initiative* utakamilika Septemba, 2012. Baada ya hapo, taratibu za ujenzi zitaanza na mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zitakazofanyika katika mwaka 2011/2012, chini ya mradi wa Mradi wa Electricity V ni kutayarisha zabuni za ujenzi na kupata wakandarasi. Kazi ya ujenzi itaanza mwezi Machi, 2012 na kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa bomba la gesi asili kutoka Mtwara - Dar es Salaam - Tanga umekamilika, Serikali kupitia *TPDC* itasimamia utekelezaji wa mradi mpya wa ujenzi wa bomba la gesi lenye kipenyo cha inchi 24 kutoka Mnazi Bay (Mtwara) hadi Somanga Fungu (km 290) ambalo litaunganishwa na bomba la gesi litakalojengwa kutoka Songo Songo kupitia Somanga Fungu hadi Dar es Salaam (km 232), lenye kipenyo cha inchi 20 upande wa baharini na inchi 30 upande wa nchi kavu. Mradi huu unaotarajiwa kugharimu takriban dola za Marekani milioni 778 utagharimiwa na mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Mradi utatekelezwa kwa awamu tatu kwa kuanza na bomba la Songo Songo hadi Dar es Salaam ili kuhakikisha kuwa miradi ya kuzalisha umeme kutokana na gesi asili itakayokamilika mwaka 2013 inapata gesi asili ya kutosha. Awamu ya pili itakuwa ujenzi wa bomba kutoka Mnazi Bay hadi Somanga Fungu ili kuongeza upatikanaji wa gesi asili Dar es Salaam na awamu ya tatu itahusisha ujenzi wa bomba la gesi asili kutoka Dar es Salaam hadi Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itakamilisha upatikanaji wa fedha za mradi. Shughuli za tathmini ya mazingira, upimaji wa njia ya bomba, kubaini gharama za fidia kwa waathirika zitafanyika na ujenzi utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Shirika la Mandeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* itaanza ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asili kutoka Ubungo hadi Mikocheni viwandani. Aidha, *TPDC* itakamilisha uunganishwaji wa nyumba 57 kwenye mtandao wa usambazaji wa gesi asili katika eneo la Mikocheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia, inatarajia kuanza mradi wa usambazaji wa gesi majumbani, kwenye taasisi na magari. Mradi huo unatarajiwa kuanza kwa kutafuta maeneo ya ujenzi wa vituo vya kujazia gesi, vibali vya njia za kupitishia bomba na utayarishaji wa michoro ya njia za kusafirisha gesi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa maandalizi ya Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta wa Pamoja na Kanuni za kusimamia mfumo huo, mfumo huo utaanza kutumika rasmi mwaka 2011/2012. Pamoja na matarajio ya kuleta nafuu ya bei za mafuta nchini, mfumo huu utasaidia kupata takwimu sahihi za mafuta yanayoingizwa nchini na kuboresha makusanyo ya kodi itokanayo na biashara ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuangalia vyanzo vya fedha ili kutekeleza mpango wa kuanzisha Hifadhi ya Mafuta ya akiba na dharura hapa nchini. Aidha, kitengo cha kusimamia uanzishaji wa Hifadhi ya Mafuta kitaanzishwa *TPDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*, kwa kushirikiana na Kampuni ya *Global Fluid International* itaendelea na kazi ya kudhibiti uchakachuaji wa mafuta kwa kutumia vinasaba pamoja na zoezi la ukaguzi wa kushtukiza kwa kutumia *mobile laboratories*. Zoezi la kuweka vinasaba, pamoja na kuzuia uchakachuaji vilevile linazuia *fuel dumping* ili kuwa na mazingira sawa ya ushindani miongoni mwa wafanyabiashara wa mafuta nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *EWURA* itapitia upya na kuboresha kanuni za ukokotoaji wa bei za mafuta hapa nchini. Uboreshaji huo utazingatia tozo na gharama mbalimbali ambazo zinatozwa na mamlaka zinazotoa huduma katika mfumo mzima wa uagizaji na upokeaji wa mafuta. Serikali imeamua kufanya mapitio ya namna ya kukokotoa tozo hizo ili zizingatie gharama halisi za mamlaka husika katika kutoa huduma hizo. Tathmini pia itafanywa ili kubaini tozo stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza utafutaji wa mafuta na gesi asili hapa nchini, majadiliano kati ya Serikali na kampuni mbalimbali za utafutaji yanatarajiwa kufanyika. Kampuni hizo ni *Petrobras* (Kitalu Na. 8), na *Ndovu Resources* eneo la Nyuni (Kitalu Na. 2). Kampuni za *Orphir/BG Group* na *Ndovu Resources* zitaendelea na shughuli za uchimbaji katika maeneo ya Vitalu Na. 1, 3, 4 eneo la bahari ya kina kirefu na kisima cha Nyuni - 2 sawia. Vilevile, kampuni ya *Dominion* itafanya utafiti wa mitetemo katika eneo la *Selous* baada ya kukamilika kwa tathmini ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna makampuni 13 yanayofanya utafutaji wa mafuta na gesi hapa nchini katika maeneo ya nchi kavu na baharini (kwenye kina kirefu na kina kifupi). Idadi ya vitalu vinavyomilikiwa na makampuni mbalimbali ni 23 ikimaanisha kwamba kuna makampuni ambayo yanamiliki zaidi ya kitalu kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchorongaji wa visima vya utafutaji mafuta na gesi asili unaendelea kufanyika na sasa hivi kampuni ya *Aminex* ya Uingereza ikishirikiana na Kampuni ya Ndovu ya Australia inachoronga kisima kisiwani Nyuni, Kaskazini mashariki mwa Songosongo. Uchorongaji huo unatazamiwa kumalizika kati ya mwezi Julai na Agosti, 2011. Aidha, kampuni ya *Petrobras* ya Brazil inayomiliki Vitalu Na. 5 na 6 kwenye kina kirefu baharini Mashariki mwa Kisiwa cha Mafia, imezindua meli maalumu ya uchorongaji visima vya utafutaji mafuta na gesi kwenye kina kirefu baharini.

Meli hiyo iitwayo *POSEIDON* ambayo imemalizika kuundwa kwenye kiwanda cha *SAMSUNG* nchini Korea ilizinduliwa na Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda tarehe 08 Julai, 2011. Meli hiyo inatarajiwa kutia nanga bandarini Mtwara ikijitayarisha kuanza kazi mwezi Septemba, 2011. *Petrobras* watachoronga visima viwili kwenye Kitalu Na. 5 na baada ya hapo meli hiyo itaanza kuchoronga Kitalu Na. 2 kwenye kina kirefu baharini Mashariki mwa Lindi, kinachomilikiwa na kampuni ya *Statoil*. *Petrobras* imeingia mkataba wa miezi 20 na wamiliki wa meli hiyo na itaweza kuchoronga visima zaidi ya hivi vitatu nilivyovitaja hapa kwa mikataba na makampuni mengine yanayomiliki vitalu kwenye kina kirefu baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *BG* pia imeingia mkataba na wamiliki wa meli ya *METRO-2* kwa ajili ya kuchoronga visima kwenye Vitalu Na. 1, 3 na 4 wanavyomiliki kwenye kina kirefu baharini. Nao pia watakuwa na mkataba wa muda mrefu na wanatarajia kuchoronga visima vitano. Meli hiyo inaundwa nchini Korea na inatarajiwa kuwasili hapa nchini mwezi Desemba, 2011 au Januari, 2012 na kuanza kazi mara moja. Serikali kupitia *TPDC* inajivunia hali hii nzuri ya uwekezaji na ni mategemeo yetu kwamba itazaa matunda mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya gesi asili ni mengi na Serikali imeweka vipaumbele vya matumizi ya gesi inayopatikana hapa nchini. Kutokana na matatizo ya umeme hapa nchini yatokanayo kwa kiasi kikubwa na ukame ambao umesababisha vina vya maji kwenye mabwawa ya ufuaji umeme kushuka kwa kiasi kikubwa, Serikali imetoa kipaumbele cha matumizi ya gesi asili katika kuzalisha umeme. Kipaumbele kingine ni uzalishaji wa mbolea ili kufanikisha malengo ya Kilimo Kwanza. Matumizi mengine ya gesi asili ni uzalishaji wa saruji, matumizi ya majumbani, uzalishaji wa *plastics* na *petrochemicals* kama *methanol*. Gesi asili pia itapoozwa kuzalisha *LNG* kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TPDC* inaendelea kutangaza maeneo mengine ambayo kwa sasa hayana wawekezaji. Juhudi zinazofanywa ni pamoja na

kuchambua na kuboresha takwimu za kitaalamu ili kuwavutia wawekezaji. Aidha, *TPDC* hivi karibuni ilitangaza zabuni ya kuwekeza Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika ambapo kampuni kumi zilijitokeza kuwania eneo hilo. Uchambuzi wa zabuni hiyo umekamilika na mshindi atatangazwa hivi karibuni. Serikali na *TPDC* iko kwenye mazungumzo na kampuni ya *Heritage* ya Uingereza kuendeleza utafutaji wa mafuta na gesi katika maeneo ya Ziwa Rukwa na inatarajiwa yatakamilika mwezi huu wa Julai, 2011. *TPDC* pia imeanza mazungumzo na mwekezaji kwa ajili ya utafutaji mafuta na gesi asili kwenye maeneo ya Ruhuhu na Ziwa Eyasi/Natron na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa umeme utokanao na nishati jadidifu na mbadala ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini. Vyanzo hivyo ni pamoja na mionzi ya jua, upepo, tungamotaka, maporomoko madogo ya maji, jotoardhi, biyofueli na bayogesi. Vilevile, nishati ya biyofueli itaendelezwa kwa kuweka mazingira yatakayowezesha wananchi kunufaika katika eneo hilo jipya hususan kwa kupata ajira na kuwaongezea kipato na kuhakikisha upatikanaji wa nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya nishati hapa nchini, Serikali itaandaa sheria, kanuni pamoja na viwango vya ubora wa nishati kwa vifaa vya umeme vitakavyotengenezwa na kuingizwa hapa nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuelimisha na kuhamasisha matumizi ya *LPG* na bayogesi kwa ajili ya matumizi ya nishati ya majumbani kwa nia ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Katika mpango huo, Serikali itaendelea kuhamasisha majiko bora na njia za kisasa za utengenezaji wa mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itadurusu Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003 ili iendane na mabadiliko yanayojitokeza katika Sekta ya Nishati. Aidha, Sera ya Nishati Vijijini itaandaliwa ili kuharakisha upatikanaji wa huduma za nishati bora vijijini kwa kuweka miongozo thabiti juu ya kusimamia, kuratibu na kutekeleza mipango mbalimbali. Baada ya kukamilisha durusu ya Sera ya Taifa ya Nishati, mikakati mbalimbali itaandaliwa ikiwa ni pamoja na kutayarisha Mkakati wa Matumizi ya Gesi Asili *(Gas Utilisation Master Plan),* Kudurusu Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Sekta ya Umeme *(Power System Master Plan)* na Mpango Kabambe wa Usambazaji wa Umeme Vijijini *(Rural Electrification Master Plan).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mchango mkubwa wa gesi asili katika uchumi wa nchi yetu, Serikali imekamilisha maandalizi ya rasimu ya sheria ya gesi asili na Muswada wa Sheria hiyo utawasilishwa Bungeni katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Sekta ya Madini ni kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Madini kwa kusimamia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini, hususan kwenye maeneo ya utafutaji na uongezaji thamani ya madini, kuendeleza uchimbaji wa kati na mdogo ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo ya uchimbaji mdogo, kuimarisha Mfuko wa Wachimbaji Wadogo, kuendelea kuimarisha ukaguzi wa shughuli za migodi ili kuongeza utunzaji wa usalama,

afya na mazingira, kuimarisha Mfumo wa Usimamizi na Utoaji Leseni *(MCIMS)* wa Makao Makuu na Ofisi za Kanda ili kuongeza kasi ya utoaji leseni, kuimarisha na kuwezesha mashirika/taasisi zilizo chini ya Wizara za *STAMICO*, *GST*, *TMAA*, *TANSORT* na Chuo cha Madini kutekeleza majukumu yake ipasavyo, na kudurusu sheria mbalimbali za madini zikiwemo Sheria ya Usonara sura ya 228, Sheria ya Baruti Sura ya 45 na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 imefanya marekebisho mbalimbali ili kuboresha usimamizi wa Sekta ya Madini nchini. Marekebisho hayo ni pamoja na mfumo wa ukokotoaji wa mrabaha na viwango vipya vya mrabaha na ada mbalimbali za leseni za madini. Kisheria, marekebisho hayo yatagusa wawekezaji wapya na kampuni ambazo hazina mikataba na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakamilisha majadiliano na wamiliki wa migodi yenye mikataba *(MDAs)* ya *Bulyanhulu Gold Mine; Resolute Tanzania Limited; Geita Gold Mine; North Mara Gold Mine; Tulawaka Gold Mine;* na *Buzwagi Gold Mine*, ili mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Madini yaweze kuzigusa kampuni hizo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuimarisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na miamba zinazofanyika kwenye Kituo cha *Arusha Gemstone Carving Centre.* Aidha, chini ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini *(SMMRP),* mashine zaidi za ukataji, usanifu na utengenezaji wa mapambo ya vito zitanunuliwa. Moja ya jengo la kituo hicho litakarabatiwa ili kupata madarasa ya kufundishia stadi mbalimbali za uongezaji thamani. Wakufunzi wenye ujuzi kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi wataajiriwa ili kituo hicho kiweze kutoa mafunzo ya elimu ya jemolojia, ukataji, usanifu vito na usonara kwa nia ya kukuza uongezaji thamani madini ya vito na dhahabu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Madini ya mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 zinasisitiza suala la uongezaji thamani madini na usonara nchini. Ili kukidhi utekelezaji wa Sera hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyabiashara wa Madini –*TAMIDA*, itafufua maonyesho ya kimataifa ya vito na usonara yatakayofanyika Jijini Arusha kati ya tarehe 26 - 29 Aprili, 2012. Lengo la maonyesho hayo ni kuvutia wafanyabiashara wa madini wa kimataifa, wakiwemo wafanyabiashara kutoka nchi jirani kama Msumbiji, Madagaska, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na hatimaye kukuza soko la madini ya vito la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kubaini maeneo yanayofaa kwa uchimbaji mdogo na kuangalia uwezekano wa kuyatenga kwa ajili ya kuyagawa kwa wachimbaji wadogo. Vilevile, mafunzo yataendelea kutolewa kwa wachimbaji wadogo wakiwemo wazalishaji wa chumvi katika Mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Mbeya, Lindi, Singida, Mtwara, Tanga, Dar es Salaam na Pwani juu ya teknolojia sahihi na salama ya uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini na taratibu za kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakamilisha kazi iliyobaki ya kujenga mtaro ili kuepusha mafuriko katika eneo lenye shimo la *De Souza* huko Mirerani. Suluhisho la kudumu la changamoto za uchimbaji mdogo wa *tanzanite* huko Mirerani ni kwa wachimbaji wadogo kuungana, kuunda kampuni na kuchimba kwa njia za kisasa na kiusalama. Kwa kuwa kuungana ni jambo la hiari, tunatarajia wachimbaji hao na kwa kupitia wawakilishi wao wataona umuhimu wa kuungana na kuendeleza uchimbaji wa kisasa ili kuepusha ajali zinazotabirika kutokana na kukiuka mipaka ya leseni na mashindano ya kufukuzia eneo linalozalisha kwa wakati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kutenga fedha za kuimarisha uchimbaji mdogo na kusimamia matumizi ya mfuko wa kuwaendeleza pamoja na marejesho ya mfuko huo.

Kuimarisha Afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa masharti ya utunzaji wa mazingira katika shughuli za madini yanazingatiwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Aidha, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi katika migodi na machimbo ya mawe na kutoa maelekezo ya uchimbaji sahihi na salama kwa lengo la kuhakikisha kuwa matumizi ya baruti, kemikali na vifaa vya uchimbaji haviathiri usalama na afya za wachimbaji na wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka maeneo hayo. Vilevile, Serikali itaendelea kusimamia sheria inayozitaka kampuni zenye migodi kupitia na kufanya maboresho ya mipango ya ufungaji migodi na kuweka *rehabilitation bond.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya uchimbaji salama na matumizi sahihi ya zana za uchimbaji, kemikali na baruti yataendelea kutolewa ili kupunguza ajali zinazotokea migodini. Serikali itaendelea kusisitiza utekelezaji wa Usalama Kwanza katika shughuli za uchimbaji madini katika migodi yote mikubwa, ya kati na midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mradi wa *SMMRP*, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wa kutoa leseni za madini na kuimarisha uwezo wa usimamizi wa masuala ya sera, sheria, usalama na mazingira migodini. Chini ya mradi huu, Wizara itaimarisha usambazaji wa elimu kwa umma na upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za madini na pia itaboresha utoaji wa huduma za ugani na kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu ujasiriamali katika uendelezaji wa madini, hususan, ya viwandani na vito na shughuli za uongezaji thamani madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zitakazofanyika chini ya mradi huo ni pamoja na ukusanyaji wa takwimu za kijiolojia kwa njia ya anga *(airborne geophysical survey);* kuendeleza Kituo cha *Arusha Gemstone Carving Center* kilichopo Arusha kwa kufanikisha utekelezaji wa shughuli za uongezaji thamani wa madini kwenye kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, asasi ya uhamasishaji uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya uziduaji Tanzania *(Tanzania Extractive Industries' Transparency Initiative – TEITI).* Kamati inayohusika na Utekelezaji wa *TEITI* itaendelea na usimamizi wa

mchakato wa utekelezaji wa vigezo, kanuni na matakwa ya *EITI* ikiwa ni pamoja na uelimishaji na uhamasishaji wa wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu asasi hii. Aidha, Kamati itaandaa ripoti ya pili ya *TEITI* kwa kuchanganua taarifa za malipo na mapato kwa mwaka 2009/2010. Vilevile, Kamati itaratibu taratibu na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria yatakayozingatiwa wakati wa kuandaa Sheria ya Usimamizi wa shughuli za *EITI* nchini. Lengo ni kuweka uwazi, uwajibikaji na utawala bora katika uvunaji wa raslimali za madini, gesi asili na mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuimarisha Ofisi za Madini zilizopo Mikoani kwa kuzijengea uwezo wa kuwa na vitendea kazi. Serikali itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Singida na kuanza ujenzi wa Ofisi za Madini za Mtwara, Mpanda, Mbeya na Dar es Salaam. Aidha, ukarabati utafanyika kwa ofisi za madini za Shinyanga na Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania itaendelea kutoa mchango wake na kushikiza Wataalamu wenye uzoefu *(secondment)* kwenye Kituo ili kukiimarisha na kukiwezesha kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma kwa Sekta za Madini za nchi wanachama. Aidha, Kituo kitapatiwa umeme wa uhakika *(dedicated line)* na nchi za Rwanda, Burundi na Zambia zitashawishiwa kujiunga na Kituo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa vyumba sita vya mihadhara kwa ajili ya kusomea, kuanzisha Kituo cha Mafunzo ya Ugani Kanda ya Ziwa kwa kushirikiana na wadau, kutoa mafunzo ya kozi ndefu za ufundi sanifu madini ikiwa na lengo la kupanua udahili wa wanafunzi kutoka 196 kwa sasa hadi 240. Aidha, Chuo kitaendelea kufanya shughuli za utafiti wa namna bora ya uchimbaji mdogo ili kubaini mahitaji ya mafunzo kwa wachimbaji wadogo na kutoa mafunzo husika, kuanza taratibu za kutoa mafunzo ya masafa, na kuwajengea uwezo wa kitaalamu na kitaaluma wakufunzi wa chuo ili kuimarisha utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza azma ya Serikali ya kutangaza hazina ya madini na kuvutia wawekezaji nchini, Wakala utaendelea na shughuli zifuatazo: kuchora ramani za jiolojia na jiokemia katika *QDS* nne za 194, 212, 230 na 178 katika Wilaya za Manyoni na Dodoma Vijijini, kukusanya takwimu za kijiofizikia *(High Resolution Airborne Geophysical Survey)* katika maeneo ya Mikoa ya Singida, Dodoma, Morogoro na Tanga pamoja na eneo la Lupa – Chunya; na kukusanya sampuli za choronge za miamba kutoka kwenye makampuni ya utafutaji na uchimbaji madini nchini na kuzihifadhi kwenye ghala la kutunzia sampuli hizo *(core library).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala utaendelea kupanga sampuli na kumbukumbu nyingine za kijiosayansi katika jengo la kutunzia sampuli za miamba na madini *(national geo-museum),* kubadilisha mfumo wa sasa wa kutunza kumbukumbu za maktaba na takwimu kuwa kwenye mfumo wa kompyuta *(Computer-Based Meta-Data Management System)* na kuboresha mfumo wa usambazaji wa taarifa hizo ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu hizo kwa wadau kwa njia ya mtandao wa kompyuta *(web–based Information dissemination system).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA)* utaendelea na ukaguzi na udhibiti wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini nchini ili kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika ipasavyo na raslimali za madini. Aidha, Wakala utaendelea kuelimisha umma kuhusu manufaa yanayopatikana kwenye Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha Taifa linanufaika ipasavyo na mapato yatokanayo na madini, Serikali itaendelea kuliwezesha Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* ili lishiriki kimkakati *(strategically)* katika uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa niaba ya Serikali. Kufuatia mgodi wa Buhemba kukabidhiwa kwa *STAMICO*, Shirika litaendelea kutafuta mbia mwenye uwezo wa kifedha na kiufundi ili kushirikiana naye katika kufanya utafiti wa kina kwa lengo la kubaini uwezekano wa kuufungua tena mgodi huo.

Kabla ya kukabidhiwa *STAMICO*, mgodi wa Buhemba ulikuwa chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi kuanzia mwezi Februari, 2008. Aidha, Shirika litaendelea kujadiliana na kampuni binafsi ya *Pan African Refinery* kutoka Afrika Kusini ili kampuni hiyo ianzishe vituo vikubwa zaidi vya kukodisha vifaa, kuchenjua miamba na kusafisha dhahabu kwa njia ya ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo ya Watumishi, Wizara itaendelea kuwapeleka mafunzoni watumishi 150. Kati yao, watumishi 34 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 116 mafunzo ya muda mfupi. Aidha, msisitizo umewekwa katika kutoa mafunzo ya uchambuzi na uthaminishaji wa almasi na madini ya vito, teknolojia ya urani na mionzi na mafunzo ya vitendo kwa wahandisi, wajiolojia na mafundi sanifu ili kuimarisha ukaguzi wa migodi na wachumi madini na nishati. Vilevile, mafunzo ya uongozi yataendelea kutolewa ili kuboresha usimamizi wa utendaji katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma kwa Watumishi wa Wizara wenye virusi vya UKIMWI na wanaougua magonjwa nyemelezi yanayosababishwa na UKIMWI itaendelea kutolewa na Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kutumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwa ajili ya kurekebisha mishahara ya watumishi baada ya kupandishwa cheo na kuwatoa ambao utumishi wao ulikoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini ilinufaika kwa misaada na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Serikali za nchi za Jamhuri ya Watu wa China, Japani, Kanada, Korea ya Kusini, Marekani, Norway Sweden, Uswisi na Ujerumani. Natoa pia shukurani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Raslimali ya Ulaya, Umoja wa Ulaya, pamoja na mashirika ya *BADEA, CIDA, DBSA, ECDF, FMO, GEF, GiZ, IAEA, JICA, MCC, NDF, NORAD, OFID, ORIO, SIDA, SAEDF, IFC, IDF, UNDP, UNESCO, UNICEF, UNIDO* na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola. Katika Mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kushirikiana na washirika hao na wengine katika kuendeleza Sekta za Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa ushirikiano wa hali ya juu, anaonipa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara hii. Aidha, nawashukuru Bwana David Kitundu Jairo - Katibu Mkuu, Makamishna wa Nishati na Madini, Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Viongozi na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara, wakiwemo wenyeviti na wajumbe wa Bodi, Kamati zilizo chini ya Wizara, wadau mbalimbali wa Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa katika kipindi cha uongozi wangu.

Kwa namna ya pekee niwashukuru wasaidizi wangu, Bwana Sosthenes Massola - Katibu wa Waziri, Mama Barah Mwamsaka na Mama Abia Maregesi - Makatibu Mhutasi, Bwana Paulo Mtulo – Dereva, Mama Aginess Senerwa pamoja na Wasaidizi wa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna wanavyotuwezesha kutimiza majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naliomba Bunge lako likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya Sh. 402,402,071,000/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka 2011/2012. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

Bajeti ya Maendeleo ni Sh. 325,448,137,000/= kati ya fedha hizo Sh. 236,311,391,000/= ni fedha za ndani na Sh. 89,136,746,000/= ni fedha za nje; na

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni Sh. 76,953,934,000/= ambapo Sh. 10,053,413,100/= ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake, na Sh. 66,900,520,900/= ni matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii itasomwa pamoja na kitabu cha hotuba ambacho kimewasilishwa pamoja na *adendum* iliyowasilishwa mezani kwako. Baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yako. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo!

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Ukurasa wa 108 kipengele Namba 10 eneo la Mradi 23 Nkasi, Namanyere; "upimaji wa njia ya umeme wa msongo mkubwa umekamilika na usimikaji wa nguzo umetekelezwa kwa asilimia 62."

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana msimamizi wa Rukwa, Meneja wake wa *TANESCO* amemdanganya. Hakuna hata nguzo moja ambayo imesimamishwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri taarifa iliyopo kwenye kitabu chake asahihishe, aseme ukweli. Hiyo siyo taarifa ya ukweli kabisa, tumechoka kudanganywa. Mara umeme mwezi wa Tatu, mara mwezi wa Tisa, mara mwezi wa Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaja hapa Bungeni kudanganywa, tumenyanyaswa kiasi cha kutosha. tunataka umeme Namanyere. Hii taarifa siikubali ni ya uongo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally K. Mohamed. Ningependa tu kusema kwa wataalamu wa Serikali wanaotengeneza vitabu hivi kuwa makini katika taarifa ambazo zinawekwa mezani mbele ya Bunge, zinapaswa kuwa sahihi. Kwa jinsi hiyo, nitatoa Mwongozo wangu baadaye kadri tunavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri kuweza ku-*cross check* taarifa zake, wakati muafaka nitatoa mwongozo wangu. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Namwona Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini - Mheshimiwa January Makamba anakuja kuwasilisha taarifa ya Kamati yake. Mheshimiwa January Makamba, karibu. *(Makofi)*

**MHE. JANUARY MAKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2010/2011, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 30 Mei hadi 1 Juni, 2011, Kamati ilifanya vikao na Wizara ya Nishati na Madini katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam kwa lengo la kupokea na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Aidha, pamoja na mambo mengine, Wizara ilielezea kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi fulani Wizara imeyafanyia kazi mapendekezo hayo ya Kamati. Hata hivyo, utekelezaji wa baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati bado unaendelea. Yapo mapendekezo ambayo bado hayajatekelezwa kwa sababu moja au nyingine. Kamati inaihimiza Wizara iharakishe kutekeleza mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilitengewa bajeti ya shilingi bilioni 281.7. Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha, yaani tarehe 30 Juni, 2011 ni shilingi 226.9 zilizokuwa zimepokelewa. Maana yake ni kwamba, Wizara ya Nishati na Madini pamoja na umuhimu wake kwa maendeleo na ustawi wa nchi, ilipokea asilimia 80.5 tu ya fedha ilizokuwa imetengewa mwaka jana.

Waziri alieleza kuwa, upatikanaji wa fedha hizo uliwezesha Wizara kutekeleza baadhi ya kazi ilizojipangia na kupata mafanikio ambayo Waziri ameyaelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 inaomba jumla ya Sh. 402,402,071,100/=. Kati ya fedha hizo, Sh. 76,953,934,100/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo, Sh. 10,053,413,100/= ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Mashirika yaliyo chini yake na Sh. 66,900,521,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC).* Aidha, Miradi ya Maendeleo inaombewa jumla ya Sh. 325,448,137,000/=, kati ya fedha hizo Sh. 236,311,391,000/= ni fedha za ndani na Sh. 89,136,746,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kinachoombwa ni nyongeza ya asilimia 42 ya kiasi cha Sh. 281,741,179,253/= kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2010/2011. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Wizara hii hususan katika Miradi ya Maendeleo ambayo bajeti yake imeongezeka kutoka Sh. 184,001,395,000/= mwaka 2010/2011 hadi kufikia Sh. 325,448,137,000/= mwaka 2011/2012 sawa na ongezeko la asilimia 78.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ongezeko hili, Kamati inaamini kwamba kiasi cha fedha kilichotengwa, hasa kwa miradi ya maendeleo ni kidogo mno na bado kingeweza kuongezwa zaidi kwa kuzingatia umuhimu na udharura wa shughuli za Wizara, hasa uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia Bajeti ya Wizara, yapo mambo kadhaa ambayo Kamati iliyabaini na ambayo tungependa kuyatolea maoni na mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kutumia maneno mengi, Kamati inapenda kutamka jambo lililo dhahiri kwa Watanzania wote kwamba hali ya uzalishaji umeme nchini ni mbaya. Tatizo hili sasa limedumu kwa muda mrefu na sasa limekuwa janga. Janga hili limeleta adha kwa wananchi, athari kubwa kwa uchumi na fedheha kwa nchi na kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji viwandani unazorota, gharama za uzalishaji zinaongezeka na hivyo bei za bidhaa kupanda, wajasiriamali wadogo wanaathirika, mikopo kwenye mabenki inashindwa kurudishwa, huduma mahospitalini zinaathirika, mapato ya Serikali yanashuka, na iko hatari kwamba pato la Taifa na ukuaji wa uchumi utaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua juhudi mbalimbali zilizofanywa na zinazofanywa na Serikali kukabiliana na tatizo hili. Hata hivyo, juhudi hizi kwa miaka kadhaa sasa hazijazaa matunda kwani tatizo limeendelea kuwepo. Kamati inakubali kwamba upungufu wa mvua umeendelea kuathiri uzalishaji wa umeme kwa sababu kwa kiwango kikubwa nchi yetu inategemea umeme unaozalishwa kwa nguvu ya maji yanayotokana na mvua. Hata hivyo, Kamati inaamini kwamba sababu hii ya upungufu wa mvua haiwezi kuendelea kuwa sababu ya kudumu kwa sababu mbili:-

(i) Mwenendo wa mvua na majira ya mvua yanajulikana kwa miaka mingi sasa, na Serikali katika kuhimiza kilimo cha kisasa, imekuwa inasema kwamba kilimo cha umwagiliaji ndio mkombozi kwa sababu mvua hazitabiriki. Kwa msingi huo huo, kama mvua haziwezi kuaminika katika kuendeleza kilimo, basi pia haziwezi kuaminika katika kuzalisha umeme.

(ii) Nchi yetu imejaliwa kuwa na vyanzo karibu vyote vya kuzalisha umeme, yaani gesi, jua, upepo, makaa ya mawe, joto-ardhi na vyanzo vingine mbadala ambavyo ni nchi chache duniani zenye neema kama hii. Kwa msingi huo, badala ya kuendelea kutaja uhaba wa mvua kama sababu ya mgawo, juhudi ziongezwe kwenye kuwekeza katika kuzalisha umeme kwa vyanzo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kwamba, katika karne ya sasa na kwa kuzingatia uwepo wa vyanzo vingi vya kuzalisha umeme, Serikali isiendelee kutegemea majaaliwa ya mvua kumaliza tatizo la mgao wa umeme. Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya uwekezaji katika vyanzo vingine vya umeme. Aidha, Kamati imeshangazwa kwamba, katika miaka saba iliyopita ni Megawati 145 tu za umeme wa kudumu ndizo zilizowekezwa wakati mahitaji ya umeme yanaongezeka kwa wastani wa Megawati 100 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na tatizo la umeme, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) Serikali ilichukulie tatizo la umeme katika udharura kama ilivyolichukulia tatizo la mdororo wa uchumi duniani mwaka 2008, kiasi cha kuamua kutenga shilingi trilioni 1.7 kukabiliana nalo. Kamati inaamini kwa dhati kabisa kwamba, athari za tatizo la umeme kwa uchumi wa nchi zinalingana au hata zinazidi athari za mdororo wa uchumi duniani.

Kwa kuwa, Serikali kupitia Waziri wa Nishati imekwishatangaza tatizo la umeme kuwa ni janga la Taifa, basi hatua zinazoendana na kauli hiyo zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kutenga fedha ambazo zitawezesha kupatikana kwa Megawati 500 na ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa gesi. Aidha, Kamati inapendekeza Serikali itengeneze Mpango wa Dharura wa kulinusuru Taifa na janga la umeme. Kamati inapendekeza mpango huu ujumuishe uharakishaji wa miradi iliyopo kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, uliopitishwa hapa Bungeni katika Mkutano huu.

(ii) Katika Bajeti ya Wizara kwa mwaka huu, Serikali imetenga shilingi bilioni 111.3 kwa miradi miwili ya dharura ya kuzalisha umeme, ambayo hata hivyo ilikuwa ikamilike mwaka 2010. Miradi hiyo ni mradi wa mtambo wa gesi wa Megawati 100 Ubungo na Mradi wa mtambo wa mafuta mazito *(HFO)* wa Megawati 60 Mwanza. Hata hivyo, Kamati imebaini na ina maoni yafuatayo kuhusu miradi hiyo:-

(a) Kuhusu mradi wa Megawati 100 za umeme wa gesi Ubungo utakaokamilika Desemba, 2011, Kamati imebaini kwamba utekelezaji kamili wa mradi huo unategemea kuongezwa kwa kiasi cha gesi inayosafirishwa kutoka Songosongo hadi Ubungo, Dar es Salaam. Kamati imejulishwa kwamba mitambo ya kusafisha gesi na bomba la kusafirisha gesi imefikia ukomo wa juu, na hata mtambo wa Symbion uliopo sasa hauzalishi umeme kwa uwezo wake wa Megawati 112 kutokana na kutokuwepo kwa gesi ya kutosha Ubungo. Hata juhudi za sasa za kuongeza uwezo wa kusafisha gesi (*re-rating*) haziwezi kukidhi mahitaji haya mapya hadi upanuzi wa miundombinu ya gesi utakapokamilika miezi 18 baadaye.

Kwa maana hiyo, Kamati inapendekeza Serikali iuhakikishie umma kwamba mtambo huu utapata gesi mara utakapofungwa mwezi Desemba na hautakuwa Tembo Mweupe (*White Elephant*). Kamati pia inapendekeza Serikali itoe maelezo kwamba ilikuwaje *TANESCO* inunue mtambo mkubwa na wa gharama kama huu bila kupanga kuwepo kwa gesi ya kuundesha ikizingatiwa kwamba mtambo huu umeagizwa zaidi ya miezi 18 iliyopita.

(b) Kuhusu mradi wa Megawati 60 za umeme wa kuzalishwa na mafuta mazito *(HFO)* Mwanza, mradi uliopaswa kukamilika mwaka jana, na ambao sasa utakamilika mwezi Juni, 2012, licha ya taarifa ya Serikali hapa Bungeni mwezi Februari kwamba ungekamilika mwezi Januari, 2012, Kamati haikupata maelezo ya kuridhisha juu ya upatikanaji wa mafuta mazito ya kutosha na pamoja na utaratibu na gharama za kuyasafirisha hadi Mwanza ukizingatia umbali kutoka bandari ya Dar es Salaam, ambapo mafuta yanaingia, ukizingatia ugumu wa kusafirisha mafuta mazito kwa barabara, na ukizingatia historia ya mradi kama huu wa kuzalisha umeme kwa mafuta Mwanza wa *Alstom Power Rentals* mwaka 2006/2007 ambao haukuzalisha umeme hata Megawati moja licha ya Serikali kulipa dola za Kimarekani milioni 21 bila ya mafanikio yoyote.

Pamoja na ushauri wa Kamati ambao haukuzingatiwa hapo awali, Kamati inaendelea kuishauri Serikali ijiridhishe na iuridhishe umma wa Watanzania kuhusu upatikanaji wa mafuta katika eneo la uzalishaji (Mwanza). Aidha, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa mtambo huo wa kutumia mafuta mazito uende sehemu ambayo upatikanaji wa mafuta hayo ni rahisi kama Dar es Salaam na badala yake mtambo wa kutumia dizeli ndiyo uende Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika bajeti hii, Wizara pia imetenga shilingi bilioni 12 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya kuendesha mitambo ya *IPTL*. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo za matumizi ya mtambo huo, fedha hizi zilizotengwa zitawezesha kununua mafuta siyo zaidi ya mwezi mmoja kutokana na matumizi ya mafuta kwa mwezi kuwa ni shilingi bilioni 15.

Kamati inaamini kwamba fedha hizi ni kidogo, ukizingatia hoja ya Serikali kwamba kuendelea kutumika kwa mtambo huu ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kupunguza mgao wa umeme au ni sehemu ya mkakati wa dharura wa kumaliza tatizo hili. Kamati inapendekeza fedha hizi ziongezwe ili mtambo huu uzalishe umeme kwa uwezo wake wa juu wa *MW 100* na kwa muda mrefu zaidi ya sasa. Kamati inapendekeza kwamba fedha hizi ziongezwe ili mtambo huu uzalishe umeme kwa kiwango chake cha juu cha Megawati 100 hadi hali ya umeme nchini itakapotengemaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya mgawanyo mpya wa fedha *(reallocation*) katika mwaka wa fedha uliopita na kuipa Wizara kiasi cha shilingi bilioni 28.5 kwa ajili ya kununua mafuta ya kuendesha mtambo huu. Hata hivyo, Kamati inapendekeza uwepo utaratibu mzuri na wa wazi wa manunuzi ya mafuta haya, na mchanganuo utolewe kuonyesha mapokeo ya fedha kutoka Hazina kwenda Wizarani, na kutoka Wizarani kwenda Mfilisi wa *IPTL*, na hatimaye kwa wauzaji wa mafuta, na hatimaye mchanganuo wa kiasi cha matumizi ya mafuta yenyewe kulingana na mauzo ya umeme kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini uwazi huu utasaidia kuondoa shaka kwamba fedha hizi nyingi za umma zinazotengwa kwa manunuzi ya mafuta zimekuwa hazitoi matokeo yanayotarajiwa kuhusiana na uzalishaji wa umeme kutoka kwenye mtambo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali iliahidi hapa Bungeni mwezi Februari mwaka huu kwamba, itakapofika mwezi huu wa Julai, zitakuwa zimepatikana Megawati 260 za umeme wa dharura, na kwa kuwa hadi sasa hakuna dalili za ahadi hiyo kutimia, Kamati inashauri, ili kuimarisha imani ya wananchi kwa Serikali juu ya uwezo wake wa kumaliza tatizo hili, basi Serikali itoe maelezo kuhusu sababu za kutotimia kwa ahadi hiyo na ni lini umeme huo utapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kasi ndogo ya uwekezaji wa Sekta Binafsi katika miradi ya muda mrefu ya uzalishaji umeme. Zaidi ya miradi ya *IPTL (1997)* na *Songas (2004)*, hakuna uwekezaji wowote wa sekta binafasi katika uzalishaji umeme uliofanyika nchini, zaidi ya miradi ya dharura ya muda mfupi. Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya na kuboresha mazingira ya uwekezaji wa sekta binafsi katika uzalishaji umeme nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Nishati inayotumika ni ya mwaka 2003 na haijaongelea suala la matumizi ya urani, na kwa kuwa nchi yetu imegundua kuwepo madini hayo muhimu. Kamati inashauri Serikali itengeneze mwongozo wa matumizi na udhibiti wa madini ya urani nchini ikiwemo matumizi katika uzalishaji wa nishati ya umeme

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na kasi ndogo ya uwekezaji na uhaba wa fedha za kuwekeza katika Sekta ya Nishati, Kamati inapendekeza Serikali ianzishe mfuko wa kuendeleza nishati ya umeme nchini. Mfuko huo utatumika kama mtaji katika

kuwekeza katika mitambo ya ufuaji umeme na miundombinu ya usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa umeme. Kamati inapendekeza mfuko huo utunishwe kwa vyanzo vifuatavyo:-

(a) Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* itokanayo na mauzo ya umeme iwe inalipwa moja kwa moja kwenye mfuko badala ya kwenda Hazina;

(b) Kodi ya kuagiza vipuri na mafuta ya kuendesha mitambo ya kufua umeme iwe inalipwa moja kwa moja kwenye mfuko huo badala ya kwenda Hazina; na

(c) Kama ilivyo katika nchi nyingine Serikali ianzishe ushuru wa huduma ya nishati ya umeme *(surcharge*) kwa makampuni yanayotumia umeme mwingi ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi zitasaidia *TANESCO* kupata fedha za kutosha na hivyo kuweza kujiendesha tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba gesi asili kama ikitumika vizuri kama inavyopaswa, inayo fursa ya kubadilisha kabisa sura ya uzalishaji wa umeme, maendeleo ya viwanda na uchumi wa nchi.

Hata hivyo, Kamati imepata mashaka kwamba nchi hainufaiki ipasavyo kutokana na kuwepo kwa gesi nchini, kwa maana ya unafuu wa bei, uharaka wa upatikanaji wa gesi na kujenga uwezo kwa Watanzania katika uwekezaji na utaalamu katika masuala ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kwamba gesi ni maliasili muhimu kwa uchumi na usalama wa nchi, Kamati imebaini kwamba biashara na utaratibu mzima wa uchimbaji, usafishaji, usambazaji na uuzaji nchini, vimegubikwa na utata mkubwa wa kimkataba usio na maslahi kwa Taifa pamoja na ukiritimba. Kamati haijaridhishwa na ushiriki, ufanisi na uadilifu wa Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania* katika mchakato wa uendelezaji gesi nchini. Hivyo basi, kufuatia utata huu uliopo, Kamati ya Nishati na Madini inaunda Kamati yake ndogo ili kufuatilia utata huu na tutadhihirisha wazi mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Kamati pia inashauri:-

(i) Serikali, kupitia *TPDC*, sasa ichukue uongozi madhubuti katika suala zima la gesi na sio tu kukaa pembeni na kusubiri tu mapato.

(ii) Serikali ichukue hatua za haraka za kuondoa ukiritimba uliopo katika biashara ya usafirishaji na usambazaji wa gesi nchini kwa kushinikiza Makampuni ya Songas na *Pan-African Energy* yaruhusu wachimbaji na watumiaji wengine wa gesi watumie miundombinu ya kusafisha na kusafirisha gesi. Aidha, fedha zote zitokanazo na mapato ya uzalishaji wa Petroli *(Production Sharing Agreement)* ambazo *Pan African Energy* wameipunja *TPDC* zikabidhiwe kwa *TPDC*.

(iii) Ili kuvutia wawekezaji, Serikali ihakikishe inaondoa vikwazo vya urasimu visivyo vya lazima husuan katika upatikanaji wa leseni.

(iv) Kwa kuwa Taifa sasa linaelekea kutegemea umeme utokanao na gesi kwa kiasi kikubwa, Kamati inapendekeza Serikali ihakikishe inaweka ulinzi wa kutosha katika maeneo yanayochimbwa gesi ili kuweza kukabiliana na maharamia.

(v) Kutokana na unyeti wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na kutoka Songosongo hadi Somanga Fungu, Serikali ichukue jitihada za makusudi za kuhakikisha bomba hili linajengwa na kumilikiwa na Serikali yenyewe au Shirika ambalo linamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Kamati inatoa angalizo kuwa bila ya ujenzi wa bomba, hili miradi iliyopangwa kutekelezwa yenye zaidi ya *MW 570* haitawezekana.

(vi) Kwa kuwa Rasimu ya Sheria ya Gesi imeshaandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tangu mwaka 2009, ni vyema basi mchakato wake uharakishwe ili iweze kujadiliwa na Bunge na hatimaye kuwa sheria rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kwamba siyo sahihi na wala siyo haki kwa Watanzania wachache wa maeneo ya mijini kunufaika na umeme wakati asilimia 86 za kaya zote hapa nchini hazina umeme. Kamati inapendekeza kwamba mipango ya usambazaji umeme vijijini iharakishwe ili nchi yetu ipate maendeleo ya uwiano sawa katika maeneo yote.

Serikali ilianzisha Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* ili kuhamasisha, kuwezesha na kuratibu uendelezaji wa miradi ya nishati bora vijijini. Pamoja na nia nzuri ya *REA* ya kuhakikisha inaendeleza miradi ya nishati bora vijijini, bado imekuwa ikipata changamoto hasa za kutotengewa fedha za kutosha na pia kutopata fedha zote na kwa wakati. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya shilingi bilioni 58.9 zilipitishwa, lakini hadi kufikia Mei, 2011 ni shilingi bilioni 13.6 tu sawa na asilimia 23 tu ndiyo zilikuwa zimetolewa. Hali hii haiendani na dhamira ya Serikali ya kupeleka umeme kwa kasi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka huu, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya *REA* ni shilingi bilioni 56.7. Kiasi hiki ni kidogo kuliko kilichotengwa mwaka jana na ni kidogo pia ukilinganisha na mahitaji. Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Serikali kutunisha Mfuko wa *REA*, na inapendekeza fedha hizi, tofauti na mwaka jana, zitolewe zote na kwa wakati. Kamati pia inapendekeza maamuzi ya maeneo ya kupeleka umeme yasizingatie nguvu au ushawishi wa viongozi na Watendaji Waandamizi wa Serikali wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango ya kusambaza umeme nchini, bado gharama za kuunganisha umeme majumbani kwa wananchi wengi wa vijijini ni kubwa mno. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya utaratibu wa manunuzi ya vifaa (kwa maana ya nguzo, nyaya, vipoza umeme na *meter*) vya kusambaza umeme ili kupata

vifaa hivyo kwa gharama nafuu. Kwa kuwa mpango wa usambazaji umeme vijijini ni mkubwa na wa muda mrefu, Kamati inaamini kabisa kwamba Serikali inaweza kuingia mkataba wa kutengenezewa na kununua kwa mkupuo vifaa vya usambazaji wa umeme na hivyo kupunguza gharama za vifaa hivyo.

Vilevile, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kubadilisha utaratibu ambapo sasa wananchi watalipa asilimia 25 ya gharama za kufungiwa umeme na kumalizia asilimia 75 kidogo kidogo wakati wakiwa na umeme ndani ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* linajihusisha na kazi za msingi za utafiti, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asili nchini. Pia Shirika hili linalo jukumu la kusimamia shughuli za utafutaji na uchimbaji unaofanywa na makampuni ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shughuli za utafutaji mafuta na gesi zimepiga kasi kubwa katika miaka ya karibuni, na kwa kuwa dalili zote zinaonyesha kwamba nchi yetu inayo gesi nyingi baharini, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuchukua hatua madhubuti na za haraka za kuliimarisha Shirika hili. Kwa hali ya sasa, kuwa upande wa fedha, kwa maana ya mtaji, na rasilimali watu, Shirika hili haliko katika hali nzuri. Kwa mantiki hiyo basi Kamati inashauri:-

(i) Serikali itekeleze dhamira yake ya kuidhamini *TPDC* ili iweze kupata mikopo itakayowezesha utekelezaji wa miradi yake, hasa mradi wa kusambaza gesi majumbani, kwenye magari na viwandani ambao utaleta ahueni kwa Watanzania kiuchumi na kimazingira. Katika mahitaji ya fedha za kutekeleza miradi kiasi cha shilingi bilioni 164, *TPDC* wameruhusiwa kutumia shilingi bilioni nane tu zinazotokana na asilimia 50 ya mapato yake. Kamati inapendekeza *TPDC* waruhusiwe kuchukua mapato yake yote kwa asilimia 100 ili kutekeza miradi yake muhimu.

(ii) Serikali itoe kibali ili *TPDC* waweze kuajiri watumishi wengine kutokana na watumishi wengi kuanza kustaafu.

(iii) Kutokana na fursa tuliyonayo ya kuwa na gesi, Serikali ichukue hatua za makusudi za kusomesha vijana wa kutosha kila mwaka wakachukue elimu ya juu katika nchi na vyuo duniani vilivyobobea kwenye masuala ya utafutaji na uchimbaji gesi na mafuta pamoja na ukaguzi wa raslimali hizi ili tujenge kada kubwa ya Watanzania wenye utaalamu na sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

(iv) *TPDC* wahusishwe kikamilifu katika shughuli zote za uagizaji, uhifadhi na usambazaji wa mafuta jamii ya Petroli na ili kupata ufanisi na manufaa, wakati umefika sasa *TPDC* isimamie uanzishwaji wa kampuni ya Taifa ya Mafuta *(National oil Company)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua katika kupunguza bei ya mafuta. Hata hivyo, hadi sasa bei ya mafuta bado haijashuka kwa kiwango kilichotarajiwa, na bei ya mafuta ya taa imepanda kwa kiwango ambacho

hakikutarajiwa. Kamati imebaini hadi sasa maelekezo ya Serikali ya kuondoa tozo mbalimbali za mafuta hayajatekelezwa mpaka sasa. Kamati inaishauri Serikali itoe maelezo ya kina na fasaha kuhusu sababu za bei kuendelea kubaki juu na jitihada zinazofanyika kudhibiti bei na kuhakikisha bei inashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na hali hii, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(a) *EWURA* ipewe uwezo na mamlaka zaidi ya kudhibiti bei ya mafuta, na hatua kali zichukuliwe kwa wale wataokuwa wanauza mafuta kwa bei ya juu ya bei elekezi;

(b) *Destination Inspection* ambayo ni asilimia 1.2 ya gharama halisi ya manunuzi ya mafuta *(FOB)* iondolewe. Aidha, gharama ya kudhibiti ubora kwa kutumia vinasaba ya dola 3.9 kwa kila lita 1000 na yenyewe ipunguzwe; na

(c) Serikali inashauriwa kuwa makini katika kudhibiti usambazaji wa mafuta ya ndege na yale yanayosafirishwa kwenda nchi jirani *(Transit Cargo)* ili yasije yakaingia sokoni na kuharibu dhamira nzuri ya Serikali. Aidha, mafuta yote ya ndege yalipiwe ushuru yanapotoka kwenye hifadhi na kampuni husika zidai kurudishiwa fedha zake baadaye ili kuweza kudhibiti mafuta haya kutumika tofauti na ilivyolengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini athari kubwa za kasi ndogo ya ushushaji wa mafuta bandarini kutokana na ufinyu wa miundombinu. Ili kuongeza ufanisi wa ushushaji wa mafuta kwa mahitaji ya sasa na baadaye kupitia bandari ya Dar es Salaam, Kamati imeona kuna haja kubwa ya kujenga Boya kubwa la kupakuwa mafuta baharini *(SPM)* na kujenga *KOJ* mpya, ambapo:-

(a) Kwa hali ya uharaka, mipango ya *TPA* ya ujenzi wa *SPM* iwekwe wazi kwa wadau wote. Aidha, Kamati inapendekeza mipango ya ujenzi wa *SPM* izingatie usalama katika upokeaji wa mafuta, mahitaji ya baadaye, ubora kulingana na thamani ya fedha *(value for money)* kwa mlaji;

(b) Kama uwezo mdogo wa fedha wa *TPA* ni kikwazo katika utekelezaji wa haraka wa mradi wa *SPM*, Serikali ialike wawekezaji wengine mara moja chini ya mpango wa *Build Operate Transfer (BOT)* na *Public Private Partnership (PPP);*

(c) Makampuni ya mafuta pamoja na *TPA* chini ya uongozi wa *EWURA* waanze mipango ya urekebishaji wa mfumo wa mabomba *(Expansion of Pipelines)* ambayo kwa kiasi kikubwa yanachangia ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta;

(d) Ili kuleta ufanisi katika upakuaji wa mafuta na kumpunguzia gharama mlaji, *flow meter* zenye uwezo wa kupakua mafuta mengi kwa wakati mmoja na kutoa takwimu sahihi zitafutwe na zitumike. Kamati inayo barua ya tarehe 2 Februari, 2011 kutoka kwa Wakala wa Mizani na Vipimo akipiga marufuku, kwa mujibu wa Sheria, matumizi ya *flow meter* kutokana na kuchakachuliwa. Lakini, hadi leo *flow meter* hiyo

inatumika na hivyo kutia shaka juu ya usahihi wa takwimu na hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato; na

(e) Serikali kwa kushirikisha wadau husika, isimamie uboreshaji na hatimaye ufanisi ya hifadhi ya mafuta ya *TIPER*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa mafuta na uchakachuaji ni tatizo kubwa sana hapa nchini. Serikali inapoteza kodi kati ya shilingi bilioni 25 hadi 33 kwa mwezi kutokana na tatizo hili. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka uwiano wa ushuru wa dizeli na petroli ili iendane na mafuta ya taa. Kamati inaamini kwa kuwepo uwiano wa bei hizo kutapunguza uchakachuaji wa mafuta. Pamoja na hayo, Kamati inaendelea kushauri yafuatayo:-

(a) *EWURA* iongeze jitihada kwa kutafuta njia zinazoweza kuzuia tatizo hili. *EWURA* itumie teknolojia tofauti ya kudhibilti ubora na kodi kwani teknolojia ya kuweka vinasaba inayotumika sasa imebainika kushindwa kudhibiti tatizo hili kwa kiwango kinachotakiwa.

(b) Kutokana na gharama kubwa za kupima sampuli za mafuta nje ya nchi, na kwa kuzingatia kwamba zipo maabara ndani ya nchi zinazoweza kufanya kazi hiyo, kwa mfano maabara ya *TBS*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mkemia Mkuu wa Serikali, Serikali izijengee uwezo maabara hizi ili ziweze kutoa huduma hii kwa gharama nafuu.

(c) Kwa kuwa *EWURA* na *TBS* wanafanya shughuli inayofanana ya kupima ubora wa mafuta na wote wanatoza kwa huduma hiyo hiyo, Serikali ifanye uamuzi wa kuiachia taasisi moja ifanye shughuli ya kudhibiti ubora wa mafuta.

(d) Adhabu kali zitolewe kwa wale wanajihusisha na uchakachuaji wa mafuta ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni, kutozwa faini kubwa kwa mfano shilingi bilioni mbili kwenye hifadhi *(Depot)*, shilingi milioni 500 kwenye Kituo cha Mafuta na shilingi milioni 100 kwenye magari na pia iwepo adhabu ya kifungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja *(Bulk Procurement System).* Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikiria kuanzisha Mfumo wa Ununuaji Mafuta kwa wingi *(Bulk Procurement).* Kamati inatambua faida za mfumo huu hasa katika kudhibiti bei ya mafuta. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa utayarishaji wa kanuni zitakazoongoza utaratibu huu haukushirikisha wadau wote. Hali hiyo imeleta mashaka kwa baadhi ya wadau ambao wanatarajiwa watoe ushirikiano. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri:-

(a) Wadau wote wakuu katika ununuzi wa mafuta kwa wingi *(TPA, TIPER, EWURA, TPDC* na Makampuni ya Mafuta) wakae pamoja na Serikali kwa uhuru na kuondoa mashaka miongoni mwao. Kamati imegundua kutokuwepo mawasiliano ya msingi katika jambo ambalo wanalolenga kulitekeleza kwa pamoja.

(b) Utekelezaji wa utaratibu wa *Bulk Procurement* uende sambamba na matumizi ya miundombinu itakayoleta manufaa yanayokusudiwa kama matumizi ya *SPM* (upakuaji wa tani 3000 kwa saa) na *KOJ* iliyoboreshwa (upakuaji wa tani 1200 kwa saa).

(c) Kwa kuwa mpaka sasa hamna mfumo ulio rasmi na madhubuti kwa ajili ya kupokea mafuta, na kwa kuwa utekelezaji wa mfumo huu utaanza karibuni kama Waziri alivyoeleza, ni vyema basi mabomba na matenki ya *TIPER* yakarabatiwe ili kuweza kupokea mafuta hayo.

(d) Utaratibu wa ununuzi kwa wingi ufanyike kwa mfumo ambao utakuwa wazi, utaondoa mianya ya rushwa na upendeleo, hautaiweka biashara ya kuagiza mafuta kwenye ukiritimba na hautawaingiza watu wa kati *(Middle men)* na kuongeza gharama kwa mlaji.

(e) Wakati Serikali inapanga kutekeleza mfumo huu wa *Bulk procurement*, ni vyema iwaeleze Watanzania namna itakavyoweza kuweka usalama kutokana na vitendo vya uharamia vinavyoendelea ili nchi isije kukosa mafuta kabisa endapo meli itatekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuamua kulibakisha Shirika la Madini la Taifa *STAMICO* katika mikono yake ili liweze kusimamia uwekezaji wa Serikali katika Sekta ya Madini. Hata hivyo, mafanikio ya Shirika hili yatategemea Shirika hili kuwezeshwa hasa ikizingatiwa lilisimama kwa takribani miaka13. Kwa mantiki hiyo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) *STAMICO* ikabidhiwe fedha zilizopatikana kutokana na kuuzwa kwa nyumba zake nne na mali zake nyingine ili zitumike katika kutekeleza kazi zake za maendeleo;

(ii) Uwekezaji au hisa katika Sekta ya Madini kunahitaji fedha nyingi. Fedha zaidi zitengwe kwa *STAMICO* ili kuhakikisha Shirika linawekeza na kusimamia vyema Sekta ya Madini kwa manufaa ya Taifa; na

(iii) Serikali ihakikishe kuwa mgodi wa Buhemba iliyoikabidhi *STAMICO* unasimamiwa kwa umakini ili kuondoa hujuma na malalamiko yaliyopo kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania ulianzishwa kwa lengo la kuhakikisha kiasi na ubora wa madini yanayozalishwa na kuuzwa nje ya nchi, kukagua gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa na ya kati kwa lengo la kukusanya taarifa sahihi za kodi na kuziwasilisha *TRA* na vyombo vingine vya Serikali, kufuatilia na kukagua shughuli za utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi, bajeti iliyotengwa na matumizi ya fedha kwa ajili ya ukarabati endelevu wa mazingira, kufuatilia na kuzuia utoroshaji wa madini na ukwepaji wa kulipa mrabaha na kutathmini thamani ya madini yaliyozalishwa ili kupata mrabaha stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na utendaji kazi wa Wakala kwani wakala umesaidia nchi kwa kiasi fulani kunufaika na madini kutokana na makampuni yenye migodi kuanza kulipa mrabaha stahiki pamoja na kodi nyinginezo. Kamati inatambua mchango na kazi hii nzuri ya *TMAA* na inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali itenge fedha ili kuwezesha Wakala kujenga ofisi yake tofauti na ilivyo sasa inatumia fedha nyingi kulipa kodi ya pango;

(ii) Serikali iiwezeshe Wakala huu ili iwe Mamlaka badala ya Wakala kwani itasaidia kuipa nguvu ya udhibiti, ufanisi na utendaji kazi wake; na

(iii) Kutokana na fursa ya madini tuliyonayo, Serikali ichukue vijana kila mwaka na kuwadhamini kwa mafunzo ya elimu ya juu ya uchumi wa madini na ukaguzi na udhibiti wa mapato ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 18 Novemba, 2008, Serikali ya Tanzania ilitoa tamko juu ya nia yake ya kujiunga na Asasi ya *EITI* kwa dhamira ya kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa raslimali za madini, gesi asili na mafuta na ilipatiwa usajili wa awali tarehe 14 Februari, 2009. Tangu ilipoanzishwa *TEITI* imetoa taarifa yake ya kwanza juu ya kodi zilizolipwa Serikalini na makampuni makubwa ya uchimbaji wa madini na gesi asilia katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Juni, 2009. Taarifa hiyo inaonyesha makampuni yamelipa jumla ya shilingi bilioni 174.9 wakati Serikali imeonesha kupokea jumla ya shilingi bilioni 128.4 hivyo kufanya tofauti ya malipo na mapato kuwa ni shilingi bilioni 46.5 kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza juhudi zilizofanywa za kuanzishwa kwa chombo hiki ambacho kinahusisha wadau kutoka makundi ya vyama vya kijamii, Serikali na Kampuni za madini. Aidha, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali kukitumia chombo hiki ipasavyo ili kuleta uhuru na uwazi katika mapato ya rasilimali za madini;

(ii) Serikali sasa ilete Muswada wa Sheria Bungeni ili chombo hiki muhimu kiwepo rasmi kisheria; na

(iii) Tofauti iliyojitokeza ya shilingi bilioni 46.5 za malipo yaliyofanywa na makampuni ya madini kwa Serikali zitolewe ufafanuzi ili kuleta dhana ya uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wengi wadogo wadogo ni wazawa wa nchi na wengi wao wanakaa na kufanya kazi karibu na maeneo ya migodi ya wachimbaji wakubwa. Wachimbaji hawa wamekuwa wakitegema kazi hii kama njia ya kujikimu kimaisha na wamekuwepo katika maeneo hayo hata kabla wachimbaji wakubwa hawajafika. Hata hivyo, yamekuwepo malalamiko mengi kutoka miongoni mwao kuwa wamekuwa wakikosa haki ya kutumia rasilimali zao wakati wageni wakinufaika.

Malalamiko ya namna hiyo yamesababisha kudhoofisha mahusiano kati ya pande hizo mbili na hivyo kuhatarisha hali ya usalama na amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba jitihada kubwa zaidi zifanyike kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo waweze kuendesha shughuli zao kwa tija, katika mazingira ya usalama zaidi na waweze kunufaika na jasho lao.

Katika bajeti ya mwaka huu, Mfuko wa Wachimbaji Wadogo umetengewa Sh. 1,189,630,000/= kwa ajili ya kuwasaidia. Kamati haijaridhishwa na fedha hizi kwani ni ndogo mno ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya Wachimbaji, hivyo Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa shughuli za uchimbaji wa madini zinahusisha kuwaondoa wakazi wa maeneo husika ili kupisha shughuli za uchimbaji, Kamati inashauri kuwa wakazi hao wapewe fidia stahiki kabla shughuli za uchimbaji madini hazijaanza. Aidha, kwa nia ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo wanaokutwa katika maeneo hayo, Serikali iweke utaratibu utakaowezesha wachimbaji hao kunufaika.

(ii) Wachimbaji wadogo wadogo watengewe fedha za kutosha ambazo zitawawezesha kununua vifaa ambavyo ndiyo nyenzo muhimu katika biashara yao;

(iii) Kwa kuwa Wizara ilieleza ina mpango wa kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwaunganisha kwenye vikundi, ni vyema wachimbaji hawa wakahamasishwa na kushawishiwa na wakaungana katika vikundi ili kurahisisha azma ya Serikali ya kuwasaidia;

(iv) Ili kuleta mahusiano mazuri kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo wadogo, Kamati inashauri wachimbaji wakubwa wachangie katika mfuko wa wachimbaji wadogo wadogo;

(v) Serikali iweke program maalum ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo wa Nyamongo na maeneo mengine ili waweze kunufaika na teknolojia na miundombinu ya uwekezaji mkubwa katika Mgodi wa *North Mara* na maeneo yanayofanana na hayo;

(vi) Kutokana na uchimbaji wa madini ya *Tanzanite* kuwa unatofautiana na uchimbaji wa madini mengine, kwa maana ya jiolojia ya kipekee ya madini ya *Tanzanite*, Serikali ihakikishe inatunga kanuni mahsusi kwa ajili ya uchimbaji wa madini hayo yatakayowahusisha wachimbaji wote;

(vii) Baada ya sheria ya madini kupitishwa ambayo inayomilikisha madini kwa asilimia 100 kwa wazawa na kufuatia maelekezo ya Waziri ya kuzuia usafirishaji wa madini ghafi nje ili kuleta thamani ya madini, ipo haja ya Serikali kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo kwa kuanzisha vituo vya kuongeza thamani ya madini kabla ya kuuzwa nje ya nchi; na

(viii) Serikali ihakikishe inadhibiti ajira ya watoto katika migodi ambao hujulikana kama nyoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuundwa kwa Kamati hii, muda mwingi imeutumia katika kushughulikia masuala ya nishati kwa maana ya umeme na mafuta. Hata hivyo, Kamati imejipanga kwa siku zijazo kujikita zaidi katika Sekta ya Madini ili kuweza kuifahamu vizuri. Pamoja na hayo, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Kutokana na Makampuni yenye mikataba ya madini ambayo yamekuwa yakinufaika msamaha wa kodi ya mafuta kutumia vibaya fursa hiyo na kuiibia Serikali kodi yake, Kamati inashauri Serikali ifuatilie suala hili ili kuhakikisha fursa hiyo inatumiwa vizuri; na

(ii) Kwa kuwa Watanzania wengi hawashiriki katika kutoa huduma za ugavi kwenye migodi, na kwa kuwa huduma hii ina faida sana hasa katika kukua kwa pato la Taifa, Kamati inashauri Serikali isaidie ili Watanzania wengi zaidi waweze kujikita katika huduma na kunufaika na hatimaye kuinua pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Madini Dodoma ni muhimu sana katika kuendeleza taaluma ya masuala ya madini nchini hivyo kinahitaji kuangaliwa kwa maana ya kuwezeshwa ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Chuo hiki kinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa Jengo la Utawala, ukumbi wa Mikutano, ufinyu wa bajeti, ukosefu wa vitendea kazi vya kutosha na miundombinu isiyoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua mchango mkubwa unaotolewa na chuo hiki na inaamini kuwa endapo kitaboreshwa, basi kitasaidia ukuaji wa Sekta ya Madini na Nishati. Kutokana na umuhimu huo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Fedha za kutosha zitengwe ili miundombinu muhimu iweze kujengwa;

(ii) Badala ya Chuo hiki kuwa kitengo cha mafunzo cha Wizara, basi kijitegemee na kuwa kama kilivyo chuo cha *DIT* (Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam) au Chuo cha Maji cha Rwegalulira;

(iii) Wanafunzi wanaomaliza katika Chuo cha Madini wathaminiwe na makampuni ya madini na kuwezeshwa kufanya mazoezi ya vitendo kwenye migodi na kupewa kazi ambazo uwezo wao na elimu yao inastahili; na

(iv) Kwa kuwa mitaala ya mafuta na gesi inaanzishwa katika chuo hicho, na kwa kuwa sasa nchi yetu inapiga kasi katika utafutaji wa gesi na mafuta, Kamati inashauri mtazamo wa sasa uwe ni kukiwezesha Chuo hiki kuwa Chuo cha Nishati na Madini badala ya kuwa Chuo cha Madini peke yake kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo kadhaa kuhusiana na mgawanyo wa fedha za Bajeti ya Wizara ambayo Kamati inaona ni muhimu kuyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uendelezaji wa Gesi ya SongoSongo na Mnazi Bay umetengewa kiasi cha Sh. 8,373,000,000/=. Hata hivyo, kati ya fedha hizi, Sh. 1,820,000,000/= ni kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi SongoSongo, na Sh. 5,173,000,000/= ni kwa ajili ya ruzuku kwa kampuni binafsi ya *Wentworth Resources* ya kuuza umeme Mtwara na Lindi ili iuze umeme sawa na bei ya *TANESCO*.

Kamati inaamini kabisa kwamba miradi hii miwili haihusiani kabisa na Uendelezaji wa Gesi ya Songo Songo na Mnazi Bay. Pia, Kamati inaamini kwamba siyo kazi ya Wizara ya Nishati na Madini kujenga Kituo cha Polisi.

Kamati inapendekeza fedha hizi zipelekwe *TPDC* ili kuwaongezea uwezo wa kutekeleza miradi yao ya kusambaza gesi katika Jiji la Dar es Salaam; na Serikali, kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ipeleke ulinzi katika eneo la SongoSongo ukizingatia tishio la maharamia kuvamia eneo hili. Aidha, kutokana na umuhimu wa kuwa na Kituo cha Polisi katika eneo la Kijiji cha Songosongo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ianze mchakato wa kujenga kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara. Kwenye bajeti ya Wizara, zimetengwa Sh. 3,889,000,000/= kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara jijini Dar es Salaam.

Kamati imebaini kwamba gharama za mradi mzima hazijajulikana, na inashauri kwamba, siyo vyema kwa Serikali kuanza mradi wa ujenzi bila kujua gharama halisi za ujenzi wenyewe na uwezo wa Serikali kwa siku zijazo kumalizia mradi huo. Aidha, kwa mujibu wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 212 (d) inaelea wazi kuwa: "kuanzia sasa Majengo mapya ya Wizara za Serikali yajengwe Dodoma badala ya Dar es Salaam." Kamati inashauri ujenzi wa Mako Makuu hayo ya Wizara uwe Dodoma kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuchukua nafasi hii kutambua mchango wa Wajumbe wa Kamati kwani wamekuwa makini katika kuchambua Bajeti hii na walifanya kazi hadi usiku kwa moyo wote na hatimaye kukamilisha taarifa hii. Napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Januari Y. Makamba - Mwenyekiti na Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa Amos G. Makala, Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aesh, Mheshimiwa Abia M. Nyabakari, Mheshimiwa Charles J. P. Mwijage, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Christopher O. Ole Sendeka, Mheshimiwa Mussa Khamis Silima na Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mheshimiwa Mwanamrisho T. Abama, Mheshimiwa David E. Silinde, Mheshimiwa Suleiman N. Suleiman, Mheshimiwa Kisyeri W. Chambiri, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Sarah M. Ally, Mheshimiwa Munde T. Abdallah, Mheshimiwa Vicky P. Kamata na Mheshimiwa John J. Mnyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William M. Ngeleja (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam K. Malima, (Mb), kwa kuwasilisha hoja vyema mbele ya Kamati na ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati. Napenda pia kumshukuru Katibu Mkuu, Ndugu David Jairo pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara *TANESCO*, *TPDC STAMICO*, Chuo cha Madini, Taasisi ya Geolojia na wengineo kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa Kamati yetu na ufafanuzi walioutoa katika mambo mengi tuliyoyauliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah lakini hasahasa Ndugu John Joel na Katibu wa Kamati hii Ndugu Pamela Pallangyo, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano waliotupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wananchi wangu wa Bumbuli, kwa kunichagua na kuniamini niwe Mbunge wao. Kazi yetu ya maendeleo ni kubwa, tutaifanya na tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mwisho baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini, Fungu 58 kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, jumla ya shilingi 402, 402, 071,100/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati kwa niaba ya Kamati nzima ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa hotuba hii nzuri. Wapo waliosema Kamati imenunuliwa, kwa hotuba hii ukiisoma, ni dhahiri maneno hayo ni uongo kabisa.

Sasa naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa John John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI, WIZARA YA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha maoni haya ya

Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge (Toleo la mwaka 2007) Kanuni ya 99(7) ikiwa ni sehemu ya kuchangia katika wajibu wa Bunge wa kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Ubungo kwa kuniamini bila kujali tofauti zingine na kunituma kuwawakilisha kwa kunitunuku heshima ya kuwa mtumishi wa umma. Nawashukuru pia kwa kunipa Madiwani wa kufanya nao kazi. Ahsanteni wazee kwa busara zetu, wanawake kwa sala zenu na vijana wenzangu tuliokuwa pamoja kipindi cha kampeni na kukesha wote Loyola katika kulinda ushindi. Tumeandika historia kwamba hakuna hujuma inayoweza kudhibiti nguvu ya umma *(people's power).* Mabadiliko yameanza kuonekana na kwa pamoja tuendelee kutimiza wajibu kwa kurejea dira yetu: A.M.U.A; Maslahi ya Umma Kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wanafamilia yetu ya Dalali, wazazi wangu na ndugu zangu kwa upendo wenu ambao umechangia katika furaha yangu na motisha ya kuendeleza ujasiri na uadilifu katika kusimamia ukweli, haki na ustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwa shukrani mchango wa viongozi wenzangu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Makao Makuu, Mkoa wa Kinondoni, Kanda Maalum Dar e Salaam, Jimbo la Ubungo na wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika hatua ambayo tumefikia. Mahitaji na matumaini ya Watanzania yanatutaka tuendelee kuongoza kwa umoja, umakini na uwajibikaji mpaka kieleweke dhidi ya ubinafsi, uzembe na ufisadi ambao unazidi kushamiri katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wote katika mamlaka ambao mmenipa ushirikiano kwenye Serikali Kuu, Manispaa ya Kinondoni, katika Kamati ya Nishati na Madini na Wabunge wengine kwa ujumla katika kutekeleza majukumu ya Kibunge kwa manufaa ya Taifa letu na watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini ambayo tunatolea maoni bajeti yake leo ni Wizara nyeti sana katika Taifa letu nyakati za sasa na kwa vizazi vijavyo. Sekta ya nishati ni moyo wa Taifa wakati madini ni mtaji wa nchi yetu. Tanzania imejaliwa rasilimali nyingi, watu, ardhi yenye rutuba, maji (bahari, mito na maziwa), kuwa katika eneo la kimkakati la kijiografia kwa biashara, maliasili ikiwemo za utalii na madini. Hata hivyo, tunaelekea kuwa na laana ya rasilimali hali ambayo inafanya wananchi walio wengi kuendelea kuwa katika lindi la umasikini na wakiendelea kusukumwa pembezoni nje ya urithi ambao Taifa linao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tishio la usalama na amani katika Taifa letu kwa sasa sio migomo wala maandamano bali ni migogoro inayoendelea ya kirasilimali maeneo mbalimbali ya nchi ambayo ni bomu la wakati litakalolipuka iwapo kasi ya ukuaji wa

uchumi wenye kutoa fursa kwa wengi haitaongezwa. Sekta ya nishati ni moyo wa kurekebisha hali hii na sekta ya madini ni mtaji wa kufanikisha dhamira hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakutana leo ikiwa ni miezi michache kuelekea kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru Taifa likiwa gizani kutokana na mgawo wa umeme unaoendelea, idadi ndogo ya Watanzania waliounganishwa kwenye Gridi ya Taifa na matatizo ya sekta ya nishati kwa ujumla. Tunakutana wakati ambao urithi wetu mkuu ambao mababu zetu waliupigania wakati wa kudai uhuru; ardhi na rasilimali zake ikiwemo madini ukiwa mashakani kutwaliwa na kutawaliwa kwa ubeberu mamboleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 21 Juni 2011, Bunge lilipitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ambapo Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani tulipiga kura ya 'Hapana' lakini ikapita kutokana na uwingi wa Wabunge wa upande wa pili bila kuzingatia maslahi ya umma. Tulipiga Kura ya 'Hapana' kwa kuwa ilikuwa ni bajeti yenye maneno matupu bila matendo katika mipango na utekelezaji; athari za bajeti hiyo zimeshaanza kudhihirika kwenye uchumi wa nchi na maisha ya wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka 2011/2012 ilielezwa kwa maneno matupu kuwa imeweka nishati kuwa ni kipaumbele cha kwanza. Hata hivyo, vitabu vya Bajeti ya Serikali iliyopitishwa vinathibitisha ukweli mchungu kwamba jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya nishati na madini ni shilingi bilioni 539.3 tu. Kwa mujibu wa Vitabu vya Bajeti ya Serikali 2011/2012 iliyopitishwa, Wizara ya Nishati na Madini imetengewa jumla ya shilingi 402.4 bilioni kwenye Fungu 58. Fedha hizo zimegawanywa katika mafungu ya Matumizi ya Kawaida shilingi 76,953,934,000 na bajeti ya Maendeleo zimetengwa shilingi 325,448,137,000 tu. Fedha nyingine kidogo za maendeleo shilingi bilioni 126.6 zipo kwenye Fungu la 50 miradi ya *MCC* kwa kutegemea wahisani. Hivyo, bajeti hii haijaichukulia kwa uzito unaostahili sekta za nishati na madini hususani umeme hali ambayo inaibua maswali iwapo Serikali ina dhamira ya dhati ya kukabiliana na changamoto za msingi zinazolikabili Taifa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imepitia Kitabu cha Pili cha Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Nishati na Madini *( Volume II Supply Votes)*, Fungu la 58, vifungu 1001-1009, 2001-2012 na 3001 na kubaini kwamba hii ni bajeti ya mgawo mkubwa wa posho na ufujaji. Mathalani Idara ya Kitengo cha Mawasiliano katika kulipana posho zitatumika Sh. Milioni 405.62 sawa na asilimia 63% ya fedha yote iliyotengwa Sh.Milioni 641.99 kwa Idara hii. Idara ya Fedha na Uhasibu itatumia Sh.Milioni 598.49 sawa na asilimia 42% ya fedha yote iliyotengwa. Kanda ya Ziwa – Mwanza kulipana posho inatumia Sh.Milioni 389.68 sawa na asilimia 40% ya fedha yote iliyotengwa. Kuna posho kuwanunulia mavazi wafanyakzi wanaosafiri nje ya nchi, sherehe na maonesho, chakula na vinywaji, huduma kwa wageni, posho za kukaimu nafasi na posho nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Wizara ya Nishati na Madini inakadiriwa kutumia Sh. Bilioni 7.9 kulipana posho na matumizi mengine ya kawaida ya anasa. Kwani jumla hii ni nje ya posho za msingi kama vile posho za uhamisho, posho za

mafunzo, nyumba, maji na umeme. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali ifanye marekebisho kwenye bajeti ili fedha hizi zipunguzwe ziweze kuongezwa kwenye kuongeza ujenzi wa miundombinu wa Chuo cha Madini Dodoma na kuongeza kiwango cha fedha katika Mfuko wa Wachimbaji Wadogo wa Madini. Aidha, yako matumizi mengine ya ujenzi wa maofisi na gharama kubwa za kisheria ambayo yanapaswa kuhamishiwa katika miradi muhimu ya maendeleo ikiwemo ya umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba tarehe 15 Juni 2011, Kambi ya Upinzani iliwasilisha Bajeti Mbadala ambayo ilitenga fedha za kutosha katika kukabiliana na changamoto za sekta za nishati na madini. Bajeti Mbadala ilitenga Fedha za Maendeleo Sh.Bilioni 977 kwa ajili ya Wizara ya Nishati na Madini ukilinganisha na ile Serikali iliyotenga Sh.Bilioni 452 kwa maendeleo (Fungu 58 na 50) ambayo ni sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 100 (100 %) kutoka kwenye Bajeti ya Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kiwango cha bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kuongezwa ili vipaumbele vifuatavyo viweze kuzingatiwa kwa uzito unaostahili:-

- Kuwekeza fedha za kutosha kwenye sekta ya umeme na gesi ili kumaliza kabisa tatizo la nishati ya umeme na kupunguza gharama za maisha. Hatua hizo ziambatane kuwekeza katika Bomba la Gesi kutoka Mtwara, pamoja na ujenzi wa mtambo wa kutengeneza gesi *(LPG extraction Plant)* ili kuwezesha gesi kutumika kwenye magari, viwandani na majumbani.

- Kuhakikisha tunazalisha 360MW za umeme kila mwaka ili kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na kumaliza tatizo la mgawo wa umeme.

- Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya usafirishaji na usambazaji wa umeme vijijini ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba wakati wote Serikali imekuwa ikitoa visingizio kuwa kiasi cha fedha kilichopo ni kidogo na hivyo kutegemea zaidi fedha za wahisani. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani imewasilisha vyanzo vya mapato ambavyo vinaweza kutumika kuongeza kiwango cha bajeti kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Baadhi ya misingi muhimu ya mapato ambayo tumeiwasilisha ni pamoja na:

- Kupunguza misamaha ya kodi ikiwemo kuondoa msamaha wa ushuru wa mafuta Kampuni za Madini, peke yake kutaongeza mapato ya shilingi bilioni 59.
- Kutoka Vyanzo vipya vya mapato tulivyovianisha; kwa upande wa sekta ya madini, kwa Kurekebisha Kodi Sekta ya Madini peke yake tunaweza kukusanya shilingi bilioni 240 katika mwaka wa fedha 2011/2012.
- Kupunguza fedha kwenye Wizara zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida yasiyokuwa ya lazima na kuelekeza fedha katika miradi ya maendeleo hususani ya umeme na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muktadha huo pamoja na Kanuni ya 106 ya Kanuni za Bunge kutenguliwa kuruhusu Sheria ya Fedha 2011 kupitishwa tarehe 22 Juni

2011; ni muhimu mjadala wa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini uhusishe pia kupitia Kitabu cha Kwanza cha Mapato *(Volume 1- Revenue Estimates)* ili kuongeza wigo wa mapato. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia maoni na mapendekezo yanayoendelea kutolewa na kuwasilisha marekebisho (*amendments*) ya Sheria ya Fedha ili kuongeza wigo wa mapato. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka kuwasilisha Bajeti ya Nyongeza *(Supplimentary Budget)* kwa ajili ya Wizara ya Nishati na Madini ili kuwa na Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi kwa mujibu wa Kanuni 107 kwa ajili ya miradi ya umeme na gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo sugu la mgawo wa umeme ambalo sasa limekomaa na kuwa janga la Taifa limetokana na ufisadi na udhaifu wa kiuongozi na kiutendaji ambao umeikabili sekta ya nishati nchini kuanzia Awamu ya Pili, likaongezeka katika Awamu ya Tatu na kukomaa katika Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ufisadi na udhaifu huo wa kiutendaji unajidhihirisha zaidi katika maamuzi mbalimbali yaliyofanyika Awamu ya Pili hususani 1990 mpaka 1995; Awamu ya Tatu hususani 1996 mpaka 2004 na Awamu ya Nne hususani 2006 mpaka 2011 kwenye maamuzi na mikataba mbalimbali mathalani kashfa ya *IPTL*, hasara ya mchakato wa ubinafsishaji wa *TANESCO*, uzembe wa *NetGroup Solution*, ufisadi wa Kiwira, kashfa ya Alstorm *Power Rentals*, sakata la *Songas*/*Pan African Energy,* ufisadi wa *Richmond*, madhara ya Dowans (ambayo sasa mitambo yake iko chini ya *Symbions* bila Serikali kueleza kashfa kuhusu mitambo hiyo zimekwisha baada ya umiliki kuhamia kwa kampuni ya Marekani na iwapo taratibu za zabuni zilifuatwa) ambapo mkazo haukuwekwa katika mipango ya muda mrefu ya kuondokana na tatizo la mgawo wa umeme nchini ambayo imetajwa bayana katika nyaraka mbalimbali za mipango ya Kiserikali. Pamoja na maamuzi ya Bunge la Tisa ya kuhusu masuala hayo bado Kambi ya Upinzani inataka hatua kamili kuchukuliwa kwa wahusika wa kashfa hizo kama walivyotajwa kwenye orodha ya mafisadi ili kujenga msingi wa kuepusha hali kama hiyo kujirudia katika uwekezaji unaondelea hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za upungufu wa umeme kwenye uchumi wa nchi na maisha ya wananchi kubwa sana. Taarifa za Serikali zinaonyesha kwamba Mamlaka ya Mapato inapoteza mapato ya Bilioni 840 kwa mwaka kutokana na mgawo wa umeme na ripoti za wadau wengine zimeeleza bayana upungufu wa ajira unaosababishwa na mgawo wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba katika Mkutano wa Pili wa Bunge, Kikao cha Sita, tarehe 15 Februari 2011, Waziri wa Nishati na Madini alitoa kauli Bungeni kuhusu mipango ya dharura ya Serikali kupunguza tatizo la mgawo wa umeme. Kati ya hatua ambazo zilielezwa ni ukodishaji wa mitambo ya dharura ya MW 260 na kuongeza matumizi katika mitambo ya *IPTL*. Kambi Rasmi ya Upinzani imefadhaishwa na taarifa iliyotolewa kwa umma na *TANESCO* wakati wa kuanza kwa mgawo wa umeme unaoendelea hivi sasa kuwa umechangiwa na mitambo ya *IPTL* kuzalisha chini ya kiwango kutokana na upungufu wa mafuta mazito *(HFO)* suala ambalo linatosha kwa Serikali kuwajibika kutokana na uzembe wenye kulitia hasara Taifa kwa sababu suala hili lilikuwa likijulikana kwa miezi mingi bila hatua stahili kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 1 Aprili 2011, Rais Jakaya Kikwete alitoa ahadi kupitia hotuba yake kwa Taifa kwamba mitambo ya MW 260 ingekodishwa na kuanza kufanya kazi mwezi Julai kukabiliana na mgawo wa umeme. Kambi ya Upinzani haijaridhika na visingizio ambavyo vimekuwa vikitolewa na Serikali kwa kutumia sababu za matatizo ya nje ya nchi kuelezea uzembe wa kiutendaji wa kushindwa kusimamia maamuzi ya ndani na inaitaka Wizara ya Nishati na Madini ieleze kwa uwazi na ukweli sababu za kuchelewa kwa mpango huo na hivyo kuongeza kwa kiwango kikubwa muda na kiwango cha mgawo wa umeme unaoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine mgawo wa umeme unaoendelea hivi sasa ni matokeo ya Serikali kushindwa kutekeleza kwa wakati mpango wa kuweka mitambo ya MW 100 Ubungo (Dar es salaam) na MW 60 Nyakato (Mwanza) ambayo iliwekwa kwenye mpango wa umeme wa mwaka 2009 ambao ulicheleweshwa na hatimaye wakati wa Bajeti ya mwaka fedha 2010/2011, Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Madini wote waliahidi kukamilisha uwekaji wa mitambo hiyo mapema mwaka 2011 suala ambalo halijakamilika mpaka hivi sasa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze sababu za kuchelewa kutekelezwa kwa mpango huo na hatua za uwajibikaji zilizochukuliwa kutokana na udhaifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa Taifa kuendelea kutegemea vyanzo ambavyo vilianzishwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza iliyoongozwa na Hayati Mwalimu Nyerere na Awamu zilizofuata sio tu kushindwa kuongeza kasi ya kuzalisha umeme bali pia kushindwa kukarabati mitambo hiyo na hivyo kuzalisha chini ya kiwango. Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2010 inaonyesha kuwa vituo vyetu vya umeme vinazalisha 3694.74 jigawati kwa saa yaani MW 421.8 sawa na asilimia 53.5 ya uwezo wa vituo hivyo MW 788.68. (Rejea Kielelezo cha Pili). Sababu zinazotolewa za uzalishaji kidogo ni uchakavu wa mitambo na ukame unaoliathiri Taifa. Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kuacha kuwalaghai wananchi kwa sababu zisizo za msingi kwani ikumbukwe kwamba zipo nchi zilizo katika hali ya jangwa lakini vituo vya kuzalisha umeme vina uwezo wa kuzalisha umeme wa wastani wa zaidi ya asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010, Serikali ilieleza kupitia Taarifa ya Hali ya Uchumi kwamba mahitaji ya umeme yalifikia MW 791 na Waziri wa Nishati na Madini akatoa matumaini hewa kwa wananchi kupitia bajeti ya mwaka 2010/2011 kuelekea uchaguzi kwa kutaja miradi ambayo jumla yake iliahidi uzalishaji wa MW 2,960. Hata hivyo, Serikali haikutenga fedha za kutosha kufanikisha mipango husika au walau kuweka mazingira wezeshi kwa taasisi zingine na sekta binafsi kwa ujumla kufanikisha utekelezaji hali ambayo imejirudia tena katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo ya mgawo wa umeme unaoendelea na kasi ndogo ya usambazaji wa umeme vijijini na majibu yaliyotolewa na Serikali kupitia kwa maswali ya papo kwa papo ya Waziri Mkuu tarehe 14 Julai 2011, yameonyesha kwamba Serikali halichukulii tatizo la umeme kwa udharura na uzito unaostahili. Hata majibu yaliyotolewa leo tarehe 15 Julai, 2011, nayo hayajaonyesha dhamira ya Serikali kushughulikia suala hili kwa dharura. Mpaka sasa kauli iliyotolewa

mtaani, nje ya Bunge na Waziri kueleza ni janga la dharura, Serikali haijatoa kauli Bungeni ya kutangaza umeme ni Janga la Taifa na kutaja hatua mahususi. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa hoja kwa Bunge kupitisha Azimio la kutangaza kwamba ukosefu wa nishati ni Janga la Taifa na kupitisha maamuzi ya hatua za haraka ambazo Serikali inapaswa kuzichukua kwa uwajibikaji wa pamoja. Bunge lichukue nafasi yake kwa niaba ya wananchi kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 (2) (3) ili kuisimamia Serikali kuondoa Janga hili la Taifa. Maazimio ya Bunge yatawezesha taarifa za mara kwa mara kutolewa Bungeni kuhusu hatua za utekelezaji na adhabu kutolewa kwa Mawaziri wa Serikali watakaozembea katika kuchukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani isipopata maelezo ya kueleweka na ya kina hapa Bungeni, tutalazimika kwenda kuunganisha nguvu ya umma kupitia maandamano ya wananchi kuishinikiza Serikali kuunda chombo cha pamoja cha kuchukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/2012-2015/2016) umelenga kuongeza uzalishaji wa umeme mpaka kufikia MW 2780 kwa kuongeza MW 1788 kwa mujibu wa miradi iliyotajwa kwenye mpango. Lengo hili ni dogo ukilinganisha na rasilimali ambazo zipo katika Taifa letu. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya mapitio ya mpango huo na kuongeza miradi mingine mikubwa ukiwemo wa *Stiggler Gorge* ambao una uwezo wa kuzalisha MW 2100 na kuingiza pia makadirio ya ujumla ya MW zinazotokana na miradi midogomidogo itakayoanzishwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kwamba hata lengo hili dogo la MW 1788, ambalo ni sawa na ongezeko la wastani wa MW 360 kila mwaka; halijaanza kutekelezwa kwa ukamilifu. Hii ni kwa sababu katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali imepanga katika bajeti kuongeza MW 160 ambazo kimsingi zilipaswa ziwe zimekamilika mwaka wa fedha 2010/2011. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza mradi mwingine wa MW 200 ambao unapaswa kukamilika katika mwaka huu wa fedha na rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kufanikisha mradi husika. Kambi Rasmi ya Upinzani, inasisitiza kwamba mradi wa Kiwira wa MW 200 awamu ya kwanza upewe kipaumbele maalum katika mwaka huu wa fedha ili kuweza kuziba pengo lililopo. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Kauli ya Serikali kuhusu pendekezo letu la kutenga fedha za ndani kutekeleza mradi wa njia za kusafirisha umeme huo kutoka Kiwira mpaka Mbeya katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza miradi iliyosalia kwa wakati, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Nishati na Madini kueleza mazingira wezeshi ambayo yanakusudiwa kuandaliwa ili miradi ifuatayo iweze kupata rasilimali kwa wakati na makubaliano kukamilishwa mapema. Dar es salaam-Kinyerezi (Gesi Asilia MW 240), Iringa-Mchuchuma na Ngaka (Makaa ya Mawe-300), Mtwara – Somanga Fungu (Gesi Asilia-MW 300) na Morogoro/Iringa- Ruhudji (Maji- MW 358).

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2010/2012 na makadirio ya bajeti ya mwaka

wa fedha 2011/2012 unaonyesha uwezo mdogo na kasi ndogo ya kufikisha umeme vijijini. Mathalani katika bajeti yake ya mwaka huu, Wizara imetenga Sh.Bilioni 1.1 kupeleka umeme katika vijijini vine (4) tu (Kijiji cha Magindi, Kijiji cha Mbwewe, Kijiji cha Mgwashi, Kijiji cha Kiwanga) kati ya Vijiji 12,176 vilivyosajiliwa kutokana na taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa hali hiyo, itachukua karibu miaka elfu mia mbili sawa na karne mbili kufikisha umeme katika vijiji vyote kama ambavyo tumetumia miaka 50 ya uhuru kuunganisha umeme kwa 14% tu kwenye Gridi ya Taifa. Kasi ndogo ya kusambaza umeme inadhihirishwa na idadi kubwa ya maombi ya wananchi wanaotaka kufungiwa umeme huku Shirika la Umeme *(TANESCO)* likiwajibu kuwa halina uwezo kwa sasa mpaka lipate miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali iliahidi kutekeleza Mradi wa *MCC (Millenium Challenge Cooperation)* wa kuvipatia umeme Vijiji 289 katika Mikoa sita (6). Mwanza (42), Tanga (129), Dodoma (45), Mbeya (18), Iringa (17) na Morogoro (38). Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa ya kina ya utekelezaji kutokana na malalamiko ya kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi kwa kulinganisha na kiwango cha fedha kilichotumika. Aidha, tathmini ifanyike kuhusu utekelezaji wa mradi husika ili kuwezesha umeme kufika Vijijini kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tulieleza kwenye Bajeti Mbadala 2011/2012 kwamba Kipaumbele chetu cha muhimu ni kuwezesha ukuaji wa sekta za uzalishaji na hasa ukuaji wa uchumi vijijini ili kuboresha kilimo, kuanzisha viwanda vidogovidogo vya kuongeza thamani za bidhaa, kuongeza ajira na kupunguza umaskini kwa wananchi walio wengi. Mkakati huu ambao utapunguza vijana wengi kukimbilia Mijini na kuliokoa Tanzania kuwa Taifa la wachuuzi unahitaji uwekezaji wa kutosha kwenye miundombinu ya Vijijini ikiwemo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga bilioni 150 kwa ajili ya Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* ili kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya uzalishaji wa umeme toka vyanzo vidogo vya maeneo mbalimbali pamoja na usambazaji wa umeme katika maeneo ya Vijijini. Chanzo cha nyongeza ikiwa ni fedha ambazo zinaendelea kutozwa hivi sasa kutokana na ongezeko katika kodi ya mafuta ya taa ambayo ikiendelea kwa mwaka mzima Serikali itakusanya kiasi kisichopungua shilingi bilioni 70. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba utekelezaji wa mradi kabambe wa kusambaza umeme katika Mikoa 16 unasuasua kutokana na Serikali kutokupeleka fedha kwa *REA* kwa mujibu wa bajeti zinazopitishwa na Serikali. Mpaka mwezi Mei mwaka 2011, Serikali ilikuwa imepeleka shilingi bilioni 23.3 tu kwa ajili ya malipo ya wakandarasi wakati ambapo fedha zinazohitajika ni shilingi bilioni 78.3. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, fedha ambazo hazikutolewa na Hazina ni shilingi bilioni 25.3 huku mwaka wa fedha 2010/2011 mpaka mwezi Mei zikiwa zimetolewa shilingi bilioni 13.6 tu ambazo ni sawa na chini ya robo (23%) ya bajeti iliyopangwa. Aidha, Kambi ya Upinzani inashauri Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* afanye ukaguzi wa ufanisi wa miradi inayoendelea kutekelezwa ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa mapema kuwezesha wananchi wa Vijijini kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani hairidhiki na kasi ya kuboresha utendaji wa Shirika la Umeme *(TANESCO)* na tunataka Serikali ieleze hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mpango Maalum wa Kurekebisha Hali ya Kifedha ya Shirika (2006-2010). Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni lini mapitio ya mikataba ambayo inaipa mzigo mkubwa wa kifedha *TANESCO* na kusababisha bei ya umeme kupanda itafanyiwa mapitio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imekuwa ikiidhamini *TANESCO* kupata mikopo ambayo kwa sehemu kubwa imekuwa ikitumika kwenye kukodi mitambo ya dharura; hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwe na udhibiti wa kutosha ili mikopo hiyo isigeuke kuwa mzigo kwa Taifa baadaye. Kwa upande mwingine, *TANESCO* imekuwa ikizidai Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ankara za umeme zinazofikia shilingi bilioni 76; hivyo Serikali inapaswa ionyeshe mfano kwa kufanya malipo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pamekuwepo malalamiko mbalimbali kuhusu mazingira ya kupitishwa kwa zabuni za ununuzi wa nguzo, transfoma na nyaya za umeme kwa kiwango kikubwa toka nje ya nchi huku viwanda vya ndani mathalani *TANALEC ABB*, *East African Cables* (hususani kampuni tanzu ya Tanzania *Cables*) na vingine vikididimia. Hali hii imesababisha pia kukwama kwa utekelezwaji wa miradi mbalimbali ya kusambaza umeme kutokana kwa kile kinachoelezwa kuwa ni vifaa kutokupatikana kwa wakati toka nje ya nchi. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuandaa mkakati wa kupunguza gharama za manunuzi na pia kupunguza kiwango cha uagizaji wa nguzo na vifaa vingine kutoka nje ili kutumia rasilimali za ndani ili kuchangia katika kukuza uzalishaji na uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani hairidhiki na hatua ambazo Serikali inachukua katika kupunguza gharama wanazototozwa wananchi za kuunganishiwa huduma ya umeme suala ambalo linapunguza kasi ya uunganishwaji wa umeme. Tumepokea malalamiko toka kwa wananchi wanaotakiwa na *TANESCO* kulipia nguzo na gharama nyingine za kuunganishwa umeme kwa kiasi kinachozidi milioni moja ambacho ni vigumu kwa wananchi wa kawaida kumudu. Hivyo, Serikali itoe kauli ya hatua inazopanga kuchukua ikiwemo za kubadili mfumo wa ankara ili kuruhusu kuingiza kwa mteja gharama hizo kidogokidogo katika kipindi hiki cha mpito. Aidha, *TANESCO* inahimizwa kutangaza kwa umma Kanuni za Sheria ya Umeme zilizotolewa kwenye gazeti la Serikali tarehe 4 Februari 2011 (GN 63) ambazo Kifungu cha Nne kinaeleza namna mteja atakavyofidiwa na kampuni ya usambazaji pale ambapo mteja anajigharamia mwenyewe kuvutiwa umeme ili fursa hiyo iweze kutumika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kasi ndogo ya usambazaji wa umeme, pamoja na kuondoa kodi katika vifaa vya umeme wa jua; Serikali ieleze hatua ilizochukua katika kuweka mazingira wezeshi kwa vifaa vya umeme wa dharura kuweza kupatikana kwa urahisi mathalani vifaa vya kuhifadhia umeme *(invetors)*. Aidha, Serikali iongeze kasi ya kutekeleza miradi ya kuhamasisha nishati mbadala hususani vijijini kwa kufanya marekebisho ya msingi katika Sheria ya Fedha na Sheria ya Umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gesi Asilia, nchi yetu imejaliwa utajiri wa gesi asilia katikati ya lindi la umasikini wa wananchi. Gesi asilia iligunduliwa nchini mwaka 1974, ikaanza kutumika kuzalisha umeme viwandani 2004 mpaka sasa inatumika kuzalisha MW 440 sawa na 60% ya matumizi yote ya umeme kila siku na inatumiwa na takribani viwanda 25 kwa uzalishaji. Kwa mujibu wa tafiti tuna zaidi ya 12 *tr cf* za gesi na uko uwezekano wa kugundua zaidi kutokana na utafutaji unaoendelea. Taifa letu lina fursa ya kuwa nchi kiongozi katika gesi Afrika na kushindana Kimataifa ikiwa tutaweka mstari wa mbele upeo, umakini na uadilifu katika sekta ya nishati kuepusha laana ya rasilimali. Hata hivyo, kwa mwelekeo wa ufisadi na udhaifu wa kiuongozi unaoendelea hivi sasa, rasilimali hii inaweza kuwa chanzo cha migogoro na kuhatarisha pia usalama wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara kupitia Dar es Salaam mpaka Tanga uwekwe kipaumbele katika Bajeti ya Nyongeza ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hivyo, Serikali itenge shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuchangia kwenye mradi wa Bomba la Gesi na kuchangia katika ujenzi wa Kiwanda cha Gesi kama sehemu ya mkakati wa kushughulikia upungufu wa nishati kama Janga la Taifa. Aidha, usiri katika majadiliano ya Mradi wa Bomba la Gesi ni muhimu ukaondolewa wakati nyaraka rasmi za Kiserikali zinaonyesha majadiliano yanayoendelea kati ya Tanzania na China kuhusu mradi husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inayo mawasiliano baina ya Watendaji Wakuu wa Kampuni ya *Orca Exploration Limited* na baadhi ya Maofisa wa Ikulu kutaka kupatiwa mradi husika; wakati kampuni yao tanzu ya *Pan African Energy (PAT)* imekuwa ikilalamikiwa kuhusu mradi mwingine wa gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Rasmi ya Upinzani inasisitiza mradi kwa kujenga kiwanda cha kujaza gesi kwenye mitungi (LPG) na mradi wa usambazaji wa gesi Dar es salaam pamoja na mradi wa matumizi ya gesi kwenye magari inayotekelezwa na Shirika la Petroli Nchini (TPDC) inapaswa kuongezewa rasilimali katika mwaka wa fedha 2011/2012. Hatua hii itapunguza pia matumizi ya umeme katika maeneo yenye kuweza kutumia gesi na kubakiza umeme mwingine utakaoweza kutumika kwenye maeneo ikiwemo ya viwandani yenye upungufu wa nishati mbadala. Uamuzi huu utawezesha pia kupunguza gharama za uzalishaji na za maisha zinazotokana na kupanda kwa bei ya mafuta ambayo pamoja na mizigo ya kodi na gharama zinazotokana na mfumo mbovu wa uingizaji inasababishwa pia na kupanda kwa bei katika soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuongeza mapato kwa Serikali na *TPDC,* Kambi Rasmi ya Upinzani inataka mrabaha wa asilimia 12 kwenye gesi uanze kutozwa kwa mujibu wa Sheria na isitishe mara moja utaratibu wa baadhi kuachiwa kutokulipa malipo husika kwa mujibu wa Sheria. Mapitio ya kitabu cha mapato yameonyesha kwamba wakati kwenye Kifungu cha 2001 cha madini kuna mrabaha hakuna kasma hiyo kwenye Kifungu 3001 kinachohusika na gesi na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujiandaa kitaaalum kama Taifa kwa mipango kabambe ya gesi, Serikali itekeleze mkakati wa kuwaambatanisha wataalam wazawa na makampuni makubwa yenye uzoefu wa sekta husika. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani

inataka Wizara ya Nishati na Madini iharakishe kukamilisha Mtaala wa Uhandisi wa Gesi na Mafuta ili fani hizo ziweze kutolewa kwenye Chuo cha Madini, Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuwa Serikali wakati wa kuhitimisha mjadala wa Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ilikubali pendekezo la kuanzisha Chuo Kikuu cha Mtwara. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Nishati na Madini kueleza maandalizi ambayo inakusudia kuyafanya kwa kushirikiana na mamlaka zingine husika ili kuwezesha uanzishwaji wa Chuo Kikuu hicho muhimu ambacho kitatoa mchango mkubwa kwa Taifa katika masuala ya gesi na bidhaa zitokanazo na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa Taifa letu limekuwa likitegemea mradi mkubwa wa SongoSongo kwa shughuli za uendelezaji, uzalishaji, usafishaji na usafirishaji ambao uko chini ya Kampuni ya Songas. Hata hivyo, kampuni ya Songas imeiajiri Kampuni ya *PanAfrican Energy Tanzania (PAT)*, ambayo ni mshirika wa *TPDC* katika uzalishaji, usambazaji na ugavi wa gesi asili. *PAT* imepewa pia Mradi wa Kusambaza Gesi Asili *(Ring Main and CNG Project)* Jijini Dar es Salaam. Taarifa mbalimbali zinaonyesha kuwa Kampuni ya *PAT* ililipwa kiasi kikubwa cha fedha zaidi ya gharama ilizoingia wakati wa kujenga mtandao wa usambazaji wa gesi asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, upo mwenendo usioridhisha wa kampuni hii ambao unapelekea upungufu wa gesi unaosababisha mgawo wa umeme, mfumo wa bei kubwa unaoongeza mzigo wa watumiaji na pia upotevu wa mapato ya Serikali. Hivi karibuni kampuni hii ilipewa na *TPDC* mabilioni ya fedha kinyume cha taratibu mpaka sasa Serikali inadai; ni muhimu Serikali ikawaeleza Watanzania ni viongozi gani walinufaika na malipo hayo na kiasi gani mpaka sasa hakijarejeshwa. Kutokana na uzito wa tuhuma na usiri katika mikataba; Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuundwe Kamati Teule ya Bunge itayofanya mapitio ya mikataba, sheria, kanuni pamoja na tuhuma za upungufu wa mgawo wa mapato na ufisadi kutokana na mauzo ya gesi kuanzia mwaka 2004 mpaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafuta. Taarifa za Hali ya Uchumi nchini zinaeleza kuwa mfumuko wa bei unaombatana na kupanda kwa gharama za maisha unazidi kuongezeka katika Taifa letu kutoka asilimia 4.2% Oktoba, 2010 mpaka 6.4% Aprili, 2011. Kama utaendelea kupanda hivi kwa ari, nguvu na kasi zaidi kwa miezi michache ijayo, utakuwa zaidi ya tarakimu moja. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba ukiondoa kupanda kwa bei ya chakula kunakutokana na kushuka kwa uzalishaji, chanzo kikuu cha hali hii ni ongezeko la bei ya nishati hususani mafuta, umeme na gesi hali ambayo isipodhibitiwa kwa mikakati makini, ni tishio kwa utulivu wa Taifa kiuchumi, kijamii na kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 Juni 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani iliishukuru Serikali kwa kutoa Kauli ya Kukubali Matakwa ya Umma na Pendekezo la Kambi Rasmi ya Upinzani la Kupunguza Kodi na Tozo kwenye bidhaa za mafuta ili kupunguza bei na mzigo mkubwa wa gharama za wananchi na kuonyesha mashaka kuhusu kiwango ambacho kitaondolewa na Serikali. Mashaka hayo yalidhihirishwa kwenye kupitishwa kwa Muswada wa Sheria ya Fedha tarehe 22 Juni 2011 ambapo

Serikali haikuonyesha kivitendo dhamira ya kupunguza kodi kwenye mafuta kwa kiwango cha kuwapunguzia ugumu wa maisha badala yake ikajikita kwenye kupunguza tatizo la uchakachuaji pekee ambalo limedumu kwa sababu ya Serikali kushindwa kusimamia utawala wa Sheria. Ushahidi ni kwamba katika marekebisho ya kodi, Serikali haikupunguza hata senti moja katika mzigo wa kodi kwenye petrol. Aidha, Serikali ilipunguza kodi ya dizeli kwa shilingi 99 tu huku ikiongeza kodi ya mafuta ya taa kwa shilingi 358. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilikuwa na dhamira ya kuwianisha bei ya mafuta ya taa na dizeli ili kupunguza tatizo la uchakachuaji lakini si kwa kuongeza kwa kiwango kikubwa kodi ya mafuta kama ilivyofanya Serikali. Matokeo ya uamuzi huu ni kwamba wakati bei ya petroli na dizeli zikibaki bila kupungua au zikipanda katika maeneo mengi ya nchi, bei ya mafuta ya taa imepanda kwa ari, nguvu na kasi zaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuleta Marekebisho ya Sheria ya Fedha ili kurekebisha hali hiyo na kueleza mkakati wa kweli wa kupunguza gharama za maisha kwa wananchi. Aidha, Serikali ijieleze Bungeni kutokana na udhaifu ulionyeshwa na taasisi zake ikiwemo Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA)* katika kusimamia bei elekezi na kupunguza bei za mafuta ambazo Serikali iliahidi Bungeni kuwa zingepungua kuanzia Julai 2011. Aidha, kama sehemu ya mchakato wa kupunguza gharama za mafuta kufuatilia mabadiliko ya kodi, tozo na mfumo wa uingizaji wa mafuta, Serikali ifanye mapitio ya mkataba baina ya *EWURA* na kampuni ya *Global Fluids International (T) Ltd* kuhusu ufanisi na gharama za kuweka vinasaba na kuleta vifaa maalum vya kupima ubora *(XRF). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoa kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na ukubwa wa kodi zinazotozwa na Serikali bei ya mafuta inakuwa juu kutokana na mfumo mzima wa uagizaji, usafirishaji, uingizaji na usambazaji. Mfumo uliopo sasa unanufaisha makampuni makubwa mengi yakiwa ya kigeni na wafanyabiashara wachache wa ndani pamoja na baadhi ya viongozi wa Serikali wasiokuwa waadilifu kwa kulinyonya Taifa na kuongeza gharama za maisha kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ndiyo iliyokwamisha kwa muda mrefu kuanza kwa Mfumo wa Uagizaji na Uingizaji wa Mafuta ya Pamoja *(Bulk Procurement System)* ili kupunguza gharama. Suala ambalo Julai 2010, Serikali ilisema liko katika hatua za mwisho na Julai 2011 mwaka mmoja baadaye bado Serikali imerudia kutumia lugha ileile. Aidha, Serikali iwajibike kwa kutoanzisha Hifadhi ya Mafuta mpaka hivi sasa wakati mwaka 2010 ilitoa kauli ya kufufua Kampuni ya Taifa ya Mafuta (COPEC). Kwa ujumla, kupanda kwa gharama ya mafuta kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na udhaifu wa Serikali wa kutochukua hatua zinazostahili kwa wakati. Kama imeshindwa kufufua Kampuni ya Taifa ya Mafuta, itekeleze pendekezo lililotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani la kuchukua hisa 100% katika Kampuni ya *BP* ambayo Serikali ina hisa na kuigeuza kuwa chombo cha kutimiza azma husika. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini ieleze hatua mahsusi za kulinda maslahi ya nchi katika Kampuni ya *TIPER* ambayo Serikali ina hisa 50% katika hatua za uingizaji na uhifadhi wa mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza tija na ufanisi wa *TPDC*, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo kuhusu hatua iliyofikiwa katika kutekeleza ushauri wa Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma wa kulifanyia marekebisho Shirika hilo ili kuwa na mamlaka itakayohusika na kutoa vibali kwenye leseni na kusimamia uchimbaji wa mafuta na gesi na kampuni itakayoshiriki katika biashara ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi rasmi ya Upizani Bungeni inaendelea kusikitishwa na uamuzi uliofanywa wa tarehe 22 Juni 2011 wa kuondoa msamaha wa kodi ya mafuta kwa kampuni za utafutaji ya mafuta na gesi. Uzoefu kutokana na misamaha ambayo imekuwa ikitolewa kwa makampuni ya madini unadhihirisha kwamba makampuni mengi yanatumia mwanya huo kuleta mafuta yasiyo na kodi na kuyaingiza kwenye soko la ndani la rejareja. Mathalani takwimimu zimedhihirisha kuwa kupitia misamaha iliyotolewa kwa makampuni matano tu ya madini ni karibu robo ya mafuta yote ya Dizeli yaliyoingia nchini na kampuni hizi zililipa dola laki mbili tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha hii haina maslahi ya Taifa na ni mianya mingine ya uhujumu uchumi; hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufikiria upya uamuzi huo na kuleta Marekebisho ya Sheria ya Fedha ili kuifuta misamaha hiyo kwa kuwa kampuni za utafutaji mafuta na gesi zinayo fursa kwa mujibu wa mikataba *(PSA)* kurejeshewa gharama zao mara baada ya mafuta kupatikana. Aidha, uamuzi huu uhusishe pia kampuni za madini bila kujali mikataba *(MDA)* kwa kuwa imethibitika kampuni hizi zote hutengeneza faida nono bila kulipa kodi inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini, kwa upande wa sekta ya madini mwaka 2010/2011, kumekuwa na ongezeko la uzalishaji huku mauzo ya nje ya madini yakiwa yameongezeka; dhahabu pekee ikifikia thamani ya dola 1,516.6. Hata hivyo, mchango kwenye mauzo ya nje umeendelea kuwa uleule wa asilimia 3.3 wa mwaka 2009/2010 na mchango kwenye Pato la Taifa ni asilimia 7.1 tu licha ya maelezo matamu ya Serikali kuwa mapato yameongezeka kutokana na kutungwa kwa Sheria Mpya ya Madini. Nyaraka ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inazo toka vyanzo vya Serikali yanaonyesha kwamba sehemu kubwa ya makampuni yenye mikataba yamekataa kukubaliana na Serikali. Hatua za haraka zinahitajika kulinusuru Taifa na hali hii ambapo utajiri wetu unaendelea kuondoka huku Watanzania wakiendelea kuwa masikini; hatua ambazo zitahusisha mwingiliano baina ya sekta ya madini na sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukirejea Kitabu cha Kwanza cha Mapato ya Serikali kwa mwaka 2011/2012, nchi yetu itakusanya shilingi bilioni 99.5 tu; hii ni aibu ya Taifa ukilinganisha na mauzo ambayo sekta hii inauza nje hasa kwa kuzingatia sehemu kubwa ya kampuni hizo hazilipi kodi inavyostahili. Kambi ya Rasmi ya Upinzani inaishauri Wizara ya Nishati na Madini kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kuboresha mfumo wa utoaji wa taarifa za malipo ya kodi kwa kampuni za madini ili malipo ya kila kampuni na mchangunuo wake yafahamike kwa umma badala ya mfumo wa sasa ambapo hurundikwa pamoja katika takwimu za Idara ya Walipa Kodi Wakubwa. Aidha, Wakala wa Madini *(TMAA)* ufanye ufuatiliaji maalum wa madini ya *Tanzanite*; ambapo bei katika soko iko kati ya dola 250-400 na zaidi kwa kwa karati wakati viwango

vinavyotumiwa na mamlaka husika kukadiria vidogo hali inayosababisha upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kuongeza kiwango cha mapato ikiwemo ya kodi kutokana na uchimbaji wa madini; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutekeleza mikakati ya kupenya kuta za umiliki na mitaji *(capital and ownership structures)* zilizojengwa kwa muda mrefu na makampuni ya kimataifa kwa kutumia mianya ya udhaifu wa kisheria na ushawishi wa kifisadi uliosababisha mikataba mibovu katika sekta ya madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza bayana hatua ambazo imechukua kufuatia Ripoti ya Tume/Kamati mbalimbali ambazo ziliundwa na Serikali kwa nyakati mbalimbali kwa kutumia fedha nyingi za walipa kodi lakini mapendekezo yake bado hayajatekelezwa kwa ukamilifu wake. Mathalani ripoti za karibuni za Kamati ya Masha na ile ya Bomani (2008) zilieleza bayana namna ambavyo makampuni makubwa ya madini yamekuwa yakitumia sehemu kubwa ya uwekazaji wao kama mkopo *(debt financing).* Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba makampuni hayo yamekuwa yakitumia mianya hiyo ya kisheria na kimikataba kuwezesha wamiliki na wanahisa kupata faida mapema kuliko kuweka mtaji kwa kuwa riba ya mikopo huondolewa katika kukokotoa kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali iwaeleze Watanzania ni trilioni ngapi za mapato tumezikosa kati ya mwaka 1995 mpaka 2010 katika kipindi cha miaka 15 ya kuachia mianya ya upotevu wa mapato kwa kuruhusu asilimia kubwa ya mikopo kuwa mitaji. Aidha, ni hatua gani zimechukuliwa kwa waliohusika kuliingiza Taifa katika mikataba mibovu iliyoruhusu makampuni hayo kujitangazia hasara kila mwaka huku yakipata faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia Kitabu cha Mapato, Serikali imeweka malengo madogo ya mapato kwa upande wa Wizara ya Nishati na Madini hali ambayo inadhihirisha kwamba inakusudia kuendelea kutoza mrabaha wa asilimia tatu (3%); tofauti na mapendekezo ya Kamati ya Bomani ya asilimia tano (5%) na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ambayo inaitaka Serikali kutoza asilimia nne (4%). Kwa upande mwingine, bado Serikali inaachia mianya kwa makampuni ya madini kukotoa mrabaha baada ya kuondoa gharama za usafiri *(net back value)* badala ya kutoa kwenye mahesabu ya ujumla *(gross)*. Hatua hizi zikichukuliwa zinaweza kuongeza mapato ya Serikali kufikia zaidi ya bilioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti hali hii ya ukwepaji kodi na kuongeza mapato ya Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Nishati na Madini ieleze hatua mahususi ambazo itazichukua kutekeleza mapendekezo yafuatayo yaliyotolewa kwenye Bajeti Mbadala: Kutunga Sheria ya kuhakikisha kwamba mikopo kwenye makampuni ya uwekezaji wa madini katika mahesabu ya kodi isizidi 70% ya mtaji; Kutunga Sheria kuhakikisha kwamba riba ya mikopo kwenye makampuni yanayohusiana haitaondolewa kwenye mahesabu ya kodi; Kufanya marekebisho ya sheria kuhakikisha kwamba kodi ya mtaji *(capital gains)* inatozwa katika mauziano ya makampuni yote ya madini ambayo mali zake au uwekezaji wake uko nchini hata kama mauziano hayo yamefanyika nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuendelea kuporomoka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Wizara ya Nishati na Madini kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Fedha katika kuweka mikakati na usimamizi wa kuhusisha sekta ya madini katika kuimarisha fedha yetu. Kwa kuwa mauzo ya madini yetu yanaongezeka huku shilingi ikishuka, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ieleze hatua ilizochukua za kushirikiana na Wizara ya Fedha katika kuwezesha Benki Kuu kutunza sehemu ya hifadhi yetu ya fedha za kigeni katika mfumo wa madini ya dhahabu. Wizara ya Nishati na Madini ishirikiane na Benki Kuu kuweka mfumo wa kununua dhahabu kwa wachimbaji wadogo na pia kutoza sehemu ya mrabaha wa dhahabu kwa ajili ya uhifadhi kama ilivyoshauriwa na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Taratibu hizi ziende sambamba na kusimamia mfumo wa kuhakikisha kwamba makampuni hayo yanatunza sehemu kubwa ya fedha za nje (walau 60%) kwenye benki za ndani ili kusaidia kudhibiti kuporomoka kwa shilingi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 imeipa majukumu muhimu *STAMICO* ya kuwa mwakilishi na msimamizi wa rasilimali za madini nchini kwa niaba ya Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani hairidhishwi na kasi ya kuliwezesha Shirika hili muhimu kutekeleza wajibu wake. Mwaka mmoja umepita bila ya Serikali kukamilisha mchakato wa marekebisho ya *STAMICO* kuweza kukidhi haja. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni kwa nini marekebisho ya Sheria Ndogo iliyoanzisha *STAMICO (Establishment order)* katika mwaka wa fedha 2010/2011 kama ilivyoahidiwa na kurejesha fedha za nyumba nne za *STAMICO* ambazo ziliuzwa na Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)?*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa msingi katika sekta ya madini ni kuhakikisha Watanzania wanaumiliki katika miradi mikubwa ya madini ama kupitia hisa za makampuni hayo kuwekwa katika soko la ndani *(DSE)* au kwa kampuni ya umma kushikilia sehemu kubwa ya uwekezaji hasa katika madini nyeti ikiwemo urani. Hivyo, ni lazima mtaji wa *STAMICO* uongezwe haraka kwa kurekebisha sheria na kanuni lakini pia kuongeza mtaji wa shirika. Ukiondoa albaki ya bilioni 5.25, Serikali ieleze hatua ambazo inakusudia kuongeza mtaji wa *STAMICO* katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba Wakala Jiolojia *(GST)* anaendelea na utekelezaji wa mradi wa kutambua maeneo ya madini. Kambi ya Upinzani inataka mradi huu uende sambamba na kufanya tathmini ya kina *(mineral appraisal)* ya madini yetu na kupendekeza mabadiliko ya kisheria na kimikataba ambayo yatawezesha utajiri wa madini yetu kutumika kama mtaji na dhamana katika hatua ya kuhakikisha Taifa letu linanufaika na rasilimali zake. Pia, ili kuongeza uwezo wa *GST* kutimiza wajibu wake, malipo yote yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo iliyounda Wakala husika *(Establishment Order)* yafanyike kwa mujibu wa taratibu kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012. Aidha, ramani na ripoti zinazotokana na utafiti na uchunguzi huo zitolewe kwa uangalifu ili kuhakikisha maslahi ya Taifa yanalindwa katika hatua zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikitishwa na maamuzi ya Serikali ya kuendelea na hatua za mbele katika utafutaji na uchimbaji wa madini ya urani bila kukamilisha

maandalizi ya kisera, kisheria, kikanuni na kitaasisi yanayohitajika, suala ambalo litaachia mianya ya upotevu wa mapato kwa Taifa kama ilivyokuwa kwenye madini mengine na pia itahatarisha usalama. Kambi ya Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kuhusu mauzo na mabadilishano ya umiliki yaliyofanyika baina ya kampuni ya Australia *(Mantra Resources)* na Kampuni ya Urusi ya *ARMZ Uranium Holding* kampuni tanzu ya Rosato. Mauzo hayo ambayo yanaelezwa Kimataifa kuwa yamefanyika kwa bei ya dola bilioni 1.16 ambayo ni zaidi ya trilioni mbili. Mauzo hayo yamehusisha kuhamishiana umiliki wa maeneo ya Tanzania Mkuju *River* (Mbamba Bay) na Bahi Kaskazini (Dodoma). Iwapo tungepata asilimia 30 tu ya mauzo hayo kama kodi, Taifa letu lingepata bilioni 600 ambayo ni fedha nyingi kuliko bajeti nzima ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka mzima. Izingatiwe kwamba eneo husika lina madini ya urani takribani paundi 108 sawa na asilimia 77 ya uchimbaji wote wa urani kwa mwaka jana. Hii ni aibu kwa Taifa linalokwenda nje kuomba huku ikiachia bwerere fursa za rasilimali za ndani na kufikia hatua hata ya Mbuga za Wanyama kuvamiwa kwa uchimbaji usiokuwa na tija ya moja kwa moja kwa Watanzania walio wengi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kusimamisha kwa muda taratibu zinazoendelea za uchimbaji wa urani mpaka maandalizi ya msingi yafanyike yatakayohakikisha umiliki, manufaa na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ahadi ya Serikali kumaliza migogoro katika sekta ya madini baina ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo pamoja na kuepusha migogoro ya leseni mathalani mgogoro wa wachimbaji wadogo eneo la Winza, Wilaya ya Mpwapwa ambao Serikali iliahidi Bungeni tarehe 9 Julai 2010 kuumaliza. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kauli ya Serikali kuhusu mgogoro huo kwa kuwa tayari wachimbaji wadogo wameanza kuhamishwa kwa nguvu toka maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia migogoro ya wafanyakazi katika makampuni ya madini. Wizara ya Nishati na Madini ilieleze Taifa hatua ilizochukua kushirikiana na Wizara nyingine husika kutatua malalamiko ya wafanyakazi wa *Tanzanite* kuhusu ongezeko la wafanyakazi wageni; Wafanyakazi walioachishwa katika kampuni ya Bulyankulu; kampuni ya Caspiani katika mgodi wa Mwadui, Shinyanga ambayo yapo Wizarani kwa muda mrefu bila hatua za msingi kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 25 Mei 1946 kampuni iitwayo *Alamasi Limited* ilipewa leseni ya kuchimba madini ya almasi Kaskazini ya Kijiji cha Luhumbo katika eneo la Mwadui, Wilaya ya Shinyanga. Leseni hiyo ijulikanayo kama Hati ya Uchimbaji *(Mining Lease)* Na. 224 ilitolewa chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 1929 iliyokuwa inatumika wakati huo na ilihusu eneo la ukubwa wa ekari 3007. Ili kuchimba almasi katika eneo hilo, *Alamasi Limited* ilipewa Hati Miliki ya Ardhi, Na. 5954. Muda wa leseni hiyo ulikuwa miaka ishirini na moja kuanzia tarehe 14 Juni 1944 na ulitakiwa kwisha tarehe 31 Mei 1965. Kwa mujibu wa leseni hiyo, *Alamasi Limited* ilitakiwa kulipa kodi ya ardhi ya senti hamsini kwa ekari moja kwa nusu ya mwaka 1944 iliyokuwa imebakia na baadaye kodi ilitakiwa kupanda hadi shilingi moja kwa ekari kwa mwaka 1945; shilingi moja na thumni kwa mwaka 1946; shilingi mbili kwa mwaka 1947 na baada ya hapo kodi ilitakiwa kuwa shilingi mbili na thumni kwa ekari kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilipofika Januari Mosi 1963, *Alamasi Limited* ilihamisha umiliki wa leseni hiyo kwa muda uliobakia kwa kampuni mpya iitwayo New Alamasi (1963) Limited. Uhamisho wa milki hiyo ulithibitishwa na Msajili wa Hati Msaidizi mnamo tarehe 23 Mei 1963 baada ya taratibu zote za kisheria za uhamisho kukamilika. Kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Hati Mkuu Msaidizi, Mary J. Mziray iliyotolewa tarehe 30 Januari 2006, milki ya leseni ya New Alamasi (1963) Limited ilikwisha muda wake tarehe 31 Mei 1965 na eneo la leseni hiyo lilirudishwa katika miliki ya Rais. Kwa sababu hiyo, kwa mujibu wa barua ya Kamishna wa Madini ya tarehe 27 Machi 2006, Leseni Na. 224 Hati Miliki Na. 5954 ilifutwa katika rejesta ya leseni za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya muda wa leseni Na. 224 kwisha na leseni yenyewe kufutwa katika rejesta ya leseni za madini, New Alamasi (1963) Limited iliendelea kuchimba madini ya almasi katika eneo hilo na kuyauza nchi za nje bila ya kuwa na leseni yoyote ile kwa miaka thelathini na tano! Aidha, kwa kipindi chote hicho, hakuna takwimu zozote zinazoonyesha kiasi cha almasi iliyochimbwa kinyume cha sheria na wala fedha zilizopatikana kutokana na mauzo ya almasi hiyo na zilikoenda fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika,  kwa hili, tunaitaka Serikali itoe Kauli Rasmi juu ya shughuli za New Alamasi Limited uhalali wa shughuli zake za uchimbaji almasi katika eneo la Luhumbo, kiasi cha almasi iliyochimbwa kwa kipindi chote tokea tarehe 1 Juni 1965 hadi tarehe 8 Mei 2000 na zilikoenda fedha zilizotokana na mauzo ya almasi hiyo! Aidha, Serikali ieleze ni kwa nini kampuni iliruhusiwa au iliachwa kuendesha shughuli za uchimbaji haramu wa almasi kwa miaka thelathini na tano na hatua ambazo zimechukuliwa au zinatarajiwa kuchukuliwa dhidi ya wale wote waliohusika na ukiukaji huu mkubwa wa sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 9 Mei 2000, Waziri wa Nishati na Madini wakati huo Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda aliipatia New Alamasi (1963) Limited leseni Na. ML. 71/2000 kwa ajili ya kuchimba almasi katika eneo hilohilo kwa kipindi cha miaka ishirini na tano. Kwa mujibu wa Kamishna wa Madini kwa barua yake ya tarehe 21 Machi 2006, tarehe 25 Mei 2005, "eneo lililokuwa na leseni hiyo liliunganishwa pamoja na maeneo mengine na kuwa leseni ya uchimbaji Na. SML 216/2005 ya Williamson Diamond Ltd. kwa maombi ya wamiliki wa leseni hiyo ya awali." Hii ina maana kwamba wamiliki wa New Alamasi (1963) Ltd. waliomba leseni yao iunganishwe na maeneo mengine na leseni hiyo mpya kukabidhiwa kampuni ya Williamson Diamond Ltd. ambayo imekuwa ikichimba almasi katika eneo la Mwadui kwa zaidi ya miaka sitini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shaka kubwa na ya kimsingi juu ya uhalali wa miliki hii mpya ya leseni ya uchimbaji almasi katika eneo la Luhumbo. Kwanza, kwa mujibu wa Kifungu cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998 iliyokuwa inatumika wakati huo, leseni pekee inayoweza kutolewa kisheria kwa ajili ya uchimbaji almasi ni Leseni ya Uchimbaji wa Mawe ya Vito *(Gemstone Mining Licence)*. Leseni ya Uchimbaji *(Mining Licence)* hutolewa tu kwa madini yasiyokuwa mawe ya vito au dhahabu. Hii ndio kusema

kwamba ML. 71/2000 isingeweza kuwa na leseni halali kwa uchimbaji wa almasi katika eneo la Luhumbo au eneo lingine lolote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa mujibu wa barua ya Kamishna wa Madini ya tarehe 27 Machi, 2006, ML. 71/2000 iligeuzwa na kuwa Leseni Maalum ya Uchimbaji *(Special Mining Licence)* Na. 216/2005 mnamo tarehe 25 Mei 2005. Hii ndio inayosemekana kuwa leseni ya Williamson Diamond Ltd. na ina ukubwa wa kilometa za mraba 29.73. Hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya 1998, madini ya almasi hayawezi kuchimbwa kihalali kwa kutumia Leseni Maalum ya Uchimbaji kwani leseni ya aina hii hutumika tu kwa uchimbaji wa madini ya vyuma *(metals)* kama vile dhahabu na sio kwa mawe ya vito.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, madai yaliyotolewa kwa maandishi na Kamishna wa Madini kwamba ML. 71/2000 iliunganishwa na leseni nyingine na kugeuzwa kuwa SML. 216/2005 yanaelekea kutokuwa na ukweli wowote. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa barua ya Kamishna wa Madini ya tarehe 19 Aprili 2008, leseni pekee ambayo Williamson Diamond Ltd. wanayo katika eneo la Mwadui ni Leseni ya Uchimbaji namba ML 02/92 iliyotolewa tarehe 20 Mei 1992 na aliyekuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Luteni Kanali Jakaya Mrisho Kikwete. Eneo la leseni hiyo ni kilometa za mraba 12.33. Kwa mujibu wa barua nyingine ya Kamishna wa Madini ya tarehe 21 Aprili 2008, ML 02/92 bado 'iko hai' na "haijaunganishwa na eneo au maeneo ya *mining licence* nyingine"! Miezi mitatu baadaye, Kamishna wa Madini alipigilia msumari wa mwisho katika madai haya alipoandika ifuatavyo mnamo tarehe 24 Julai 2008: "Hapakuwa na leseni ya uchimbaji madini ya Williamson Diamond Limited iliyotumika kuunganishwa na leseni namba ML 71/2000 na kuwa moja, *Special Mining Licence* SML 216/2005"! Ni wazi, kwa nyaraka hizi za Serikali, kwamba kuna jambo ambalo limefichwa kuhusiana na shughuli za uchimbaji almasi za New Alamasi (1963) Ltd. na uhalali wa shughuli hizo. Tunaitaka Serikali itoe kauli rasmi ya kufafanua mustakabali wa sasa wa eneo la iliyokuwa Hati ya Madini Na. 224. Tunaitaka Serikali ifafanue utaratibu wa kisheria ambao umeiruhusu *Williamson Diamond Ltd.* kuendelea kuchimba almasi katika eneo la Luhumbo wakati haina leseni halali katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nani hasa walikuwa wamiliki na Wakurugenzi wa *New Alamasi Ltd?* Kwa mujibu wa Waraka wa Msajili Msaidizi wa Makampuni katika Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* juu ya kampuni hiyo, wamiliki wa *New Alamasi Ltd.* walikuwa ni mabwana Sylvanus Mipawa aliyekuwa na hisa tatu na Phares Kitanzi Songo aliyekuwa na hisa na *Williamson Diamonds Ltd*. iliyokuwa na hisa 96! Aidha, kampuni hiyo ilikuwa na mtaji wa shilingi za Tanzania 2000 ikiwa na maana kwamba kila hisa ilikuwa na thamani ya shilingi ishirini tu! Waraka huu wa *BRELA* uliandikwa tarehe 22 Septemba, 2006. Kufuatana na Waraka huu, kuanzia mwaka 2002 *New Alamasi (1963) Ltd.* ilipeleka fomu za *Annual Returns* ambazo hazikukamilika. Aidha, "... wenye hisa wawili Sylvanus Mipawa na Phares Kitanzi Songo hawaonekani katika *returns* na maelezo na utaratibu wa kutoka katika kampuni haukuzingatiwa."

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa mujibu wa Waraka wa Msajili Msaidizi Mwandamizi wa Makampuni wa *BRELA* wa tarehe 13 Julai 2007, kati ya mwaka 1965 na

1970, Wakurugenzi wa kampuni hiyo walikuwa mabwana George Faulkner Hunt, Gabriel Jacobus Du Toit na Ian David Livingstone. Kati ya mwaka mwaka 1970 na 1972, Wakurugenzi walikuwa George Faulkner Hunt, Gabriel Jacobus Do Toit na Alexander John Prescott. Aidha, kati ya mwaka 1973 na mwaka 1983 watu waliopata kuwa Wakurugenzi wa kampuni hiyo ni pamoja na Samuel Lweyemamu Lwakatare, Robert Macbain Bisset, Ignace Herack Marandu, Jeremias Norbert Rweyemamu, William Henry Manning, John Robert Dawson Kiwia na Phares Kintazi Songo. Kwa mujibu wa Waraka wa *BRELA* wa Septemba 2006, Wakurugenzi wa Kampuni hii wanaonekana tofauti "... lakini utaratibu wa mabadiliko haukufuatwa." Tunaitaka Serikali itoe maelezo sahihi ya kuhusu wamiliki na Wakurugenzi wa Kampuni hii na kwa nini taratibu za kisheria hazijafuatwa kwa miaka mingi? Aidha, tunaitaka Serikali itoe maelezo iliwezekanaje kwa kampuni yenye mtaji wa shilingi 2000 imeweza kuchimba almasi kwa zaidi ya miaka arobaini?

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano kati ya *New Alamasi (1963) Ltd.* na *Williamson Diamonds Ltd.* umegubikwa na utata mkubwa. Hii ni kwa sababu mnamo tarehe 21 Machi, 2006, wakati akijibu swali la Mwandishi wa Habari wa Gazeti la Uhuru aliyetaka kujua uhusiano wa makampuni haya mawili, Kamishna wa Madini alidai kwamba yeye hatunzi kumbukumbu za makampuni hivyo "... siwezi kujua uhusiano wa *New Alamasi (1963) Ltd.* na *Williamson Diamonds Ltd.* na kama tulivyoona, taarifa zilizotolewa na *BRELA* Septemba 2006, zinaonyesha kwamba Williamson Diamonds Ltd. ina 96% ya hisa zote za *New Alamasi (1963) Ltd.* Hata hivyo, katika tarehe isiyojulikana ya mwaka 1992, *New Alamasi (1963) Ltd.* iliingia mkataba na *Williamson Diamonds Ltd.* ambao kwayo *New Alamasi (1963) Ltd.* ilifutwa kwa hiari na kuhamisha hisa na mali zake zote "zilizoko kwenye Hati ya Madini Na. 224, Hati Milki Na. 5954" kwa *Williamson Diamonds Ltd.* Mkataba huu unaelekea ulisainiwa na Sylvanus Mipawa kwa upande wa *New Alamasi* na watu watatu wasiojulikana kwa niaba ya *Williamson Diamonds Ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu kati ya *New Alamasi (1963) Ltd.* na *Williamson Diamonds Ltd.* umezua maswali mengi ambayo yanahitaji majibu kutoka kwa Serikali. Kwanza, mkataba huu unatamka kwamba kinachohamishwa ni Hati ya Madini Na. 224 na mali zilizoko kwenye eneo hilo ambavyo kama tulivyoonyesha ilikwisha muda wake tarehe 31 Mei 1965. Pili, mkataba huu unataja Hati Miliki ya Ardhi Na. 5954 ambayo nayo ilikwisha kurudi kwenye miliki ya Rais tangu mwaka 1965 leseni ya uchimbaji ilipokwisha muda wake!

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mkataba huu unaonyesha ulifanyika chini ya *Mining Ordinance* ya mwaka 1929 ambayo ilikwisha kufutwa tangu mwaka 1979 wakati Sheria ya Madini ya mwaka huo ilipotungwa! Nne, makubaliano haya yanataja makubaliano mengine ya kuhamisha haki za *New Alamasi (1963) Ltd.* yanayodaiwa kufanyika tarehe 31 Januari 1967, 17 Januari 1972 na 14 Februari 1978. Hata hivyo, hakuna ushahidi wowote wa makubaliano ya aina hiyo kati ya makampuni haya mawili kwa vipindi vilivyotajwa. Aidha, makubaliano yanadai kwamba *New Alamasi (1963) Ltd.* walipewa leseni ya eneo hilo tarehe 25 Mei 1965 kwa kipindi cha miaka kumi na sita kuanzia tarehe 13 Juni 1965 "ambayo ilisajiliwa na Idara ya Madini." Hata hivyo, kama

tulivyoona, Idara ya Madini yenyewe imekanusha madai hayo kwa kuonyesha kwamba Hati ya Madini Na. 224 ilikwisha muda wake tangu tarehe 31 Mei 1965!

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tulizonazo zinaonyesha kwamba mkataba kati ya *New Alamasi (1963) Ltd.* sio halali bali ni wa uligushiwa kwa lengo la kuwezesha uchimbaji wa almasi kuendelea katika eneo hilo kinyume cha sheria na ili kuendeleza wizi wa rasilimali ya nchi yetu ambao umeendelea kwa miaka zaidi ya arobaini! Tunaitaka Serikali itoe kauli rasmi na sahihi juu ya uhusiano huu kati ya makampuni haya mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika,  mamia ya wananchi waishio maeneo jirani na eneo la *New Almasi* wamekuwa wakinyanyaswa kwa miaka mingi na vyombo vya dola kama vile Polisi, Mahakama na vyombo vya utawala kwa madai kwamba ni wavamizi wa eneo la leseni ya *New Alamasi*. Watu kadhaa wameuawa na Askari Polisi na Mgambo baada ya kukutwa ndani ya eneo hilo. Wengi wengine wamepigwa na kuteswa katika vituo vya Polisi na wengine wengi wamefungwa kwa tuhuma za uongo za kuvamia eneo la Mgodi wa *New Almasi (1963) Ltd.* na kwa kutumia hati za kugushi za kuonyesha umiliki wa eneo hilo. Wote hawa walioteswa namna hiyo na/au ndugu zao wanastahili sio tu kuombwa msamaha kwa mateso ya miaka mingi na ya bure, bali pia wanastahili kulipwa fidia kwa madhara yote waliyoyapata katika muda huo. Tunaitaka Serikali itoe kauli kama iko tayari kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata haki zao kutokana na uovu waliotendewa na vyombo vya Serikali. Aidha, Serikali itoe taarifa rasmi juu ya hatua inazotarajia kuzichukua dhidi ya *Williamson Diamonds Ltd.* kwa kushiriki katika kugushi nyaraka za kuiwezesha kuchimba almasi kinyume cha sheria.

Mheshimimiwa Spika, hitimisho. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhitimisha kwa kusisitiza kwamba kwa sehemu kubwa matatizo katika sekta za nishati na madini yamechangiwa na sababu za kibinadamu za kutowajibika ipasavyo kisera, kimaamuzi, kiusimamizi na kiutendaji kwa viongozi wa Kiserikali kuanzia kwa Viongozi Wakuu wa nchi, Waziri mwenye dhamana na watendaji wengine na hivyo kusababisha ugumu wa maisha kwa wananchi na kuathiri uchumi wa nchi, wahusika wanapaswa kuwajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwajibikaji huo unapaswa kufuatiwa na hatua za haraka za kusimamia sera sahihi, uongozi makini na taasisi thabiti zenye kuelewa kwamba sekta ya nishati ni moyo wa Taifa na sekta ya madini ni mtaji wetu kwa sasa na kuchukua hatua kali dhidi ya ufisadi uliofanyika katika sekta husika, kufanya mapitio ya mikataba, kuharakisha utekelezaji wa mipango kwa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi na kwa ujumla kuwajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako lijadili makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa kuzingatia maoni tuliyoyatoa ya kuongeza bajeti ya Wizara husika; kupokea mapendekezo yatayopelekea kufanyika kwa mabadiliko katika Sheria ya Fedha na kupitisha Maazimio mahususi ikiwemo ya kukabiliana na upungufu wa nishati ambao sasa ni Janga la Taifa pamoja na kuhakikisha Taifa letu linanufaika na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha na naomba majibu ya kina kwa Serikali kuhusu ufisadi wa Kampuni ya Almasi kufanya Biashara ya Madini kwa zaidi ya miaka 35 bila leseni na madini yakitoroshwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnyika.

Katika orodha ya wachangiaji niliyonayo hapa ambayo ningeomba sasa mtu yeyote asiombe tena kuchangia, ambao hawajachangia ninao nane, waliochangia mara moja ninao 48, waliochangia mara mbili ninao 21, waliochangia mara tatu watatu. Kwa hiyo, naomba nisipate tena maombi mengine, msinitie majaribuni.

Moja kwa moja, sasa naomba mchangiaji wetu wa kwanza Mheshimiwa Anne Kilango Malecela achukue nafasi na kama muda unaobaki utamtosha Mheshimiwa Mbowe, nitaomba autumie.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa unyenyekevu mkubwa, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema yote anayolitendea Taifa langu la Tanzania na kwa mema makubwa aliyoitendea familia yangu. Pia niwashukuru Watanzania wenzangu na Waheshimiwa Wabunge, kwa maombi yenu, nikarejea nyumbani nikiwa na mume wangu akiwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kunukuu kwa faida ya Serikali na faida kwa Wabunge wote. Naomba nimnukuu Waziri Mkuu wa India wa zamani kwenye miaka ya 1960, alisema hivi:- *"There is nothing good in war except its end"*. Hakuna lolote jema katika vita isipokuwa mwisho wake. Waziri Mkuu huyo alikuwa anaitwa Nehru**,** alikuwa Mwanaharakati wa Haki za Binadamu. Alisema maneno haya wakati wa mwisho wa vita kati ya India na China.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taifa la watu walio makini, Taifa la Viongozi walio makini, Taifa la Wanasiasa walio makini, *the war is over!* Sasa Serikali na sisi Wabunge humu ndani kazi ni moja tu ya kuondoa matatizo ya Watanzania, stop! Wote tunashirikiana pamoja, Serikali na sisi tuliosimama kwenye majukwaa na wenzetu waliongia hapa kupitia Viti Maalum, kutafuta maendeleo ya Watanzania, mambo mengine yote tutakayofanya yatakuwa ni ya kitoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nimeisikiliza vizuri, nimeielewa. Unaweza ukawakuta mapacha wanne wamefanana sana, lakini ni sura tu, inapokuja kwenye mitazamo mapacha hawafanani. Sisi ni Wabunge, tunawakilisha wananchi, Serikali inatoka humuhumu ndani, lakini hatufanani katika mitazamo. Katika suala la umeme Serikali haifanani na sisi. Sisi tunalitazama tofauti, mimi nitatoa mtazamo wangu ni tofauti na mtazamo wa Serikali. Tatizo la umeme linaiabisha Taifa letu, tukubali jamani! Tatizo la umeme linawaumiza Watanzania mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa nawakosea haki Watanzania nikisema vinginevyo, nitakuwa nawakosea haki wapiga kura wangu waliosimama foleni kunipigia kura nikisema vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa Serikali ikachukua na mawazo yetu sisi, hili tatizo ni letu sote, siyo tatizo la Serikali peke yake, hili ni tatizo kubwa. Nimeangalia mlolongo wa miradi mingi sana, *it is a wrong approach*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kama mtu ambaye na mimi nina familia, ndani ya familia ukishika mambo mengi kwa wakati mmoja hufiki mwisho, unaenda unachukua miradi 10 au 20, unasema kuna mradi huu, hapana! Naomba na mimi mawazo yangu kama kiongozi niangalie tofauti, sisi ni mapacha lakini kwenye sura tu. Tuna milolongo mingi mno ya miradi, Serikali mtapapasapapasa mno hakuna mradi ambao mtaumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye ukurasa wa 63, mradi wa umeme wa *Stiegler's Gorge*, Bonde la Mto Rufiji lina ukubwa wa kilomita za mraba 177,000, liligunduliwa mwaka 1902, mwaka 1978 mpaka mwaka 1979 ulifanyika upembuzi yakinifu ndiyo ulileta taarifa hii, kwamba lile bonde lina uwezo wa kutoa megawati 2100, ni tangu mwaka 1978 mpaka 1979. Hii RUBADA ilitambuliwa na Bunge la Jamhuri hili miaka 35 iliyopita. Mradi huu ulifanyiwa upembuzi yakinifu na pesa zilitumika na *NORPLAN* ya Norway. Tatizo ambalo watu wengi tunalo, hata sisi binadamu mmojammoja tunalo, mtu kabla hajaingia kwenye mtihani anafeli. Sisi tunaogopa na tunaishia kwenye *introduction stage* kila wakati kwamba mradi huu unataka pesa nyingi, ni mgumu, twende tujaribu mradi mwingine, hapana! Serikali ni vema sasa tukaamua kujikita kwenye mradi mmoja mkubwa. *After all, feasibility study* ya watu wa Norway ilitoa kwa awamu nne, megawati 300 awamu ya kwanza, megawati 600 awamu ya pili, megawati 900 awamu ya tatu na megawati 300 kwa awamu ya nne, nimefanya *research* ya uhakika. Nakubali kwamba pesa ni nyingi lakini tungeenda awamu kwa awamu, pale RUBADA mpaka sasa tangu mwaka 1978 kama tusingeshindwa kwenye *introduction stage*, tungekuwa tumeshapita *growth stage* na sasa hivi tungekuwa kwenye *maturity* lakini bado tunapapasapapasa miradi mingi. Hao ni mapacha, hatufanani kwenye mitazamo. Serikali chagueni mradi mmoja mkubwa mtuambie Watanzania tufunge mikanda, tutaifunga, tumezoea! Watanzania baada ya vita vya Idd Amin waliambiwa na Baba wa Taifa fungeni mikanda wakaifunga, sina uhakika kama wameifungua mikanda hiyo. Sasa naiomba Serikali iwe na *approach* ya kukamata kitu kimoja kuliko kupapasa papasa.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina Jimbo, naomba nirudi kwenye Jimbo langu sasa, hapa kwenye Jimbo langu, naomba nikuambie Waziri mapema kwamba sitakuunga mkono kwenye hoja yako, naomba nikatae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu wanaishi milimani, Kata kumi za wananchi wangu wanaishi milimani. Milimani kuna miti mirefu, kuna migomba, ikifika saa kumi ni giza. Kwa nini wananchi wangu walazimishwe kuwa wateja wa tochi za nchi

hii? Wao kila wakati ni tochi tu, betri na redio, wananchi wangu pia wanataka kuangalia video kama ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu hawakuchagua kuishi kwenye milima, ni umaskini umewapeleka kule kutafuta ardhi lakini wanabaguliwa inapokuja kwenye suala la nishati ya umeme. Sijui kama Waziri tutaelewana, hapa hapatatosha, naomba nirudie hili neno kwamba hapatatosha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 24 Februari, *survey* ilifanyika, tarehe 26 Februari *estimate* alipelekewa Waziri na wakati *survey* ikifanyika mimi mwenyewe nilikuwa Tarafa ya Mambavunta, nimeshinda na watu wa *TANESCO*, naongea kwa simu mimi na Mheshimiwa Ngeleja atakaponijibu aseme kama mimi ni mwongo kama kweli anamjua Mungu. Akaniambia Mheshimiwa umeme tunaweka, njia ya kwanza Hedaru Mabirioni, ikaja Papa, Vunta Sekondari, Vunta Kijijini, Kidarini mpaka Njagu. Njia ya pili ikaanza kijiji cha Makasa, Kirangare, Idaruu mpaka Vugwama. Njia ya tatu ikaanza Mamba Miamba Road, Kijiji cha Bwambo, Mweteni mpaka Ntambwe. Hakuna kilichofanyika, nikiangalia kitabu chake, kwa kweli Waziri ni mtu wa ajabu sana! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha Waziri, katika jedwali, ukurasa 103, Mkoa wa Kilimanjaro, miradi kwa mpango kabambe kwa wasambazaji umeme wa *grid* vijijini. Mkoa wa Kilimanjaro, Same Mashariki, naomba Waziri Ngeleja aniombe radhi, vile vijiji vyote pale hakuna kijiji cha Same Mashariki vyote ni vya Same Magharibi. Waziri ananitupia mchanga kwenye macho yangu. Kilimanjaro akampa Mwanga, Kilimanjaro akampa Siha, mmeona?

Mheshimiwa Naibu Spika, twendeni ukurasa wa 98, kwake Sengerema amejipangia vijiji tisa, binadamu yeyote anaishi kwa hisia, huwezi kunikataza kuhisi mimi, tayari amejipendelea kama Waziri, tayari amependelea Mawaziri wenzake, anaandika Same Mashariki vijiji ni vya Mathayo ambaye ni rafiki yake, anampa wa vijiji vya Jimbo la Mwanga, anampa wa Vijiji vya Jimbo la Siha, Waziri hapatatosha, sikuachi leo. Waziri aniombe radhi na uwaombe radhi wananchi wangu siyo vijiji vyetu hivi, ni vijiji vya Same Magharibi na huwezi kuniambia umekosea katika kuandika, ulikuwa unanifunika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye viporo vya umeme, tangu Daniel Yona akiwa Mbunge Same Mashariki ameacha kijiji cha Kadando, mradi haujaisha, ameacha kijiji cha Kizerui mradi haujaisha, ameacha kijiji cha Ivuga mradi haujaisha. Mungu ni shahidi, nimekuwa naongea na Waziri Ngeleja kila siku, kila siku tunakunywa naye chai, ananilipia chai, sitaki ulinipie chai nataka umeme, nataka umeme kwa wananchi wangu, uwezo wa kulipia chai ninao na wewe unajua, lakini wananchi wangu unawaacha gizani, wananchi wako unawapelekea umeme vijiji tisa na vijiji vya wenzio, katika hili naapa kwa jina la Mungu siungi mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuzungumzie utandawazi, mimi nilipokuwa nasoma Digrii yangu ya Kwanza, nili-*specialize* kwenye utandawazi tu, someni vitabu vyote vya

*globalisation* vinasema utandawazi una faida zaidi kwa mataifa makubwa, mataifa tajiri, sisi maskini na mataifa madogo unatuumiza hasa kama hatuko makini. Tukiwa makini tutafaidi, tusipokuwa makini hatutafaidika na utandawazi, ndivyo vitabu vya *globalisation* vyote vinavyosema. Sisi hatupo makini. Sina uhakika kama tunafaidi madini yetu na ninakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe makini katika madini yetu, sina uhakika kama mmeacha kuzoa michanga kuipeleka nje ya nchi, nitaomba Waziri anijibu hilo, kama tutakuwa tunaendelea kuzoa michanga kuipeleka nje ya nchi ikachekechwe, basi sisi tuna-*fall* kwenye hawa Mataifa maskini ambao wanagandamizwa na *globalisation*. Hivi huyu unayempa mchanga akachekeche huko nje ya nchi, mmezaliwa tumbo moja au ni ndugu yako? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali mnafanya hivyo, naomba muache. Baba wa Taifa kabla hajaondoka alisema madini hayaozi, mkiona hamjawa tayari kiteknolojia yaacheni yapumzike, watoto wenu siku hizi wanasoma sana, watakapoweza watakuja kuchangia kufanya kazi hii. Mimi nina wasiwasi, tena machozi yanarudi tumboni, tunabanwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shemeji inatosha! *(Kicheko)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Kengele ya pili tayari?

**NAIBU SPIKA:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa Mbunge.

**WABUNGE FULANI:** Bado endelea! *(Kicheko)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba sitaunga mkono hoja mpaka Waziri utakapotoa majibu ya kuridhisha wananchi wangu na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge na mimi nilikuwa naangalia kitabu hiki, vijiji vya Naibu Spika kule Kongwa, hapatatosha hapa, Waziri hapa hapatatosha! *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba Mheshimiwa Eng. Hamad Masauni kama dakika hizi zinakutosha ujaribu kuzitumia Mbunge wetu wa Afrika, hautakuwepo tafadhali endelea.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona ni dakika tano tu zimebaki, nakuomba kwa heshima na taadhima niwe mchangiaji wa kwanza mara tu tutakaporejea baada ya *lunch*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ama unaumia dakika hizi ama hutapata nafasi kwa sababu wewe unasafiri, kama nilivyosema orodha ya wachangiaji ni kubwa sana na uko mbali kweli, nimekupa nafasi hii kama una kitu cha kusema kwa dakika hizi unaweza, kama hutaweza basi ni bahati mbaya.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipo hapa kuiponda mipango mizuri katika sekta ya nishati, mipango ambayo ipo katika *Master Plan* na *East African Master Plan*, sio tu kwa sababu mimi ni mdau wake, lakini naamini kabisa kwamba kama tutawekeza vya kutosha na mipango hii ikitekelezwa siyo mipango mibaya. Pia sipo hapa kutetea mipango ambayo ina upungufu mkubwa hasa katika sekta ya gesi, mipango ambayo imesababisha kwa kiasi fulani leo hii tufikie hapa tulipofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii utaona kwamba katika sekta ya gesi hasa katika eneo la usambazaji, eneo la ujenzi wa miundombinu lina upungufu mkubwa. Nitatoa mifano miwili nikiachilia mbali mfano ambao kila mmoja wetu anaufahamu, mfano wa mtambo wa *pipe* ya gesi ambayo inatoka Songosongo kuja Dar es Salaam, mpango ambao kwa sasa hivi tumeambiwa kwamba umezidiwa, *infrastructure* imezidiwa na haiwezi kukidhi haja hata kama tutaweka mitambo ya kutosha ya kuzalisha umeme. Mbaya zaidi kuna taarifa ambazo zilikuwa zinazungumzwa, kwamba eti chini ya *East African Community* kuna mpango wa kuandaa *feasibility study* na fedha zaidi ya dola za Kimarekani nusu milioni zimetengwa kwa ajili ya kuandaa *feasibility stu*dy ya ujenzi wa mradi kutoka Mtwara mpaka Mombasa. Inasikitisha sana, kwamba leo hii tunazungumzia ujenzi wenye gharama kubwa sana ambao utagharimu zaidi ya shilingi bilioni za kimarekani 771 ama zaidi ambao utachukua zaidi ya kilomita 600 kutoka Mtwara mpaka Tanga - Mombasa tunaacha kilomita 37 kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar! Tunapozungumzia matatizo ya Muungano na Kero za Muungano, mimi nashangaa kwamba leo hii ingefika wakati tukaangalia ni kwa kiasi gani gesi hii ukitaka kuunganisha kwenda Zanzibar kwa masafa mafupi ambapo gharama zake kwa harakaharaka haziwezi kuzidi hata dola za kimarekani 48 mpaka dola 50, ingeweza kusaidia sana kubadilisha hali ya uchumi kwa Zanzibar hasa kwa kutoa ajira na kusababisha vyanzo mbadala vya kuzalisha umeme na kupunguza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo naiona katika sekta hii ya gesi ni jinsi ambavyo kuna umuhimu sana wa kuharakisha Sheria ya Gesi (*specific legislation)* kwa sekta hii ya gesi. Hili ni jambo la muhimu sana. Kwa sababu muda wangu ni mfupi, nitaomba nizungumze kwa haraka sana, changamoto ya muundo mzima ya sekta ya nishati. Watu wengi wamekuwa wakizungumza kwamba Wizara ya Nishati ni kubwa sana, naomba nikubaliane nao katika hilo lakini tukiangalia *TANESCO* peke yake nafikiri kuna changamoto kubwa sana ya muundo. Muundo wa *TANESCO* ni mkubwa sana na ushahidi ni kwamba hata ukiangalia *key performance indicators* za *TANESCO* leo hii haziridhishi kabisa. Tukiangalia upotevu wa umeme ni asilimia 21 kutokana na *technical losses*, lakini pia ukipima idadi ya wafanyakazi, *ratio* ya *number of customers per employees* nayo hailingani na *best practice* ya mashirika mengine ya Dunia. Kwa hiyo, haya ni matatizo makubwa sana. Pia tukiachilia mbali matatizo mengi ya uwekezaji na historia ambayo siyo wakati wake, lengo la msingi na jambo la kuzingatia ni kwamba

Watanzania sasa hivi wanahitaji umeme. Kwa hiyo hili ni jambo ambalo tunatakiwa sote kwa pamoja kwa kauli moja kuhakikisha kwamba tunapata maelezo ya kina kutoka Serikalini ni jinsi gani umeme unapatikana kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa ushauri kwamba jambo la kwanza na la msingi ni lazima Shirika la Umeme liweze kujiendesha kibiashara, tuache siasa katika masuala yanayohusu mambo ya kitalaamu. Mustakabali wa nchi yetu katika sekta ya umeme ni jambo ambalo kwa kweli ni la muhimu sana. Leo *TANESCO* haiwezi kukopesheka kwa sababu inajiendesha kwa hasara kabisa. *TANESCO* leo bei yake ya umeme ni ya chini sana ukilinganisha na bei ya umeme katika nchi za Afrika Mashariki lakini ukiangalia madhara yanayopatikana kutokana na kukosekana kwa umeme ni kwamba *production cost* imeweza kuongezeka kwa wastani wa asilimia 15 mpaka 20. Nina imani kabisa kwamba madhara ambayo viwanda na mashirika makubwa ya Serikali yanapata kutokana na kutumia mafuta katika kuzalisha umeme ni makubwa sana, naamini kabisa madhara haya kama yataweza kutafsirika katika bei ya umeme ambayo pia itakuwa ni chini ukilinganisha na nchi nyingine basi mashirika haya na viwanda hivi vinaweza kukidhi kwa kiasi fulani. Kwa hiyo hili ni jambo la msingi sana. Wakati umefika kupeleka madaraka Mikoani, kulivunjavunja Shirika hili hasa kwa upande wa *generation na transmission,* ni lazima tuanzie kupeleka madaraka Mikoani, ili iwe ni *mode* ya kujipanga vizuri kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ya miradi ambayo imeainishwa ni pesa nyingi sana, kwa kipindi cha miaka mitano tunahitaji wastani wa megawati 2900 ambazo zinahitajika kwa ajili ya kuwekeza katika sekta hii. Kwa upande wa *transmission* vilevile, Serikali inashindwa pia kuchangia fedha asilimia 15 mpaka 20 ambayo inapaswa iwekeze kama mchango wake katika kuendeleza sekta ya umeme katika upande wa *transmission* na *distribution*. Fedha hii ni nyingi sana ukijumlisha kwa pamoja unaweza kukuta zaidi ya dola za kimarekani 700. Fedha hizi ni lazima tujiulize zitatoka wapi. Ndiyo maana mimi naomba niipongeze sana hotuba ya Waziri kwamba imeona yale mawazo ambayo tulikuwa tunapigia makelele siku zote kwamba wakati wa kuanzisha Mfuko wa Nishati sasa umefika. Ni muhimu sana Mfuko wa Umeme uanzishwe ili fedha ziwekezwe na vyanzo vya kuwekeza katika mfuko huu viainishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee kwa kutoa mifano miwili ama mitatu. Leo hii tuna mfuko wa *REA* ambao umefanya kazi kubwa sana kwa kipindi kifupi sana. Tunazungumzia ukuaji wa sekta ya umeme kwa asilimia 14 kwa kipindi kifupi. Hii ni kazi nzuri imefanyika ni kwa sababu Serikali ilikubali kuandaa Mfuko huu wa Umeme Vijijini na Sheria ikapitishwa hapa Bungeni na sasa hivi tunaona ukuaji mkubwa sana wa sekta ya umeme kwa upande wa vijijini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba sikupata muda wa kumalizia niliyotaka kuyazungumza ambayo ni mengi, lakini naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Ninyi ni Wabunge wetu wa Afrika, tunaamini kule kuna dakika chache zaidi, kwa hiyo, tuliamini unaweza ukafanya vizuri lakini siyo mbaya utapata muda wakati mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa mapumziko umekaribia lakini niseme jambo moja kabla ya kusitisha shughuli zetu. Wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Mnyika kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuna mahali ambapo alisema kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa hoja kwa Bunge kupitisha Azimio la kutangaza kwamba ukosefu wa nishati ni Janga la Taifa na kupitisha maamuzi na hatua za haraka ambazo Serikali inapaswa kuzichukua kwa uwajibikaji wa pamoja na kadhalika na kwamba Bunge lisipofanya hivyo, wao watafanya maandamano ya nchi nzima.

Waheshimiwa Wabunge, nataka kusema kwamba bahati mbaya sana aliposema kwamba Kambi hiyo inatoa hoja hakuna aliyeunga mkono hata ndani ya Kambi hiyo.

*(Hapa Wabunge walishangilia kwa vifijo na nderemo)*

**NAIBU SPIKA:** Nazungumza mambo ya utaratibu, ni lazima tufundishane, tuelewane, wakati wowote Mbunge anapotoa hoja ni lazima awe ame-*lobby* watu wa kumuunga mkono katika hoja yake vinginevyo inakuwa imepotea palepale. Kwa hiyo, hoja ile imeyeyuka. Kama hoja ile ingeungwa mkono wakati ule alipokuwa amesema, mimi ninge-*note* ambacho ningefanya sasa ni kulihoji Bunge kuhusu hoja ambayo imetolewa, kama Bunge mngeafiki hoja hiyo, maana yake ambacho ningefanya mimi sasa ni kuipeleka hoja hiyo kwenye Kamati inayohusika na jambo hilo, ili utaratibu uendelee na baadaye ije Bungeni kwa utaratibu unaofaa. Kwa hiyo, nilitaka kusema tu kwamba hoja hii imejichakachua yenyewe.

Kwa hatua hii tuliyofikia, naomba sasa kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni na mzungumzaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Freeman Mbowe atafuatiwa na Mheshimiwa Gaudence Kayombo na wengine watafuata.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Kama nilivyotangaza asubuhi kwamba Mheshimiwa Freeman Mbowe, atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza na atafuatiwa na Mheshimiwa Gaudence Kayombo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza mchana wa leo kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu ningependa kwanza kunukuu kauli ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Rais kule London mwaka 2007 wakati akizungumza na George Michel ambaye ni Mwakilishi Rasmi wa Rais Obama anayeshughulikia masuala ya Masharikі ya Kati. Naomba kunukuu, nukuu hii ilitoka katika Gazeti la *Daily News* la tarehe 22 mwezi 5 mwaka 2007 Mheshimiwa Rais alisema hivi *"We had an emergency crisis because of our dependency on hydro generation and we had three years of consecutive draught, the dams dried up, we went into a huge crisis however and fortunately there have been good rains this year and thanks God, we have natural gas and coal. The decision we have taken is to increase generation of power from natural gas and coal"*.

Nikiongeza kipengele kilichoongeza katika taarifa hiyo hiyo ya kunukuu alisema *"We have already started doing this and I am sure we will never face another energy crisis in the future" (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maneno ya mwaka 2007. Tunahitaji kutafakari kama nchi tatizo letu liko wapi? Kauli za Serikali zimekuwa nyingi, hii ni kauli ya Rais, zimetoka Kauli za Waziri Mkuu, zimetoka kauli za Mawaziri. Tatizo la msingi ni nini? Leo nchi ina giza, viwanda vimesimama, biashara zimesimama, tunaongeza umaskini wa Watanzania, tunafukuza wawekezaji, bado tunaona ni kama jambo la kawaida ambalo tunaweza tukalizungumza kisiasa. Kiongozi wa zamani wa China Mao Tse-Tung aliwahi kusema hivi *"Resolve the primary contradiction and the secondary contradiction will take off itself"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni nini *primary contradiction,* ni nini tatizo letu la msingi, ni uongozi. Tatizo letu la msingi siyo mvua, tatizo letu la msingi siyo gesi, tatizo letu la msingi siyo makaa ya mawe, tatizo letu la msingi siyo makampuni ya uwekezaji wa umeme, tatizo letu la msingi ni *planning* inayotokana na uongozi ambao tunao katika Taifa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo haya ni mengi sana. Lakini unapozungumza suala la tatizo la uongozi tumekuwa tunazungumza hapa, tuzungumze umeme kama janga la Taifa, hivi lakini kweli janga la Taifa ni umeme, ama janga la Taifa ni wale tuliowapa dhamana ya kutuongoza sisi kutuletea umeme na maendeleo ya nchi? Kwa hiyo, ambacho ningesema, janga la Taifa leo siyo umeme, janga la Taifa ni Chama cha Mapinduzi chenye Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majanga na *natural disasters*, majanga ni mambo ambayo yanaletwa kwa nguvu ambazo siyo za kibinadamu nguvu za Mungu *(Natural Disasters) shortage* ya umeme nchini kwetu leo ni majanga yaliyosababishwa na viongozi siyo majanga yaliyosababisha na Mungu. Ni *manmade crisis,* haya ni matatizo ambayo tumeletewa na watu tuliowapa dhamana tena maisha yetu, hatuwezi tukamsingizia Mungu, hatuwezi tukazungumzia *natural calamites,* tutazungumzia wale wenye mamlaka yale. Sasa wenzetu mnapokuwa Serikalini mnaona tatizo hili lina-*escalate*, linaendelea na mnalizungumza kama jambo la kawaida kabisa. Watanzania wakisema tunaandamana mnaona haiwezekani. Nawaambieni kwa utaratibu huu watu

wataandamana. Kwa utaratibu huu katika maandamano hayo hatujui kutatokea nini kwa sababu suala la kuwa janga la Taifa, suala la kuwa ni *crisis* halionekani kama kuna *seriousness*, mimi sioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilizungumza hapa katika swali kwa Waziri Mkuu, nikimshauri Waziri Mkuu hebu tuweke siasa pembeni katika jambo hili limeshakuwa tatizo, tuunde *high level task force* ambayo itasaidiana na wadau wengine wote, hilo ni tatizo la Kitaifa, tulishughulikie kama tatizo la Kitaifa. Anayezungumza umeme ni janga la Kitaifa ni Mheshimiwa Waziri William Ngeleja, Waziri Mkuu hajasema, Rais hajasema, hakuna hatua za dharura ambazo zinachukuliwa, ni utaratibu tu wa Kiserikali wa kuleta pendekezo kwamba sijui kuna kanuni zimekosewa, tubadilishe kanuni tuingize mitambo chakavu. Hiyo siyo *solution* kwa sababu tatizo la umeme nchini limekuwepo muda mrefu na tunalijua, tuliona linakuja. *We should have to plan ahead. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulizungumza hili hebu tuangalie tunakwama wapi? Tumesema katika kutengeneza kikosi kazi maalum hii kazi imewashinda Serikali. Mtakuwa hamkiri lakini sisi tunakiri na wananchi wanakiri, tunachokiona sisi ni giza, kama tuna giza na siku zote migao inafanyika, nilikuwa sijawahi kuona mgao wakati wa kipindi cha Bunge, Wabunge tukiwa Dodoma, safari hii Wabunge tunalala kwenye giza na tunataka na nyie Mawaziri, sijui katika nyumba zenu mna jenereta, mlale kwenye giza halafu muone soo lake likoje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninalolizungumza hapa ni kwamba, kama hawa wameshindwa, Rais amesema imeshindikana, Waziri Mkuu, amesema imeshindikana, Ilani yenu ya CCM imesema imeshindikana, mnatutajia miradi hapa, miradi ambayo siyo chimbuko la fikra za ndani, miradi ambayo ni chimbuko la fikra za wawekezaji. Leo ikija kampuni inaitwa *Freeman and Mbowe MacDonald Limited* ikasema imetoka Marekani inataka kuwekeza dola laki mbili mnaiandika kwenye mpango. Tayari anakuja Freeman Mbowe kutoka Marekani anakuja kuwekeza dola laki mbili kwa ajili ya kufufua umeme, mtaingiza kwenye mpango. Hii mipango yote inafeli kwa sababu wanaoleta mipango ile siyo ninyi, mipango ile inaletwa na *Multinationals* wale wana-*interest* mbalimbali, wakitaka kuja Tanzania wanawaletea mpango, ninyi mna-*approve*, wakiona mnaleta mambo ya Uswahili wanahama wanakwenda Pakistan, mnabaki na mpango kwenye makaratasi halafu mnatuambia ni mdororo wa uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna uwezo gani na *capacity* gani? Tunasema kuna watu wa *private sector*, hawa watu wanaumia, hatuzungumzii umeme wa kuwaka nyumbani, kuna *investment* zinakufa, makampuni yanafilisika kwa sababu wanashindwa kuendesha *investment* zao kama walivyo *project*. Hii ni nchi mbaya sana katika uwekezaji kwa sababu *you can't project* kwamba mwaka ujao hali ya nchi itakuwaje, huwezi uka-*project*. Tunapozungumzia mpango wa uchumi wa miaka mitano, tunazungumzia *projection growth* ya nchi, yaani ukuaji wa uchumi wa asilimia 7.2. Lakini juzi *IMF* wame- *release* taarifa wanasema kwamba katika mwaka huu wa fedha uchumi wa Tanzania utapungua ukuaji wake utarudi kutoka 7.2 na kufikia asilimia 6.0. Ina maana tayari tumeshakuwa *off guarded*. Sasa tunasemaje, tuwasaidieje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi mmeshindwa, sisi wanasiasa tutatia *pressure* na tutaandamana. Hakuna cha hoja ya kuomba Bunge, hakuna hoja ya kuomba nani. Lakini sisi tunachosema hoja yetu ya msingi hapa ni nini? Tunataka tuunde *(high level task force)* kikosi kazi kiwe na watu kutoka *private sector*. *Private sector* kuna watu kama *TCIA*, kuna watu katika *financial,* ni *bank in industry,* hawa watu wanajua mikakati ya haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikosi hiki kifanya kazi kwa miezi sita kuondoa hili tatizo kwa sababu ninyi hamna tena *legitimacy*, hamna *moral authority* ya ku-*deal* na suala la umeme mmeshashindwa kwa miaka zaidi ya sita, leo hamuwezi kufanya miujiza yoyote. Tunasema tunahitaji watu wa kuja kuwasaidia kazi hii, watoke katika sekta mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumependekeza wawepo watalaam wa Serikali, wawepo watu kutoka kwenye *Civil Society,* wawepo watu kutoka hata ndani ya Bunge ili kama ni ku-*harmonize* masuala ya sheria, masuala ya kanuni, masuala ya uagizaji mambo haya yajulikane, katika kipindi cha miezi sita tuliondoe Taifa kwenye aibu hii. Tuna aibu ambayo haina mfano wake na ninyi ndio mnatuletea aibu katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ukubwa wa Wizara. Hii Wizara tunapozungumza masuala ya *energy* si mchezo. Mawaziri wote maskini ya Mungu nawaonea huruma, tumewarundikia mzigo, wamekuwa pale wanyonge tu hawana *solution*, kwa sababu Wizara imezidiwa kazi. Ukizungumza madini unazungumza dhahabu, almasi, lubi, *Uranium*, *coal* sijui unazungumza madini gani. Mafuta wao, biashara ya mafuta, *exploration* ya mafuta mambo ya *gas* wao. Tukizungumzia umeme wao. Hawa watu siyo miujiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapendekeza *very strong* kwamba, utaratibu wa kuigawa Wizara hii *into two* ufanyike na ufanyike haraka. Tuwe na Wizara mbili, moja ikiwa ni *Ministry of Mines and Mineral Resources* na ya pili ikiwa ni *Ministry of Energy and Petroleum Resources*. Tutenge haya masuala mawili, hapa amekiri Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta ya Nishati na Madini, Mwenyekiti anasema kwamba kwa kipindi chote hiki tangu tumeingia Bungeni anashughulikia masuala ya umeme hajaweza kushughulikia masuala ya madini. Sasa mnataka ushuhuda gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikiliza kauli iliyotolewa hapa leo na Serikali na ukisikiliza hapa leo kauli iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta huwezi, kuamini hawa watu wanaozungumza wanatoka Chama kimoja. Mnazungumza kama Chama ambacho kiko *divided* halafu mnatuletea aibu katika Taifa hapa. Kama ya Kisekta inatoa mapendekezo tofauti, mazuri sana na namsemea ndugu yangu, rafiki yangu January Makamba anangoja nini CCM? Aje huku tufanye kazi hii. Namkaribisha yeye na ile Kamati yake yote ihamie huku tufanye kazi ya kuikomboa Taifa hili kwa sababu inaonekana sijui hata kama kweli ni Mjumbe wa Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi, aje huku tusaidiane kazi. Maana yake mnaongea vitu viwili ambavyo vinagongana. Sisi tunawashangaa ninyi, ninyi ni Serikali you *are supposed to be united,* mnagombana tu,

tunavuana magamba, nchi inayoingia kwenye matatizo hatushughulikii *crisis* za msingi, tunabembelezana hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani kidogo unajua hakuna njia nyingine ya kueleza *frustration* zangu zaidi ya hii. Makampuni ya Kimataifa haya, haya ni *multinational* ni *big corporate*. Haya Mashirika makubwa ya Kimataifa, Waheshimiwa Wabunge wenzangu yana watalaam wa hali ya juu, ni lazima tuondoe *politics* katika *management* ya *economics* katika kudhibiti na kusimamia uchumi wa nchi hii, tuondoe masuala ya siasa na tuingize masuala ya utaalam, ndio sababu anapewa kwa mfano nafasi kumi za kuteua wataalam wamsaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua sana Waheshimiwa Mawaziri wetu wana elimu yao nzuri tu, sipingi kuhusu utalaam wao wana uwezo wao mzuri. Lakini hivi kweli, nazungumzia *capacity* ya Wizara, inaweza kukabiliana na makampuni makubwa kama haya ya madini au makampuni makubwa yanayo-*deal* na *gas* na mafuta haya ni ma-*multinationals*, wana-*invest billions of dollars*, wana *stock* wana hisa katika masoko ya hisa za Kimataifa. Ukienda *New York*, Hong Kong, *South Africa*, Toronto, *London stock exchange* wanakuja hapa Dar es Salaam, wanakuja kuongea na wataalam wetu katika Serikali jamani ni hivi! Nimesema natambua sana uwezo mzuri wa Waheshimiwa Mawaziri wetu hawa na elimu yao na naiheshimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema kuna maeneo mengine ya uchumi tunahitaji *extra skills*, ujuzi wa ziada kidogo. Tunasema katika *private sector* wala tusijilazimishe Waheshimiwa Wabunge kwamba eti sisi humu ndio tuna akili pekee ya kuongoza nchi hii. Huko nje wako Watanzania wengi kwenye *private sector* kwenye *Civil Society* ambao wana ujuzi, wana *exposure*, wana *experience*. Kuna Mashirika makubwa haya ya Kimataifa yanakuja Tanzania yanachukua watalaam ma-*CO* kutoka katika Jamii ya Watanzania. Wapo Watanzania, lakini tunawapataje, Rais angetumia nafasi zake hizo akawaingiza hawa watu kwenye mfumo wa siasa wakatusaidia kusimamia zile sekta za muhimu katika uchumi tukaokoa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba kila mwanasiasa akishakuwa CHADEMA ama akishakuwa CCM au *CUF*, *TLP*, *NCCR* ana uwezo wa kuwa Waziri wa Fedha, si kweli. Kuna watu ambao wana *special skills* na ni lazima tuanze kujua mchango wa Watanzania wenzetu, tuwaingize kwenye *political mainstream* watusaidie katika masuala ya msingi. Akina Mheshimiwa Ngeleja waende kwenye Wizara ya Sheria na Katiba, ndugu yangu Mheshimiwa Kigoma Malima aende *Planning*. Lakini haya masuala tunayozungumza, ni masuala *serious*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *solution* nini, nimeshasema Rais afanye nini, lakini hii *task force* niliyokuwa naipendekeza ifanye kazi miezi sita kwa sababu *I can assure* na *I stands to be corrected six months down the line* tutakuwa tuna shida ya umeme kama tutaiachia Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi ituletee *solution*. Wame-*fell* mara ya kwanza, wame-*fell* mara ya pili, *they have been felling us forever* na hatuwezi kuendelea kuwaachia na kama hatutachukua hatua na sisi tuwasaidie hii kazi mbadilike maana mnatuletea adha na aibu ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia makampuni makubwa, ukisoma taarifa mbalimbali na makampuni haya ni mambo ya aibu, hata mengine hamyajui. Ngoja niwape mfano, kuna kampuni inaitwa *ORICA* mimi sijui ni Wabunge wangapi, Mawaziri wangapi wanajua kuna Kampuni inaitwa *ORICA*. Ukiangalia biashara ya *gas* katika Taifa *complexity* ya haya mashirika *structure* zake zilivyo, *network* zake zilivyo, zinahitaji *special skills* kuzikabili. Asilimia 98 ya Mashirika ya Kimataifa yanayofanya kazi kupitia Wizara ya Madini na Nishati ni Makampuni makubwa yenye fedha, yenye *skills*, yenye *network* na ni watu ambao ni *lobbyist* wakubwa mno na wanaajiri watu maalum kwa ajili ya ku-*lob* hawa watu, *ORICA* wanaandika katika ripoti yao ya mwaka, hii ni *their annual report advancing growth ORICA 2011 interim report.* Wanazungumza jinsi wanavyoweza kukwepa kodi ya Tanzania, hawa katika kabrasha hili wame-*declare 13.3 UD million* zinakuwepo katika mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, UTARATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sikutaka kumwingilia Mheshimiwa Freeman Mbowe, nilitaka kwanza amalize hotuba yake yote. Natumia Kanuni ya 64. Najua rafiki yangu alikuwa anapiga siasa hapa, lakini katika kupiga siasa kajisahau kidogo amepitiliza. Nataka nimpe taarifa kwamba Kamati yako Tukufu ya Bunge hili inayoshughulikia masuala ya Nishati na Madini inayoongozwa na Mheshimiwa January Makamba, siyo Kamati ya CCM. Kwa hiyo, kusema kwamba Kamati yote ya Nishati na Madini ihame iende upande ule ni kulikosea Bunge hili, kwa sababu hii ni Kamati ya Bunge hili. January Makamba anafanya kazi na Mheshimiwa John Mnyika, ametajwa hapa kama Mjumbe, Mheshimiwa John Mnyika siyo Mwanachama wa CCM, kwa hiyo, nilitaka tu kumpa taarifa hiyo.

Kuhusu utaratibu ambao umevunjwa lakini pia amesema Serikali hii haina *legitimacy* nataka kumkumbusha tu, tulishindana katika kura, Chama cha Mapinduzi, kikashinda na tukapata ushindi mnono, tukawashinda, hakuna jambo kama hilo. Kwa hiyo, tumechaguliwa tutaongoza nchi. Nataka tu nimpe utaratibu ambao amevunja Mheshimiwa Freeman Mbowe sikutaka kumzuia, akipiga hiyo siasa yake, siasa yake tunaielewa lakini ukweli ndio huu. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE**: Taarifa si inabidi ijibiwe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Siyo taarifa ni kuhusu utaratibu.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema nyingi mpaka sasa na nchi yetu pia inakaribia kufika miaka 50 ya uhuru. Lakini pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Mbinga Mashariki, kwa kura nyingi za kishindo walizonipa mimi, Rais na Madiwani wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kuwashukuru wakati wa uchaguzi tuliwaomba wenzetu wa Madhehebu mbalimbali waombee nchi yetu, tupite vizuri katika uchaguzi, kazi hii wameifanya. Kwa hiyo, nawashukuru wale wote waliokuwa wanaombea nchi yetu na wanaendelea kuiombea hata sasa natambua huduma ya *Manna* ipo hapa Dodoma wakiombea nchi yetu. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile pongezi zangu nataka kuzipeleka kwa wananchi wa Mbinga hasa ndugu yetu Andoya ambaye anashughulika na umeme mdogo pale Mbinga Mjini ingawaje bado hajafanikiwa. Lakini pia Kanisa Katoliki ambalo limejenga mtambo wa umeme pale kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Ujerumani katika Kijiji cha Kindimba, kazi yao ni nzuri sana na mimi kama Mbunge naipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji ambaye amemaliza sasa hivi, amezungumza maneno mazuri kwa kiwango fulani, isipokuwa ningependa kuzungumza machache, hapo nyuma ilionekana kama Serikali ni kubwa sana na Mheshimiwa Rais alisikia akapunguza Wizara, sasa linatokea pendekezo la kuongeza tena Wizara zingine na hicho ndicho chama kinachoomba ridhaa ya kuongoza nchi hii, kilisema Serikali kubwa, ikapunguzwa, sasa kinasema iongezwe tena, sijui kama chama kama hiki kinaweza kikapata ridhaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuhusu migomo, suala hili la umeme ni letu sote na msemaji aliyepita amesema hajui kama akihamasisha migomo itatokea nini baadaye. Sasa kwa nini kwenda kwenye *option* ya kitu ambacho madhara yake huwezi kuyajua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Viongozi wa vyama ambao wamefika Jimbo la Mbinga Mashariki na kusema kwenye mradi ule wa makaa ya mawe pale kwamba hapa nyie mnauzwa, hawa wazungu watakuja, watachukua nchi, watachukua kila kitu. Huo mradi huo katika ukombozi wa kuleta umeme katika nchi yetu na baadhi ya viongozi wa vyama wanafika pale wanakwenda kubeza shughuli kama hizi, nafikiri tuna haja ya kujiuliza kama kweli tunapozungumza hapa juu ya matatizo ya nchi yetu ya kiuchumi, kweli tunayo nia ya dhati ya kutatua hayo matatizo? Tuje hapa tuwe na nia ya dhati ya kusaidia nchi yetu na ya kusaidia Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko pendekezo la kuunda *task force*, hii *task force* itaratibiwa na nani kama Serikali unaiona kwamba haifai? Haiwezi ku-*operate* tu hivi hivi, lazima Serikali iwepo na ndiyo *task force* iwepo, kwa hiyo, nafikiri maoni mengine yaliyozungumzwa mengi ni mazuri lakini yanaharibiwa kwa vitu kama hivi na hivi unaweza kujipunguzia *marks* kwa sababu namheshimu sana Mheshimiwa Mbowe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la umeme linachangiwa sana na ubaguzi, upande mmoja wa nchi umewekezwa sana katika masuala ya umeme na upande mwingine hakuna umeme. Hata sasa hapa Bungeni tunapolumbana juu ya umeme baadhi ya Mikoa wala haielewi kwa nini tunazungumza habari ya umeme kwa sababu hawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Ruvuma kwa mfano, ni tofauti sana na kule anakotoka Mheshimiwa Mbowe, hakuna umeme, hakuna kijiji chenye umeme, umeme uko pale Songea Mjini, uko Mbinga Mjini, uko Tunduru Mjini na uko kidogo Namtumbo pale, lakini ukisoma makaratasi haya, kitabu cha Mheshimiwa Waziri umeme umekwenda vijijini katika sehemu nyingi sana, sehemu hizi za Mikoa ya Kusini hakuna kitu, lakini bahati nzuri wanasema Mungu si Athumani, ndiko ameweka rasilimali kubwa ya umeme katika Mikoa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikoa hiyo ndiyo ameweka gesi, makaa ya mawe, kaweka na upepo na maji, sasa kwa nini hatutaki kutumia? Ukisoma kitabu hiki ukurasa ule wa 19 ule *Stigler's Gorge megawatts* 2,100, kwa nini tushughulikie kale kamradi ka *megawatts* 165, 230 au 60? Kwa nini miradi yote ya nchi hii iko huko Kihansi, Nyumba ya Mungu, Hale, Kidatu, yote ya maji na tukaacha mambo haya yote. Mwaka 2006 nilizungumza hapa juu ya makaa ya mawe yaliyokuwa yanaungua pale Ngaka kwenye kijiji chetu, Wilayani Mbinga, nilipata ugumu sana, lakini hatimaye nashukuru Serikali ilisikia na ikaenda kuzima ule moto. Lakini mpaka leo yale makaa ya mawe ambayo yako chini ya *NDC* na *NDC* inashirikiana na wawekezaji kutoka Australia wameunda kampuni inaitwa *TANCOAL*, mpaka sasa wamesema watatengeneza *megawatts* 400. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 19 Mei, 2011 nilipokuwa naongea na wale wawekezaji walisema wamebadilisha mpango, wanataka kutengeneza *megawatts* 100 pale Ngaka na *megawatts* 200 watakwenda kutengeneza kule Kyela ili wapeleke Malawi. Hivi ni kwa nini Serikali yetu isiipe nguvu ya kifedha *NDC* ili iweze kuwa na maamuzi makubwa juu ya mradi huu, maana yake mradi huu kila wakibadilisha Kiongozi Mkuu wa Kampuni ile maamuzi ya nyuma yote hayafuatwi tena. Kwa hiyo, nina wasiwasi kama huu mradi kweli unaweza kufanya kazi kwa sababu wenye nguvu ni wao. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, *NDC* nitakuja kuzungumza zaidi katika Wizara ya Viwanda, lakini nafikiri *NDC* ingepewa nguvu ili iweze kuumiliki mradi huu. Mazungumzo yangu ya awali na shirika la *NSSF* limeonesha nia ya kutaka kuwekeza na wanasema wanayo fedha yote inayotakiwa katika kuwekeza kwenye mradi huu. Kwa nini *NDC* na *NSSF* wasifanye kazi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru hawa wawekezaji wamefanya kazi nzuri ya utafiti, tunaweza tukashirikiana nao wakapewa *share* kidogo, *NSSF* wakachukua *share* kubwa na *NDC* wakachukua *share* kubwa, lakini bila kuwasahau wananchi pia wale na wenyewe wapewe *share* kwa sababu ndiyo wenye madini yale pale, nafikiri huu mpango utatusaidia kuliko kuendelea na hii miradi midogomidogo, kwa kipindi cha miaka saba tungewekeza huko tungekuwa tumeshatoka huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi pale Mbinga. Pale Mbinga naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kulikuwa hakuna umeme lakini tarehe 6 Septemba, 2007, umeme uliwaka. Napenda sana kuwashukuru Mawaziri waliokuwepo wakati huo na waliosaidia, lakini mpaka leo usambazaji wa umeme ule ni kidogo sana licha ya ahadi ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Malima alijibu swali langu akasema, kule

maeneo ya Ruwiko, Matarawe, Tanki la Maji ile shule ya *Agustive High School* na kule Lusonga kuna kituo cha afya kilichojengwa kwa msaada wa nchi ya Korea na kuna kituo cha shule ya msingi ya watoto walemavu wanaokaa bweni hawana umeme, waliahidi watapeleka mpaka leo hakuna kitu, kule Mbambe na kule Uzunguni hakuna usambazaji kabisa. Umeme ule ukiwasha unawasha nyumba chache na viwanda vichache. Kama ungesambazwa ungeweza kuwasha nyumba nyingi na hivyo pengine wangepata fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui mahesabu ya *TANESCO* yakoje, nina wasiwasi nao sana, kwa sababu wameutelekeza ule mradi kabisa, ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha alishughulikie vizuri. Lakini pia tunavyo vijiji ambavyo ni miji midogo, Mji wa Maguu kwa mfano ni mji ambao una shughuli nyingi sana za kiuchumi na sehemu ambayo kilimo cha kahawa ndipo kilipobobea. Kule Litembo kuna hospitali kubwa sana ambayo inategemewa na kila mtu anaifahamu. Lakini kuna miji midogo kama Matiri, Mbangamao, Kitanda na Utiri ambako umeme huu ungeweza kupelekwa, sasa napendekeza vile vijiji tisa vya Mheshimiwa Ngeleja ukigawa sita ukapeleka huko na vile vya sehemu nyingine ukavileta hapa, sisi tutakuwa tumetimia hapa na utakuwa salama, patatosha tu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee kuhusu *REA*. *REA* wanafanya kazi nzuri, lakini Mbinga kule hatujawaona na nafikiri wangeweza kufanya *mapping* ya nchi kuona wapi zipo nguvu gani kuliko kusubiri kila Mbunge aende akapige hodi kwenye ofisi ya *REA*, nafikiri huu sio utaratibu mzuri, ni vema wakafanya *mapping* ya nchi, wakajua nguvu ziko wapi na wakaenda kuzifanyia kazi, Mbinga kwa mfano iko Mito mingi wala hakuna sababu hata ya kupeleka umeme wa gridi, lakini tunahangaika hivi kwa sababu *REA* haijaweza kufanya kazi nzuri. Lakini nimeshaongea na Ndugu Mwakahesa amesema atatusaidia na tunalo andiko la mradi kule la Malindindo na Kijiji cha Kindimba ambacho wale Wajerumani wameshaweka umeme pale, Halmashauri imeweza kuunganisha shule ya msingi na hospitali na Misheni, Wale wananchi bado hawajapata huo umeme, tunaomba *REA* isaidie katika eneo la kuwapa wale wananchi ule umeme na kule Litembo pia katika hospitali kubwa pamoja na Matiri ambako kuna mitiririko mizuri sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niliongea na Mtendaji Mkuu wa *REA* alisema atatusaidia katika kutupatia *solar* katika shule zetu za sekondari na zahanati, lakini wawekezaji wadogo wa umeme wanapata shida. Yuko Mheshimiwa Andoya na Askofu wa pale Njombe wameniambia kwamba fedha zimetolewa na Benki ya Dunia zimepelekwa *TIB, TIB* wanapeleka kwenye Benki za Biashara, riba inakuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, kama jambo hili ni kweli, pendekezo langu ni kwamba, hizi fedha angeendelea kukopesha *TIB* kwa riba ya asilimia tano na ingeweza kuwafanya hawa wakakopa na wakatekeleza miradi kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni madini. Tunao wachimbaji wadogo wadogo kule maeneo yao sijaona humu hayajatengwa, lakini pia mahali pao pa kuuza zile *Safire* wanakuja Wathailand kule Kijijini. Mthailand anakuja mpaka kijijini kule Mbinga, nafikiri hii haifai, tutengeneze utaratibu mzuri utakaotuwezesha kuwafanya hawa

wachimbaji wetu wadogo wakapata hizi *Safire* vizuri zaidi na maeneo yao yakatengewa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA SPIKA**

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe taarifa kwako kwa mujibu wa kanuni namba 68(8) kwamba mzungumzaji aliyemaliza kuzungumza mahali hapa ambaye hali kadhalika sikuona ni ustaarabu kumkatiza kuzungumza na hivyo nikaona nizungumze baada ya yeye kuwasilisha. Nataka kumpa taarifa kwamba, kauli yangu kuhusu kuigawa Wizara hii katika Wizara mbili, haikusudii kwa njia yoyote kukuza ukubwa wa Serikali ila ina lengo la msingi la kukuza tija na utawala mzuri wa rasilimali na uchumi wa Taifa letu. Dhana yetu ya msingi kuhusu ukubwa wa Serikali iko palepale na sisi sio mawe tunabadilika kutokana na mahitaji yanavyokuwa yanastahili katika Taifa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hoja yetu ya msingi tulikuwa tunaangalia namna ya kuisaidia mawazo mazuri ya nia njema Serikali iweze kulegeza Wizara hii ili tuongeze ufanisi katika utendaji wa Serikali na vile vile katika dhana hiyo hiyo ya kupunguza ukubwa wa Serikali, bado tunaweza tukapunguza Wizara nyingine au tukaunganisha nyingine, lakini kwa unyeti wa Wizara hii naomba tusiingize siasa katika jambo hili. ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kayombo unaipokea taarifa?

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja na moja ni mbili, ni hesabu rahisi sana ya kujumlisha. (*Makofi*)

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo. Cha kwanza kabisa nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Maswa Mashariki, nasimama hapa kuwahakikishia kwamba sitawaangusha, nitasimamia mambo yote ambayo yanatakiwa yawafikie watu wa Maswa Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa masikitiko makubwa hasa nilivyoangalia wachimbaji wa madini hawa wanaoitwa wachimbaji wadogo wadogo. Katika Mkoa wa Shinyanga, kuna machimbo ya almasi kwenye eneo la Kijiji cha Luhumbo, eneo hilo hapo awali lilikuwa linamilikiwa na mgodi uliokuwa unaitwa *Alamasi Limited* na baadaye *New Alamasi* , lakini umiliki wake ulikuja kwisha mwaka 1965 maana umiliki wake ulikuwa ni wa miaka ishirini na moja tu, wamiliki wa mgodi huo walikuwa wamepewa mwaka 1944. Kwa hiyo, baada ya muda huo eneo hilo lilikabidhiwa kwa Rais, kuanzia hapo eneo hilo sasa halikuwa chini tena ya Almasi *Limited* au ya *New* Alamasi wala ya *Williamson Diamonds*, lakini cha kusikitisha wananchi wa kawaida waliokuwa wanajaribu kujitafutia madini hayo hapo, wamekuwa wakinyanyaswa, wamekuwa wakikamatwa na kupigwa na wengine wameuawa.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wetu wameuliwa kwenye eneo ambalo kwa kisingizio cha kuambiwa kwamba wamevamia mgodi wa *New* Almasi au mgodi wa *Williamson Diamonds,* jambo ambalo ni la uongo, kama kweli basi hii Serikali inajali utawala wa sheria, utawala unaojali watu wake, naomba Waziri aniambie hivi huyu *New* Almasi analindwa na nani hadi anaua watu wetu na Serikali imemwangalia tu. Je, Serikali bado inamtambua kwamba anamiliki huo mgodi? Ni lazima alithibitishie hili Bunge kwa sababu kwa taratibu za kawaida inaonekana kampuni hiyo ilishamaliza muda wake na ilishakabidhi hati hiyo kwa Rais tangu 1965. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hawa wachimbaji wadogo wadogo wanapouliwa, wanapojitafutia kwenye eneo ambalo halina mwenyewe inakuwaje wanaitwa wavamizi wa mgodi ambao hauna mwenyewe. Wanauliwa watu ambao ni halali yao kuyavuna madini hayo kwa maana hakuna mmiliki mwingine anayetambuliwa kumiliki eneo hilo kisheria. Watu wengi wameuliwa, nenda Shinyanga kwenye *lock up* iliyoko pale wanaita Mhumbi gereza la Shinyanga, kwanza, nimekasirika sana kwa sababu watu wengi wameuliwa pasipo uhalali. (*Makofi/kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Mhumbu pale ukiwakuta wako mia moja katika gereza hilo. Themanini wanatokana na waliokuwa wanachimba kwenye eneo ambalo wala sio la *New* Almasi. Sasa kwa sababu wanateseka, wanashtakiwa kwa jambo ambalo halina mmiliki wala sheria pale, Serikali inasema nini kuhusu watu hawa? Je, iko tayari kutamka kwamba sasa waachiwe, kwa sababu wanazuiliwa kwenye eneo ambalo wala sio la mtu mwingine isipokuwa ni lao kama wazawa? Iko tayari kufanya hivyo? Pia je, iko tayari kuwafidia wale watu ambao wameuawa ama jamaa zao kuwalipa. Naomba Serikali itoe tamko rasmi kwa nini inaruhusu ubabe wa namna hii au hiyo *New* Almasi ina wakubwa walioko Serikalini ndiyo maana sasa wanatumia kisingizio ambacho kwa kweli si halali? Naomba nipewe majibu halali ili niweze kujua kama kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatembea juu ya maneno yake inayosema kwamba inafuata utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nilikuwa na matarajio makubwa kuona kwamba *REA* watasambaza kweli umeme katika vijiji vyetu, jambo la kusikitisha Wilaya ya Maswa ina zaidi ya Vijiji mia moja na nne, lakini hapa vimetajwa vijiji viwili tu vinavyofikiriwa kupewa umeme na tena wala sio vijiji, bali ni mtaa mmojawapo ambao uko katika Mji wa Maswa lakini vimetajwa kwamba vimepewa nguzo na kwa asilimia 53, ukweli uliopo hata tukiondoka na wewe leo na Waziri mhusika hawezi akaenda kukuta hata nguzo moja katika vijiji hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini yanazungumzwa mambo matamu wakati si matamu, kwa nini wanatamanishwa watu hawa, kwa nini wanaambiwa mambo ya uongo, kwa nini hapa inaonekana pesa nyingi zaidi ya milioni mia moja na kitu zimetumika kwa kazi ambayo haipo? Nahitaji tuambiwe ni kwa nini Waziri ameamua kulidanganya Bunge. Anakusudia nini sasa kuweka mambo ambayo wala hayapo, anampendezesha nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia kabisa kuona kwamba Mawaziri watakuwa waadilifu na wataliambia Bunge kwa kazi zilizofanyika. Cha kusikitisha kabisa, anajaza takwimu kubwa nzuri wakati hali halisi haiko hivyo, ndiyo maana tumefikisha miaka hamsini hamna lolote la maana ambalo limefanyika na tukisema hivyo mnaanza kusema hawa wazushi, hawa ni wanafiki, hawashukuru, tutashukuru nini? (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, haki ya kupata umeme ni haki yetu wala hatuhitaji kuomba. Serikali imepewa nafasi ya kuhudumia wananchi ndiyo maana imepewa ridhaa ya kutoza kodi na watu hao wanatarajia wapate huduma. Watu hawa kama wanalipa kodi ya umeme, wanahitaji wapate umeme sio wapate giza, lakini matokeo yake watu wanashuhudia giza na mwishowe hata watu mnawafanya kuwa machizi, siku moja mkiamua umeme urudi, watu watashangilia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasulumbayi, nataka kukuambia kwamba bado dakika zako zinakuruhusu kuendelea. Unaweza ukaendelea tu. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamekuwa machizi, umeme unakatika, ukirudi watu wanashangilia kana kwamba wamefanyiwa mazuri. Miaka 50 ya shida. Tunahitaji tuambiwe, kinachosababisha haya yote ni nini? Ni kitu gani ambacho tunakipokea ndani ya miaka 50 tangu tumepata uhuru.

**MBUNGE FULANI:** Giza!

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Ilishawahi kuzungumzwa hapa wakati tukiwaaga wakoloni walikuwa wanaambiwa kwamba, ndani ya miaka 10 mkija mtakuta sisi tumepiga hatua. Kweli wakija watatukuta tumepiga hatua katika hali hii? *(makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niambiwe ni kwa nini vijiji viwili vimetajwa wakati hata havijapelekewa huduma hiyo hata ile hali ya kuonyesha kwamba pana dalili za umeme kuwa utafika, angalau hayo matumaini tu. Nguzo hazijapelekwa, ukifika Kijiji kinachoitwa Bukakingirija utakachoona ni nguzo zinazokwenda Malampaka tena zinakwenda kwenye Gineri. Ukienda hadi Kijiji kinachoitwa Ngh'ami ni nguzo zinazokwenda Bariadi. Zinakwenda Bariadi zinafuata mpaka Luguru huko kwenye Gineri za pamba, lakini hayapo matumaini yoyote. Kinachopita pale ni waya tu za umeme pale zinaning'inia, wakazi hao wanashuhudia nyaya, tena za miaka mingi siyo za leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nipewe ufafanuzi huo ili baadaye niweze labda kufikiria tu. Lakini nasimama na kusema kwamba, nimepinga kabisa kuiunga hoja mkono Wizara ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Sitaiunga mkono mpaka hapo atakapotoa maelezo ni kwa nini wachimbaji wadogo wadogo wameendelea kukamatwa na hivi sasa wako lokapu wakati kumbe hata madini yenyewe au hata mgodi wenyewe siyo wa huyu ni wa huyu mmiliki wa New Alamasi na siyo wa *Williamson Diamonds.* Ni sababu ipi au kuna wakubwa mle ndani ya *New Alamasi* ndiyo

wanaochimba madini miaka zaidi ya 60 na Serikali inaangalia tu wakati katazo linasema huwezi ukaruhusiwa ukachimba madini kama huna leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa wanaendeleaje kuchimba madini yetu na wanapoyauza Serikali yetu inapata nini? Naomba maelezo ya kina, vinginevyo maandamano yatafanyika tena kwa nguvu zaidi. Maandamano yanasaidia kuwaamsha wananchi waweze kutambua haki zao ambazo zimekandamizwa. Kwa hiyo, hatutaogopa vitisho, tunajua kabisa haki haiombwi kwenye kijisahani. Haki hupatikana kwa kupambana na kupiganiwa. Kwa hiyo, wananchi wote tutawaamsha. Ninyi mnaogopa maandamano kwa sababu mnaogopa wananchi watazijua haki zao na wakijua haki zao watadai na sisi CHADEMA njia sahihi ya kuwaamsha watu ambao walikuwa hawaelewi ni kwa maandamano. Maandamano ya amani tutawaambia kwa nini tunapingana na Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri na Serikali kwa ujumla itoe tamko juu ya mgodi huu, watu wameuliwa, watu sasa hivi wana ulemavu mkubwa, watu wamepigwa risasi, hakuna anayewatetea, inaonekana *New Alamasi Limited* ina wakubwa ndani yake. Kwa hayo machache, naomba niishie hapo, lakini nimekataa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Taarifa Mwenyekiti.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kasulumbayi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Taarifa Mwenyekiti.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Ester.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyikiti, napenda kumpa taarifa msemaji aliyepita. Amesema maandamano yanasaidia kuamsha watu, lakini ninachosema, maandamano tunajua ni sera ya chama fulani kwa lengo la kueneza chama chao na wala si kuwaamsha wananchi. Nataka nimpe taarifa huyu msemaji aliyepita, hata mkizomea haisaidii, ndiyo ukweli wenyewe, wananchi wameshaamka na wanajua haki zao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester naomba…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Kitu mnachokifanya mnaeneza chama chenu. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nakuomba sana tufuate taratibu. Tuvumiliane, tuwe na ngozi ngumu. Wachangiaji ni wengi, watakaofuata kama wana neno nao wajibu. Haya sasa Mheshimiwa Mansoor atafuatiwa na Mheshimiwa Rebbeca Mngodo.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kusimama mbele yako kwenye Bunge hili Tukufu na kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kushukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi ya kugombea Ubunge, Jimbo la Kwimba. Nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi. Pia naomba nichukue nafasi hii kushukuru wananchi wa Kwimba ambao wamenichagua kuwa Mbunge wao na nawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia niishukuru familia yangu, mke wangu Shagufa, na watoto wangu Alezi na Shaala, Begam kwa kuwa wavumilivu na kutoa ushirikiano wakati wa kampeni na wakati huu, sasa hivi wakati niko hapa Bungeni kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri Ngeleja kwa hotuba nzuri na pia nimwambie kwamba naunga mkono hotuba yake mia kwa mia. Jimbo langu la Kwimba hususan Wilaya ya Kwimba tuna Majimbo mawili, kuna Jimbo la Sumve na kuna Jimbo la Kwimba. Jimbo la Sumve lina Kata 15, Jimbo la Kwimba lina Kata 15. Jimbo la Kwimba Kata 15, Kata moja ndiyo ina umeme. Kata 14 ni giza. Jimbo la Sumve Kata 15, Kata nyingi wana umeme. Sioni wivu kwa Mheshimiwa Ndasa ambaye tumekaa naye jirani, lakini naona wivu wa maendeleo. Kwa hiyo, sisi ni Wabunge pacha kwenye Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwimba nashindwa kuwaeleza wananchi wangu kwamba jirani wana umeme kwenye Kata nyingi na mimi kwa nini sina umeme. Wananchi wangu wa Jimbo la Kwimba wameomba siku nyingi umeme, wameahidiwa umeme zaidi ya miaka kumi hususan Mwamashimba Tarafa ya Mwamashimba wameahidiwa zaidi ya miaka kumi kwamba kuna mradi wa Benki inakuja, Hungumarwa watapata umeme, ukiangalia gridi ya umeme inapita juu ya nyumba zao lakini chini hawana umeme. Nao wanaomba wapate umeme ili nao waweze kumwona Mbunge wao anavyoongea Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: Kwa suala la umeme ningeshauri kwa Serikali wana miradi mingi sana, wamepanga kwa pamoja. Tatizo la umeme tuna *shortage* ya *megawatt 260* mpaka 300 kwa nchi nzima na hususan nchi yetu inakua kwa asilimia 10 kwa umeme. Kwa hiyo, tuna shida ya *megawatt 350* mpaka 2,012.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kwa Waziri angekamata mradi ambao ungezalisha *megawatt 500,* haraka iwezekanavyo ili tuachane na aibu ya kutokuwa na umeme na kuendelea kuwa na giza. Mara nyingi tunapopokea wageni, tunakuta umeme hakuna, ni aibu na wewe unajitambulisha kama Mbunge, inakuwa ni aibu. Ni aibu kweli kweli, naomba ndugu zangu Serikali mtusaidie tuachane na hii aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujielekeza kwenye masuala ya mafuta. Kabla sijaongea ningeomba ku-*declare interest.* Mimi ni mfanyabiashara wa mafuta. Hili suala nalielewa vizuri zaidi, naomba nilichangie hapa. Napongeza kwa mpango mzuri wa Serikali wa kuleta *Bulk Procurement System* kwenye hotuba ya Waziri kwenye ukurasa 40 *paragraph 75* ya hotuba, amesema kwamba wamepitisha *Government Notice No. 164* tarehe 3 Juni, 2011. Hiyo ni *regulation* ambayo wameipitisha. Nawapongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningependa kutoa mapungufu ambayo yapo kwenye hiyo *regulation*, ningeshauri wayabadilishe kama ifuatavyo:- Kwenye hiyo *regulation* kwenye ukurasa wa 16 *paragraph number 5* kwenye *regulation* hiyo inasema kuna Kamati ya *Bulk Procurement Technical Committee.* Hiyo Kamati itaundwa na itateuliwa na Waziri mwenye dhamana. Hiyo Kamati atakayoteua ameweka kwenye hiyo Kamati, ameweka Wawakilishi wawili wa Wizara yake ya Nishati na Mafuta, Wizara ya Fedha, *TRA, TPDC, Tanzania Ports Authority* na ameweka mwakilishi wa kampuni moja ya *Oil Marketing Company*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa hili suala la kuweka kampuni moja ya mafuta iwakilishwe wakati hii Kamati yote inateuliwa na Waziri na hapo nyuma Waziri kwenye ukurasa wa 17 *paragraph* ya 7, Waziri ana mamlaka baada ya kuteua kwamba anaweza akatoa agizo siku yoyote kwamba wafanye hili na hili na wale inabidi watii amri yake, hawana sehemu ya kusema hapana. Inaandika naomba nisome hiyo. *"The Minister may in writing issue directions of specific or general nature to the Bulk Procurement Technical Committee on any matters or decisions and The Bulk Procurement Technical Committee shall comply with the direction or decision".*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake yeye akiteua Kamati na akipata nafasi ya kuipa maagizo na lazima waifuate, hapa unaona kwamba inaweza ikawa ina dosari. Nashauri hii *paragraph* ya 7 itoke. Awaachie ile Kamati wafanye kazi wanavyoona inafaa, asije akapata mamlaka ya kuwaagiza tena na kwa sababu amewateua wale nao watasikiliza kwa sababu amewateua, *he has the authority* ya ku-*appoint.* Kwa hilo ningeshauri waitoe. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, lingine ningependa pia kwenye Kamati ile, wamesema kwamba kampuni ya mafuta itawakilishwa na kampuni moja ya mafuta. Tuna aina tatu za kampuni ya mafuta katika nchi hii. Kuna makampuni makubwa ya kati na madogo. Sisi walala hoi wengi tuko kwenye wadogo. Sasa hawa wakubwa ukisema uweke mtu mmoja hapa na hiyo kampuni inakaa kwenye Kamati ambayo itatoa maamuzi ya kupitisha tenda ambayo itapitishwa na Kamati nyingine ya *Petroleum, Importation Coordinator.* Ile Kamati inasimamiwa na hii Kamati ya Kiutaalam sasa hii Kamati inaweza ika-*influence ile* tenda ipitishwe kwa ile kampuni ambayo inakaa ndani ya hii tenda. Ningeshauri hii kampuni inayokaa ndani ya hii Kamati isiagize mafuta, asiwe mwagizaji wa mafuta ili awe *neutral,* asiwe na *interest* ya kuagiza mafuta. Hiyo itakuwa *conflict of interest.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itakayoshinda tenda ya kuagiza mafuta ningeshauri pia iwe ni kampuni ambayo imesajiliwa Tanzania, iwe mlipa kodi wa Tanzania. Kwa sababu tunavyoongea hapa ni kwamba hata kuagiza tani laki moja au zaidi kwa mwezi maana yake atakuwa anapokea pesa zaidi ya bilioni 50. Ni muhimu kampuni ieleweke, pesa zipitie benki za Tanzania ili *TRA* na *Auditor General* aweze kuzikagua hizo *account* kwamba hizo pesa zinapita kwenda Tanzania. Tusitoe hizo tenda kwa kampuni za nje, tutoe kwa Watanzania ili hesabu iweze kueleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 18 wa *regulation paragraph* 10, inasema kwamba kuna Kamati itaundwa ya *Petroleum Importation Coordinator*. Hiyo Kamati ndiyo itasimamia mambo ya tenda. Hapo *regulation* inasema kwamba kutakuwa na wawakilishi watatu kwa kampuni kubwa, wawili kwa kampuni ya kati na kampuni ndogo atakuwa mwakilishi mmoja. Sasa ukiangalia kwenye ile ndogo ambayo unapata mwakilishi mmoja, makampuni zaidi ya 20 ya Watanzania yako pale, tunaomba iwe *prorata*, isiwe wakubwa wapate zaidi, wale wakubwa wote ni wa nje, siyo wa hapa. Tunaomba tuwe na *prorata* kulingana na kampuni zilivyo, tupate uwakilishi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kuliongelea ni kwamba kwenye masharti ya kampuni ambazo zitaruhusiwa kuagiza mafuta kwenye *pre-qualification criteria* kwenye *regulation* ambazo zimeandaliwa na Wizara wanasema naomba ninukuu kwa haraka haraka: *"A growth trading turnover at least US dollars 200 million per year evidence to be provided informal of satisfied audited accounts for the last three years."* Lingine masharti ya ku-*qualify*. *Proof of a monthly trade financing capital of US dollars 500 million, evidence like Bank Statements, letter from the banks.* Hii inasema kwamba kampuni iwe na dola milioni 500 kwa mwezi kama *financing capacity* ndiyo itapata kibali cha kuagiza mafuta.

Sasa hili linafanya ushindani upungue. Ningependa Waziri anieleze kampuni ngapi Tanzania zipo, zina uwezo wa kupata hii milioni 500. Hii inafanya kampuni zote zinakufa, watabaki wawili au mmoja tu. Hata hao ni bahati kama wapo. Maana yake ushindani unakufa. Hii inaweza ikaleta ufisadi, ukatokea kwenye biashara hii ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo machache ambayo nilikuwa nataka niyachangie. Naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Tarime kwa juhudi zao zote za pamoja wanazozionyesha kwa kutuunga mkono kwa hali na mali na napenda kuwahakikishia kabisa kwamba wamechagua jembe la kazi na sitawaangusha, nitawatumikia na tutaleta mabadiliko makubwa sana katika Wilaya yetu ya Tarime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii kushuru kwanza familia yangu hasa mke wangu Margreth Nyambari Nyangwine na watoto wangu Boki Nyangwine pamoja na Bernard Nyangwine kwa kunivumilia wakati ninapokuwa nje ya

familia hasa kwa kulitumikia taifa letu la Tanzania. Baada ya shukurani hizo mimi napenda kutamka hadharani kabisa kwamba sitaunga mkono hoja hii ikiwa kama mambo yafuatayo nitakayoongelea hayatekelezwa. *(Makofi)*

Moja, nizungumzie suala la hali halisi ya umeme katika nchi yetu ya Tanzania. Hilo nafikiri watu wengi wameliongelea. Lakini naamini kinachotakiwa tukifanye ni kuonyesha uzalendo na wala si maandamano, chuki havitasaidia kutatua tatizo ambalo linalikabili Taifa. Tuungane tuwe kitu kimoja na naamini tutaweza kufanikisha hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tufikie wakati tujiulize kwamba kwa nini tuendelee kutumia vyanzo vya maji kama ndiyo chanzo kikuu cha kuzalisha umeme katika nchi ya Tanzania. Naomba tufikiri, kwa sababu najua kabisa kwamba tuna wataalam wa kila aina kufikiri bado kungalipo, tubadilike, tubuni vyanzo vingine vya kuzalisha umeme katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile naomba kuongelea suala la umeme vijijini katika Wilaya ya Tarime ambapo mimi mwenyewe binafsi nimejaribu kufuatilia, ingawa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilinisikiliza ikanipatia baadhi ya vijiji umeme, lakini umeme ule bado hautoshi kwa hivyo kwa sababu tuna vijiji 92 na vijiji ambavyo vinapelekewa umeme ni vijiji 12 tu, tunataka vijiji vyote 92 vipate umeme. Hivyo, vijiji ni kama vile vya *Security Road* inayotoka Rorya, Susumi, Kubiterere, Sirari, Remagwe, Bhitiro, Nyabisaga, Borega, Wanyange, Kimusa na Nyantira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nisisitize kwamba naiomba Wizara na hili kama halitawezekana tutatumia nguvu, kuhakikisha kabisa kwamba ule umeme unaopita kwenda Mgodi wa Nyamongo, unatumika kuwanufaisha wananchi. Hasa katika Wilaya ya Tarime, huo umeme unapita katika Kata za Komaswa, Manga, Kibasuka na Kyole. Hata katika Wilaya ya Serengeti, huo umeme katika Vijiji vya Magatini na katika Wilaya ya Musoma Vijijini, Kijiji cha Wegero, Kongoto, Viswahili, Kiagata na vijiji vinginevyo vile ambavyo umeme unapita, tunaomba ushushwe ili uwanufaishe wananchi wa maeneo hayo. Hilo nasisitiza kwa kweli kwamba, wasipoushusha tutaushusha kwa nguvu, naomba hilo lifahamike hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hiyo pigia mstari kabisa hiyo. Mheshimiwa endelea.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa niongelee suala kubwa sana la sekta ya madini, hasa katika Jimbo langu la Tarime. Mimi naamini kabisa kwamba wote kama vijana, wazee na akinamama, tuna dhamira safi sana ya kuitumikia na kuijenga nchi yetu. Lakini inahuzunisha sana tunapoona utajiri wa nchi hii unaporwa na tunanyamaza kimya, hilo kwa kweli hatutalivumilia, tutapigana mpaka tone la mwisho, tukiipigania nchi yetu hii. *No!* Sijasema kwamba tupigane kwa kutumia chama chenu, ni Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijulishe kabisa kwamba nchi yoyote ile ambayo imeendelea duniani, imejengwa kwa kutumia maliasili zilizopo. Katika nchi ya Tanzania, ukiangalia kuna kila aina ya madini, kuna dhahabu, kuna almasi, kuna *tanzanite* na kadhalika, hasa katika Mkoa wa Lindi na Mara. Ukienda katika Mkoa wa Lindi, katika Wilaya ya Ruangwa katika Vijiji vya Mnacho, Nandagala, Nambilanje, Nangawa, Nachingwea katika Vijiji vya Nditi, Kiegeyi, Ikungu, kote kuna madini. Sasa tunajiuliza ni kwa nini Tanzania bado ni maskini? Tuzidi kufikiri kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba niongelee suala la Nyamongo, ambalo watu wengi na hasa wanasiasa uchwara wanakimbia wakifikiri kwamba wanaitetea Nyamongo, lakini Wananyamongo nawahakikishia kwamba bila Nyangwine na Chama cha Mapinduzi, matatizo yenu yatakuwa magumu. Wakae wafikirie, hata Augustine Mrema, alikwenda akashindwa! Wamekwenda CHADEMA, wameshindwa! Sasa waangalie Nyambari Nyangwine, ndiye atakayeweza kutatua matatizo hayo kwa kushirikiana na Chama cha Mapinduzi. Mikataba yao, ya wawekezaji, ninayo hapa. Nasema hadharani kabisa kwamba kama wale wawekezaji hawatatekeleza kile walichokiandika humu, mimi binafsi kwa kushirikiana na wananchi wangu nitawafukuza. Hilo halina utani kwa sababu waliokwenda na waliokimbilia huko mara nyingi sana walikuwa wakienda wakipokea *10%* wanarudi. Lakini kwangu mimi sina mchezo huo wa kupokea *10%* wala nini, nitatetea haki na ukweli kwa wananchi wa Tarime. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mgodi ufanye mambo yafuatayo:-

Kwanza uhakikishe kabisa kwamba, unalipa fidia halali kwa wananchi wa Nyamongo. Wawalipe nyumba ambazo zinazunguka machimbo, wahakikishe kabisa kwamba, wanawahamisha na sehemu ambako wanawapeleka wanawajengea nyumba nzuri, za kifahari na zenye kuleta matumaini, hapo tutaelewana. Lakini kama hawatafanya hilo, kwa kweli naomba wananchi wa Nyamongo waelewe kabisa kwamba tutashika mapanga na *tutawagecha*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusisitiza kuhusu suala la uchunguzi uliotumwa na Bunge lako kuhusu maji ya Mto Tigite ambayo kwa kweli kwa kiasi fulani yaliathiri watu wa Nyamongo na ikaonekana kabisa kwamba uchunguzi huo ulifanyika, lakini cha ajabu ni kwamba, majibu hayakutolewa, watu wa *NEMC* wakaenda kule na wao wakifika sijui wanapokea *10%!* Lakini sasa nasema kwamba, hayo majibu tunataka yatolewe na tuhakikishe kabisa kwamba kama watu waliathirika walipwe fidia halali. Hatutaki ubabaishaji wa aina yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nasisitiza mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, biashara zote na tenda zote zinazotumika katika ule mgodi tuhakikishe kwamba zinafanyika au zinaendeshwa na watu wa Tarime, hususan wale wanaozunguka ule mgodi. Hatutaki mambo ya kuagiza *juice* kutoka Dar-es-Salaam, mambo ya kuagiza chakula kutoka Dar-es-Salaam, kwenda kulisha mgodi! Tunataka wale watu wanaouzunguka ule mgodi ndio waulishe ule mgodi kwa kutumia chakula chao kile

wanachokilima kule Tarime na hapo tutakuza kipato cha mwananchi wa kawaida katika Wilaya ya Tarime. Hilo naomba lizingatiwe na kwa kweli litiliwe maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano inasikitisha kabisa kwamba kuna kazi ya kuzoa chuma chakavu, wanapewa watu kutoka Kahama na wakati watu wa Tarime wapo! Wana uwezo! Watu wa Tarime wafahamu kwamba, wale wanasiasa uchwara waliokwenda kuwachonganisha wanafikiri kwamba, nataka kuzoa chuma chakavu, sina hiyo nafasi, nataka wapewe watu wazaliwa wa Tarime; hilo lifahamike na watu wa Kahama wale waliopewa hiyo tenda na wenyewe nitawafukuza, sitawaonea haya. Ajira zitolewe kwa wakazi wanaozunguka mgodi, hatutaki ajira mtu anaagizwa kutoka Afrika Kusini, anakuja kufagia! Mtu anatoka Kenya anakuja kulinda! Hiyo kwa kweli naomba iwe marufuku. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kusisitiza kwamba, eneo la wachimbaji wadogo kama watu wa mgodi walivyoahidi kwamba wanatenga dola milioni tatu, tuhakikishe kabisa kwamba hizo dola zinapatikana na wachimbaji wadogowadogo wanaendelezwa. Nimemshangaa Waziri alipowasilisha hotuba yake, hakuweza kutaja kwamba Mgodi wa Nyamongo utatenga eneo lipi la kuendeleza wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nasisitiza mgodi uhakikishe kabisa kwamba unajenga Chuo Cha *VETA* pale Nyamongo ili kutoa ajira kwa vijana wanaozunguka ule mgodi. Kwa sababu, ukizingatia kabisa kwamba Wananyamongo tangu enzi na enzi walikuwa wanachimba yale machimbo, hawajui kulima, kazi yao wanategemea dhahabu, sasa tuwapeleke wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuongelea suala la mikataba ambayo nimekwishaitaja kwamba mikataba hii ni *fake*, haina uelekeo wa kumsaidia mtu wa kawaida na kwa kuwa, walitumia nafasi ya wanakijiji ambao bado hawajapata elimu kuwalaghai, sasa watu wa Tarime tumesoma, tuna elimu, tunafahamu kutafsiri sheria, mikataba hii itapitiwa. Lakini tunaomba watu wa mgodi hata na Wizara husika warudi kwanza kijijini kule walikosaini hii mikataba, wasaini mikataba upya au wawaeleze wananchi kwamba ni kwa nini hawajatimiza ahadi walizoziahidi za kutoa elimu, barabara, umeme, maji na afya. Ninachokisisitiza ni kwamba, kwa kweli hatutavumilia endapo wale watu wa mgodi wanatutania; akiingia kiongozi wanamdanganya kwamba eeh, nitakujengea barabara ya lami! Kwa kweli kama hiyo barabara ya lami waliyoandika hapa wataijenga kutoka Mto Mara mpaka Tarime kama hawataijenga, nitakuwa mstari wa mbele katika kuwafukuza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Mambo ya Ndani, ahakikishe kabisa kwamba anatumia muda mfupi iwezekanavyo kuondoa askari wale wanaolinda ule mgodi. Kwa sababu, Kanda Maalum, imepelekwa Tarime kulinda usalama wa raia na sio kulinda mgodi, hilo lizingatiwe na lieleweke. Hakuna mgodi unaolindwa na askari, sisi askari wetu wa Tanzania wanalinda raia na wala sio kulinda migodi. Hilo jambo lizingatiwe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ile ruzuku inayotolewa kwa Halmashauri ya dola 200,000 kwa watu wanaochimba dhahabu nyingi sana na kubwa sana, wanachukua mamilioni ya dola, wanatupatia dola 200,000, Halmashauri yetu ya Tarime! Hilo nasisitiza kabisa kwamba na lenyewe hatutaweza kukubali hizo dola 200,000 bora wabakinazo ila sisi tutakapoamua kuwashughulikia kwa kweli, naomba mtuhurumie. Nataka nitumie nafasi hii kuishauri Wizara, tukae pamoja, watuhusishe sisi wawakilishi wa wananchi na vilevile wawahusishe wale wananchi wa vijiji vile tuweze kujadiliana, tuone tufanyeje ili kutatua matatizo yale yanayotuzunguka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, napenda kutumia nafasi hii kuwaasa wananchi wa Tarime, kwamba mambo ya uchaguzi yalishakwisha. Naamini kabisa kwamba, hata kama kutakuwepo na wale mavuvuzela wanaopitapita, bado itakuwa ni ngumu sana kukishinda Chama cha Mapinduzi na kitaendelea kutawala milele na milele. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Nyangwine. Nimemwona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sina nia ya kumpinga rafiki yangu Nyangwine, nampongeza sana kwa hotuba yake. Lakini nina tatizo kidogo na matumizi ya lugha! Matumizi ya lugha yanayoashiria kutumia mapanga! Kwa ustaarabu wa Bunge hili, maana *Hansard,* itabaki hivyo hivyo. *Whether* anasema utani au ukweli, lakini mapanga ni silaha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, simwingilii kama ana uwezo wa kuwafukuza au hana uwezo. Lakini nchi hii, tunaishi kwa utaratibu na tumekuwa tunazungumza hapa. Wenzetu hapa wakisema tunataka kufanya fujo, tunawaambia tulizeni munkari!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Nyangwine, katika *Hansard* za Bunge hili, kutishia kutumia mapanga, ningefurahi sana kama Mheshimiwa Mbunge, angefuta neno la kutumia silaha katika hotuba yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika maisha yangu nimewahi kukaa kidogo Mkoa wa Mara. Tungekuwa Musoma kule, kwa kweli hivi alivyoongea Mheshimiwa Mbunge, ndio wananchi wake wanamwelewa. Lakini Mheshimiwa Nyangwine, basi wakati mwingine lainisha kidogo lugha, usichukulie kama uko kule moja kwa moja. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa George Simbachawene, atafuatiwa na Mheshimiwa Agripina Buyogera.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Lakini pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu na niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kibakwe, kwa kunisadia katika kuendeleza Jimbo letu la Kibakwe. Niwahakikishie kwamba tutaendelea kushirikiana na ndio tutapata maendeleo kwa kiwango ambacho Mwenyezi Mungu atatujalia. Nianze na masuala ya Jimbo. Nimeongea na Mheshimiwa Waziri…

**NAIBU SPIKA:** Samahani kidogo Mheshimiwa Simbachawene! Tulitangaza tangu jana kwamba, watakuwepo watu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya Wabunge ambao kuna maeneo ambayo wangependa kupata minara ya mawasiliano na simu. Watamaliza kuwepo pale robo saa ijayo, saa 12.30 wataondoka, wako pale Msekwa, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa yeyote ambaye angependa kuwasiliana nao, taratibu, mmoja mmoja katika robo saa hii tuitumie. Mheshimiwa Simbachawene, endelea.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nimesema nianze na masuala ya Jimbo. Nimeongea na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mara nyingi juu ya ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, ya kupeleka umeme kupitia *REA*, kutoka Mtera, Kisima, Chipogoro, Wiyenzele, Iramba, Mtamba hadi Rudi. Tumezungumza na Waziri, anaifahamu ahadi hii na Mheshimiwa Waziri kwa hakika, sisi vijiji hivi nilivyokutajia ndivyo vinavyotunza bwawa la Mtera, ingawa sasa hakionekani kwamba ni chanzo kizuri sana cha umeme. Lakini bado kwa kweli mvua kama itanyesha leo, bado tunategemea bwawa la Mtera, katika kuhakikisha kwamba *gridi* ya Taifa, inaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mheshimiwa Waziri atakumbuka, katika Bunge kipindi kilichopita akiwa yeye mwenyewe Waziri, aliniahidi kufanya marekebisho katika ile *line* ya kutoka Kibakwe, kupitia Ikuyu na Luhundwa. Sasa ukishafika Luhundwa pale, kwa sababu nilimweleza kwamba kuna Kituo cha Afya na kuna sekondari mbili katika eneo hilo ambako umeme sasa una-*divert*, unapita pembeni na maeneo haya, Mheshimiwa Waziri alinikubalia lakini baadaye nitasema *conclusion* ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri, pia tulikubaliana naye kwamba, umeme ukishatoka Pwaga uende Kitati, Lumuma hadi Idole kule kwa Mheshimiwa Mkulo, ambako ni sehemu kubwa sana ya kilimo cha umwagiliaji. Katika Sera, tumesema maeneo ambayo yana uzalishaji na kilimo kikubwa cha umwagiliaji kama eneo hili ambako kuna zaidi ya hekari 2,500 za umwagiliaji na kuna uzalishaji mkubwa wa kitunguu na mazao mengine, basi ni vizuri yakapelekewa umeme ili kutoa ajira kule vijijini pia. Maana maeneo kama haya yenye uzalishaji, kama yatapewa umeme, kukawepo na viwanda vidogo ni hakika kwamba vijana watapata ajira na watu kukimbilia mjini, wataacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali, kwa Sera yake hii basi mkubali na nilishaongea na Mkurugenzi wa *REA* jambo hili, akaangalia ramani, akakubaliana na mimi. Safari hii Mheshimiwa Waziri, amekuja na mapendekezo ya miradi itakayotekelezwa ya *REA*, mimi simo na Wabunge wengine wengi, hawamo! Mheshimiwa Nagu, shemeji yangu, nimeoa kule, ananiambia kule Hanang, yeye hakuguswa kabisa katika Wilaya nzima ya Hanang! Wakati Wilaya nyingine zote za karibu yake zina miradi ya umeme vijijini; tunachimbiana matatizo!

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali, kwa Waziri na Naibu Waziri, naamini mtaendelea kuwepo katika Wizara hii kwa sababu, sisi ni vijana, tunapendana, tunaaminiana; naamini matatizo yaliyojitokeza sasa ni changamoto ya kukomaa na kukua kiuongozi. Nyie wenzetu mnaokulia kwenye matatizo, baadaye mtakuwa viongozi wazuri sana. Niombe sana kwamba, kipindi kijacho cha bajeti nyingine na sisi tutazamwe, hatutakuwa na raha. Usione watu hapa ukafikiri wana raha wanapoona wenzao wana miradi mingi ya vijijini, halafu wenyewe hawana! Watu hawana raha hapa!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa niwashauri wenzangu. Pamoja na kwamba hatuna raha, hii ni bajeti ya kwanza ya awamu yetu hii ya miaka mitano. Tutakuwepo na miaka mingine tena, tutakuwa na bajeti inayofuata, kwa miaka mitano nina hakika Mheshimiwa Ngeleja, basi utahakikisha unatuangalia na sisi ambao hatukupata ili wote tunapokwenda kwenye uchaguzi unaokuja, kila mtu ashindwe kwa sababu zake binafsi lakini sio kwa sababu yake Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Malima. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, jambo langu la pili ambalo nilitaka nilizungumzie ni namna ambavyo miradi ya umeme sasa ni vizuri ikajadiliwa katika Halmashauri zetu katika *level* zote. Umeme ni maendeleo, umeme ni uhai wa uchumi, umeme ni uhai wa maendeleo, bila umeme huzungumzi maendeleo katika dunia ya leo. Mimi nadhani suala la miradi ya maendeleo ya umeme ni vizuri tukalijadili hata katika Halmashauri zetu na vizuri hata Halmashauri ikashiriki katika miradi hiyo. Kufikiri kwamba utafikisha umeme kwenye vijiji vyote kwa kutumia *REA* peke yake, mimi nadhani pengine siyo sahihi sana, kama Halmashauri inaweza ikawa katika vipaumbele vyao ni umeme turuhusiwe kufanya hivyo lakini tutaomba vibali kwao tu kwa ajili ya ufundi na utaalamu ambao sisi hatuna wahandisi wa namna hiyo katika Halmashauri. Mimi niombe sasa tujadili umeme kwa sababu suala la umeme sasa si suala la mchezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie janga linalosemwa sasa la Taifa la upungufu wa umeme, inawezekana kila mtu anajaribu kusema kwa mtizamo anauona yeye. Lakini katika hali halisi ya tatizo mpaka likafikia kuitwa janga maana yake lina ugumu katika utekelezaji wake na jambo hili kwa hakika lina ugumu wake, tukitumia nafasi ya Bunge ambayo Kikatiba Bunge kazi yake ni kuishauri Serikali na kusimamia, tukatumie kupiga mikwara na kuonyesha kwamba Serikali haiwezi, kwamba Serikali hii imeshindwa, hakuna mwingine wa kutekeleza hayo zaidi ya Serikali iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani tungetumia fursa hii kuonyesha njia, kuonyesha wapi Serikali ifanye nini ili kuondoa tatizo hili. Tukifanya vinginevyo

hatuisaidii Serikali na hatuna Serikali nyingine mpaka uchaguzi mwingine utakapofanyika, tuwatie moyo, tuwasaidie wapi, wafanye nini ili kuweza kutatua tatizo. Chanzo cha tatizo hili ni kutegemea vyanzo vya maji katika kuzalisha umeme katika nchi, tatizo letu kubwa namna tulivyoshughulikia udharura wa umeme, dharura ni dharura unaweza ukapambana na dharura ukafanikiwa, lakini dharura na mapambano yako yawe yakidharura na ndiyo lililotuletea tatizo, lakini yapo makampuni makubwa ambayo uhakika mimi nasema kwamba pengine ni vizuri kama kweli jambo hili tunatambua kwamba ni tatizo ambalo linagusa nchi kwa kiasi kikubwa, ni tatizo linaloumiza uchumi, ni tatizo ambalo yote tunayoyapanga hapa yanaweza yasiwezekane maana viwanda hivyo tunavyotegemea vitalipa kodi haviwezi kulipa kodi tunayoitarajia maana hakuna chochote kitakachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tunatambua hivyo basi jambo hili lishughulikiwe kwa udharura halisi. Achaneni na Sheria za Manunuzi zinazoweka urasimu, zinazocheleweshа kufanya maamuzi kwa haraka, hizi sheria zimewekwa mimi bahati nzuri ni Mwanasheria, siyo kila sheria ni sheria, *(not every law, is a law).* Kunaweza kukawa na sheria nyingine ikawa ni tatizo na sheria imewekwa kwa ajili ya kufanya mambo yaende vizuri, kama sheria inakwamisha unaachana nayo unafanya maamuzi, Sheria ya Manunuzi ndiyo tatizo hapo. *(Makofi)*

Leo duniani huko karibu makampuni yote makubwa yanatengeneza majenereta, Japan wana matatizo ya umeme na wenyewe wana mgao. Japan ambalo ni Taifa kubwa lakini wao imetokana na *crisis* ya mitambo yao ya *nuclear.* Kote kwenye viwanda vyote vikubwa wamefanya *order* ya majenereta kwa ajili ya kupeleka kwenye nchi yao, leo huwezi kupata wewe Mtanzania kwenye kiwanda jenereta mpya, siyo rahisi, tunachoweza kupata hapa ni jenereta zilizotumika angalau kwa kiasi kidogo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukatatua tatizo hili na kama mlivyoanza Serikali mimi niwapongeze kwa mtambo ambao umeshushwa sasa, jenereta ambazo zimeshushwa zifungwe haraka haraka tupunguze *crisis* ya Dar es Salaam tuendelee na maeneo mengine kama tutakavyofunga na Tanga wa megawati 70, Dar es Salaam megawati 100 tuendelee tupunguze ukubwa wa tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kulaumiana na kunung’unika hapa na kukatishana tamaa haitatusaidia chochote, tatizo lipo, linaumiza watu, tukija hapa tukatumia tatizo hili kutengeneza siasa, mimi nina hakika hatutasaidia Serikali na hatusaidii wananchi wetu. Imani yangu ni kwamba Serikali chukueni mawazo haya mazuri yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge, myatumie kwa kasi zaidi, nguvu zaidi na ari zaidi, mimi naamini tutaweza kutatua tatizo hili la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la madini, kama kuna siasa kubwa katika sekta ya madini ni nafasi ya wazalendo (wazawa) wa Tanzania katika sekta hiyo. Ushiriki wa Watanzania katika sekta ya madini ni lazima uonekane waziwazi, *industry* hii inaajiri watu wengi kuliko tunavyofikiria nilisema hapa juzi kwamba ilipokuja *rush* iliyotokea kule Winza jimboni kwangu Kibakwe, nilishangaa kuona mtu akisikia kuna madini anaweza kutembea hata kilomita 800 kwa mguu hata kama hana usafiri, anakwenda akiamini anaenda kutajirika, sekta hii ina watu wanaohitaji msaada,

tusiwakatishe tamaa, tuwatambue Mheshimiwa Waziri umesema katika hotuba yako, tuwatambue hebu tufanye haya kwa vitendo. Tufanye haya kwa vitendo, tuwatambue watu hawa, tuwasaidie, lakini kinachokatisha tamaa ni pale ambapo wao wanatembea kwa miguu kwenda kukamata maeneo wakishaanza uchimbaji unamsikia kuna mtu ana leseni kubwa amefanya *survey* kwa helkopita anafanya *peging* kwa helkopta. Ile Kibakwe yote, Jimbo la Kibakwe, Mpwapwa yote wilaya nzima tunaambiwa kuna leseni za watu wakubwa, mimi nimeshakuwa Mbunge kipindi cha pili, siwajui, sasa unakua na mtu amewanunua nyie mpo chini mnaishi yeye anapita juu anawanunueni nyie mnaokaa pale, Serikali tusaidieni, hatueleweki kwa wananchi wetu. Mheshimiwa Nyangwine na Mheshimiwa Bukwimba hapa, watu wote wanaotoka kwenye maeneo yenye madini siasa kwao ni wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kukubaliana na Serikali katika mambo ambayo hakika yanaonekana kutowaridhisha wachimbaji wetu wadogo, rai yangu kwa wachimbaji wadogo ni kwamba na wenyewe basi wajitahidi kufuata sheria. Sheria zetu zinapopuuzwa kufuatwa na sisi tunageuza kufanya siasa katika masuala ya sheria, hakika tunajenga Taifa na jamii ya watu ambao tutaingia kwenye migongano kila kunapo kucha.

Mheshimiwa Magufuli anapambana na watu waliovamia barabara sababu ni kutofuata sheria, ujenzi holela sababu ni kutofuata sheria, uchimbaji holela kwa sababu ya kutofuata sheria. Lakini watu wetu hawa pamoja na nafasi yao hiyo ya kutokujua vizuri sana pengine masuala haya ni vizuri Serikali ili waweze kuiona nafasi yao maana mtu akishaanza kuchimba madini hawezi kufanya kitu kingine, atakufa anatafuta madini tu. *Industry* hii sasa ina wasomi, ukienda kule Winza nimekuta wasomi mbalimbali wapo kule, wana mpaka *degrees* lakini anashika koleo, anashika sululu anachimba, ndicho alichoamua yeye kukifanya, tusipuuze *industry* hii watu wananung’unika sana ni vizuri tukajua nafasi ya Watanzania katika sekta hii bila kujali hali zao za uchumi, bila kujali ukubwa na udogo wa mitaji yao wote tuwafanyie ili waweze kulingana na hao wachimbanji wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuthamini wachimbaji wakubwa peke yao, itatuletea tatizo kubwa na hili ni bomu linalolisubiri Taifa. Mheshimiwa Nyangwine anasema hapa tutagecha, mnadhani anatania anazungumza vile anavyofikiri yeye hali ikifikia hatua hiyo kama huungwi mkono kisiasa utakachofanya ni kufanyaje, utatumia *last resort* ambayo itakuwa ni ku-*mobilize* wale ili waweze kufanya chochote watakachoweza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo baya kwa maana nchi yetu ni nchi ya utawala bora wa sheria lakini inapofika hatua ya namna hiyo ambapo kwa kweli watu wanahisi kwamba wanaonewa na watu wanachojua ni kwamba wanaonewa tu bila kujali pengine hata na wao wanawajibu wa kufuata sheria. Ni vizuri basi Serikali ikaingilia kati na kuwasaidia, kuliko kusema hamjafuata sheria ondokeni, mimi nadhani siyo jambo zuri sana.

Nimshukuru Mheshimiwa Waziri, nishukuru Wizara yao na wataalam kwa kuanza kulishughulikia tatizo la Winza, pale Winza tatizo letu kubwa ni kwamba wamepewa leseni watu wote, kila mtu ana sehemu yake lakini wanang’ang’ania kuchimba kwenye

sehemu ndogo sana ya kama mita 500 kwa 500 kila mmoja anataka kuchimba pale. Lakini ndiyo nasema tatizo la kutofuata sheria, Serikali simamieni sheria, mmefanya jambo lile vizuri, niwataarifu tu wananchi wangu wa kijiji cha Wiza kwamba jambo lililofanywa na Serikali ni jambo zuri ni kwa nia ya sisi hata kijiji na Jimbo la Kibakwe na wilaya ya Mpwapwa kwa ujumla kuwajua ni akina nani lakini tukiacha ile ya uvamizi unaofanyika watu wanachimba kwa nguvu, hatutajua ni nani na tu-*deal* na nani katika hata kuchangia maendeleo ya sehemu yetu.

Sasa Serikali ilivyofanya mimi niombe sana wananchi wa kijiji cha Wiza na kata ya Masa kwa ujumla mkae sasa mjadili namna ya kuwatambua wale wote wenye leseni ili tuwaambie sasa na wao wanachangia nini katika maendeleo ya jimbo letu la Kibakwe, vinginevyo kama ilivyokuwa huko nyuma ni kwamba watachimba na wataondoka, sisi tutabakia hatuna kitu wala mchango wowote ule, tuungane na Serikali katika jambo hili maana ni jambo zuri kuwaweka kila mmoja kwenye kitalu ili aendeshe shughuli zake na waache kuvamiana wao kwa wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nadhani yale niliyokuwa nimefikiria kuyasema nimeyamaliza na kwa sababu hiyo sina sababu yoyote ya kutokuunga mkono hoja, dhamira yangu ilikuwa ni kuisaidia Serikali kupata mawazo mazuri ili tutatue tatizo la umeme kwa haraka iwezekanavyo, bila kujali vikwazo vyovyote. *(Makofi)*

Mwisho kama mjumbe wa *STAMICO*, niwaalike sana wachimbaji wadogo wadogo tumieni *STAMICO*, Serikali niwapongeze kwa kuipa *STAMICO* nguvu na kwa kutupa uwezo na kutuwekea uwanja wa kufanya kazi kwa niaba ya Serikali katika kuwekeza katika sekta ya madini ni jambo zuri kwa Taifa au *any state to have share* kwenye maendeleo ya sekta hii bila kuwaachia wageni peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, awali ya yote ninaomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kwa kuniunga mkono kwa kunichagua mimi niwe Mbunge wao na kunipa wasaidizi, Madiwani kumi kupitia Chama cha *NCCR Mageuzi* katika jimbo lenye Madiwani 19. Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini na nawaahidi kwamba niko imara kama mnavyonifahamu, sitayumba niko tayari kuyafikisha yale mnayoyalalamikia na yale yote mnayonituma kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kuchangia katika Wizara hii, niungane na Wabunge wenzangu waliolalamika ambao wana masikitiko makubwa na mimi nitamke wazi kabisa mbele ya Waziri wa Nishati na Madini kwamba nina masikitiko makubwa kwa kuwa ukiangalia hotuba hii uliyowasilisha, Wilaya ya Kasulu ndiyo kwanza Serikali inaangalia kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya. Lakini juhudi zote zinazofanywa na Serikali za kuhakikisha zinapeleka umeme vijijini, Jimbo la

Kasulu Vijijini lenye kata 19, vijiji vyote hakuna hata kijiji kimoja chenye mradi wowote wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mwakilishi wa wananchi hao ni wazi kabisa kwamba ninasikitika na niombe Waziri mwenye dhamana utakapokuwa unafanya majumuisho, uungane na majibu ya Naibu Waziri aliyonijibu tarehe 13 Julai, 2011 kwenye swali langu la msingi ambalo swali la nyongeza niliomba kwamba Serikali ihakikishe inayatumia maporomoko ya mradi wa umwagiliaji uliopo kijiji cha Titye, kwa ajili ya kuanzisha chanzo chochote cha umeme Jimbo la Kasulu Kijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirudie, kwenye mchango wangu wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, nilionyesha masikitiko makubwa sana ya ukosefu wa umeme mkoa wa Kigoma. Lakini nikasema mkoa wa Kigoma kukosa umeme siyo bahati mbaya, ni uzembe au ni kutokukosa viongozi wenye utashi wa kuhakikisha mkoa wa Kigoma unapata umeme. Kwa sababu mkoa wa Kigoma kuna maporomoko ya kutosha, tuna vyanzo vingi ambavyo tunaweza tukazalisha umeme na mkoa wa Kigoma ukaondokana na kilio cha umeme. Nimesema vyanzo vilivyopo wilaya ya Kasulu, tuna mito ya kutosha, tuna Mto Moga, tuna huo Mto Tintye, tuna Mto Rungwe mpya ambayo watafiti wakitutembelea pale na wakaangalia vyanzo hivi tunaweza tukapata umeme wa uhakika na tukaondokana na usumbufu wa kumlalamikia Waziri na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunasikia habari za umeme, nikiwa Kasulu, nilikuwa nafikiri ni kilio cha mkoa wa Kigoma, leo ninashangaa kuona Tanzania nzima kila anayesimama hana amani na umeme. Ni kwa nini wataalamu wetu wasitumie fursa za mikoa tofauti zilizopo ili kupunguza hivi vilio, angalau wachache walalamike na wachache waondokane kabisa na adha hii ya kuilaumu Serikali. Na hatuwezi kuondokana na tatizo hili kama bado tunategemea umeme wa jenereta, kama bado tunategemea umeme ambao hauna uhakika wa kutokana na vyanzo vyetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukiangalia tunasikia kuna jenereta mpya zinataka kununuliwa, ambazo zina uwezo wa kuzalisha umeme megawati 30. Lakini ukiangalia chanzo ambacho kinaweza kuzalisha umeme Mto Malagarasi unaweza ukazalisha umeme pale, kwa hotuba yake mwenyewe Mheshimiwa Waziri, zaidi ya umeme megawati 41. Ni kwa nini Serikali isiwekeze zaidi kwenye kuzalisha chanzo hiki cha Malagarasi ili ukawa na uhakika kwamba mkoa wa Kigoma umeondokana na lawama za umeme kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Kasulu umeme haujawaka, Kigoma mjini umeme unawaka wa jenereta, lakini bado ni matatizo, leo kila mwisho wa mwezi umeme unakatika karibu wiki nzima kwa kosa la kukosa mafuta. Bado ukiangalia jenereta zilizopo Kigoma zinazalisha megawati 11, megawati zinazotumika ni megawati sita tu, si kwamba ndiyo mahitaji ya mkoa wa Kigoma yameishia hapa ni kwa sababu umeme unaozalishwa na jenereta zilizopo mkoani Kigoma hazina uwezo wa kuhudumia viwanda. Ule ni umeme ambao unatakiwa kutumia kwa huduma za nyumbani. Sasa kama unahitaji kuuokoa mkoa wa Kigoma kiuchumi na kuwaondoa wananchi wa mkoa wa Kigoma kwenye dimbwi la umaskini, ni kwa nini using’ang’anie kuzalisha umeme katika

Mto Malagarasi, ni kwa nini using’ang’anie kuzalisha umeme kwenye vyanzo vilivyopo vya uhakika, kama mito hiyo, maporomoko hayo ninayokutaji, ili kuondokana kabisa na adha hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema mimi ndiyo Mbunge wa Kasulu Vijijini ambako kuna miradi mikubwa ya uzalishaji, tuna mradi mkubwa wa Kilimo Kwanza ambao upo Kijiji cha Kitanga, tuna mradi mkubwa sana wa umwagiliaji ambao upo katika Kijiji cha Tintye, tuna mradi mkubwa sana wa umwagiliaji uliopo Kijiji cha Rungwe mpya. Serikali imewekeza mamilioni ya fedha kuanzisha miradi hii, ni kwa nini tusifikirie ni namna gani tupate chanzo cha umeme ili miradi hii inapoendelea kuzalishwa tuwe na uhakika wa kuweza kupata vitendea kazi kama mradi wa umwagiliaji, tunategemea kuvuna mpunga wa kutosha. Tukipata mpunga wa kutosha, mashine za kukobolea mpunga lazima ziwepo. Tutapataje mashine za uhakika za kukoboa mpunga kama hatuna umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kama leo tunapelekewa mradi wa Kilimo Kwanza mahali ambapo Mwenyezi Mungu ametujaalia kuwa na ardhi nzuri, mahali ambapo tunajua kabisa kwa kilimo Wilaya ya Kasulu, Jimbo la Kasulu Vijijini tuna ardhi nzuri sana. Ni namna gani haya mazao tunaweza tukanufaika nayo Watanzania wa Kasulu bila ya kuwa na viwanda vya kusindika vyakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayaongea haya ili Waziri ayasikie na niombe wakati unapofanya majumuisho ya hotuba yako, ninaomba utamke ni lini utaleta wataalam ambao tutawapeleka kuwaelekeza kwenye hayo maporomoko ili watuanzishie vyanzo vya kuzalisha umeme na sisi tujihesabu kama tuko sawa na Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Mkoa wa Kigoma upo nyuma kielimu, katika Mikoa kumi iliyofanya vibaya kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka jana ni pamoja na Mkoa wa Kigoma. Kwa nini hawa vijana wasifanye vibaya wakati jimbo lenye Kata 19 hakuna kijiji hata kimoja chenye umeme. Lazima ujifikirie hawa Watanzania waliopo huko elimu wanayoipata ni ya namna gani bila vitendea kazi? Leo wanafunzi wanajifunza kwa vitendo lakini hakuna umeme, wenzetu wanasoma kwa *computer*, hakuna umeme huko vijijini, mtihani ukija ni mtihani wa Taifa, kweli tunaelekeza kwamba Serikali inaweka *level* sawa? Ninaomba hili liangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa nafasi yangu ya ndani ya chama cha *NCCR Mageuzi* nimepata fursa ya kuzunguka mikoa mingi, nilipenda nipewe taarifa na Wizara husika kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tukisikia kuna machimbo yanayofanyika Ngara na Kampuni ya *Kabanga Nikel.* Udongo unasombwa kwa miaka mingi bila kupata tamko la Serikali kwamba kinachotolewa pale ni nini? Ni dhahabu au ni *aluminium?* Ni udongo wa namna gani? Kwa sababu lile Shirika liko pale kwa muda mrefu, Watanzania hawapati ajira, hakuna faida tunazoziona ambazo Watanzania tungeweza kunufaika nazo. Ninaomba kwa maslahi ya Taifa letu tupate tamko kwamba *Kabanga Nikel* tangu imeanza kufanya utafiti mpaka leo hii imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona kwa leo niishie hapo sina maneno mengi, ujumbe wangu umefika lakini naomba sana Mheshimiwa Waziri utakapojumuisha uthamini michango yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nyeti ili niweze kuongea machache kuhusu hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze ndugu yangu, Mjomba wangu Waziri wa Nishati na Madini kwa kufanya kazi nzuri sana katika *speech* yake hasa naweza kusema kitendo cha kukabidhi Buhemba kwa *STAMICO* kimenipa matumaini mapya. Ungefanya hivi miaka kumi iliyopita wakati napiga kelele hapa Bungeni kwamba fukuzeni MEREMETA hawa ni wahuni, wakati huo sikusikilizwa. Leo miaka kumi baadaye ndiyo mnakumbuka niliyowaambia, sasa mnasema MEREMETA haipo imekuja *STAMICO*. Kwa kifupi inaonekana ni vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikwenda na watu wa *STAMICO* Buhemba, Buhemba ambayo mimi nimekuwa naiona, Buhemba ambayo ilikuwa inamilikiwa na wanajeshi, Buhemba ambayo ilikuwa inamilikiwa na MEREMETA. Leo Buhemba ni tofauti na ile ya zamani, kila kitu kimechakachuliwa ndani ya migodi, meza, nyumba na mashine zilizoagizwa pale hakuna hata moja. Lakini ukiangalia katika ukurasa wa 90 *paragraph* ya 181. Kwa kuwa, ni muda mfupi wa kuzungumza ninapenda ninukuu uliyoyasema; “Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Taifa linanufaika ipasavyo na mapato yatokanayo na madini, Serikali itaendelea kuliwezesha Shirika la *STAMICO* ili lishiriki kikamilifu katika uwekezaji katika sekta ya madini.”*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisogea nyuma kidogo ama mbele kidogo unasema; “Kufuatia Mgodi wa Buhemba kukabidhiwa kwa *STAMICO*, shirika litaendelea kutafuta mbia mwenye uwezo wa kifedha na kiufundi ili kushirikiana naye katika kufanya utafiti wa kina kwa lengo la kubaini uwezekano wa kufungua tena mgodi huo.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo maneno ambayo ningependa tuyasikilize kwamba kabla ya kukabidhiwa *STAMICO* Mgodi wa Buhemba ulikuwa chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi kuanzia mwezi wa Februari, 2008. Wakati Bajeti inasomwa niliuliza hivi nani yupo Buhemba? Kama ni Jeshi basi ni Jeshi la Wananchi ama ni Jeshi la wahuni? Watu nadhani hawakuelewa maana yake ni nini. Lakini juzi tulipokwenda pale tulimkuta polisi mmoja tu ana bunduki, nyumba anayoishi iko sawa lakini kingine chote kimechakachuliwa vibaya kabisa, magari yameharibika na mengine yameibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mgodi siyo tena mgodi ambao unaweza kukabidhiwa kwa *STAMICO*, kweli kabisa *unless* huo ni usanii wa hali ya juu. Kama kweli mnakabidhi kwa *STAMICO* basi mngekabidhi kama ilivyokuwa miaka kumi iliyopita siyo leo maana ni pori tu na kama kweli ulikuwa unamilikiwa na Serikali basi naungana na Wapinzani wanaposema Serikali legelege pale Buhemba. Nasema hivyo

kwa uchungu maana mitambo ile ni ghali mno na wale watu walichukua fedha nyingi ili kuchimba madini. Fedha walishazilipa watu wa Afrika Kusini zaidi ya bilioni sijui ngapi, sasa leo unasema unawapa *STAMICO* ili wafanye nini? Sikuona chochote kimetengwa ndani ya Bajeti kwamba hawa wa *STAMICO* watapewa kiasi fulani ili waweze kuanza shughuli zile ama ku-*step in the shoes of MEREMETA.*

Sasa hapa tunaambiwa kweli kwamba waliokabidhi *STAMICO* ni wanajeshi lakini ni hewa hakuna kile kitu. Kabla sijaunga mkono Bajeti hii naomba Waziri unithibitishie kwamba utakwenda pale wewe ukatuambie ni nini ukachokabidhi ni yale magofu ama ni nini? Maana hakuna kitu, wananchi wale wanasema kwa kuwa Serikali imekimbia pale ime-*free* kutoka Buhemba basi waachieni wachimbaji wadogo wadogo waendeleze ule mgodi badala ya kudanganya wananchi kwamba leo *STAMICO* itafanya chochote bila kupewa kazi. Hilo la kwanza.

La pili, ni pale umeme unapokwenda Butiama kwa mashamba ya Mwalimu, ni jambo la aibu kusimama mbele yenu hapa nazungumzia matatizo ya Butiama kuhusu umeme. Mashamba ya Mwalimu hayana umeme, ile *transformer* ilishang'olewa, hakuna chochote kinachoendelea pale, ng'ombe pia wanakufa. Sasa najiuliza hivi anayelinda ile mali ya Mwalimu ama mashamba yale ni nani? Maana yake kama JKT ipo pale basi umeme ungekuwepo, ni kitu gani kimekosekana yale mashamba yakabaki aibu namna hiyo na Serikali iko pale, kuna tatizo gani? Ninapenda kujua hivyo.

Suala la tatu ambalo ninapenda kuliongelea ni kuhusu *TANESCO* kwa ujumla. Tunazungumza kwamba tunataka mitambo mikubwa kama ile ya *DOWANS* na kadhalika. Lakini nadhani tatizo la *TANESCO* siyo uzalishaji tu wa umeme, nadhani ile *transmission* ya umeme ina matatizo. Ninaposema *transmission* ina maana kwamba unaposafiri kutoka kwenye *point* ya *distribution*, unapotoka kwenye *point* ya kusafirishwa, kuna uvujaji au umeme unavuja. Lakini sikuona kwenye hotuba hii ni nini kinasemwa kuhusu *transmission problems* yaani *transmission losses*, ni kiasi gani au *percent* ngapi ya umeme ambao unapotea haufiki unakokwenda. Mitambo hii ni ya zamani lakini nyaya zinazopeleka umeme pia ni za zamani sana. Sioni mpango kabambe unaogusia tatizo la *transmission* ambalo ni kubwa zaidi.

Katika miradi mikubwa ya Serikali kuhusu umeme nadhani wenzangu wameshasema *Stiegler's Gorge* ni mfano mmoja. Juzi nilibahatika kuwa Rwanda ambapo kule wanafanya mradi mkubwa wa kutumia umeme kupitia mito mikubwa ambayo ni *Ruzizi One*, *Ruzizi Two* na *Ruzizi Three*. Hiyo inapatikana sana na sisi hatuko mbali pale, sasa nauliza kwa nini Serikali haikupeleka angalau mtu kuwakilisha kuona hii miradi itadhuru vyanzo vya maji vya Tanzania ama lah! Kama sivyo hivyo mnachukua hatua gani kuhakikisha kwamba kinachotendeka kwa majirani zetu hakitadhuru upande wa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Rais anatembelea jimbo langu mwaka jana aliwaahidi wananchi wangu wa Majita hususan Busekela. Wananchi wale kazi yao kubwa ni uvuvi, wana samaki wengi sana lakini kwa kuwa hawana umeme inakuwa vigumu kufanya *export* ya bidhaa kama hiyo kwa mfano kupeleka sehemu za mbali

maana yake hakuna mahali pa kutunza samaki, hakuna barafu maana umeme hukufika kule. Mheshimiwa Rais aliahidi wananchi wale kwamba umeme utapelekwa na *REA*, utatoka sehemu ya Mgango kwenda Busekela ambao ni umbali wa kilomita kama 80 ni karibu sana. Lakini sioni chochote kimetajwa kwenye Bajeti hii kuhusu utekelezaji wa ahadi hii muhimu.

Nakumbuka pia Waziri Mheshimiwa John Pombe Magufuli alifika pale Mgango. Mgango kuna sehemu moja maarufu inaitwa Bwai Kwitururu ama London na Paris, eneo hilo ni la wavuvi lakini linashughulikiwa sana na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Waziri alisema atatumia njia zote kwa kuishawishi Serikali kupeleka pale umeme na kwamba wananchi waweze kufaidika kwenye sehemu hizo. Sioni chochote kwenye Bajeti hii kikizungumza ni lini umeme utafika London na Paris ili kuwawezesha wananchi wangu ambao wamekuwa wakilia kwa miaka mingi waweze kufaidi na matunda ya Uhuru leo. Ninapenda kuona hayo yanafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kusema kwamba hoja hii ni nzuri iwapo utekelezaji wake utakuwa una watu wanaangalia kwa makini. Kuna Mto Mara. Mto Mara unatokea Kenya lakini ukiweka *dam* katikati ya Majimoto na Barrick ukaweka *dam* tunaweza kuzalisha *megawatt* saba za umeme, umeme huu ungeweza kulisha nadhani sehemu kubwa ya Mara ili Mara itokane ama iepukane na matatizo ya umeme maana yake siamini kabisa umeme wa Kijeto utaweza kufika. Mengine haya ni porojo tu, siamini Serikali ina uwezo wa kupeleka umeme kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nasema siungi mkono Bajeti hii mpaka mtakaponiambia ile mitambo ya Buhemba aliyeiba ni nani? Pili, yale madhara yaliyofanyika pale Buhemba mazingira ya pale ni nani atafidia nini? Ni *STAMICO* ama ni Serikali itaweka fedha nyingine pale maana yale ni madhara makubwa sana. Bila hivyo mimi siungi hoja ya Bajeti hii. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa James Lembeli. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Napenda nikiri kwamba nilijiandaa kuchangia sana na ninasikitika kwamba hamtapata mchango wangu kwani nimepatwa na matatizo. *(Makofi)*

Katika Jimbo langu katika Kata ya Rutoro kuna wananchi wamevamiwa, migomba imefyekwa na wavamizi wanalisha ng'ombe. Naiambia Serikali yangu kwamba hali kwenye Jimbo langu si nzuri. Wananchi wangu katika Kata ya Ngenge wamevamiwa na tembo, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maliasili ametuma watu lakini wale watu wamezuiwa wasifanye kazi waliyotumwa na Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, nitajitahidi.*(Makofi)*

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa hiyo, ni mchangiaji wa tatu kwenye Kamati ile, nitajazia kazi aliyofanya Mwenyekiti wa Kamati na baba yangu Waziri Kivuli. *(Makofi)*

Ninapenda niwape historia yangu kwamba mimi leo ni mwaka wa 27 nikiwa katika sekta ya nishati hususan mafuta jamii ya petroli, miaka 27. Kwa hiyo, mnaniangalia naonekana *handsome boy* lakini umri umekwenda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo ya umeme, hesabu za kweli tunahitaji labda *megawatt* 500 au 600, mimi naliita janga la giza. Lakini tofauti na wenzangu mimi nakuja na *style* tofauti kama ilivyo kawaida yangu. Nimekuja na mapendekezo na ningeomba Mheshimiwa Waziri uniambie kama haiwezekani ama inawezekana kwenye majibu yako. Wanasheria wameshazungumza mimi nasema kwamba itafutwe mitambo popote iletwe haraka ili tupate umeme tuondoe giza. *(Makofi)*

Mitambo inayoletwa inatumia gesi na mafuta, kuja kwa mitambo kama alivyosema Mwenyekiti wangu Makamba si hoja, unaweza kuleta mtambo ukafa na ukakosa umeme kwa sababu gesi hakuna. Ninachopendekeza ni kwamba gesi iko Songosongo na *Mnazi bay,* wanatuambia ni miezi 16 mpaka 18 kuleta gesi hapa. Kuna njia rahisi miezi sita au minne kuleta gesi, umbali ule ukate vipande vipande kama anavyofanya Mheshimiwa Magufuli, tengeneza wakandarasi wengi ili wafupishe umri wa kutengeneza bomba ili tulete gesi hapa, tatizo lipo kwenye janga na mimi naliita janga la giza. Siyo lazima ubadilishe Serikali, unaweza ukapewa ukadhani utaendesha lakini ukakuta mambo mazito. Serikali haifanyiwi majaribio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo pia ni pendekezo langu, nataka Serikali yangu iwaambie Watanzania ni heri kuwa na umeme wa bei ghali ambao una uhakika nao kuliko kuwa na umeme wa bei rahisi ambao kila siku unagaiwa giza. Tuwaambie ukweli Watanzania kwamba tunaingia kwenye zama za umeme ambao ni *expensive* kwa kipindi fulani na tutatoka kwenye njia hiyo baada ya kipindi fulani kwa hesabu za uhakika lakini umeme wa *fuel* au mafuta ambao Kenya wamekuwa wakiutumia bei yake ni ghali ndiyo maana *Engineer* mmoja rafiki yangu Masaburi alisema kwamba umeme wa Kenya ni ghali kuliko wa hapa, wataalamu wa viwanda wametueleza na watu wameona. Mwenye kiwanda ni heri ukampa umeme wa aghali kuliko umeme wa rahisi ambao haupo. *(Makofi)*

Pendekezo langu la nne; kuna hadithi nyingi katika ukosekanaji wa umeme; kuna wanaosema hujuma imefanyika katika mfumo unaoleta maji kwenye mabwawa. Naomba Serikali iwe makini kabisa tuanzishe mkakati wa kuwabana waliopewa dhamana watuhakikishie kama kweli vile vyanzo vya maji havikuhujumiwa. Hatuwezi kwenda kwa mpunga kwa kusababisha giza, kuna mpunga unalimwa nchi kavu, acha kulima mpunga kwenye mabonde yanayopeleka maji kwenye mabwawa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye usambazaji wa umeme. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumza kwamba wengine hawajawahi kuuona umeme. Wakati tunaweka nguvu na akili zetu zote kwenye *power generation* tusijisahau

tukazalisha umeme kumbe vijijini haupo, wananchi hawatatusaidia. Mimi namshauri Mheshimiwa Waziri na katika majibu yangu nataka aniambie *yes* au *no*, nataka leo mamlaka ya umeme vijijini wawezeshwe. Ipo dhana ilitoka Bungeni hapa ya kuongeza visenti kwenye simu tunazopiga.

Mheshimiwa Mussa Azzan, amezungumza kuna wapiga simu milioni 20, tujitahidi tuangalie tunaweza kupata shilingi bilioni ngapi tuziwekeze kwenye umeme. Niliwaambia mimi ni mtaalam wa petroli, tunatumia dizeli na petroli takribani lita bilioni 1.7 kwa mwaka, wekeni shilingi kumi kwa kila lita, tupate shilingi bilioni 17 na zenyewe mzipeleke *REA.* Mheshimiwa Waziri utajumlisha mwenyewe ili tuweze kuzalisha umeme wa kuenea vijijini tupunguze malalamiko ya wananchi, mimi sifanyi mahesabu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumefanya maamuzi magumu, tumeongeza bei ya mafuta ya taa, lazima tukiri tumeongeza bei ya mafuta ya taa, lakini pamoja na kuzuia uchakachuaji lengo lilikuwa kuzuia kodi inayopotea ambayo *TRA* inasema ni shilingi bilioni 25 kwa mwezi, makampuni ya mafuta yanasema ni shilingi bilioni 30 kwa mwezi, Kamati ya Nishati na Madini ilikuwa inahisi na ikaunda Kamati ambayo nilipewa mimi niisimamie kwamba shilingi bilioni 50 kwa mwezi zinapotea. Sasa kama ni hivyo na tumeongeza bei ya mafuta, basi kile tutakachookoa kama kodi, kama ni shilingi bilioni 20, shilingi bilioni 15, zipelekwe *REA* tupate namna ya kujitetea, wananchi tuwape umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape angalizo, mimi nawaomba msihangaike katika visiwa vyangu vingine si rahisi kupeleka nyaya za umeme. Sehemu za Gozibakelebe, Bumbiile na Makibwa muwapelekee *solar.* Huwezi kupeleka umeme Mheshimiwa Waziri, ni gharama kubwa, nipelekeeni *solar* kwenye *dispensary,* nyumba za ibada, shule ili kusudi watoto waweze kuona kompyuta, waseme hii ndiyo *CPU* na itoe mwanga wa bluu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia kuhusu *REA* naomba nitoe tahadhari, hizi pesa ukizikusanya ni bilioni nyingi kuliko ambazo baba yangu Waziri Kivuli amezisema. Unajua mimi naitwa Charles John na Waziri Kivuli anaitwa John kwa hiyo lazima nijidai kuwa mtoto wa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi pesa hatuwezi kukusanya tukawaachia wenye meno watafune. Lazima kama tunakubali kukusanya pesa hizi uwepo utaratibu mzuri wa kujua zinakusanywa vipi na zinatumika vipi na siyo siri zitembee jimbo kwa jimbo Tanzania nzima ili Tanzania yote iwe sawa. Nayasema haya kwa makini, naililia nchi yangu kwa dhati na siyo siri naisemea CCM yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta jamii ya petroli; niliwaeleza awali kwamba leo ni mwaka wa 27 niko katika sekta hii, naweza kujidai kwamba katika *distribution* na *trading* ya mafuta Tanzania kati ya watu watano mimi nimo. Mzee Mansoor alikuwa akizungumza pale, nazungumzia ile *regulation* ya *bulk procurement* na nawaomba

wataalam wa Serikali kesho hakuna kazi mnitafute, mbele ya Wabunge niwaambie ile *regulation* ilivyo hovyo, imezungumza mambo ambayo si sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1996 nikiwa *Manchester* nilishirikiana na *Chief Executive* wa Angola kuandika *regulations* za Angola akanipa pesa ya matumizi. Tumebaki kuwatumikia wengine, nyumbani Mwenyekiti wangu amesema hizi *regulations* mbona ni siri? Unatafuta kampuni ambayo *turn over* yake ni dola milioni 500? S*yndication* kubwa ya makampuni iliyowahi kufanyika Tanzania haizidi dola milioni 40, ni ile ya *Kagera Sugar*, dola milioni 500 utaipata wapi? Mje tuzungumze tunayajua haya na sita-*charge fee, if there is a fee*, *invoice* ipelekwe kwa Mheshimiwa Spika. Hatuwezi kukubali na nimekuwa nikiwaambia watoto wa Kware hawawezi kulishwa, watoto wa kuku wakafa, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mafuta. Serikali inapata matatizo katika mafuta kwa sababu ya watu kutokusema ukweli. Bei ya mafuta ina sababu zinazoipelekea kushuka na kupanda, Serikali kwa nini hamsemi *on time?* Niwe wazi, nimefanya kazi siku kumi nikiwashauri watu wa *EWURA* kwamba *talk to people, write articles*, nilikuwa siwaombi wanipe kazi ya kuandika *articles*, nilikuwa nawaambia kinachotakiwa. Wakati Bajeti inasomwa tarehe 8 Juni, 2011 pipa moja la dizeli lilikuwa ni dola 116, sasa hivi ni dola 130 bei ya jana. Shilingi yetu ilikuwa 1,540 kwa dola, leo tunapozungumza ni zaidi ya 1,600 kwa dola. Hizo *factors* zinafanya maamuzi ya Serikali yaonekane hayafai, kwa nini hawasemi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umwambie Waziri wa Nishati awabane waliopo chini yake na sisi tutambana hapa, chama chetu hakiwezi kupakwa matope. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, uwabane walio chini yako. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kuweza kupandisha bei ya mafuta, mimi nimewaandikia *TRA* bila kutuma *invoice*, nimewaambia namna gani wadhibiti mafuta ya ndege. Nazungumza hivi kwa sababu kuna kampuni zimeanza kujitia kwamba zenyewe zinauza mafuta ya ndege na zimeanza kuagiza mafuta ya ndege, walipoagiza nilijua. Lazima tuwe makini kwa sababu kama zoezi hili litafeli tutakuwa tumejipaka matope ambayo hatuwezi kujisafisha. Lazima tuwe makini na napenda niwaeleze kwamba msiende kutafuta washauri elekezi pengine, ulizeni hapa, ulizeni kwenye Kamati. Hii Kamati ina uwezo na imesheheni, asikudanganye mtu, hii Kamati *handsome boy* ni mimi tu, wengine sura zao zimekaa katika hali ya kupigana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Niabu Spika, niwaelezee hifadhi ya kimkakati. Kila siku kwenye vitabu vya Serikali wanazungumza *strategic reserve*, ni wazo zuri lakini mfumo unaopelekea ni uongo, *it can't work*. Unapaswa kuwa na *bonded warehouse* ambayo ni *floating*, ili uweze kuchukua Tanzania kama *strategic advantage* ya ku-*supply* mafuta kwa nchi ambazo zimetuzunguka, ndivyo alivyosema Rais. Huwezi kwenda kukopa pesa za kununua mafuta, una pesa ngapi wewe? Unajua mafuta tunayotumia kwa mwaka?

Unajua ni dola milioni ngapi zinahitajika? Kama hizo dola zipo kwa nini zisinunue mitambo leo? Mje mtuulize tutawaambia bure, mimi nilisomeshwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *bulk procurement* nimeishazungumza *regulation* ya Mheshimiwa Waziri kwamba ime-*flop* na niko tayari mbele ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumi au 20 niichambue moja baada ya nyingine niwaoneshe ni kipi kilichokosewa. Niwaeleze watu wa *TPA* kwamba wakati watafiti wanafanya utafiti wa *bulk procurement* na ujenzi wa *SPM* katika Watanzania waliohojiwa mimi nilihojiwa pia. Wazungu waliandika muhtasari na hawakuuliza mtu mwingine wakaondoka kwa sababu nilikuwa na nondo zote, nimetengenezwa na Serikali kwa zaidi ya miaka 27, mimi nimeingia kwenye sekta ya nishati kwa amri ya Marehemu Mheshmiwa Edward Moringe Sokoine, baada ya sekta ya mafuta kuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeandaliwa na chama, inabidi tuseme, mambo mengine hatukutaka kuyasema, tunayasema sasa. Kwa hiyo, hiyo *bulk procurement* ina mambo ya kulazimisha lazimisha, kuna mambo ya miundombinu, unamwambia mtu bomba liwe na nchi kumi lakini meli ipakue mafuta kwa uwezo wa saa 36, haiwezi ku-*pump* hivyo, nakueleza kama *operator*. Mkimuona Mkurugenzi wa Petroli mumuulize, mimi ndiyo *pump over* wa kwanza Tanzania, nimevaa kaki mimi, nikatoka nikafika hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie gesi asili. Nchi yetu inayo bahati ya gesi asili, lakini haitumiki. Gesi asili haitumiki, *TPDC* haijapewa nguvu, haijapewa rasilimali, haijaelekezwa kusudi iitumie gesi asili inavyopaswa na ndiyo maana Serikali yetu inaulizwa magari yanayotumia gesi yako wapi? Gesi itakuja lini majumbani? Lakini *TPDC* wana wataalam wa kutosha, wanaweza kufanya hivyo. Jibu ninalotaka kujua, ua-*locate* pesa zaidi kwa hawa watu, uwawezeshe waende wakope ili wafanye kazi, hiyo ndiyo namna ya kutatua matatizo, ndiyo namna ya kuwatuliza Watanzania. Gesi tunayo, lakini kama walivyosema waswahili tumeikalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie gesi asili kama nishati mkombozi. Sasa hivi tunatoka kwenye *hydro* tunakwenda kwenye gesi, masikitiko yangu makubwa, gesi asili haitumiki, kinachofanyika hatukijui, kinachoendelea zinabaki ni hadithi. Leo mnaambiwa mmeliwa mdomo, kesho mtaambiwa mmeliwa pua. Unaweza kuwa na binti yako ameolewa, ukasikia huyo mkwe wako anavyomfanya ukabaki kugugumia huku huwezi kwenda kumuamulia. Ndoa ya *TPDC* na *Pan African Energy* ina mashaka. Mara visima vimeoza, mara pesa zimechukuliwa, amezungumza Waziri Kivuli pale nikainamisha kichwa nikasema, sijui ameipata wapi. Ndiyo kuna matatizo na ndiyo maana Kamati yetu ikasema tusiunde tume na ndiyo maana Waziri Kivuli wetu wa *opposition* hawakuunga mkono. Tumesema iundwe Kamati, ikatafute vielelezo, tukishapata vielelezo hivyo ni kumpeleka mtu na kumshughulikia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongezee muda.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nitawasilisha kwa maandishi zaidi. Naunga mkono hoja kwa sababu najua mapendekezo yangu yatafuatwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mwijage ahsante sana, sana. Umenikosha hata mimi hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikiingia ndani ya ukumbi huu jioni ya leo, nimepokea ujumbe kutoka kwa mpiga kura wa Kahama na kwa ridhaa yako naomba nimtaje jina anaitwa Muddy Kipindula. Ujumbe huo unasema na kwa ridhaa yako naomba niusome; “Kama wewe kweli ni mwakilishi wa wananchi wa jimbo la Kahama na wilaya ya Kahama, usiunge mkono hoja hiyo“ na sababu ameziandika nitazisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo kwa sababu jimbo bado ninalitaka, nakubaliana kabisa na Ndugu Kipindula na napenda niseme sitaunga mkono hoja hii hadi hapo yale ambayo ninayafahamu mimi, wananchi wa jimbo la Kahama wanayafahamu na wanataka ufumbuzi wake, yaelezwe bayana ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wilaya ya Kahama ni wilaya pekee hapa nchini ambayo ina migodi miwili mikubwa ya dhahabu, Bulyankulu na Buzwagi na yote inafanyakazi. Mmoja umefanyakazi zaidi ya miaka kumi lakini hivi ninavyozungumza leo, wilaya ya Kahama kwa ujumla wake ina majimbo mawili, Jimbo la Kahama ambalo Mbunge wake ni mimi na Jimbo la Msalala kwa Mheshimiwa Ezekiel Maige, bahati mbaya hayuko hapa lakini nitamsemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wilaya hii pamoja na utajiri huo watu wake ni maskini na ni ya mwisho kwa kila kitu. Kwenye sekta ya elimu wilaya ya Kahama ni ya mwisho, kwenye sekta ya afya wilaya ya Kahama ni ya mwisho, kwenye sekta ya miundombinu wilaya ya Kahama ni ya mwisho kila kitu, lakini kila siku wananchi wa Wilaya ya Kahama wanashuhudia makontena ya mchanga wa dhahabu yakisafirishwa kutoka Kahama sijui yanapitia wapi, yanakokwenda sifahamu, wana-*enjoy*. Wakati mwingine wanajipanga barabarani kushangilia kwa sababu wengine hawajawahi kuona msururu wa malori kama huo na unasindikizwa kwa *escort*. Umaskini unashamiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeisoma hotuba ya ndugu yangu Waziri Mheshimiwa William Ngeleja sikuona mahali popote katika hotuba yake ambapo amezungumzia namna ya kutatua matatizo na migogoro iliyoko kule Kahama, Nzega na Nyamongo. Hakuna, kana kwamba Serikali haijui kwamba watu wanauawa kwenye migodi, watu wanaendelea kuzulumiwa kwenye migodi, hawajalipwa na wale waliolipwa wamepunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano, mzee mmoja anaitwa Mwanakusundwa ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wa Kata ya Mwendakulima pale ulipo Mgodi wa Buzwagi, Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima anamfahamu na kesi yake anaifahamu. Ni mwaka mwaka wa tano sasa tangu alipokuja kushughulikia shida ya yule mzee, yule mzee hajalipwa na anaendelea kukopwa. Mzee huyu alikuwa anadai fidia ya shilingi milioni 51, akasainishwa *payment vocher* ya shilingi milioni 51, alipoenda benki akakuta shilingi milioni 18 tu, shilingi milioni 33 wakawa wamechukua, Mheshimiwa Adam Kigoma Malima huyu hapa ananiangalia, anafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzozana nao yule mzee amelipwa shilingi milioni zingine 17, jumla inakuwa shilingi milioni 35, shilingi milioni 15 yule mzee hajalipwa na Serikali ipo na mimi kuna baadhi ya watu wananiambia niunge mkono hoja, siungi mkono hoja hii mpaka nihakikishe watu kama huyu mzee, tena wa CCM basi angekuwa wa chama kingine nisingesema hapa watu waliguna.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo makubwa sana na mimi kila siku nasema, Mheshimiwa William Ngeleja utaenda wapi ukitoka pale? Kamishina wa Madini ni mtu wa Kahama, lakini ndiye kinara wa kuwadhulumu wachimbaji wadogo wadogo. Nataka niliseme hili, ni la Mheshimiwa Ezekiel Maige, Chama cha Ushirika wa Wachimbaji wadogo wadogo, kuliomba eneo moja zuri na nyeti, baada ya leseni ile kuwa imekwisha muda wake, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Waziri mwenyewe amewaendesha na kuwapeleka pale Nishati na Madini, wamekabidhi maombi yao mapema kabla ya wakubwa hawajaja, siku ilipotolewa leseni, lile eneo zuri na nyeti amepewa Barrick, wale ndugu zangu wametupwa nje. Afisa wa Madini alipoulizwa, alisema *it was a typing error* lakini waliwasilisha maombi safi. Sasa mimi nataka kuuliza, hata kwa Waziri kwenyewe nako mnafanya mambo kama hayo (mnachakachua)? Nyamongo nyingine inatengenezwa kule Kahama na mimi sitastaajabu. Wachimbaji wadogo wadogo ambao tangu nchi ya Kahama na Tanzania hii iundwe wameishi hapo kwa kuchimba chimba tu kidogo kidogo, leo hii wanatangatanga kama mbuzi ambao hawana mwenyewe na ni Watanzania hao, tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili niweze kuunga hoja mkono naomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini mara ya mwisho Barrick ambaye anamiliki miradi minne mikubwa hapa nchini amelipa kodi *(corporation tax),* aniambie. Tulawaka ilikuwa ifungwe mwaka huu, tunaambiwa hawajawahi kutengeneza faida na ndiyo maana hawalipi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina taabu hapa, sasa sijui kama Waziri Mheshimiwa William Ngeleja analo ambalo linaonyesha hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2010 Barrick walikuwa wametengeneza faida ya zaidi ya dola 309,077,000 kabla ya kodi. Baada ya kuondoa kodi faida waliyopata ni dola 222,606,000, hili hapa, hawajalipa kodi. Halafu Waziri anataka kuniambia mimi niunge mkono hoja, siwezi. Bahati mbaya sana ndani ya vigogo sita wanaoongoza Barrick yupo Mtanzania, nafikiri yupo hapa ndugu yangu Deo Mwanyika, *Vice President* na yeye anadiriki *at times* kusema kwamba *these people they don't make profit.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchungu nasema baadhi ya matatizo yanayojitokeza hapa nchini sasa hivi ni kwa sababu ya kutokuenzi baadhi ya mambo ya msingi kabisa ambayo Baba wa Taifa aliyasema hata kabla ya Uhuru wa nchi hii. Hivi kwa nini unishawishi mimi mwananchi wa Kahama nikubali kwamba hawa Barrick wanasaidia uchumi wa nchi hii, siwezi kukubali. Ukiwauliza wananchi wa Kahama leo maisha yao yakoje, leo na kabla ya migodi hii miwili haijaanza kufanya kazi kule Kahama watakuambia tunachoambulia ni vumbi. Nenda Kahama ni vumbi, mabati yote yamegeuka rangi kwa sababu ya vumbi linalotoka pale, lakini ukiwaambia wapitishe boza pale wamwage maji hawataki. Wananchi waliwapokea kwa mikono miwili kwa ahadi zilizokuwa zimetolewa, leo nenda Kahama pale ulizia ajira, utakuta vijiwe pale vijana hawana kazi. Waliahidiwa fursa za biashara hata kuuza maji ndani ya ule mgodi wameajiri mtu sijui kutoka wapi na sheria ipo. Ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja hapa amefanya nini au watu wake wamefanya nini, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli sitaunga mkono hoja hii hadi hapo nitakapopewa majibu yanayoridhisha. Nchi hii ni yetu sote, hata nyie mliokaa huko mbele ni Watanzania kama sisi, tukipiga kelele mtusikilize. Wameniambia Ndugu Ngeleja alienda pale Mwendakulima wakamlalamikia na wakamwambia hizi nyumba walizojenga hawa Barrick zinapata *crakes* na zile za wananchi zinapata *crakes* kwa sababu ya milipuko. Ina maana *EIA* haikufanyika vizuri ni kosa la Serikali. Kama hawajui ni kwa nini wanapofanya *blasting* wanazunguka na kitoroli wanawaambia msikae ndani kaeni nje saa nane, wanaogopa wakiwaambia tulipeni fidia hawataki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Buzwagi wana umeme wa kudumu hauzimiki. Lakini katika miji ambayo ina shida ya umeme kukatika hata wakati wa neema ni Kahama. Nimezungumza ndani ya Bunge hili zaidi ya mara nne na ahadi kwamba Serikali ipo kwenye mchakato wa kujenga kituo cha kupoza umeme mpaka lini? Dhahabu inaondoka, tupo kwenye mchakato, hicho kituo kinagharimu kiasi gani? Mimi nimeshangaa Waziri anasema umeme vijijini unapelekwa kijiji cha Mwakata sasa yapo maeneo pale mjini na nimeuliza swali hili mara nyingi kilomita mbili kutoka katikati ya Mji wa Kahama Nyakato kuna shule ya sekondari *Under Lake* ipo barabarani, Bukondamoyo kilomita tatu, Mungula, Lugela, Manzese hawana umeme leo unapeleka umeme kilomita 30 kutoka mjini akili ya wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Ndugu zangu turejeshe moyo wa uzalendo wa kuipenda kwanza nchi yetu na kuwapenda Watanzania wenzetu. Wizara hii kila mwaka inalalamikiwa, tatizo ni watendaji na mambo ya ajabu sana utakuta mtu amelalamikiwa aundiwe Tume lakini anapandishwa cheo, akaharibu na kule anakopelekwa. Tufike mahali tuseme ukweli na msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Ukimhukumu mtu kwa kusema ukweli wewe ndio utakwenda kunyongwa mbele ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema nitaunga mkono hoja hii tu pale ambapo maswali niliyouliza yatakuwa yamejibiwa. Sipendi kuendelea kwa sababu nazidi kupanda mori nisije nikasema maneno ambayo hayalingani lingani na heshima niliyonayo. Nimesema Wanyamwezi, Wasukuma ni watu wapole, lakini kwa jinsi ambavyo

mnawaletea wawekezaji ambao hawana hata utu itafikia siku moja tutasema hapana. Kijiji cha Mwendakulima ulipo Mgodi wa Buzwagi hawana maji. Wao ndani wana maji bwelele wanamwagilia kila siku hakuna vumbi kule ndani, kijijini pale ni pua na mdomo hawana maji, jamani namwomba Waziri Mkuu ukija Kahama nikupeleke pale, wasikupangie, watakupeleka katika maeneo mazuri mazuri, nitakupeleka uone shule ambayo ipo mita 50 kutoka kwenye *fence* huwezi kuamini macho yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema siungi mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mwongozo wa Spika

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa James Lembeli, Mwongozo Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7) labda noisome; “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambako hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi.”

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikiliza toka asubuhi unaona moja ya kilio cha Wabunge wengi na kwa kweli kilio cha nchi ni tatizo kubwa umeme. Moja ya jambo ambalo limesemwa vizuri sana hata na Waziri kwamba tunalo tatizo tunaweza tukapata leo mashine za umeme tunalo tatizo la gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nipate Mwongozo wako gesi ni ya Watanzania, lakini gesi hii amekabidhiwa *Pan African Energy*. Nataka kuomba Mwongozo wako na baada ya kutoa Mwongozo wako Bunge liamue, mimi napendekeza mkataba wa *TPDC* na *Pan African Energy* uvunjwea kwa ajili ya maslahi ya nchi hii ili tuachwe kuweka rehani wakati Watanzania na uchumi wa nchi hii unapotea wakati makampuni yanafaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nimekusikia. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sikutarajia kabisa kama nitachangia leo, lakini nakushukuru sana nadhani umeona mada yenyewe ni mada ambayo mimi ni mdau mkubwa sana wa muda mrefu. *(Makofi)*

Lakini pili pamoja na kwamba Mheshimiwa Mwijage yeye miaka 27 ameitumia katika eneo la mafuta, mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba baada ya kuteuliwa kwenye Kamati ya Jaji Bomani niliamua kwenda kujiongezea maarifa na kusoma Shahada yangu ya Uzamili katika eneo la *Mineral Economics* na nimeandika katika eneo la *fiscal regime* maeneo ya kikodi katika mikataba ya madini na mafuta. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa kupata fursa hii ambayo sikuitegemea kabisa kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nitaanza na eneo la madini. Ripoti ya Jaji Bomani kuna mapendekezo ambayo iliyapendekeza yameshughulikiwa katika Sheria mpya na kuna mapendekezo ambayo bado hayajashughulikiwa na hasa kwenye kanuni. Utakumbuka kwamba katika Sheria mpya ya madini tulipitisha viwango vipya vya mirahaba. Zamani tulikuwa tunatoza asilimia tatu na tukapitisha kwamba sasa tutoze asilimia nne, ingawa ripoti ya Jaji Bomani ilipendekeza asilimia tano. Lakini jambo kubwa kuliko yote ambalo tulipendekeza katika ripoti ile lilikuwa ni suala la kubadilisha mfumo wa kukokotoa mrahaba kutoka *netback value* kwenda *gross value*. Kwa maana ya kwamba sasa hivi Makampuni ya Madini yanapozalisha dhahabu kwa mfano yakiuza yanaondoa gharama za usafirishaji ambazo hatuna *control* nazo, yanaondoa gharama za *insurance* ambazo hatuna *control* nazo na gharama nyinginezo ambazo zinaendana na ule usafirishaji katika kukokotoa mrahaba. *(Makofi)*

Sasa ukiangalia tuna mirahaba kwa madini tofauti tofauti. Nilipiga hesabu hapa mwaka jana tumeuza nje dhahabu ya thamani ya dola bilioni 1.6 ambazo ni sawa sawa na shilingi za Kitanzania takriban shilingi trilioni 2.6 kwa *exchange rate* ya sasa. Katika hiyo tuliuza dhahabu peke yake ya thamani ya dola bilioni 1.4, lakini *royalty* ambayo ilikusanywa mwaka jana ilikuwa ni shilingi bilioni 80 tu. *Royalty* ambayo tunaitarajia kuikusanya mwaka huu wa fedha kwa mujibu wa kitabu *volume one* na Waziri Kivuli wa Nishati na Madini amezungumza ni shilingi bilioni 99.5. Hizi ni sawa sawa na asilimia 3.8 ya mauzo yote ya dhahabu ambayo tumefanya nje pamoja na madini mengine. Iwapo tungetekeleza ripoti kwa kubadilisha mfumo wa kukokotoa mrahaba na kupandisha hiyo asilimia moja tungekusanya *royalty* ya shilingi bilioni 198 ambayo ingekuwa sawa na asilimia 7.6 ya madini yote ambayo tunauza nje. *(Makofi)*

Katika hotuba ya Waziri amesema kwamba Serikali bado inazungumza na Makampuni ya Madini. Serikali imeanza kuzungumza na Makampuni ya Madini mwaka 2006 ni lini itamaliza mazungumzo hayo na Makampuni ya Madini. Lazima ifikie wakati kwamba tujione kwamba sisi ni dola iliyo huru, tuna mamlaka yetu katika ukusanyaji wa kodi na hao wenzetu wakubali kwamba na sisi tunapaswa kufaidika na rasilimali zetu za madini. Nilikuwa naomba kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 Makampuni ya Madini yapelekewe *invoice* ya *royalty* kutokana na Sheria Mpya ya Madini ili tuweze kupata mapato ya kutosha na kuweza kuiendesha nchi yetu.

La pili, tulitoa mapendekezo, Makampuni ya Madini yanapouza dhahabu yao nje, sheria yetu ya *Foreign Exchange Act* inawaruhusu kuweka fedha zote nje. Fedha ya mapato yote ambayo nimesoma hapa ya *1.6 billion dollars* ambazo zinatokana na mauzo yetu ya madini nje yote inawekwa nje, hakuna hata senti inayorudi kwenye benki za ndani na ndiyo maana mnaona pamoja na mapato makubwa tunayoyapata kwenye madini

na bei ya dhahabu kuongezeka shilingi yetu inatetereka kwa sababu hatuna dola za kutosha ndani ya *economy* ya ndani. Sasa tulipendekeza kwamba asilimia 60 ya *procurement* ambayo Makampuni ya Madini yanafanya ni *locally* na sasa hivi wananunua vitu vya ndani asilimia 60. Ripoti ya Jaji Bomani ikapendekeza asilimia 60 ya mauzo ya dhahabu kwa maana fedha za kigeni inayouzwa nje irudi iwekwe kwenye fedha za ndani na ikirudi sasa hivi dola haitakuwa shilingi 1,600 tena itashuka mpaka shilingi 1,200 kwa mujibu wa taarifa za watalaamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika *regulations* za Sheria mpya ya Madini hili liangaliwe, tuweze kuhakikisha kwamba tunaweka kipengele hiki ili asilimia 60 ya mauzo yanayotokana na dhahabu nje irudi kwenye benki za ndani. Tuwe na dola ya kutosha kwenye *economy* yetu tuweze kudhibiti mabadiliko makubwa sana kuporomoka kwa shilingi yetu.

Kuhusu *Geological Survey,* Mheshimiwa Hamad Rashid katika jambo ambalo nadhani ni *trademark* yake ni *mapping* ya nchi kwenye madini. Amekuwa akizungumza sana, nashangaa sijui kwa nini hatumsikilizi. Sasa hivi hatujui ni kiwango gani mashapo ya madini kiasi gani tuliyonayo nchi nzima. Chombo pekee ambacho kinaweza kutusaidia kufahamu ni *Geologocal Survey of Tanzania (GST).* Tembelea *Geological Survey* zote duniani ni Taasisi zenye nguvu sana. Sisi Taasisi yetu tunaipa fedha kidogo sana kwa hiyo hatufanyi *mapping.* Matokeo yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya mfumo wa kutoa leseni za utafutaji wa madini kwa anayekuja kwanza anapewa kwanza bila ya kujua kiwango cha mashapo ambacho tunacho. Wakati kama tukiitumia vizuri *Geological Survey* huko siku za usoni tunapokwenda inaweza ikawa inafanya *tendering.* Inatangaza *tender* kwa sababu itakuwa inajua wapi kuna dhahabu kiasi gani na matokeo yake ni kwamba tutapata fedha nyingi na tunatumia huu mfumo kwa *TPDC* sasa hivi. *TPDC* vitalu vyote vya mafuta ambavyo vinatolewa vinafanywa kwa zabuni, kwa *tender* kwa sababu tumewapa jukumu hilo, lakini kwa upande wa leseni za madini hatufanyi hivi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba *Vote 58* tuangalie vifungu vya ndani vya *Vote 58*, tufanye *reallocation* nitapendekeza hili siku ya Jumatatu ili tuongeze fedha kidogo kwenye *Geological Survey of Tanzania*, tuipe kazi ya kufanya *mapping* ya nchi tujue rasilimali za madini ambazo tunazo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie gesi. Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuzungumza na napenda nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa vijana wenzangu wawili, nimewatangulia Bungeni kwa hiyo ni vijana wangu, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa January Makamba kwa hotuba zao ambazo zinaonyesha dhahiri kwamba imefikia wakati sasa vijana wachukue utawala wa nchi hii. Kwa sababu hotuba zao zimetoa mwelekeo wa namna gani ambapo tunaweza tukamiliki rasilimali zetu. Tuna tatizo kwenye mikataba ya gesi, tumeingia mikataba hii inawezekana hatukuwa tunajua ni nini ambacho tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Freeman Mbowe amezungumza hapa kuhusu Kampuni ya *Orca* ambayo ndiyo Kampuni mama ya *Pan African Energy,* ndiyo yenye mkataba na Shirika la *TPDC, Production Sharing Agremeent (PSA). Pan African Energy* ina-*operate* vile

visima. *Orca* Mheshimiwa Mbowe amesema hapa katika taarifa yake ya mwaka na naomba kununukuu; *"Under the terms of the PSA with TPDC, the company is liable for income tax in Tanzania at the corporate rate of 30%, however where income tax is payable this is recovered from TPDC by deducting an amount from TPDC's profit share. This is reflected in accounts by adjusting the company's revenues by appropriate amount."*

Leo tunavyozungumza Sweden kuna ripoti iliyotolewa na *Action Aid* zaidi ya dola milioni 13.3 zimekwepwa kama kodi kunatokana na mkataba wa *Orca* na *TPDC* kwa *PSA.* Kwa lugha nyepesi ni kwamba *Orca* hawalipi kodi ya mapato, wakilipa kodi ya mapato wakati tunapofikia ku-*share* ile gesi ya ziada ambayo imekuwa imeuzwa wanaondoa fedha yao ambayo waliiilipa kama kodi ya mapato, hili jambo sio jipya. Mwaka 2009 mwezi Aprili, katika Taarifa ya mwaka ya Kamati ya Mashirika ya Umma tulielezea hapa kwamba tulipoteza shilingi bilioni mbili kutokana na kodi ambayo *Pan African Energy* walipaswa wailipe kama kodi ya mapato lakini wakairejesha kinyume kupitia *TPDC* kufuatia mkataba huo wa *Production Sharing Agreement. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Orca* inamiliki *Pan African Energy. Pan African Energy* ndio mmiliki wa gesi. Kimsingi gesi inamilikiwa na *TPDC.* Lakini kwa sababu kwanza hatujapewa asilimia 20 yetu ambayo tunatakiwa tuichangie katika umiliki wa gesi. Lakini pili kwa sababu *Pan African Energy* imesajiliwa, *offshore* hiyo ndiyo mambo ambayo niliyokuwa nayazungumza juzi wakati wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamba *Orca* imesajiliwa *offshore*, *Pan African Energy Corporation* imesajiliwa *offshore.* Halafu *you have Pan African Energy Tanzania.* Ukishaona tu mfumo wa namna hiyo ni mfumo mkubwa sana wa kupoteza kodi. Naungana na Kamati ya Nishati na Madini, naungana na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa John Mnyika kwamba *investigation* ya kina ifanyike kuhusiana na *Production Sharing Agreement* kati ya *TPDC* na *Orca* na *Pan African Energy*.

Lakini pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda timu ya kuchunguza Mkataba wa Umeme kati ya *Songas* na *Tanesco* mwaka 2008. Tunaomba ripoti ambayo alikabidhiwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ionekane na tuweze kuona namna gani ambapo tunalitatua tatizo hili kwa sababu tunalipa fedha nyingi sana kama *capacity charge* kwa *Songas* zaidi ya shilingi bilioni tano kila mwezi tunalipa na sasa hivi nasikia sijui imefika bilioni sita hata kama hawajazalisha umeme. Lakini ikitokea matatizo ya uzalishaji wa umeme ni yao. Kwa mfano, juzi ilipotokea visima vikawa na kutu wakashindwa kuzalisha umeme wao hawatulipi, ila sisi tunaendelea kuwalipa *capacity charges.* Mambo kama haya ni lazima tuyaangalie na tuyafanyie marekebisho makubwa. *(Makofi)*

Kiongozi wa Upinzani Bungeni ametoa mapendekezo hapa kwamba Wizara ya Nishati na Madini iwe-*split into two.* Tuwe na Wizara ya *Energy and Petroleum Resources* na Wizara ya *Mine and Minerals Resources.* Mbunge mmoja akatoka akasema kwamba nyie ndio mnalilia Serikali mnasema kwamba ni kubwa, lazima wakati mwingine tujaribu kuangalia mazingira yanayotuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Wizara hapa ya Vitoweo, unaweza ukaivunja ikawa ni Idara tu, lakini uhakikishe kwamba una mtu mmoja akilala, akiamka anawaza umeme. Akilala, akiamka anawaza gesi na mikataba, uwe na mwingine ashughulike na madini. Hili sio pendekezo jipya sababu amesema Kiongozi wa Upinzani ndio watu wakaanza kubeza, pendekezo hili Jaji Bomani alilitoa pia na kwenye ripoti ya Bomani kuna pendekezo hili pia. Sio kila jambo ambalo Kambi ya Upinzani inalitoa ni baya na sisi ndio tunaathirika na umeme. Wapiga kura wetu wanakosa ajira, nchi inaumia.

Sasa hivi *IMF* wamesema kwamba *forecast* ya *growth* imeshuka mpaka *1.5% more than one trililion* kwenye *economic.* Mtu mwingine wa kawaida ambaye hajui hizi *economic* za *energy*, za *mining* mtu akadhani hilo ni jambo dogo sana. 1.5% ya *growth* maana yake ni kwamba unaondoa *from the economy one billion dolar*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hili ulisikie, ushauri huu ambao wameutoa Kiongozi wa Upinzani Bungeni uuzingatie na uufanyie kazi mara moja ili tuweze kutatua hili tatizo kubwa ambalo tunalo la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeiambia Serikali mara kwa mara, kwanza sijui kama nitawahi kumaliza. Sasa hivi tuna *SYMBION* inazalisha umeme sijui megawati ngapi kupitia mitambo iliyokuwa ya *DOWANS*, mitambo hii tuliambiwa ni mitambo chakavu na kelele zilipigwa sana na wengine tulipewa majina mengi sana. Leo sisikii mtu kila mtu ameufyata, *nobody is saying anything* kwa sababu sijui ni Wamarekani. Lakini mimi *I am happy* kwamba niliyoyasema mwaka 2009 mnayatekeleza mwaka 2011. Tumeumia sana. Lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba kabla sijaondoka duniani limeonekana nililolisema na watu wote ambao walikuwa wanapinga, wanaona aibu hawasemi sasa hivi. Sijui kwa sababu Mmarekani amechukua, *we don't know*. Mheshimiwa Mrema alimuuliza Mheshimiwa Ngeleja, maana yake mimi na wewe Ngeleja ndio tulisema tununue, tutekeleze hili. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa naomba iwe fupi sana kwa sababu ya muda.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Wakati Mheshimiwa Zitto anaanza kuchangia alisema Charles Mwijage wakati alikaa kwenye nishati miaka 27 yeye alikwenda kusoma. Kwa manufaa ya wanajimbo wangu nataka nimjulishe kwamba mimi nimejifunza mambo ya usalama na ulinzi kuhusu *installation* muhimu huko Zimbabwe. *Infact* mimi ninayo *MBA* kutoka Solvod ya London.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru Mheshimiwa Mwijage kwa kuweka sawasawa haya maneno, huyu kijana alitaka kukukadiria, lakini alichotaka kumaanisha ya kwamba na yeye ni gwiji katika eneo hilo hilo kwa sababu amekuwa akisoma mambo hayo huko Ujerumani yanayohusiana na mambo ya nishati. *(Makofi)*

Sasa muda wetu ni mdogo sana naomba tusikilizane Waheshimiwa Wabunge kwa mambo mawili, matatu ya haraka sana.

La kwanza ni masuala ya Mwongozo. Mwongozo wa Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed ambao ulitolewa asubuhi tutaushughulikia siku ya Jumatatu baada ya Mheshimiwa Waziri kutoa hotuba yake. Naamini katika hotuba yake atakuwa ametoa na ufafanuzi, kwa hiyo, atakayekuwepo kwenye kiti hapa atashughulikia Mwongozo huo, tunaachiana Makatibu hapa tutapeana taarifa. *(Makofi)*

Mwongozo wa pili wa Mheshimiwa Peter Serukamba. Yeye amesema kwamba Bunge liamue ule mkataba kati ya *TPDC* na *Pan African Energy* mkataba huo uvunjwe kwa kuamuliwa na Bunge. Tunayo mapendekezo ya Kamati ambayo yalisomwa hapa mapema Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ukurasa wa tisa yanasema ifuatavyo; "Licha ya kwamba gesi ni maliasili muhimu kwa uchumi na usalama wa nchi, Kamati imebaini kwamba biashara na utaratibu mzima wa uchimbaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji nchini vimegubikwa na utata mkubwa wa kimkataba usio na maslahi kwa Taifa pamoja na ukiritimba. Kamati haijaridhishwa na ushiriki, ufanisi na uadilifu wa Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania* katika mchakato wa uendelezaji gesi nchini, hivyo basi kufuata utata huo uliopo Kamati ya Nishati na Madini inaunda Kamati yake ndogo ili kufuatilia utata huo." *(Makofi)*

Sasa mimi nilidhani kwa mapendekezo haya ya Kamati ni mapendekezo mazuri, tuipe nafasi Kamati ifanye kazi yake ili hata itakapolihitajia Bunge kama anavyosema Mheshimiwa Serukamba sasa lifanye maamuzi, ili Bunge lifanye maamuzi ambayo ni *informed* ambayo yameshafanyiwa kazi vizuri na Kamati yetu. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba Mwongozo wangu ni kwamba tuipe nafasi Kamati na sisi katika uongozi wa Bunge tutafanya kazi na Kamati yetu kwa karibu kuhakikisha kwamba mapendekezo ambayo wanayatoa yanafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Vinginevyo, Waheshimiwa Wabunge kwa kweli wachangiaji ni wengi. Bunge leo limekuwa moto, Bunge la Kumi tangu lianze sijawahi kuliona likawa la moto kiasi hiki, lakini ni Wabunge wanafanya kazi yao. Jumatatu ataanza Mheshimiwa Omary Badwel, atafuatiwa na Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Sylivestry Koka, Mheshimiwa Lolesia Bukimbwa na wengine watafuatia. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, niwaambie tu Makatibu kuwa Bunge hili la moto. Sasa mwiteni *boss* wangu huko aliko jamani Jumatatu awe hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli za Bunge zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika ninaomba sasa niliahirishe Bunge hadi siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.48 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 18 Julai, 2011 saa tatu asubuhi)*